JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA




MACHI
2022

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: 255 (026) 2321759, Nukushi: 255(026)2117527, Baruapepe: ocag@nao.go.tz, Anwani: www.nao.go.tz

**Kumb. Na.FA. CGA.319/421/01A** **30 Machi 2022**

Mh. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu, S.L.P. 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: KUWASILISHA RIPOTI KUU YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418, ninayo furaha kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

Nawasilisha,

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

## KUHUSU OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**Mamlaka**

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi, Sura ya 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi ya kiwango cha hali ya juu katika ukaguzi wa sekta ya umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za ukaguzi wa sekta ya umma zenye ubora wa hali ya juu zinazoimarisha utendaji, uwajibikaji, na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

**Kaulimbiu**: "Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma".

**Misingi ya Maadili**

Katika kutoa huduma zenye ubora, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaongozwa na misingi ya maadili ifuatayo:

i. Kujitegemea na Kutopendelea
ii. Uwezo wa Kitaaluma
iii. Uadilifu
iv. Ubunifu na Uvumbuzi
v. Kutoa Matokeo
vi. Kufanya Kazi kwa Pamoja

**Tunafanya haya kwa:**

- ✓ Kusimamia fedha za umma kwa kuhakikisha kuwa wakaguliwa wanawajibika ipasavyo kwa rasilimali walizokabidhiwa.
- ✓ Kusaidia kuimarisha ubora wa huduma za jamii kwa kuunga mkono juhudi za ubunifu katika matumizi ya rasilimali za umma.
- ✓ Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakaguliwa kuhusu mapungufu ya kiutendaji katika mifumo yao ya uendeshaji.
- ✓ Kuwashirikisha wateja wetu katika mchakato wa ukaguzi na hatua zake; na
- ✓ Kuwapatia wakaguzi mafunzo sahihi, na vitendeakazi vya kutosha ambavyo vitachangia kuwa huru katika kufanya kazi zao.

## YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ................................................................ v
ORODHA YA VIELELEZO.................................................................vii
ORODHA YA VIAMBATISHO ...........................................................viii
VIFUPISHO NA MANENO ................................................................ x
TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ...... xii
DIBAJI ..........................................................................................xiii
MUHTASARI....................................................................................xv
SURA YA 1 ....................................................................................... 1
HATI ZA UKAGUZI ............................................................................ 1
SURA YA 2 ....................................................................................... 4
HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA ................................................................................... 4
SURA YA 3 ....................................................................................... 8
TATHMINI YA MFUMO YA UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA MIFUMO YA UTAWALA BORA ...................................................... 8
SURA YA 4 ..................................................................................... 26
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI.............................................. 26
SURA YA 5 ..................................................................................... 38
USIMAMIZI WA MAPATO.................................................................. 38
SURA YA 6 ..................................................................................... 60
USIMAMIZI WA MATUMIZI ............................................................... 60
SURA YA 7 ..................................................................................... 73
USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA .......................... 73
SURA YA 8 ..................................................................................... 79
UKAGUZI WA MIRADI YA KIMKAKATI, MAENDELEO.......................... 79
NA MIRADI MINGINE....................................................................... 79
SURA YA 9 ..................................................................................... 85
USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA ...................................... 85
SURA YA 10 ...................................................................................110
UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU ........................110
SURA YA 11 ...................................................................................119

UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA AFYA .......................... 119
SURA YA 12 .......................................................................... 130
UFANISI WA MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA .............................. 130
NA WATU WENYE ULEMAVU .................................................... 130
SURA YA 13 .......................................................................... 137
UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA MASOKO NA VITUO VYA MABASI ....... 137
SURA YA 14 .......................................................................... 147
MAPITIO YA UFANISI KATIKA UWEKEZAJI .................................... 147
SURA YA 15 .......................................................................... 161
MATOKEO YA UKAGUZI MAALUMU ............................................ 161
MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO ....................................... 206

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1-1: Mwenendo wa hati za ukaguzi ........................................... 3
Jedwali Na. 2-1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya nyuma ........................ 5
Jedwali Na. 2-2: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC ................................. 7
Jedwali Na. 2-3: Halmashauri zenye maagizo ya muda mrefu ............................ 7
Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani ....................... 27
Jedwali Na. 4-2: Halmashauri zilizokusanya mapato zaidi ya bajeti ................... 28
Jedwali Na. 4-3: Halmashauri zilizokusanya mapato chini ya bajeti ................... 29
Jedwali Na. 4-4: Uwiano wa mapato ya ndani na ruzuku ya matumizi ya kawaida... 29
Jedwali Na. 4-5: Jumla ya ruzuku kutoka serikali kuu.................................. 30
Jedwali Na. 4-6: Ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa ....................... 31
Jedwali Na. 4-7: Ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa zaidi ya bajeti ..... 32
Jedwali Na. 4-8: Mapokezi ya ruzuku ya matumizi ya kawaida pungufu ya bajeti ... 33
Jedwali Na. 4-9: Fedha za ruzuku ya maendeleo zilizotolewa .......................... 34
Jedwali Na. 4-10: Ruzuku ya maendeleo iliyotolewa zaidi ya bajeti ................... 35
Jedwali Na. 4-11: Ruzuku ya maendeleo iliyotolewa pungufu ya bajeti ............... 36
Jedwali Na. 5-1: Ankara zilizorekebishwa bila viambatisho ............................. 40
Jedwali Na. 5-2: Vyanzo vya mapato visivyokusanywa .................................. 43
Jedwali Na. 5-3: Wadaiwa wa mapato mbalimbali....................................... 44
Jedwali Na. 5-4: Halmashauri zisizohuisha sheria ndogo................................ 46
Jedwali Na. 5-6: Kiasi kisichowasilishwa na mawakala kimkataba...................... 49
Jedwali Na. 5-7: Wazabuni waliotunukiwa kwa kiwango cha chini ..................... 50
Jedwali Na. 5-8: Madai yasiyokusanywa kutoka leseni za biashara ..................... 52
Jedwali Na. 5-9: Leseni za biashara zilizotolewa nje ya mfumo ........................ 53
Jedwali Na. 5-10: Makusanyo ya ushuru wa huduma bila uthibitisho................... 55
Jedwali Na. 5-11: Ushuru wa huduma usiokusanywa .................................... 56
Jedwali Na. 5-12: Madai ya ada za ukusanyaji wa taka ................................. 58
Jedwali Na. 5 -13: Mwenendo wa madai ya muda mrefu ............................... 59
Jedwali Na. 6-1: Mwenendo wa matumizi yasiyo na manufaa.......................... 61
Jedwali Na. 6-2: Malipo yasiyokatwa kodi ya zuio ....................................... 63
Jedwali Na. 6-3: Risiti za kielekitroniki zisizo halali...................................... 64
Jedwali Na. 6-4: Malipo kwa fedha taslimu ............................................... 65
Jedwali Na. 6-5: Mamlaka zenye matumizi nje ya bajeti ............................... 67
Jedwali Na. 6-6: Mwenendo wa malipo yasiyo na viambatisho.......................... 69
Jedwali Na. 6-7: Madeni yasiyooneshwa katika taarifa za fedha........................ 70
Jedwali Na. 6-8: Mwenendo wa madeni yasiyolipwa..................................... 71
Jedwali Na. 7-1: Malipo kwa watumishi wasiokuwapo kazini ........................... 74
Jedwali Na. 7-2: Michango ambayo haijapelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi zingine ........................................................................ 75
Jedwali Na. 7-3: Madai ya wafanyakazi ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu ...... 77
Jedwali Na. 7- 4: Wastafu kutolipwa gharama za usafirishaji wa mizigo baada ya kustaafu ........................................................................... 78
Jedwali Na.9-1: Ununuzi bila idhini ya bodi za zabuni ................................. 86
Jedwali Na. 9-2: Ununuzi ambao haukuripotiwa kwa bodi ya zabuni.................. 86
Jedwali Na. 9-3: Ununuzi uliofanyika nje ya mpango wa ununuzi ..................... 87
Jedwali Na. 9- 4: Ununuzi uliofanyika bila ushindani.................................... 88

Jedwali Na.9- 5: Ununuzi uliofanyika bila hati ya kuagiza vifaa ........................ 89
Jedwali Na. 9-6: Malipo ya bidhaa na huduma kabla ya ukaguzi ........................ 90
Jedwali Na. 9-7: Kuanza miradi bila tathmini ya athari kwa mazingira ................ 91
Jedwali Na. 9-8: Mikataba isiyohakikiwa na mwanasheria .............................. 92
Jedwali Na.9-9: Ununuzi kwa Wazabuni wasiokuwa na mikataba ....................... 93
Jedwali Na. 9-10: Malipo bila ya vipimo vilivyoidhinishwa .............................. 98
Jedwali Na. 9-11: Miradi iliyotekelezwa bila kuzingatia sheria ........................ 101
Jedwali Na. 9-12: Miradi iliyotekelezwa bila kuzingatia ubora ......................... 103
Jedwali Na. 9-13: Miradi iliyotekelezwa bila mchangunuo wa vifaa ................... 104
Jedwali Na. 9-14: Utunzaji usiofaa wa vifaa vya ujenzi ................................ 106
Jedwali Na. 9-15: Malipo bila kuwapo kwa mikataba na mafundi ..................... 107
Jedwali Na. 9-16: Bidhaa zilizonunuliwa zaidi ya mahitaji halisi ...................... 108
Jedwali Na.10-1: Vitabu vya kiada vilivyotolewa pungufu .............................. 111
Jedwali Na. 10- 2: Uhaba wa miundombinu ya shule .................................... 113
Jedwali Na. 10-3: Idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo ........................... 115
Jedwali Na. 10-4: Kiwango cha chini cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi ............ 116
Jedwali Na. 11-1: Miradi ya majengo yaliyochelewa kukamilika ....................... 120
Jedwali Na. 11-2: Halmashauri zenye miradi iliyochelewa kuanza ujenzi wa vituo vya afya ............ 122
Jedwali Na. 11-3: Vituo vya afya viliyokamilika lakini havitumiki ..................... 123
Jedwali Na. 11-4: Mwenendo wa halmashauri zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi ............ 124
Jedwali Na. 11-5: Madai ambayo hayakulipwa na mfuko wa afya ya jamii ........... 126
Jedwali Na. 11-6: Halmashauri zenye mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa zisizokuwa na ufanisi ............ 127
Jedwali Na. 11-7: Dawa na Vifaatiba ambavyo Havikupokelewa ....................... 128
Jedwali Na. 12- 1: Mikopo isiyorejeshwa ................................................ 132
Jedwali Na. 12-2: Halmashauri ambazo hazikuhamishia fedha katika akaunti maalumu za mikopo ............ 133
Jedwali Na. 12-3: Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara ............ 133
Jedwali Na.12-4: Halmashauri zilizotoa mikopo bila kuzingatia uwiano wa utoaji wa mikopo ............ 134
Jedwali Na.12-5: Kiasi kisichochangwa kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ............ 135
Jedwali 13-1: Masoko na vituo vya mabasi yaliyo wazi ................................. 138
Jedwali Na.13-2: Orodha vibanda visivyo na wapangaji ................................ 139
Jedwali Na.14-1: Mwenendo wa bei ya soko kwa kila Hisa ............................ 149
Jedwali Na.14-2 Fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege ................................ 159
Jedwali Na 15 -3: Marekebisho ya miamala katika Mfumo wa Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuidhinishwa ............ 170
Jedwali Na 15 -4: Hati ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi ......................... 171
Jedwali Na 15 -5: Madeni hewa katika taarifa za fedha ................................. 171

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 2-1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ..................................5
Kielelezo Na. 5 -1: Mapato ya ndani ........................................................ 38
Kielelezo Na. 5-2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowasilishwa benki.................. 41
Kielelezo Na. 5-3: Mwenendo wa madai .................................................... 45
Kielelezo Na. 10-1: Mwenendo wa kukatisha masomo kwa wanafunzi wa shule za msingi ...................................................................................116
Kielelezo Na. 10- 2: Mwenendo wa Uandikishaji wa Wanafunzi wa Shule za Msingi kwa Miaka Mitatu...........................................................................117

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na.1-1: Hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu .......................... 207
iambatisho Na.2 - 1: Mapendekezo ya ukaguzi yasiyotekelezwa ....................... 214
Kiambatisho Na.2-2: Halmashauri zenye mapendekezo yasiyotekelezwa kwa muda mrefu ........................................................................... 216
Kiambatisho Na.2-3: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya kamati ya LAAC............. 217
Kiambatisho Na. 3-1: Mapungufu katika vitengo vya ukaguzi wa ndani ............... 221
Kiambatisho Na. 3-2: Mapungufu katika utendaji wa kamati za ukaguzi.............. 224
Kiambatisho Na. 3-3: Mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu... 226
Kiambatisho Na. 3-4: Mapungufu katika udhibiti wa ndani wa TEHAMA .............. 228
Kiambatisho Na. 3-5: Mapungufu katika udhibiti wa mashine za POS ................. 230
Kiambatisho Na. 4-1: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani................. 232
Kiambatisho Na. 4-2: Halmashauri zenye ukusanyaji wa mapato ya ndani zaidi ya bajeti ........................................................................... 239
Kiambatisho Na. 4 -3: Halmashauri zenye ukusanyaji wa mapato ya ndani chini ya bajeti ........................................................................... 242
Kiambatisho Na. 4 – 4: Mapato ya ndani dhidi ya Matumizi ya kawaida............... 246
Kiambatisho Na. 4-5: Fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa zaidi ya bajeti ........................................................................... 249
Kiambatisho Na. 4-6: Halmashauri zilizopokea ruzuku ya kawaida ya Serikali pungufu ya bajeti ........................................................................... 251
Kiambatisho Na.4-7: Halmashauri zilizopokea ruzuku ya miradi ya maendeleo ya Serikali zaidi ya bajeti ........................................................................... 256
Kiambatisho Na. 4-8: Halmashauri zilizopokea ruzuku ya miradi ya maendeleo pungufu ya bajeti ........................................................................... 257
Kiambatisho Na. 4-9: Fedha ya mapato ya ndani isiyopelekwa katika miradi ya maendeleo ........................................................................... 263
Kiambatisho Na.5-1: Makusanyo yasiyopelekwa benki.................................. 265
Kiambatisho Na.5-2: Vyanzo vya mapato visivyokusanywa ............................. 267
Kiambatisho Na.5-3: Madai ya muda mrefu ya mamlaka za serikali za mitaa........ 272
Kiambatisho Na.6-1: Matumizi yasiyo na manufaa ...................................... 275
Kiambatisho Na.6-2: Malipo ya bidhaa na huduma zisizopokelewa .................... 276
Kiambatisho Na.6-3: Malipo yaliyofanywa bila kudai risiti za kielektroniki........... 278
Kiambatisho Na.6-4: Matumizi katika akaunti ya amana yasiyosimamiwa ipasavyo . 279
Kiambatisho Na.6-5: Halmashauri zenye ukosefu wa hati za malipo pamoja na viambatisho........................................................................... 280
Kiambatisho Na.6-6: Mchanganuo wa madeni yasiyolipwa ............................. 281
Kiambatisho Na.7-1: Halmashauri zenye malipo kwa watumishi wasiokuwepo kazini ........................................................................... 285
Kiambatisho Na.7-2: Makato ya watumishi yasiyopelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii ........................................................................... 287
Kiambatisho Na.7-3: Malimbikizo ya mishahara yasiyolipwa kwa muda mrefu....... 289
Kiambatisho Na.8-1: Taarifa kuhusu miradi isiyokamilika.............................. 294
Kiambatisho Na.8-2: Taarifa kuhusu miradi iliyotelekezwa kwa muda mrefu........ 305
Kiambatisho Na.8-3: Miradi ya ujenzi iliyokamilika lakini haitumiki .................. 308
Kiambatisho Na.8-4: Fedha iliyochukuliwa na Hazina .................................. 311
Kiambatisho Na.9-1: Miradi Iliyotekelezwa kwa njia ya Nguvukazi kwenye Halmashauri ........................................................................... 314
Kiambatisho Na.10-1: Ruzuku ya elimu bila malipo kutolewa pungufu ............... 317
Kiambatisho Na.10-2: Upungufu wa walimu wa shule za msingi na sekondari ....... 321
Kiambatisho Na.11-1: Halmashauri zenye ujenzi wa vituo vya afya usiokamilika ... 323

Kiambatisho Na.11-2: Halmashauri zisizoteketeza dawa zilizoisha muda wa matumizi ........ 324
Kiambatisho Na.11-3: Madai yaliyokataliwa na mfuko wa bima ya afya ........ 325
Kiambatisho Na.12-1: Orodha ya Halmashauri zenye mikopo isiyorejeshwa ........ 327
Kiambatisho Na.12-2: Mapato ya ndani yasiyopelekwa katika mfuko wa wanawake na vijana ........ 329
Kiambatisho Na.14-1: Uwekezaji katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ........ 331

## VIFUPISHO NA MANENO

| | |
|---|---|
| AGPAHI | Mradi wa Ariel Glaser wa Kutokomeza UKIMWI kwa Watoto na Familia |
| CDCF | Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo |
| CHF | Mfuko wa Afya ya Jamii |
| CSR | Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii |
| EGPAF | Mfuko wa Elizabeth Glaser wa Kusaidia Afya ya Mtoto |
| EIA | Tathmini ya Athari kwa Mazingira |
| EMA | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira |
| EQUIP-T | Mpango wa Kuboresha Ubora wa Elimu |
| ESDP | Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu |
| FFARS | Mfumo wa Taarifa za Kifedha Unaotumiwa katika Ngazi za Chini za Serikali |
| GACS | Mfumo wa Kuuunganisha Hesabu za Serikali |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mikataba |
| GoT-HoMIS | Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania |
| GPE II | Mradi wa Ushirika wa Kilimwengu kwa ajili ya Elimu - II |
| H/Jiji | Halmashauri ya Jiji |
| H/M | Halmashauri ya Manispaa |
| H/Mji | Halmashauri ya Mji |
| H/W | Halmashauri ya Wilaya |
| HCMIS | Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara |
| HSCDG | Ruzuku ya Maendeleo ya Sekta ya Afya |
| iCHF | Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa |
| IFMS | Mifumo Shirikishi ya Taarifa za Usimamizi wa Fedha |
| IFRS | Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Taasisi za Kibiashara |
| IMEI | Namba ya Utambulisho wa Kifaa |
| IPSAS | Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha kwa Taasisi za Umma |
| ISSAI | Viwango vya Kimataifa kwa Taasisi Kuu za Ukaguzi |
| LGA | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| LGDG | Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa |
| LGFM | Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 |
| LGRCIS | Mfumo wa taarifa wa ukusanyaji mapato katika Mamlaka za serikali za Mitaa |
| LPO | Hati ya Kuagiza Vifaa |
| MDH | Menejimenti na Maendeleo ya Afya |
| MSD | Bohari Kuu ya Dawa |
| MUSE | Mfumo wa Ulipaji Serikalini |

| | |
|---|---|
| Na. | Namba |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NPL | Mikopo Isiyofanya Vizuri |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaaa |
| RBF | Mradi wa Ufadhili kwa Matokeo |
| Sh. | Shilingi |
| SWASH | Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni |
| TAKUKURU | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa |
| TAMISEMI | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| TANePS | Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi Tanzania |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TEA | Mamlaka ya Elimu Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TSCP | Mradi wa Majiji ya Kimkakati Tanzania |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UNDP | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |

## TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI



Ninayo furaha kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya ukaguzi wa mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Kwa heshima kubwa, ninachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jitihada zake binafsi za kuiwezesha na kuhakikisha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatekeleza majukumu yake ya kikatiba.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaoendelea kuipatia ofisi yangu.

Mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa kiasi kikubwa, uligubikwa na athari kubwa za janga la UVIKO -19, lakini imenitia moyo kwa namna ambavyo Serikali imekuwa ikikabiliana na janga hili. Serikali imehakikisha rasilimali zote muhimu zinaelekezwa katika kuokoa maisha ya watu na wakati huohuo kuimarisha uchumi na kuhakikisha huduma endelevu kwa jamii.

Mwisho, nitambue mchango wa watumishi wenzangu ambao wamekuwa wakifanya kazi bila kuchoka wakisukumwa na wito wa kitaaluma kukamilisha majukumu waliyopangiwa kwa kuzingatia ubora wa hali ya juu sambamba na viwango vya kitaaluma. Kutokana na nia yao thabiti pamoja na kujitoa ndio kumeniwezesha kuwasilisha ripoti hii ndani ya muda uliowekwa kisheria.



Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Machi, 2022**

## DIBAJI

Ripoti hii ya mwaka ni nyenzo ya uwazi inayoliwezesha Bunge na wananchi kuisimamia serikali, na imejikita katika uongozi bora, uwajibikaji na usimamizi wa mapato, matumizi, mali, ufanisi wa kiutendaji na uzingatiaji wa sheria, maagizo na maelekezo, ikiwa ni pamoja na ukaguzi maalumu.

Ripoti hii inatoa kwa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ambayo chimbuko lake ni ukaguzi wa taarifa za fedha na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, na Miongozo mbalimbali uliofanyika katika mamlaka 185 za serikali za mitaa katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara kwa mwaka 2020/21. Ripoti hii inagusa masuala yote muhimu ya ukaguzi yaliyobainika katika ukaguzi wa taarifa za fedha na ufanisi wa kiutendaji ndani ya mamlaka za serikali za mitaa katika utekelezaji wa majukumu yao ya msingi.

Mathalani, ripoti hii imegusia mapitio ya mifumo ya udhibiti wa ndani, mapitio ya bajeti na mapato hasa katika changamoto zinazozikabili mamlaka za serikali za mitaa katika kukusanya mapato na changamoto za mifumo ya mapato. Miongoni mwa maeneo mengine, taarifa hii pia imebainisha madhaifu katika usimamizi wa matumizi, rasilimali watu, manunuzi, ikiwa ni sambamba na yaliyojitokeza katika utekelezaji wa miradi kupitia 'Force Account'.

Katika mwaka huu wa fedha, nimetathmini ufanisi katika sekta ya elimu na afya, ufanisi katika uwekezaji unaofanywa na mamlaka za serikali za mitaa na uendeshaji wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu.

Niliagiza kaguzi maalumu 37 zenye hadidu maalum za rejea ambapo muhtasari wa matokeo ya kaguzi hizo yamejumuishwa katika ripoti hii.

Jukumu la ofisi yangu ni kusisitiza dhana ya umuhimu wa uwajibikaji, uwazi na uadilifu ndani ya sekta ya umma ikiwa ni pamoja na mamlaka za serikali za mitaa kama msingi imara katika kusimamia rasilimali za umma ili kufikia malengo yetu ya maendeleo kwa jamii yenye ustawi. Ni matarajio yangu kuwa

kupitia taarifa hii, ufanisi wa matumizi ya rasilimali katika Mamlaka za serikali za Mitaa utaongezeka.

## MUHTASARI

Ripoti hii inatoa uchambuzi wa kina wa matokeo, mapendekezo na hitimisho yanayotokana na ukaguzi wa taarifa za fedha na kujiridhisha na uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi katika mamlaka 185 za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii:

### (i) Hati za Ukaguzi

Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, nimekagua na kutoa hati kwa mamlaka 185 za serikali za mitaa. Kati ya hizo; Mamlaka 178 zilipata hati inayoridhisha, Halmashauri sita zilipata hati zenye shaka na Halmashauri moja ilipata hati mbaya.

Ingawa mamlaka nyingi za serikali za mitaa zimepata hati zinazoridhisha, bado kuna mapungufu mengi yaliyobainika yanayotokana na Mamlaka hizo kushindwa kufuata maagizo ya Bunge, Sheria, Kanuni, Sera za Serikali, na Miongozo mbalimbali. Hata hivyo, mapungufu haya hayakuwa na athari za moja kwa moja katika taarifa za hesabu za mwisho zilizowasilishwa.

### (ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Miaka ya Nyuma

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika Halmashauri 185 si ya kuridhisha kwani mapendekezo 1,864 (asilimia 17) kati ya 10,824 yaliyotolewa hayajatekelezwa, mapendekezo 3,637 (asilimia 34) yapo katika utekelezaji na mapendekezo 1,395 (asilimia 13) yamejirudia katika ripoti ya mwaka huu.

Aidha, tathmini yangu ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa ilibaini kuwa maagizo 123 yaliyotolewa na Kamati katika Halmashauri 99 yalikuwa katika utekelezaji na maagizo 264 hayajatekelezwa.

**(iii) Tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi, Mfumo wa Udhibiti wa Ndani na Mifumo ya Utawala Bora**

Tathmini yangu ya mifumo ya utawala bora katika Mamlaka za serikali za mitaa nilibaini mgongano wa majukumu ya madiwani ya usimamizi na majukumu ya kiutendaji. Kwa mfano, Mwenyekiti/Mstahiki Meya wa mamlaka za serikali za mitaa husaini mikataba, taarifa za fedha na hati za makabidhiano ya ofisi ya Mkurugenzi.

Aidha, Mabaraza ya Madiwani yamepewa mamlaka ya kufanya maamuzi yote katika Halmashauri ambayo katika baadhi ya maeneo yameleta athari mbaya ikiwa ni pamoja na kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na kukinzana kwa maamuzi ya madiwani. Baadhi ya miradi iliyoathiriwa na maamuzi yanayokinzana baina ya madiwani ni pamoja na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambazo zilipokea jumla ya shilingi bilioni 2.75 kutoka Hazina.

Vile vile, tathmini yangu ya udhibiti wa marekebisho ya miamala ilibainisha kuwa, Halmashauri zilifanya marekebisho mbalimbali ya miamala bila ushahidi wa idhini na nyaraka za kuthibitisha uhalisia wake.

Hayo yamebainishwa katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na iliyokuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ambazo zilifanya marekebisho ya miamala ya jumla ya shilingi bilioni 8.66 kama masahihisho ya makosa na Halmashauri 27 ambazo zilirekebisha bili za mapato zenye thamani ya shilling bilioni 1.66 bila nyaraka za kuthibitisha uhalali wa marekebisho hayo.

**(iv) Utayarishaji na Utekelezaji wa Bajeti**

Nilibaini kuongezeka kwa ruzuku ya maendeleo katika mamlaka 19 za serikali za mitaa kwa shilingi bilioni 47.19 (asilimia 52) na ruzuku ya kawaida katika Halmashauri 39 kwa shilingi bilioni 74.38 (asilimia 8). Aidha, ruzuku ya maendeleo katika Halmashauri 163 kutolewa chini ya bajeti kwa shilingi bilioni

312.53 (asilimia 38) na ruzuku ya kawaida kutotolewa katika Halmashauri 144 kwa shilingi bilioni 647.89 (asilimia 16).

Aidha, mamlaka 92 za serikali za mitaa zilichangia pungufu kiasi cha shilling bilioni 24.24 katika shughuli za maendeleo kulingana na asilimia ya michango inayotakiwa.

**(v) Usimamizi wa Mapato**

Aidha, tathmini yangu ya taarifa za mfumo wa LGRCIS kuhusiana na mapato kutoka vyanzo vingine yaliyokusanywa kupitia mashine za POS inaonesha kuwa jumla ya shilingi bilioni 20.3 hazikupokelewa katika akaunti za benki za Halmashauri husika. Vile vile, nilipitia makusanyo ya mapato na kubaini kuwa, jumla ya shilingi bilioni 33.91 hazikukusanywa mathalani tozo za kupangisha maduka na nyumba zilizopo katika stendi za mabasi za Halmashauri na masoko, vibanda vya soko, mauzo ya viwanja, mazao ya kilimo, leseni za vileo, ushuru wa uchimbaji wa madini ya ujenzi, leseni za biashara na ushuru wa huduma.

Pia, Halmashauri 43 zilikusanya ushuru wa huduma kiasi cha shilingi bilioni 9.01 bila takwimu za mauzo za makampuni, na kutoza viwango vinavyoanzia asilimia sufuri hadi asilimia 0.3 bila takwimu kunaweza kutoa mwanya kwa makampuni kukwepa kulipa tozo hiyo.

Aidha, mapato kwa miaka mitatu mfululizo yameongezeka kidogo hadi kufikia shilingi bilioni 176.28 kutoka shilingi bilioni 103.30 kwa mamlaka 158 za serikali za mitaa zilizoripotiwa mwaka wa fedha 2019/20 na shilingi bilioni 131.85 katika mamlaka 170 za serikali za mitaa zilizoripotiwa mwaka wa fedha 2018/19.

**(vi) Usimamizi wa Matumizi**

Nilibaini kuwa mamlaka 24 za serikali za mitaazilitumia shilingi milioni 664 katika matumizi yasiyo na manufaa. Pia, mamlaka 61 za serikali za mitaa ziliagiza na kulipa shilingi bilioni 8.44 kwa ajili ya bidhaa/huduma ambazo hazikupokelewa toka kwa wazabuni kwa muda wa hadi kufikia miezi 24; na mamlaka 64

za serikali za Mitaa hazikuwa na hati za malipo na viambatisho vya matumizi ya thamani ya shilingi bilioni 3.87.

Aidha, Halmashauri tano zililipa shilingi milioni 376.48 kwa wafanyabiashara mbalimbali ambapo walipatiwa risiti za EFD za kughushi ikimaanisha kuwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya shilingi milioni 57.43 haikuwasilishwa TRA; Halmashauri 71 ziliwalipa shilingi bilioni 6.07 wafanyabiashara bila kudai risiti za EFD, wakati Halmashauri 24 hazikukata kodi ya zuio kiasi cha shilingi milioni 338.06 kutoka katika malipo ya wafanyabiashara.

Aidha, nilibaini kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Longido ilitumia kiasi cha shilingi milioni 341.82 zilizotengwa kwa ajili ya fidia ya ardhi ili kupisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa KV 400, katika shughuli za uchaguzi mkuu, wakati huo Halmashauri 30 zililipa shilingi bilioni 2.92 kutekeleza shughuli zilizo nje ya bajeti.

**(vii) Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara**

Ukaguzi wangu wa mishahara ya watumishi katika Halmashauri 25 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021, ulibaini kuwa shilingi milioni 556.84 zililipwa kwa wastaafu, waliofariki, watoro, walioachishwa kazi na watumishi waliopewa likizo bila malipo. Aidha, makato ya kisheria yenye thamani ya shilingi milioni 845.24 hayakupelekwa katika taasisi husika. Aidha, nilibaini deni la shilingi bilioni 180.70 linalohusiana na adhabu zilizotolewa kwa Halmashauri tano kwa kushindwa kuwasilisha makato ya kisheria.

**(viii) Tathmini ya Miradi ya Maendeleo**

Tathmini yangu ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ilibaini ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mamlaka 128 za serikali za mitaa yenye thamani ya shilingi bilioni 195.65, ambayo inaweza kusababisha kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na athari za mfumuko wa bei katika gharama za vifaa. Aidha, katika mamlaka 30 za serikali

za mitaa, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 7.68 ilikuwa imekamilika lakini haitumiki.

Aidha, nilibaini kiasi cha shilingi bilioni 14.76 katika Halmashauri 80 ambazo zilirejeshwa Hazina baada ya mwisho wa mwaka kutokana na kushindwa kuzitumia kwa wakati. Hata hivyo, fedha hizo hazikurejeshwa kwa Halmashauri husika kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo zilizopangwa.

**(ix) Usimamizi wa Manunuzi na Mikataba**

Nilitathmini jinsi manunuzi na usimamizi wa vifaa vya ujenzi ulivyofanywa na mamlaka za serikali za mitaa, uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa katika kusimamia miradi inayotekelezwa kwa njia ya 'force account' na ubora wa miundombinu ambapo nilibaini malipo ya shilingi milioni 947.92 yalilipwa kwa mafundi bila ya kuwa na mikataba ya kisheria na utekelezaji wa miradi ya ujenzi yenye thamani ya shilingi bilioni 4.78 katika mamlaka 17 za serikali za mitaa bila kuandaa vipimo vya kazi zilizotekelezwa. Pia nilibaini kuwa Halmashauri hazina watumishi wa kutosha katika ngazi za chini, kimsingi zinategemea walimu na watumishi wa Idara ya Afya.

Aidha, kuwatumia walimu na wahudumu wa afya kama wajumbe wa kamati kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi kwa njia ya 'Force Account' kumeathiri utendaji wao katika majukumu yao ya msingi amabayo ni kufundisha na kutoa huduma za matibabu.

**(x) Ufanisi wa Uendeshaji katika Sekta ya Elimu**

Ukaguzi wangu wa mahitaji ya vitabu vya kiada katika Mamlaka za Selikali za Mitaa 22 ulibaini kuwa, vitabu 6,323,566 vilitakiwa kukidhi mahitaji ya wanafunzi katika shule za msingi za Serikali. Hata hivyo, ni vitabu 1,467,829 (asilimia 23) pekee vilivyosambazwa katika mwaka huo, ikionesha uwasilishaji mdogo wa vitabu 4,855,737 vinavyogharimu shilingi bilioni 19.42. Aidha, mapitio yangu ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya elimu bila malipo katika Mamlaka za Selikali za Mitaa 111 ilibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kulikuwa na

ruzuku pungufu kwa shule za msingi na sekondari kiasi cha shilingi bilioni 5.18.

Aidha, tathmini yangu ya uwiano wa walimu kwa wanafunzi ilibaini kuwa katika Mamlaka za Selikali za Mitaa 103 zenye mahitaji ya walimu 120,534 wa shule za msingi zilikuwa na walimu 100,043 ikimaanisha upungufu wa walimu 20,491 sawa na asilimia 17. Pia, nilifanya sampuli za Mamlaka za Selikali za Mitaa 27 na kubaini kuwa kati ya mwaka 2018 na 2021, wanafunzi 53,755 walioandikishwa darasa la kwanza hawakumaliza elimu yao ya msingi.

**(xi) Ufanisi wa Uendeshaji Katika Sekta ya Afya**

Nilibaini miradi iliyokamilika ya vituo vya afya yenye thamani ya shilingi bilioni 3.98 katika mamlaka 20 za serikali za mitaa lakini ilikuwa haitumiki. Aidha, nilibaini mamlaka 46 za serikali za mitaa zenye dawa zilizoisha muda wake wa matumizi kwa muda wa kuanzia miezi mitatu hadi miaka 20 zenye gharama ya shilingi bilioni 3.49 ambazo hazikuteketezwa. Pia, tathmini yangu ilibaini madai ya jumla ya shilingi bilioni 2.34 kwa mamlaka 111 za serikali za mitaa yalikataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kutokana na kutofuata mwongozo wa NHIF.

**(xii) Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu**

Tathmini yangu ya ufanisi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu imebaini kuwa vikundi katika Halmashauri 155 havijarejesha mikopo ya shilingi bilioni 47.01 iliyotolewa kwa vikundi hivyo. Pia, ufuatiliaji wangu wa uzingatiaji wa matakwa ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5.04.2019) ulibaini kuwa, mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia jumla ya shilingi bilioni 6.86 kutoka katika vyanzo vyao vya mapato.

**(xiii) Ufanisi wa kiutendaji katika Usimamizi wa Masoko na Stendi za Mabasi**

Nilitembelea soko la mchele na ghala lililokamilika tangu tarehe 7 Mei, 2017 katika kijiji cha Mahiga katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba. Mradi huu ulifadhiliwa na MIVARF kwa gharama ya shilingi milioni 617.42. Pamoja na kiasi kikubwa kilichowekezwa, niligundua kuwa miundombinu ya soko likiwemo ghala, ilitelekezwa kwa muda mrefu kutokana na ukosefu wa umeme wa kuendesha mashine ya kukoboa mpunga.

Aidha, soko lililopo Tarime ambalo lilikuwa na wastani wa makusanyo ya shilingi milioni 300 kwa mwaka (sawa na shilingi milioni 900 kwa miaka 3), lilibomolewa miaka mitatu nyuma ikiwa ni maandalizi ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kisasa la Tarime kwa mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 8.07. Hata hivyo, Serikali ilisitisha miradi yote ya kimkakati ya masoko katika Halmashauri zilizochaguliwa ambayo ilikuwa haijaanza ukiwemo mradi wa Soko la Tarime, na kusababisha hasara ya shilingi milioni 900 kwa mapato ambayo hayakukusanywa kwa miaka mitatu.

**(xiv) Mapitio ya Ufanisi katika Uwekezaji**

Tathmini yangu ilibaini kuwa mamlaka tano za serikali za mitaa ambazo zimewekeza hisa 24,036,348 zenye thamani ya shilingi bilioni 5.77 katika benki moja ya biashara yenye utendaji usioridhisha kwani kufikia tarehe 30 Juni 2021 hisa 24,036,348 zilishuka thamani kwa shilingi bilioni 1.20. Pia, mamlaka 85 za serikali za mitaa ziliwekeza shilingi bilioni 4.88 katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa bila manufaa yoyote.

Vile vile, Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata mkopo kutoka benki moja ya biashara kwa ajili ya ujenzi wa soko la Mwanjelwa ambao unatakiwa kurejeshwa kufikia mwaka 2033 huku shilingi bilioni 35.44 zikiwa bado hazijalipwa hadi Desemba, 2021. Tathmini yangu imebaini kuwa, ili Halmashauri ya Jiji la Mbeya iweze kukidhi masharti ya urejeshaji wa mkopo ifikapo mwaka 2033, ni lazima irejeshe shilingi bilioni 2.95 kwa mwaka. Hata hivyo, niliarifiwa na uongozi wa Halmashauri

kuwa makusanyo ya mapato kutoka sokoni ni kati ya milioni 750 hadi milioni 850 kwa mwaka ambayo hayawezi kurejesha malipo ya mkopo huo kwa mwaka.

Uwekezaji katika miradi isiyotekelezeka husababisha upotevu wa fedha za Umma ambazo zingeweza kutumika kufanya shughuli zingine za maendeleo kwa ajili ya kutoa huduma kwa maslahi ya jamii.

**(xv) Matokeo ya Ukaguzi Maalumu**

Nilifanya kaguzi maalumu 37 katika Halmashauri 36 na kubaini jumla ya shilingi bilioni 19.72 zilikusanywa kutoka vyanzo mbalimbali lakini hazikupelekwa benki; kati ya hizo, kiasi cha shilingi bilioni 10.13 (asilimia 51) zinahusiana na iliyokuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Kati ya shilingi bilioni 10.13, shilingi bilioni 4.64 hakikupelekwa benki na mawakala 20 wakati kiasi cha shilingi bilioni 5.49 hakikupelekwa benki na watumishi 19 waliokuwa wakikusanya mapato.

Aidha, nilibaini kuwa Halmashauri 16 zilifanya marekebisho ya miamala katika mfumo wa mapato wa LGRCIS kwa kufuta mapato yenye jumla ya shilingi bilioni 28.33 bila kuzingatia taratibu zilizowekwa hivyo kusababisha uwezekano wa uwapo wa ubadhirifu. Pia, Halmashauri 7 hazikuwasilisha kwangu hati za malipo zenye thamani ya shilingi bilioni 1.37, hivyo nilishindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, nilibaini wakazi 94 ambao hawakuweza kutambuliwa na viongozi wa ngazi za chini kulipwa jumla ya shilingi bilioni 2.16 kama fidia ili kupisha ujenzi wa miradi ya DMDP, hali inayoashiria kuwa malipo hayo ya fidia yanaweza kuwa na udanganyifu.

# SURA YA 1

# HATI ZA UKAGUZI

## 1.0 Utangulizi

Hati ya ukaguzi inatolewa kwa kuzingatia tathmini ya mahitimisho yanayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliofanyika, na kuangalia kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha (kama vile IFRS au IPSAS). Hati ya ukaguzi inatolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) 1200.

Hili linafanikiwa kwa kuandaa ukaguzi kwa njia ambayo itamwezesha mkaguzi kupata uthibitisho kulingana na tathmini ya matokeo dhidi ya kiwango kilichowekwa.

## 1.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne tofauti za hati za ukaguzi, ambazo ni hati inayoridhisha, hati yenye shaka, hati mbaya, na kushindwa kutoa hati kama zinavyofafanuliwa hapa chini.

(i) **Hati Inayoridhisha -** Aina hii ya hati hutolewa baada ya kuwa nimejiridhisha kwamba, kutokana na ushahidi uliokusanywa wakati wa ukaguzi, halmashauri zilizokaguliwa zimeandaa taarifa zao za fedha kwa usahihi kwa kuzingatia vigezo vyote vinavyotumika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

(ii) **Hati yenye Shaka** – Inatolewa wakati taarifa za fedha zilizokaguliwa zinapokuwa zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa kwa athari ya jambo/mambo yafuatayo:

- Kulingana na ushahidi nilioupata, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa, ama kwa kutozingatia ipasavyo viwango vya kimataifa vya uhasibu pamoja na sera za uhasibu au kulikuwa na kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi kutokana na kutopatikana kwa nyaraka zote zilizohitajika ili kufanikisha malengo ya ukaguzi lakini makosa hayo hayakuwa na madhara

makubwa kiasi cha taarifa hizo kwa ujumla wake kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi.

- Kushindwa kupata ushahidi wa kutosha wa kuweza kunisaidia kutoa maoni, lakini athari ya makosa ambayo sikuweza kuyaona (kama yapo) hayakuwa na madhara makubwa kiasi cha taarifa hizo kwa ujumla wake kushindwa kutumika katika kufanya maamuzi.

(iii) **Hati Mbaya -** Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha, hivyo kusababisha taarifa hizo kutokuwa sahihi.

**(iv)** **Kushindwa Kutoa Maoni** – Hali hii inatokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana. Hivyo, ninaonesha katika ripoti yangu ya ukaguzi kuwa kutokana na ukubwa wa madhara yaliyopo au yanayoweza kutokea kwa kukosa ushahidi wa kutosha, nimeshindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Mkaguzi atashindwa kutoa maoni, katika hali nadra sana inayohusisha kutokuwa na uhakika wa kutosha, atahitimisha kwamba, ingawa amepata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu kila hali, haiwezekani kutoa maoni juu ya taarifa za fedha kwa sababu ya kutokuwa na uhakika na uwezekano wa athari zake katika taarifa za fedha.

## 1.2 Aya ya Masuala ya Msisitizo katika Ripoti ya Ukaguzi

Nikiona ni muhimu kutoa angalizo kwa watumiaji kuhusu suala lililowasilishwa au kuelezwa katika taarifa za fedha ambalo, kwa maoni yangu, ni la muhimu na la msingi sana kwa uelewa wa watumiaji wa taarifa za fedha, nitajumuisha aya ya masuala ya msisitizo katika taarifa yangu ya ukaguzi ilimradi nimepata ushahidi wa kutosha kwamba suala hilo halijaripotiwa kimakosa katika taarifa

za fedha. Aya hiyo inarejea masuala yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha.

## 1.3 Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Masuala muhimu ya ukaguzi hutoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia katika kuelewa masuala ambayo, kwa maoni yangu, yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi fulani. Kueleza mambo muhimu ya ukaguzi huongeza thamani ya mawasiliano ya taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa kutoa uwazi zaidi kuhusu ukaguzi nilioufanya.

## 1.4 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka Unaohusika

Katika mwaka wa fedha 2020/21, hati 185 zilitolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa, Kati ya hizo, hati zinazoridhisha ni 177, hati zenye shaka ni saba (7), hati mbaya ni moja (1) na hakuna niliposhindwa kutoa maoni. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa na aina za hati zililizotolewa inaoneshwa katika **Kiambatisho Na.1-1.**

## 1.5 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

Mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2016/17 hadi 20120/21 ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.1-1.**

**Jedwali Na. 1-1: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

| Aina ya Hati | Ripoti Kuu ya Mwaka | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2016/17 | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Hati Inayoridhisha | 166 | 176 | 176 | 124 | 178 |
| Hati Yenye Shaka | 16 | 7 | 9 | 53 | 6 |
| Hati Mbaya | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| Kushindwa Kutoa Maoni | 3 | 1 | 0 | 8 | 0 |
| **Jumla** | **185** | **185** | **185** | **185** | **185** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa Taarifa za Fedha Zilizokaguliwa*

# SURA YA 2

# HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI YA MIAKA ILIYOPITA

## 2.0 Utangulizi

Nimefanya tathmini ya mapendekezo ya ukaguzi ya miaka iliyopita ili kubaini iwapo Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Maofisa Masuuli wamechukua hatua stahiki za utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Ili kuhakikisha kunakuwapo na mfumo wa udhibiti wa ndani ulio thabiti, Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kutathmini na kuchukua hatua zinazofaa kushughulikia matokeo ya ukaguzi na mapendekezo kwa wakati muafaka.

Aidha, kama sehemu ya majukumu yake ya usimamizi, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa inafanya vikao na ufuatiliaji kila mara ili kubaini pamoja na mambo mengine, endapo Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Maofisa Masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa wanachukua hatua stahiki za kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati.

Hata hivyo, wakati wa kuwasilisha majibu ya Serikali kuhusu ripoti kuu ya jumla ya mwaka ya mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20, Mlipaji Mkuu wa Serikali hakutoa taarifa ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kuhusiana na mamlaka za serikali za mitaa.

Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yanafafanuliwa katika aya zinazofuata.

## 2.1 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Kila Halmashauri kwa Mwaka 2019/20

Kwa mujibu wa Kanuni ya 93 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009, kila Ofisa Masuuli wa taasisi iliyokaguliwa anatakiwa kuandaa majibu ya ripoti yake ya ukaguzi na kuiwasilisha ndani ya kipindi cha siku 21 tangu tarehe ambayo ripoti kuu imewasilishwa Bungeni.

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa mwaka 2019/20 imeonesha kuwa katika Serikali za Mitaa 185, jumla ya mapendekezo ya ukaguzi 10,824 yalitolewa. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi hairidhishi kwani mapendekezo ya ukaguzi 1,864 sawa na asilimia 17 hayajatekelezwa, mapendekezo ya ukaguzi 3,637 sawa na asilimia 34 yapo katika utekelezaji na mapendekezo ya ukaguzi 1,395 sawa na asilimia 13 yamejirudia tena katika Ukaguzi wa mwaka huu. Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Jedwali Na. 2-1**.

**Jedwali Na. 2-1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya nyuma**

| Hali ya mapendekezo | Idadi ya mapendekezo | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Yametekelezwa | 3,511 | 32 |
| Utekelezaji unaendelea | 1,864 | 17 |
| Hayajatekelezwa | 3,637 | 34 |
| Yamejirudia | 1,395 | 13 |
| Yamepitwa na wakati | 417 | 4 |
| **Jumla ya mapendekezo** | **10,824** | **100** |

***Chanzo**: Taarifa za ukaguzi kwa waka 2020/21*

Vile vile nilibaini kuwa mwenendo wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2017/18 mpaka 2019/20 sio wa kuridhisha kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 2-1.**

**Kielelezo Na. 2-1: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo**



**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI iweke mikakati na Maofisa Masuuli wa Halmashauri husika ili kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayajakamilika.**

## 2.2 Mapendekezo Ambayo Hayajatekelezwa Takribani Miaka 10

Uchambuzi wangu wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita umebaini kuwa, idadi kubwa ya mamlaka za serikali za mitaa hazioneshi juhudi za kutosha za kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi. Nilibaini kuwa katika mamlaka 114 za serikali za mitaa zilikuwa na mapendekezo 746 yaliyotolewa kipindi kati ya 2014/15 na 2016/17 ambayo yalikuwa hayajatekelezwa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 2-1**; wakati huo mapendekezo 147 niliyoyatoa kati ya mwaka wa fedha 2010 na 2014 kwa mamlaka 61 za serikali za mitaa yalikuwa hayajatekelezwa kwa takribani miaka 10 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 2-2.** Pia nilibaini kuwa, Halmashauri husika hazija andaa mipango kazi ya kushughulikia mapendekezo ya hoja za nyuma za ukaguzi

Bado mwenendo wa utekelezaji hauridhishi licha ya wito wangu wa mara kwa mara wa kuzitaka mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza mapendekezo ya miaka ya nyuma.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa zifanye juhudi za kutosha ili kuhakikisha mapendekezo ya ukaguzi yote ambayo hayajatekelezwa yanatekelezwa.**

## 2.3 Utekelezaji Usioridhisha wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa

Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 kama ilivyorekebishwa na kifungu cha 40 cha Sheria ya Fedha, 2021 kinamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maofisa Masuuli kuzingatia maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusiana na masuala ya usimamizi wa fedha kwa mujibu wa miongozo iliyowekwa na Bunge.

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21 ilibainisha kuwa, kati ya maagizo 619 yaliyotolewa na Kamati katika mamlaka

99 za serikali za mitaa, maagizo 232 (asilimia 37) yalitekelezwa; maagizo 123 (asilimia 20) utekelezaji unaendelea na maagizo 264 (asilimia 43) yalikuwa hayajatekelezwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 2-2 na** kufafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 2-3.**

**Jedwali Na. 2-2: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC**

| Hali ya Utekelezaji | Idadi ya Maagizo | Asilimia |
|---|---|---|
| Yametekelezwa | 232 | 37 |
| Hayajatekelezwa | 264 | 43 |
| Utekelezaji unaendelea | 123 | 20 |
| **Jumla** | **619** | **100** |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa mwaka 2020/21*

Vile vile, nilibaini kuwa mamlaka tisa za serikali za mitaa zilikuwa na maagizo 31 ambayo hayajatekelezwa kwa kipindi kati ya miaka saba mpaka miaka 10 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2-3.**

**Jedwali Na. 2-3: Halmashauri zenye maagizo ya muda mrefu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miaka | Idadi ya Maagizo |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mufindi | 7 | 6 |
| 2. | H/W Muheza | 10 | 1 |
| 3. | H/W Iringa | 7 | 5 |
| 4. | H/W Bahi | 10 | 3 |
| 5. | H/W Kilolo | 7 | 3 |
| 6. | H/W Sikonge | 8 | 3 |
| 7. | H/M Tabora | 8 | 3 |
| 8. | H/W Korogwe | 8 | 4 |
| 9. | H/W Pangani | 8 | 3 |
| | **Jumla** | | **31** |

*Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mwaka 2020/21*

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe kuwa Maofisa Masuuli wote wa mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika wanatekeleza maagizo yote ambayo hayajatekelezwa na kuwasilisha hatua walizochukua katika Kamati.**

## SURA YA 3

## TATHMINI YA MFUMO YA UDHIBITI WA NDANI, USIMAMIZI WA VIHATARISHI NA MIFUMO YA UTAWALA BORA

### 3.0 Utangulizi

Agizo la 11 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuwa na mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani. Ufanisi katika udhibiti wa ndani unaziongezea mamlaka za serikali za mitaa uhakika wa kufikia malengo yake katika uendeshaji wa shughuli zake, utoaji wa taarifa na uzingatiaji wa sheria na taratibu zilizopo.

Katika kuboresha udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi vya ubadhirifu ni muhimu ili kuziwezesha mamlaka za serikali za mitaa kubaini, kutathmini na kuzuia vihatarishi vinavyoweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Sambamba na hilo, uwapo wa utawala bora ni muhimu kwa ajili ya kutoa taarifa, kuelekeza, kusimamia na kufuatilia shughuli za mamlaka za serikali za mitaa (ikiwa ni pamoja na udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi) ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Katika sura hii nimefanya mapitio ya ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika mamlaka za serikali za mitaa, usimamizi wa vihatarishi pamoja na mifumo ya utawala bora na kubaini maeneo ambayo yanahitaji maboresho.

### 3.1 Madiwani Kushiriki Katika Shughuli za Kiutendaji Sambamba na Usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili ya Wahasibu (IESBA), wasimamizi wa taasisi wana jukumu la kusimamia mwelekeo wa kimkakati na uwajibikaji wa taasisi, ikiwa ni pamoja na kusimamia mchakato wa utoaji wa taarifa za fedha.

Aya ya 21 (a) (ii) ya Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 315) inamtaka mkaguzi kupata uelewa juu ya mazingira ya udhibiti

yanayohusiana na utayarishaji wa taarifa za fedha, kwa kufanya tathmini ya vihatarishi, na kupata uelewa wa mifumo ya udhibiti, michakato na miundo ambayo inashughulikia kutofautisha shughuli za wasimamizi wa taasisi na zile za menejimenti.

Sambamba na Agizo la 5 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, Baraza la Madiwani limekasimiwa jukumu la maamuzi yote katika mamlaka za serikali za mitaa. Kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 (Ilivyorekebishwa 2019) na Kifungu cha 24 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 (Ilivyorekebishwa 2019) halmashauri inaundwa na wajumbe ambao wanachaguliwa kutoka kila Kata za mamlaka za selikali ya mitaa husika, Wabunge wa viti maalumu na wale walioteuliwa na Rais ambao ni wakazi wa Mamlaka husika za Serikali za Mitaa, Madiwani wa viti maalumu na wale waliochaguliwa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa pamoja na Wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa.

Nimebaini kuwa, Madiwani wamekuwa wakishiriki katika shughuli mbalimbali za kiutendaji za mamlaka za serikali za mitaa ambazo kimsingi zilitakiwa zitekelezwe na menejimenti hivyo kuathiri dhana ya utawala bora. Baadhi ya shughuli hizi ni kama ifuatavyo:

(i) Mwenyekiti/Meya wa Halmashauri kusaini mikataba kati ya mamlaka za serikali za mitaa na wazabuni/mawakala wa ukusanyaji wa mapato kama ilivyoelezewa katika Kanuni ya 22 (2) ya Kanuni za Bodi za Zabuni za mamlaka za serikali za mitaa (Uanzishaji na Uendeshaji) za Mwaka 2018;

(ii) Mwenyekiti/Meya wa Halmashauri kusaini taarifa za mwaka za hesabu kama ilivyoanishwa katika Agizo la 31(7) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009;

(iii) Mwenyekiti/Meya wa Halmashauri kusaini hati za makabidhiano ya ofisi baina ya Wakurugenzi kama inavyoelezwa katika Agizo la 84(4) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009;

(iv) Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani kuwa na wajibu wa kujadili majibu ya taarifa za ukaguzi kabla ya kuyawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoelezwa katika Aya ya 6.9.4 (e) ya Mwongozo wa Uhasibu na Usimamizi wa Fedha za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019;

(v) Kamati ya Fedha na Baraza la Madiwani kupewa jukumu la kuidhinisha mali zote ambazo mamlaka za serikali za mitaa zimeamua kuacha kuzitumia kama ilivyoelezwa katika Aya ya 9.8.2 (b) ya Mwongozo wa Uhasibu na Usimamizi wa Fedha za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019;

(vi) Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 (Ilivyorekebishwa 2019), Baraza la Madiwani ndio mamlaka ya nidhamu ya watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa; na

(vii) Agizo la 5 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linalipa Baraza la Madiwani jukumu la maamuzi yote katika mamlaka za serikali za mitaa.

Kwa kutekeleza shughuli tajwa hapo juu, Baraza la Madiwani linajihusisha na shughuli za kiutendaji za mamlaka za serikali za mitaa na hivyo kusababisha uwapo wa uwezekano wa migongano ya kimaslahi katika kufanya maamuzi na uchukuaji wa hatua katika maeneo ambayo Madiwani wamehusika katika utekelezaji wake.

Kwa mfano, mwezi Mei 2021, Serikali iliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Nzega shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala. Baraza la Madiwani kupitia kikao cha mwezi Mei 2020 lilikuwa limekwisha chagua eneo ndani ya Kijiji cha Ndala kwa ajili ya ujenzi huo.

Hata hivyo, Baraza jipya la Madiwani lililoundwa baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kupitia kikao cha mwezi Juni 2021, lilibadili maamuzi hayo na kuchagua eneo jingine ndani ya Kijiji cha Lubisu kwa ajili ya mradi huo. Maamuzi haya yalipelekea kutokuanza kwa ujenzi wa jengo hili hadi wakati nakamilisha ukaguzi wangu.

Nilibaini hali kama hiyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ambayo ilipokea shilingi 749.62 hata hivyo haikuanza kutekeleza ujenzi wa jengo la utawala kwa sababu zinazofanana na hizo, ambapo kulikuwa na mgongano wa mawazo juu ya eneo la ujenzi kuwa kati ya Kijiji cha Tabaruka au Kijiji cha Isung'ang'oro. Vilevile, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo pia ilipokea shilingi bilioni moja haikuwa imeanza ujenzi wa jengo la utawala kwa sababu madiwani walikuwa na mashaka juu ya mfumo wa manunuzi kwa njia ya nguvukazi.

Kwa mtazamo wangu, kushirikisha Baraza la Madiwani katika shughuli za kila siku za utendaji kazi kunaathiri usimamizi wake kwa menejimenti ya halmashauri husika. Majukumu yao yajikite katika uangalizi ikiwa ni pamoja na uwakilishi wa Kata zao katika mikutano ya Baraza, ufuatiliaji wa rasilimali, kuimarisha uzingatiaji wa taratibu zilizopo, kupitisha bajeti za Halmashauri kupitia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali baada ya kusainiwa na kuwasilishwa Bungeni, kutunga sheria ndogo ndogo, kutetea maendeleo ya jamii na utatuzi wa migogoro kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 [Ilivyorekebishwa 2019], Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 [Ilivyorekebishwa 2019], na Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

Hii itaondoa hatari ya maamuzi yanayokinzana ambayo katika baadhi ya matukio husababishwa na ubinafsi, mgongano wa maslahi na hali ya kujitathmini mwenyewe.

Ni maoni yangu kuwa, Bodi za Uongozi zikianzishwa zitaweza kuwa kiungo kati ya shughuli za uangalizi na shughuli za menejimenti katika mamlaka za serikali za mitaa. Bodi hizi zitakuwa na jukumu la pamoja la kusimamia shughuli za Mamlaka ikiwa ni pamoja na zile za kiutendaji kama vile kusaini mikataba, taarifa za fedha, kushughulikia taarifa za awali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya kusainiwa na kufanya maamuzi juu ya miradi ya maendeleo na kuwajibika katika Baraza la Madiwani.

Kazi nyingine ya bodi hizo itakuwa ni kuandaa na kufuatilia dhima ya mamlaka za serikali za mitaa husika pamoja na vipaumbele na mikakati yake; kufanya tathmini ya mara kwa mara ya mazingira ya kiutendaji ya Mamlaka ili kujiridhisha kuwa malengo yaliyopangwa yanaweza kufikiwa; kutathmini rasilimali zilizopo na kuona kama zinatosha ili kupata matokeo kusudiwa; kusimamia programu za Mamlaka na utoaji wa huduma; usimamizi wa vihatarishi; kuwajibika katika Baraza la Madiwani na kudumisha mahusiano mazuri na wadau wakuu kwa kuunda sera zinazokidhi mahitaji yao.

**Naishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Mamlaka zinazohusika kuangalia upya Sheria, Kanuni na Miongozo kuhusu kazi na wajibu wa Madiwani ili kuhakikisha maamuzi ya Baraza la Madiwani yanakuwa ya ufanisi na manufaa kwa jamii linayoiwakilisha.**

**Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha bodi za uongozi zinazojumuisha wataalam kutoka nje ya mamlaka za serikali za mitaa wenye uzoefu na ujuzi wa kutosha katika uendeshaji wa taasisi mbalimbali, ambapo bodi hiyo itasimamia moja kwa moja utendaji wa Menejimenti na kuwajibika kwa Baraza la Madiwani.**

## 3.2 Mapungufu Katika Utendaji wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani

Agizo la 13 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuajiri wakaguzi wa ndani ambao watakuwa na jukumu la kukagua na kutathmini ufanisi na utoshelevu wa mifumo ya udhibiti wa ndani.

Nilipitia muundo, mgawanyo wa rasilimali na kazi zilizofanyika katika vitengo vya ukaguzi wa ndani katika mamlaka za serikali za mitaa na kubaini mapungufu ambayo yamefafanuliwa kwa kina hapa chini na katika **Kiambatisho Na. 3-1**:

(i) Taarifa za wakaguzi wa ndani kwa Mwaka 2020/21 zilijikita zaidi katika maeneo ya matukio na miamala. Ni maoni yangu kuwa, pamoja na kazi nzuri iliyofanyika katika maeneo hayo, wakaguzi wa ndani wanapaswa kuweka msisitizo katika ukaguzi wa maeneo yanayohusiana na usimamizi wa vihatarishi pamoja

na mifumo ya udhibiti wa ndani katika eneo la TEHAMA ili kuongeza thamani katika juhudi za menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kutambua, kutathmini na kuzuia vihatarishi mbalimbali ikiwamo vya ubadhirifu;

(ii) Mamlaka za serikali za mitaa hazikutoa mafunzo kwa wakaguzi wa ndani ili kuwajengea uwezo katika maeneo mbalimbali ya muhimu kama vile Mfumo wa Kuandaa Hesabu jumuifu za Serikali (GACS), Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HoMIS), Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi Tanzania (TANePS) na Mfumo wa Ulipaji Serikalini (MUSE). Hii inawaondolea wakaguzi wa ndani uwezo wa kuhakiki utendaji na kutoa maoni yenye ufanisi katika maeneo tajwa;

(iii) Mamlaka 87 za serikali za mitaa zilikuwa na upungufu wa jumla ya wakaguzi wa ndani 219. Hii inaashiria uwapo wa mzigo mkubwa wa kazi kwa wakaguzi wa ndani waliopo na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yao kwa ukamilifu katika mamlaka za serikali za mitaa;

(iv) Nilitathmini utekelezaji wa bajeti na kubaini kuwa, Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani katika mamlaka 79 za serikali za mitaa havikupatiwa fedha kulingana na bajeti zilizopangwa. Kati ya hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu haikutoa asilimia 100 ya fedha za mapato ya ndani iliyopangwa kwa ajili ya Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

(v) Wakaguzi wa ndani katika mamlaka 49 za serikali za mitaa walikuwa na upungufu wa vitendeakazi kama vile magari, kompyuta mpakato na samani, jambo ambalo liliongeza changamoto katika utendaji na kupunguza ufanisi katika kazi zao; na

(vi) Wakaguzi wa Ndani katika mamlaka 78 za serikali za mitaa hawakukamilisha kazi zilizopangwa katika mpango wa mwaka wa ukaguzi. Hii inaashiria kuwa menejimenti katika mamlaka za serikali za mitaa husika haikupatiwa ushauri kuhusiana na

ufanisi wa udhibiti wa ndani katika maeneo ambayo hayakukaguliwa.

**Natoa wito kwa menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa mipango kazi ya Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani inatoa kipaumbele katika maeneo ya udhibiti wa vihatarishi na TEHAMA, kuvipatia Vitengo vya Ukaguzi rasilimali watu na fedha pamoja na kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani ili kuendana na wakati uliopo, uboreshaji wa utendaji kazi na matokeo ya kazi zao.**

## 3.3 Mapungufu Katika Utendaji wa Kamati za Ukaguzi

Kamati za Ukaguzi ni kamati za usimamizi katika mamlaka za serikali za mitaa zenye jukumu la kutathmini na kushauri katika masuala yanayohusiana na utawala bora, usimamizi wa vihatarishi, uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani. Kwa mujibu wa Agizo la 12 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Aya ya 3.5 ya Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi wa Mwezi Juni 2019, kila mamlaka ya serikali za mitaa inatakiwa kuwa na Kamati za Ukaguzi ambayo itajumuisha wajumbe wasiopungua watatu na wasiozidi watano. Wajumbe wote au wengi wao wanatakiwa watoke nje ya taasisi husika.

Tathmini niliyoifanya juu ya ufanisi wa Kamati za Ukaguzi katika mamlaka za serikali za mitaa ilibainisha mapungufu yafuatayo ambayo kwa kina yameainishwa katika **Kiambatisho Na. 3-2:**

(i) Nilipitia kumbukumbu za vikao vya Kamati za Ukaguzi na kubaini kuwa, katika kujadili taarifa za wakaguzi wa ndani, Kamati za Ukaguzi zimekuwa zikijikita katika kujadili hoja ambazo hazijafungwa pekee. Hakuna msisitizo unaowekwa katika kuangalia hoja ambazo zimejibiwa na kufungwa, ili kufanya tathmini na kubaini chanzo cha hoja hizi kuwapo na kuangalia kama menejimenti imekwisha weka mfumo wa udhibiti wa ndani kuzuia kujirudia kwa mapungufu yaliyobainishwa. Jambo hili linasababisha baadhi ya hoja za

ukaguzi kujirudia katika kila taarifa za robo mwaka za wakaguzi wa ndani;

(ii) Vikao vya Kamati za Ukaguzi vimekuwa vikijadili zaidi taarifa za ukaguzi wa ndani kuliko maeneo mengine kama vile ufanisi katika usimamizi wa vihatarishi, ufuatiliaji wa mazingira ya udhibiti wa ndani na namna mamlaka za serikali za mitaa zinavyozingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Jambo hili linaziondolea kamati nafasi ya kuhusika katika kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani na ufanisi wa utawala bora katika mamlaka za serikali za mitaa;

(iii) Kamati za Ukaguzi katika mamlaka 31 za serikali za mitaa hazikuandaa taarifa ya utendaji ya mwaka na hivyo kutowasilisha taarifa hii kwa Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mkuu wa Mkoa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyoagizwa kupitia Agizo la 12(5)(g) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. Hii ilizinyima fursa mamlaka husika kupata taarifa kuhusu utendaji wa Kamati za Ukaguzi katika mamlaka za serikali za mitaa husika;

(iv) Kamati za ukaguzi katika mamlaka 21 za serikali za mitaa hazikupitia taarifa za fedha na hivyo kutotoa ushauri kwa menejimenti juu ya maboresho katika uandaaji na uhakiki wa taarifa hizo, jambo ambalo ni kinyume na Agizo la 12(5) (f) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009;

(v) Mamlaka saba za serikali za mitaa hazikuwapatia mafunzo ya awali wajumbe wake wapya wa kamati za ukaguzi ili kuwapa uelewa juu ya majukumu yao. Pia, mamlaka 15 za serikali za mitaa hazikuwapatia mafunzo wajumbe wake wa kamati za ukaguzi katika maeneo mbalimbali muhimu kama vile usimamizi wa ununuzi, usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya taarifa kama vile FFARS, GoT-HoMIS, HCMIS, TANePS, MUSE na LGRCIS; na

(vi) Kamati za Ukaguzi katika mamlaka nane za serikali za mitaa hazikujifanyia tathmini ya kazi zake jambo ambalo ni kinyume

na Aya ya 5.1 ya Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi wa Mwezi Juni 2019 inayozitaka Kamati za Ukaguzi kila mwaka kujifanyia tathmini ya utendaji na matokeo yaliyopatikana kwa kulinganisha na Mwongozo wa kamati ya Ukaguzi.

**Napendekeza kuwa Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa ziboreshe utendaji wa Kamati za Ukaguzi kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wajumbe wa kamati hizo na kuzipatia kamati rasilimali za kutosha ili ziweze kutekeleza majukumu yake kama inavyoagizwa katika Agizo la 12 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.**

**Kamati za Ukaguzi zinashauriwa kuboresha wigo wa kazi zao kwa kujadili chanzo cha hoja za ukaguzi (hata zile zilizofungwa na wakaguzi wa ndani) ili kutathmini, kubaini na kushauri kuhusu mfumo sahihi wa udhibiti au hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuzuia kujirudia kwa dosari hizo. Kwa upande mwingine, kamati hizo zinashauriwa kuweka mkazo katika maeneo mengine yanayohusu udhibiti wa ndani na uzingatiaji wa sheria na miongozo.**

## 3.4 Mapungufu Katika Udhibiti wa Vihatarishi vya Ubadhirifu

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA 240), ubadhirifu ni kitendo cha kujipatia maslahi fulani kwa njia ya udanganyifu. Aya ya 3.7.2 ya Mwongozo wa Kuunda na Kutekeleza Mfumo wa Udhibiti wa Vihatarishi vya Ubadhirifu katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2015 inanipa mamlaka ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo huo.

Tathmini niliyoifanya katika mamlaka 185 za serikali za mitaa ilibaini mapungufu yafuatayo katika udhibiti wa vihatarishi, na mchanganuo wake ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 3-3**.

(i) Mamlaka za serikali za mitaa hazikutoa mafunzo kuhusiana na masuala ya usimamizi wa vihatarishi hususani kwa watumishi walioko katika ngazi za chini kama vile Shule, Vituo vya Kutolea Huduma za Afya na Kata. Ni muhimu kwa watumishi wote wa mamlaka za serikali za mitaa kuwa na ufahamu juu ya

vihatashiri vya ubadhirifu kama inavyoelezewa katika aya ya 3.3.3.3 ya Mwongozo wa Kuunda na Kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Ubadhirifu katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2015 ili kuboresha uzingatiaji wa sheria na ushiriki wa watumishi wote katika usimamizi wa vihatarishi;

(ii) Mamlaka 39 za serikali za mitaa hazikufanya tahmini ya vihatarishi vya ubadhirifu katika maeneo mbalimbali kama vile katika uandaaji wa taarifa za fedha, mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS) na usimamizi wa mali. Hii imesababisha kutoweka mifumo ya udhibiti wa ndani inayoendana na mazingira hayo. Kwa mfano, mamlaka za serikali za mitaa baada ya kuwasilisha kwangu taarifa zake za fedha za mwaka, zililazimika kufanya marekebisho ya taarifa hizo kwa zaidi ya mara mbili ili kusahihisha makosa niliyoyabaini.

(iii) Mamlaka 20 za serikali za mitaahazikuwa na rejesta ya vihatarishi iliyohuishwa. Hii inapunguza ufanisi katika kubaini na kusimamia vihatarishi vilivyobainika kwa sababu ya kukosekana kwa kumbukumbu juu ya vihatarishi hivi pamoja na mfumo wa ufuatiliaji wake;

(iv) Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, Halmashauri ya Wilaya ya Mlele, Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba hazikuwa na waratibu wa masuala ya vihatarishi vya ubadhirifu na wasimamizi wake katika idara/vitengo, hivyo kuathiri ufanisi katika usimamizi wa vihatarishi katika Mamlaka husika za Serikali za Mitaa; na

(v) Mamlaka 13 za serikali za mitaa hazikuwa na sera ya usimamizi wa vihatarishi na hivyo kukosa mwongozo juu ya usimamizi huo pamoja na namna ya kulinda watumishi, mali na uimara wa kiuchumi katika mamlaka za serikali za mitaa husika.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha mambo yafuatayo (a) zizingatie kikamilifu Mwongozo wa Kuunda na Kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Ubadhirifu katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2015 kwa kuhakikisha**

**utoaji wa mafunzo juu ya maadili na masuala ya ubadhirifu yanayopaswa kutolewa kwa watumishi wote; (b) tathmini ya vihatarishi vya ubadhirifu iwe inafanyika kila mwaka na rejesta ya vihatarishi inahuishwa ipasavyo; na (c) kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa inakuwa na sera ya usimamizi wa vihatarishi na inateua waratibu wa masuala ya vihatarishi vya ubadhirifu na wasimamizi wake katika idara/vitengo ili kuboresha ufanisi katika kubaini, kutathmini na kudhibiti vihatarishi vya ubadhirifu.**

## 3.5 Mapungufu katika Udhibiti wa TEHAMA na Mifumo ya Kihasibu

Ongezeko la matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika shughuli za Serikali linapelekea uhitaji wa udhibiti wa ndani madhubuti katika mifumo hiyo.

Udhibiti huu unajumuisha sera, taratibu na shughuli zilizoundwa ili kuwezesha upatikanaji, usahihi na usiri wa mifumo ya TEHAMA na taarifa zake.

Katika ukaguzi wa mwaka 2020/21, nilibaini mapungufu yafuatayo katika udhibiti wa ndani wa mifumo ya TEHAMA katika mamlaka za serikali za mitaa na mchanganuo wake ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 3-4**:

(i) Mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa zinatumia Epicor kama mfumo wa kihasibu kwa ajili ya kuchakata, kutunza na kutoa taarifa za fedha hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021. Kuanzia tarehe 01 Julai, 2021 mamlaka za serikali za mitaa zilihamia katika mfumo wa MUSE. Hata hivyo, mifumo hii yote haijaunganishwa na mifumo mingine inayotumika, kwa mfano, mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS), Mfumo wa Pamoja wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Mfumo wa Taarifa za Kifedha Unaotumiwa katika Ngazi za Chini za Serikali (FFARS) na Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT-HoMIS). Vilevile, baadhi ya moduli kama vile udhibiti wa mali, udhibiti wa madeni na madai hazitumiki. Hii inapelekea uhamishaji usio wa kimfumo wa taarifa kutoka katika mifumo mingine kwenda katika

mfumo wa kihasibu, na pia kulazimu taarifa za fedha kuandaliwa bila kutumia mfumo, jambo linaloathiri usahihi wa taarifa hizo na vilevile kuongeza muda wa uandaaji na ukaguzi wake;

(ii) Mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS) hautoi nafasi kwa Halmashauri kupata taarifa kuhusu wadaiwa wa mapato katika tarehe maalumu ambayo mtumiaji wa mfumo angehitaji kupata taarifa yake. Badala yake, kwa wakati wote mfumo hutoa taarifa ya deni lililopo hadi kufikia tarehe ambayo mtumiaji anapakua taarifa ya wadaiwa hata kama mtumiaji ataingiza tarehe ya siku tofauti;

(iii) Mamlaka 26 za serikali za mitaa zilikuwa na upungufu wa jumla ya watumishi 83 katika vitengo vya TEHAMA hivyo kusababisha ufinyu katika kupata msaada wa kitaalamu na utoaji wa huduma za TEHAMA kwa watumishi na jamii kwa ujumla;

(iv) Mamlaka 22 za serikali za mitaahazikuwa na kamati ya uendeshaji wa TEHAMA pamoja na mpango mkakati wa TEHAMA, jambo ambalo linaweza kusababisha kutokuwapo kwa utawala bora katika masuala ya TEHAMA;

(v) Mamlaka 34 za serikali za mitaa hazikuwa na mpango wa kurejesha taarifa na huduma panapotokea majanga ili kujikinga na upotevu wa taarifa endapo yatatokea majanga kama vile moto, mafuriko au kukatika kwa umeme;

(vi) Mamlaka 23 za serikali za mitaa hazikuwa na mpango wa mafunzo ili kuwajengea uwezo watumishi na kuongeza tija katika utumiaji wa vifaa vya TEHAMA na usalama wa taarifa;

(vii) Mamlaka 22 za serikali za mitaa hazikuwa na programu iliyohuishwa ya kuzuia Virusi katika Kompyuta (Anti-virus software) kwa ajili ya kulinda taarifa zake dhidi ya virusi; na

(viii) Mamlaka 35 za serikali za mitaa hazikuwa na vifaa vya kutosha kama vile vifaa vya kuzima moto, mifumo ya

kutambua uwapo wa moto na viyoyozi, kwa ajili ya kulinda vifaa vya TEHAMA dhidi ya majanga na uharibifu.

**Nashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ifanye mapitio ya mfumo wa MUSE ili mfumo huu uweze kuchukua moja kwa moja taarifa kutoka katika mifumo mingine. Vilevile, marekebisho ya taarifa ya madeni katika mfumo wa LGRCIS yafanyike ili mtumiaji aweze kupata taarifa za kipindi chochote atakachohitaji kwa wakati wowote atakaopakua taarifa kutoka katika mfumo.**

**Aidha, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa ziboreshe udhibiti wa ndani katika eneo la TEHAMA kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyoelezewa hapo juu ili kuongeza usalama wa taarifa katika mifumo ya TEHAMA na kuongeza ufanisi katika matumizi ya vifaa vya TEHAMA.**

### 3.6 Mapungufu Katika Udhibiti wa Mashine za POS

Aya ya 6.11 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa Mwaka 2019 unazitaka mamlaka za serikali za mitaa kutekeleza udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato. Udhibiti huu ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha uwajibikaji, kulinda mapato yanayokusanywa, kuhakikisha uwapo wa kumbukumbu sahihi za mapato, kuzingatia taratibu za ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha ufanisi katika zoezi la kukusanya mapato.

Tathmini yangu juu ya udhibiti katika mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS) katika mamlaka za serikali za mitaa ilibaini mapungufu yafuatayo katika udhibiti wa mashine za POS, na mchanganuo wake ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 3-5**:

(i) Mamlaka 46 za serikali za mitaa zilikuwa na jumla ya mashine za POS 1355 ambazo hazikuwa zimeonekana katika mfumo wa kukusanyia mapato kwa kipindi cha kati ya siku 3 hadi siku 4274, bila uwapo wa taarifa juu ya sababu ya mashine hizi kutoonekana katika mfumo;

(ii) Nilibaini kuwa, mamlaka nane za serikali za mitaa zilikuwa na upotevu wa jumla ya mashine 34 za POS;

(iii) Mamlaka 20 za serikali za mitaazilikuwa na jumla ya walipa kodi 890 ambao walikuwa wamesajiliwa katika mfumo wa kukusanyia mapato (LGRCIS) kwa namba ya utambulisho zaidi ya moja;

(iv) Rejesta za POS katika mamlaka 14 za serikali za mitaa hazikuwa na taarifa za kutosha na hivyo kusababisha kutokuwapo taarifa muhimu kama vile majina ya wakusanyaji wa mapato ambao wamepatiwa mashine za POS na maeneo ambayo mashine za POS zinatumika;

(v) Mamlaka sita za serikali za mitaa hazikufanya usuluhishi wa taarifa za mapato kati ya mashine za POS, mfumo wa kukusanyia mapato na taarifa za benki jambo ambalo ni kinyume na Aya ya 3.4 (ix) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa Mwaka 2019 unaotaka usuluhishi wa taarifa hizi ufanyike angalau kila wiki; na

(vi) Mashine za POS zilizopatikana kutoka OFISI YA RAIS - TAMISEMI kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2018/19 hazioneshi namba ya utambulisho wa kifaa (IMEI Number) katika mfumo wa kukusanyia mapato. Mashine hizi zote zimerekodiwa kwa namba ya utambulisho inayofanana ambayo ni -100 na hivyo kusababisha ugumu katika kutambua kifaa halisi na kile ambacho kimerekodiwa katika mfumo.

**Ninashauri Uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa:**

**Kuboresha udhibiti wa mashine za POS kwa kuhakikisha kila wakati taarifa inakuwapo kuhusiana na mashine za POS ambazo hazijaonekana katika mfumo kwa zaidi ya saa 48 ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa mapato kutokana na mashine zinazokusanya mapato bila kuunganishwa katika mfumo wa kukusanyia mapato; Kutoa taarifa kwa mamlaka husika juu ya mashine za POS zilizopotea na pia kuondoa usajili wake katika mfumo wa kukusanyia mapato; Kuondoa namba za utambulisho za wakusanyaji wa mapato ambao wamesajiliwa kwa namba zaidi ya**

**moja na kuhakikisha kila mlipa kodi amesajiliwa kwa namba moja pekee; Kuhakikisha usuluhishi wa taarifa za mapato unafanyika kila wiki ili kuondoa uwezekano wa kuwa na fedha nyingi za makusanyo ambazo hazijapelekwa benki; Kuhakikisha rejesta za mashine za POS zinahuishwa na kuwa na taarifa zinazojitosheleza; na Kushirikiana na OFISI YA RAIS - TAMISEMI ili kuhakikisha namba za utambulisho 'IMEI" za mashine zote za POS zinaonekana katika mfumo wa kukusanyia mapato.**

### 3.7 Mapungufu Katika Utaratibu wa Kuandaa Taarifa za Fedha Unaosababisha Makosa na Marekebisho mengi

Agizo la 31 la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Kifungu cha 48 (4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (Iliyorejewa 2019) linamtaka Ofisa Masuuli kuandaa taarifa za fedha na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya tarehe 30 Septemba kila Mwaka wa Fedha.

Baada ya kukagua taarifa hizo, nilibaini makosa mbalimbali ya kihasibu na hivyo kupendekeza taarifa hizo zifanyiwe marekebisho. Makosa hayo yalisababishwa na mapungufu yafuatayo:

(i) Taarifa za fedha hazikuandaliwa kutoka katika mfumo mmoja wa kihasibu. Wahasibu walipakua taarifa kutoka katika mifumo na maeneo mbalimbali kama vile Epicor, FFARS, HCMIS, LGRCIS, GoT-HoMIS pamoja na rejesta mbalimbali;

(ii) Waandaaji wa taarifa za fedha kutokuwa na uelewa wa kutosha wa kanuni na viwango vya uhasibu;

(iii) Kutokuwapo kwa wahasibu ambao wamepewa jukumu maalumu la kukusanya taarifa za kila siku zinazohusiana na uandaaji wa taarifa za fedha. Nilibaini kuwa, uandaaji wa taarifa za fedha ni jambo linalofanyika mwisho wa mwaka pekee na kuhusisha wahasibu ambao kimsingi wana majukumu yao tofauti ndani ya Idara ya Fedha;

(iv) Waandaaji wa taarifa za fedha kutokuwa na taarifa sahihi kutoka idara/vitengo vingine au kutofanya usuluhishi wa

taarifa zao na zile zilizo katika idara/vitengo vingine ilipelekea uwapo wa tofauti kati ya taarifa zilizoonekana katika taarifa za fedha na zile zilizopo katika idara/vitengo vingine. Mfano wa taarifa hizi ni taarifa ya madeni kutokana na hati za madai ambazo hazijalipwa, taarifa za mikopo ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu iliyotolewa, iliyorejeshwa na ambayo bado haijarejeshwa na taarifa ya madai ya watumishi;

(v) Upungufu wa wahasibu wasaidizi ambao wangesaidia kukusanya, kuandaa na kuripoti taarifa za fedha kutoka ngazi za chini kama vile Shule, Vituo vya Kutolea Huduma za Afya, Kata na Vijiji; na

(vi) Udhibiti wa ndani usioridhisha katika taratibu za kuandaa taarifa za fedha ikiwa ni pamoja na kutofanya usuluhishi wa miamala na bakaa mbalimbali na kutosimamia ipasavyo marekebisho ya miamala ya mwisho wa mwaka katika taarifa za fedha.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe mfumo mpya wa uhasibu ulioanzishwa na Serikali, MUSE, unachukua taarifa kutoka maeneo yote muhimu kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha. Wizara inahimizwa kuajiri wahasibu wasaidizi wa kutosha kwa ajili ya kuboresha kazi za uhasibu katika ngazi za chini.**

**Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe kuwa taarifa za fedha zinafanyiwa uhakiki wa kutosha wa ubora wake kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi, ili kuondoa makosa ya kihasibu katika taarifa hizo.**

**Mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuwajengea uwezo wahasibu wake kupitia mafunzo ya mara kwa mara na pia zianzishe kitengo cha taarifa za fedha ndani ya Idara ya Fedha, ambacho kitakuwa na jukumu la kufanyia kazi matukio na miamala ya kila siku inayohusiana na taarifa za fedha ikiwa ni pamoja na kufanya usuluhishi wa taarifa kati ya Idara ya Fedha na Idara/vitengo vingine.**

## 3.8 Mapungufu Katika Udhibiti wa Marekebisho ya Miamala

Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, nilibaini kuwa, mamlaka za serikali za mitaa zilifanya marekebisho kadhaa ya miamala bila kuwa na ushahidi wa idhini pamoja na viambatisho vya kuthibitisha uhalali wa marekebisho hayo.

Nilibaini kuwa, iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kutumia hati za marekebisho ya miamala (JVs), ilifanya marekebisho ya miamala mbalimbali yenye jumla ya shilingi bilioni 3.44. Pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilifanya miamala yenye jumla ya shilingi bilioni 5.22 katika daftari la fedha kwa maelezo kuwa ni marekebisho ya makosa ya mfumo wa kihasibu. Aidha, marekebisho ya miamala hii yenye jumla ya shilingi bilioni 8.66 hayakuwa na vielelezo vya kuthibitisha uhalali wake.

Vilevile, nilibaini kuwa, mamlaka 27 za serikali za mitaa zilifanya marekebisho ya ankara za mapato zenye jumla ya shilingi bilioni 2.05 bila kuwa na vielelezo vya kuthibitisha uhalali wake **(Rejea aya** ya **5.1 katika Sura ya 5)** kinyume na Agizo la 29(4) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 ambayo inataka kila marekebisho yawe na hati ya marekebisho inayoonesha vifungu vilivyoathirika na marekebisho hayo pamoja na sababu za marekebisho.

Marekebisho haya yasiyo na vielelezo yalisababishwa na mapungufu katika udhibiti wa ndani katika matumizi ya mifumo ya Epicor na LGRCIS ikiwa ni pamoja na watumiaji wa mifumo hii kuchangia nywila, Maofisa Masuuli kukasimisha kazi ya kuidhinisha marekebisho ya miamala kwa watumishi walio chini yao na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kutofanya mapitio ya mara kwa mara ya marekebisho ya miamala.

Uwapo wa marekebisho ya miamala bila kuwa na vielelezo inaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma kwa njia ya udanganyifu katika taarifa za mapato, bakaa za fedha au taarifa za matumizi ili kuficha taarifa juu ya ubadhirifu.

**Ninashauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuboresha udhibiti katika mifumo yake kwa kuweka wigo wa**

**kufanya marekebisho ya miamala na kuzuia watumiaji wa mifumo kuchangia nywila; Kuhakikisha Maofisa Masuuli wanaweka ukomo wa viwango vya fedha ambavyo wanaweza kukasimisha marebisho yake kwa watumishi walio chini yao; Kufanya mapitio ya mara kwa mara ya marekebisho ya miamala katika mifumo ya mamlaka za serikali za mitaa; na kuhakikisha kuwa marekebisho yote ya miamala yanapitia ngazi sahihi na kuwa na vielelezo vya kuthibitisha uhalali wake.**

## SURA YA 4

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaainisha thatmini ya bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa chini ya mamlaka za serikali za mitaa; itokanayo na ukusanyaji na matumizi yenye ufanisi wa fedha zilizopatikana kutokana na mapato ya vyanzo vya ndani, ruzuku kutoka Serikali Kuu, pamoja na fedha kutoka kwa wahisani na wadau wa maendeleo ikilinganishwa na hali halisi ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2021.

Nchini Tanzania, Serikali huandaa bajeti kwa msingi wa fedha taslimu ambapo taarifa za fedha huzingatia misingi ya uhasibu ya IPSAS. Bajeti zilizoidhinishwa ni vipengele muhimu vya mipango ya fedha, udhibiti na hutumika kupima utendaji wa mamlaka za serikali za mitaa.

Bajeti iliyoidhinishwa ina maana ya matumizi yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo ya Serikali na maamuzi mengine yanayohusiana na makisio ya mapato katika kipindi cha bajeti.

Kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa 2019) kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kwa muda usiopungua miezi miwili kabla ya kila mwanzo wa mwaka wa fedha, katika kikao maalumu, kupitisha bajeti ya makadirio ikionesha kiasi cha mapato kinachotarajiwa kupokelewa; kiasi kinachotarajiwa kutolewa na Mamlaka katika mwaka wa fedha husika; na kukiwa na ulazima mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kupitisha bajeti za ziada katika mwaka wa fedha husika.

### 4.1 Mapitio ya Bajeti

Mapitio yangu ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/21 yalikuwa na lengo la kutathmini kama Halmashauri zinaendana na Sera ya Bajeti ya Serikali, Tamko la Mfumo wa Fedha na Sheria ya Bajeti. Pia, kujiridhisha kama bajeti zilizoidhinishwa zimezingatia Kifungu cha 46 (1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (Iliyorekebishwa 2019). Ninapendekeza kwamba mapitio ya bajeti

yaendane na upatikanaji wa fedha na uwazi kama ilivyoainishwa katika vifungu hivyo.

Nilifanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/21 na kubaini mambo yafuatayo:

## 4.2 Mwenendo wa Bajeti na Tathmini ya Kiwango cha Utegemezi wa Mamlaka za Selikali za Mitaa

### 4.2.1 Mwenendo Mapato ya Ndani dhidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Mapitio ya taarifa za fedha zilizowasilishwa za mamlaka 185 za serikali za mitaa yalionesha kuwa makusanyo ya mapato katika mwaka wa fedha 2020/21 yalikuwa shilingi bilioni 769.42 ambayo ni asilimia 94 ya makadirio ya bajeti ya shilingi bilioni 822.38.

Pia, ulinganisho wa makusanyo kati ya mwaka husika na mwaka wa fedha 2019/20 ya shilingi bilioni 709.57 ulionesha kuwa Halmashauri katika mwaka husika zilikusanya zaidi kwa shilingi bilioni 59.85 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4-1** na **Kiambatisho Na. 4-1**.

**Jedwali Na. 4-1: Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani**

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Makusanyo Pungufu (Sh.) | % ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 822,375,950,562 | 769,422,329,061 | 52,953,621,501 | 94 |
| 2019/20 | 759,907,423,938 | 709,573,567,541 | 50,333,856,397 | 93 |
| 2018/19 | 725,633,451,671 | 639,401,151,405 | 86,232,300,266 | 89 |
| 2017/18 | 677,965,549,714 | 566,729,291,189 | 111,236,258,525 | 84 |
| 2016/17 | 628,045,048,644 | 523,564,835,716 | 104,480,212,928 | 83 |

Licha ya mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kuonekana kupanda katika miaka 5, bado makadirio ya mapato yaliyoidhinishwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yanaonekana si halisia kutokana na kushuka kwa ukusanyaji wa mapato ikilinganishwa na bajeti kutokana na mapungufu katika udhibiti wa vyanzo vya mapato.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya mapato vya ndani vilivyopo na kuibua vyanzo vipya ndani ya maeneo yao ya mamlaka. Pia, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuandaa**

**makadirio halisi na yenye tija ili kuziwezesha kufikia viwango bora vya ukusanyaji wa mapato.**

### 4.2.2 Tathmini ya Jumla ya Vyanzo vya Ndani vya Mapato

#### a) Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato zaidi ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Katika tathmini ya bajeti iliyoidhinishwa ya Mamlaka 64 za Serikali za Mitaa ya shilingi bilioni 346.13, nilibaini mamlaka hizo zilikusanya mapato halisi ya shilingi bilioni 376.30 ikiashiria mafanikio ya ukusanyaji kwa asilimia 109 ya mapato yote yaliyokadiriwa kukusanywa na mamlaka hizo. Aidha, ulinganisho wa ukusanyaji wa mapato halisi yaliyokusanywa mwaka uliopita 2019/20 ni asilimia 115 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-2** na **Kiambatisho Na. 4-2.**

**Jedwali Na. 4-2: Halmashauri zilizokusanya mapato zaidi ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Tofauti (Sh.) | % ya utekelezaji | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 346,128,129,473 | 376,302,581,046 | 30,174,451,573 | 109 | 64 |
| 2019/20 | 315,579,839,663 | 363,859,170,229 | 48,279,330,566 | 115 | 62 |

#### b) Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizokusanya Mapato chini ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Nilibaini kuwa Mamlaka 121 za Serikali za Mitaa zilipanga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 476.25 kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato yao lakini zilifanikiwa kukusanya mapato halisi ya shilingi bilioni 393.12; kuashiria mafanikio kwa asilimia 83 ya makadirio ya mapato yote ikilinganishwa na asilimia 78 ya makusanyo ya mwaka uliopita 2019/20 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-3** na **Kiambatisho Na. 4 - 3.**

**Jedwali Na. 4-3: Halmashauri zilizokusanya mapato chini ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.) | Makusanyo halisi (Sh.) | Tofauti (Sh.) | % ya Utekelezaji | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 476,247,821,089 | 393,119,748,015 | 83,128,073,074 | 83 | 121 |
| 2019/20 | 442,034,532,275 | 343,421,345,312 | 98,613,186,963 | 78 | 123 |

Ni dhahiri menejimenti hazijaweza kukusanya kikamilifu mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vilivyopo ambavyo vingeweza kuchangia mapato ya kutosha kumudu uendeshaji wa shughuli zake.

**Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kukusanya mapato kikamilifu na kuibua vyanzo vipya ili kuhakikisha zinafikia malengo yaliyowekwa.**

### 4.2.3 Makusanyo Halisi ya Mapato ya ndani Yakilinganishwa na Matumizi ya Kawaida

Ufanisi wa makusanyo katika mamlaka 131 za serikali za mitaa nilibaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 615.58 zilikusanywa kutoka vyanzo vya ndani. Aidha, matumizi ya kawaida ya mamlaka za serikali za mitaa yalikuwa shilingi trilioni 3.38 ambapo inaonesha kuwa mapato ya ndani ni asilimia 18 ya matumizi yote ya kawaida. Kiwango cha utegemezi katika mamlaka za serikali za mitaa ni asilimia 82 kutokana na kushuka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4-4** na **Kiambatisho Na. 4-4.**

**Jedwali Na. 4-4: Uwiano wa mapato ya ndani na ruzuku ya matumizi ya kawaida**

| Mwaka wa fedha | Makusanyo Halisi (Sh.) | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida (Sh.) | % Utegemezi |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 615,579,732,914 | 3,379,889,357,327 | 82 |
| 2019/20 | 709,573,567,541 | 4,773,489,160,809 | 85 |
| 2018/19 | 639,401,151,405 | 4,139,568,491,180 | 85 |
| 2017/18 | 566,729,291,189 | 4,373,555,868,608 | 87 |
| 2016/17 | 523,564,835,716 | 4,656,643,395,963 | 89 |

Kwa ujumla, kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kutasaidia kuimarisha uendeshaji wa Halmashauri na kupunguza kwa

kiasi kikubwa utegemezi wa ruzuku ya Serikali Kuu na ufadhili kutoka nje kugharamia shughuli au bajeti za Halmashauri.

**Ninaishauri Serikali kutoa fedha kama zinavyoidhinishwa na Bunge jambo ambalo litaimarisha na kurahisisha utekelezaji wa shuguli zilipangwa na kupunguza bajeti ya nyongeza isivyostahili. Pia, mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa iimarishwe ili kuendana na makadirio halisi ya malengo ya ukusanyaji mapato yaliyopangwa.**

## 4.3 Ufanisi Katika Matumizi ya Fedha za Ruzuku Kutoka Serikali Kuu

Nilifanya tathmini ya fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa pamoja kutoka Serikali Kuu kwa mamlaka 185 za serikali za mitaa na kubaini kuwa kulikuwa na makadirio ya bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 5.98 ambapo fedha zilizopokelewa ni shilingi trilioni 5.14, hivyo, shilingi bilioni 840 hazikupokelewa sawa na asilimia 14 ya ruzuku ya Serikali Kuu iliyoidhinishwa.

Upelekeji wa fedha pungufu za ruzuku ni kiashiria cha kutofanyika tathmini kwa kina ya makadirio ya mapato kwa kuzingatia hali halisi ya mwaka husika sambamba na mwaka unaofuata. Vile vile, hali hii inachangiwa na kasi ndogo ya matumizi ya fedha katika miradi na programu za maendeleo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4-5.**

**Jedwali Na. 4-5: Jumla ya ruzuku kutoka serikali kuu**

| Maelezo ya Ruzuku | Makisio ya Mapokezi ya Ruzuku (Sh.) | Kiasi Halisi Kilichopokelewa (Sh.) | Kiasi Ambacho Hakikutolewa (Sh.) | % ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| Miradi ya Maendeleo | 928,045,662,685 | 662,702,003,065 | 265,343,659,620 | 71 |
| Matumizi ya Kawaida | 5,053,202,263,366 | 4,479,692,402,938 | 573,509,860,427 | 89 |
| **Jumla** | **5,981,247,926,051** | **5,142,394,406,003** | **838,853,520,048** | **86** |

### 4.3.1 Tathmini ya Jumla ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Kutoka Serikali Kuu

Makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 katika mamlaka 185 za serikali za mitaa ilikuwa shilingi trilioni 5.05 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 5.43 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi trilioni 5.06 kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Nilipitia taarifa za fedha katika mamlaka 185 za serikali za mitaa, na kubaini kuwa Halmashauri zilipokea shilingi trilioni 4.48 za ruzuku ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 89 ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi trilioni 5.06 ikimaanisha kuwa shilingi bilioni 573.51 hazikupokelewa.

Pia, matumizi katika mwaka husika wa fedha yameongezeka kwa shilingi bilioni 133.10 sawa na asilimia 3 ya fedha zilizopokelewa kiasi cha shilingi trilioni 4.48 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.35 zilizopokelewa mwaka 2019/20. Mwenendo wa makisio pamoja na kiasi halisi kilichopokelewa kwa kipindi cha miaka mitano ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-6.**

**Jedwali Na. 4-6: Ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa**

| Mwaka wa fedha | Kiasi halisi kilichotolewa (Sh.) | Kiasi ambacho hakikutolewa (Sh.) | Kiasi Pungufu (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 5,053,202,263,366 | 4,479,692,402,938 | 573,509,860,427 | 11 |
| 2019/20 | 5,058,633,670,916 | 4,346,587,656,245 | 712,046,014,671 | 14 |
| 2018/19 | 5,305,420,943,498 | 4,343,261,816,245 | 962,159,127,253 | 18 |
| 2017/18 | 5,323,497,887,360 | 4,378,343,613,609 | 945,154,273,751 | 18 |
| 2016/17 | 4,899,139,596,169 | 4,400,097,208,661 | 499,042,387,508 | 10 |

Kwa kuzingatia mchanganuo hapo juu, makadirio ya ruzuku ya matumizi ya kawaida yamekuwa yakipungua kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2017/18. Hali hii inaashiria hatari kwa mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kutekeleza majukumu yake kama zitaendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku ya Serikali Kuu badala ya kugharamia shughuli zake kutokana na makusanyo ya mapato ya vyanzo vya ndani.

### 4.3.2 Ulinganisho kati ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida iliyopokelewa na Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Baadhi ya Halmashauri

#### a) Mapokezi ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Zaidi ya Bajeti

Nilifanya tathmini ya taarifa za bajeti ya ruzuku ya matumizi ya kawaida kutoka Serikali Kuu na kubaini kuwa, mamlaka 39 za serikali za mitaa ziliidhinishiwa shilingi bilioni 938.90 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya mamlaka hizo. Hata hivyo shilingi trilioni 1.01 zilipokelewa na mamlaka hizo ikiashiria ziada ya shilingi bilioni 74.38 sawa na asilimia nane ya makisio ya mwaka kwa halmashauri husika. Mwenendo wa fedha za ruzuku ya matumizi ya kawaida zilizopokelewa zaidi ya bajeti na halmashauri husika kwa miaka mitano umeainishwa katika **Jedwali Na. 4-7** na **Kiambatisho Na. 4-5.**

**Jedwali Na. 4-7: Ruzuku ya matumizi ya kawaida iliyopokelewa zaidi ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti Iliyoidhinishwa (Sh.) | Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.) | Kiasi Kilichopokelewa Zaidi (Sh.) | % | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 938,898,887,797 | 1,013,274,495,952 | 74,375,608,155 | 8 | 39 |
| 2019/20 | 868,358,072,467 | 930,769,374,966 | 62,411,302,499 | 7 | 29 |
| 2018/19 | 369,440,284,951 | 395,432,102,867 | 25,991,817,916 | 7 | 26 |
| 2017/18 | 473,197,252,447 | 515,832,995,318 | 42,635,742,871 | 9 | 23 |
| 2016/17 | 909,489,550,054 | 991,974,389,012 | 82,484,838,958 | 9 | 14 |

Kuna hatari ya fedha zilizotolewa zaidi ya bajeti kuwa na viashiria vya ubadhirifu

**Kama nilivyopendekeza mwaka uliopita, natoa wito kwa Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kupeleka fedha katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na endapo kuna fedha zaidi iliyopelekwa; mamlaka za serikali za mitaa ziwe zinaomba idhini ya bajeti ya nyongeza kwa mamlaka husika kabla ya kufanya matumizi. Pia, uchunguzi ufanyike ili kubaini iwapo fedha iliyotolewa zaidi ya bajeti haikuwa na viashiria vya ubadhirifu.**

## b) Mapokezi ya Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Pungufu ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Tathmini ya makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 inaonesha kuwa mamlaka 144 za serikali za mitaa zilikuwa na makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi trilioni 4.06 kama na ruzuku ya matumizi ya kawaida. Hata hivyo, nilibaini kuwa shilingi trilioni 3.41 ndizo zilizopokelewa, ikiashiria mapokezi pungufu kwa shilingi bilioni 647.89 sawa na asilimia 16 ya bajeti ya mwaka husika kama ilivyoanishwa katika **Jedwali Na. 4-8** na **Kiambatisho Na. 4-6.**

**Jedwali Na. 4-8: Mapokezi ya ruzuku ya matumizi ya kawaida pungufu ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti Iliyodhinishwa (Sh.) | Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.) | Kiasi Kilichopokelewa Pungufu (Sh.) | % | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 4,058,443,028,569 | 3,410,557,559,986 | 647,885,468,582 | 16 | 144 |
| 2019/20 | 4,190,275,598,449 | 3,415,818,281,279 | 774,457,317,170 | 18 | 150 |
| 2018/19 | 4,935,980,658,547 | 3,947,829,713,378 | 988,150,945,169 | 20 | 167 |
| 2017/18 | 4,850,300,634,913 | 3,862,510,618,291 | 987,889,016,622 | 20 | 165 |
| 2016/17 | 3,989,650,046,115 | 3,408,122,819,649 | 581,527,226,466 | 15 | 146 |

Kwa kuzingatia tathmini ya mwenendo uliooneshwa katika **Jedwali Na. 4-8,** utoaji wa fedha ruzuku pungufu ya bajeti iliyoidhinishwa zinaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa hivyo mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa kutokana na uhaba wa fedha.

Pia, nilibaini kuwa ni Halmashauri mbili tu, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara zilizopata shilingi bilioni 55.86 kwa pamoja ambazo ni sawa na makadirio ya bajeti zao.

**Naishauri Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida zinatolewa kwa mujibu wa makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa ili kuziwezesha mamlaka za serikali za mitaa kufikia malengo ya uendeshaji wa shughuli zake kama ilivyopangwa.**

### 4.3.3 Fedha za Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Zilizopokelewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa ya mamlaka 185 za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21 itokanayo na ruzuku ya miradi ya maendeleo ya Serikali yalikuwa shilingi bilioni 928.05, ambapo inaonesha kupungua kwa shilingi bilioni 29.54 (sawa na asilimia 3) ikilinganishwa na makadirio ya bajeti ya shilingi bilioni 957.59 yaliyoidhinishwa ya mwaka 2019/20.

Nilipitia taarifa za fedha za mamlaka 185 za serikali za mitaa na kubaini kuwa shilingi bilioni 662.70 za ruzuku ya miradi ya maendeleo zilitolewa sawa na asilimia 71 ya makadirio yaliyoidhinishwa.

Aidha, ruzuku ya matumizi ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa shilingi bilioni 95.48 ikilinganishwa na shilingi bilioni 567.22 zilizopokelewa mwaka wa fedha 2019/20. Mwenendo wa makisio na mapokezi ya fedha za ruzuku ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-9.**

**Jedwali Na. 4-9: Fedha za ruzuku ya maendeleo zilizotolewa**

| Mwaka wa fedha | Kiasi kilichiidhinishwa (Sh.) | Kiasi halisi kilichotolewa (Sh.) | Tofauti (pungufu/zaidi) (Sh.) | % |
|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 928,045,662,685 | 662,702,003,065 | 265,343,659,620 | 29 |
| 2019/20 | 957,587,667,725 | 567,217,692,153 | 390,369,975,572 | 41 |
| 2018/19 | 1,258,923,356,355 | 724,887,032,125 | 534,036,324,230 | 42 |
| 2017/18 | 1,061,442,721,967 | 603,557,933,616 | 457,884,788,351 | 43 |
| 2016/17 | 1,078,569,747,137 | 564,428,940,402 | 514,140,806,735 | 48 |

Tathmini ya mwenendo wa makadirio ya fedha katika **Jedwali Na. 4-9,** inaonesha kumekuwa na kupungua kwa makadirio ya ruzuku ya fedha za maendeleo kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha 2018/19. Fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo hazikutolewa zinaathiri shughuli za utekelezaji wa miradi iliyopangwa ikiwa ni pamoja na mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kutimiza masharti ya mikataba hivyo kusababisha kutozwa riba na adhabu nyingine zinazoweza kuisababishia Serikali mzigo wa madeni.

### 4.3.4 Ulinganisho kati ya Fedha za Ruzuku ya Maendeleo zilizopokelewa na Bajeti Iliyoidhinishwa kwa Baadhi ya Halmashauri

#### a) Halmashauri Zilizopokea Ruzuku ya Maendeleo zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa

Mapitio ya taarifa za fedha za mamlaka 19 za serikali za mitaa yanaonesha kuwa, halmashauri hizo ziliidhinishiwa ruzuku ya miradi ya maendeleo ya shilingi bilioni 90.18. Fedha za ruzuku zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa shilingi bilioni 137.37 ikiashiria ziada ya shilingi bilioni 47.19 (sawa na asilimia 52) ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa.

Aidha, tathmini ya mwenendo wa utoaji wa ruzuku ya maendeleo kwa halmashauri husika inaonesha kuongezeka kwa utoaji wa fedha zaidi ya bajeti kwa shilingi bilioni 27.14 kutoka shilingi bilioni 20.05 kwa mwaka wa fedha 2019/20 mpaka shilingi bilioni 47.19 kwa mwaka wa fedha 2020/21. Mwenendo wa utoaji fedha zaidi ya bajeti ya halmashauri kwa kipindi cha miaka mitano ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4-10** na **Kiambatisho Na. 4-7.**

**Jedwali Na. 4-10: Ruzuku ya maendeleo iliyotolewa zaidi ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Makisio ya mapokezi ya ruzuku (Sh.) | Kiasi halisi kilichopokelewa (Sh.) | Kiasi ambacho hakikutolewa (Sh.) | % | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 90,184,385,862 | 137,371,891,387 | 47,187,505,525 | 52 | 19 |
| 2019/20 | 67,272,409,002 | 87,319,960,255 | 20,047,551,253 | 30 | 29 |
| 2018/19 | 73,433,637,673 | 96,250,291,206 | 22,816,653,533 | 31 | 26 |
| 2017/18 | 84,214,721,967 | 106,275,933,616 | 22,061,211,649 | 26 | 23 |
| 2016/17 | 44,446,747,137 | 62,520,940,402 | 18,074,193,265 | 41 | 14 |

Fedha zaidi ya bajeti huenda zikatumika isivyostahili na pengine kwa njia za ubadhirifu iwapo hazitasimamiwa ipasavyo.

**Naishauri Serikali kutoa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Pia, Serikali ifanye uchunguzi ili kujiridhisha kama fedha zilizotolewa zaidi ya bajeti hazikuwa na viashiria vya ubadhirifu.**

## b) Halmashauri Zilizopokea Ruzuku ya Maendeleo Pungufu ya Bajeti Iliyoidhinishwa

Mapitio ya makadirio ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2020/21 inaonesha kuwa mamlaka 163 za serikali za mitaa zilikuwa na makadirio ya ruzuku ya miradi ya maendeleo toka Serikali Kuu ya shilingi bilioni 831.48. Jumla ya shilingi bilioni 518.95 zilipokelewa na Halmashauri hizo, hivyo kusababisha shilingi bilioni 312.53 kutopokelewa sawa na asilimia 38 ya bajeti iliyoidhinishwa kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 4-11** na **Kiambatisho Na. 4-8.**

**Jedwali Na. 4-11: Ruzuku ya maendeleo iliyotolewa pungufu ya bajeti**

| Mwaka wa fedha | Bajeti Iliyoidhiniswa (Sh.) | Kiasi Kilichotolewa (Sh.) | Pungufu (Sh.) | % | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|---|---|---|
| 2020/21 | 831,478,155,338 | 518,946,990,193 | 312,531,165,145 | 38 | 163 |
| 2019/20 | 890,315,258,723 | 479,897,731,898 | 410,417,526,825 | 46 | 150 |
| 2018/19 | 1,185,489,718,682 | 628,636,740,919 | 556,852,977,763 | 47 | 167 |
| 2017/18 | 977,228,000,000 | 497,282,000,000 | 479,946,000,000 | 49 | 165 |
| 2016/17 | 1,034,123,000,000 | 501,908,000,000 | 532,215,000,000 | 51 | 146 |

Kwa maoni yangu, utoaji wa fedha pungufu za ruzuku ya miradi ya maendeleo kwa mamlaka za serikali za mitaa unaathari shughuli zilizopangwa kutekelezwa kutokana na kuongezeka kwa gharama na riba katika utekelezaji wa mradi hali ambayo itaipa Serikali mzigo mkubwa wa madeni.

Halmashauri tatu pekee ndizo ambazo zilipokea kiasi halisi cha makadirio ya bajeti iliyopangwa ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu zenye jumla ya shilingi bilioni 6.38 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa.

**Naishauri Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ruzuku ya maendeleo zinatolewa kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa ili kuziwezesha mamlaka za serikali za mitaa kufikia malengo ya utekelezaji wa shughuli zake kama ilivyopangwa.**

## 4.4 Mapato ya Ndani ambayo Hayakutengwa kwa Ajili ya Miradi ya Maendeleo Shilingi Bilioni 24.24

Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa barua yenye kumbukumbu Na.CBD.421/422/01/43 ya tarehe 3 Januari, 2018 ambapo Halmashauri ziliwekwa katika makundi “A” na “B na kuzielekeza kutenga asilimia 40 na asilimia 60 ya mapato ya vyanzo vyake vya ndani, mtawalia kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pia, Mwongozo wa Maandalizi ya Mipango na Bajeti ya mwaka wa 2019/20 hadi 2021/22 ulitolewa kuhakikisha kuwa asilimia 40 na asilimia 60 ya mapato ya mamlaka za serikali za mitaa zinatengwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo.

Nilifanya tathmini ya fedha zilizotengwa na mamlaka za serikali za mitaa kutoka vyanzo vya mapato ya ndani kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo na kubaini kuwa Halmashauri 92 zilitenga fedha kidogo au hazikutenga fedha kabisa kulingana na asilimia inayotakiwa. Aidha, zilishindwa kutenga na kuchangia miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 24.24. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikutenga fedha kama inavyostahili imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 4-9.**

**Nasisitiza mapendekezo yangu ya mwaka uliopita kwamba Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuzingatia maelekezo na miongozo ya bajeti ya Serikali kwa kuhakikisha kuwa sehemu sahihi ya mapato yao inatengwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo; na pia kuhakikisha fedha zote za maendeleo zilizotengwa zinatumika katika miradi iliyokusudiwa, badala ya kutumika kukidhi shughuli za kawaida.**

# SURA YA 5

# USIMAMIZI WA MAPATO

## 5.0 Utangulizi

Mamlaka za serikali za mitaa zina vyanzo mbalimbali vya mapato vikiwemo kodi za ndani, leseni, ada, faini na adhabu, mapato yatokanayo na ubadilishanaji wa bidhaa au huduma, na mapato mengine. Ukusanyaji bora wa mapato ni muhimu katika kuimarisha maendeleo na uendelevu wa mamlaka za serikali za mitaa ili kuwezesha uwekezaji katika rasilimaliwatu, miundombinu na uboreshaji wa utoaji huduma kwa jamii. Mwenendo unaonesha kuwa, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita, makusanyo ya mapato ya ndani ya mamlaka za serikali za mitaa yamekuwa yakiboreka kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5 -1.**

**Kielelezo Na. 5 -1: Mapato ya ndani**




Ukusanyaji wa mapato katika mamlaka ya serikali za mitaa kimsingi hufanywa kupitia mifumo mitatu ya taarifa za mapato ambayo ni Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato (LGRCIS), Mfumo wa Taarifa za Kifedha unaotumiwa katika ngazi za chini za serikali (FFARS) na Mfumo wa Serikali wa Usimamizi wa Hospitali Tanzania (GoT–HoMIS). Lengo la mifumo hii ni kuboresha ufanisi katika michakato ya ukusanyaji wa mapato, usimamizi wa fedha, kanzidata za walipakodi, utunzaji kumbukumbu, utoaji wa taarifa, na nyenzo ya udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mapato.

Tathmini niliyoifanya katika usimamizi wa ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa pamoja na uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo ya bajeti, na maagizo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa mapato, imebaini udhaifu mbalimbali kama unavyoelezwa hapa chini.

## 5.1 Marekebisho ya Ankara za Thamani ya Shilingi Bilioni 1.66 bila Viambatisho Toshelevu

Agizo la 37 (6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaeleza kwamba, kama stakabadhi imekosewa, itenguliwe mara moja na itolewe mpya. Stakabadhi halisi iliyotengeliwa ihifadhiwe kwa ukaguzi. Pia, Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha marekebisho na ufutaji wa ankara zisizo sahihi katika Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Usimamizi wa Fedha (IFMIS) au Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato (LGRCIS) kuidhinishwa na mkurugenzi wa halmashauri.

Nilipitia marekebisho ya ankara yaliyofanyika katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato katika mamlaka za serikali za mitaa na kubaini kuwa, mamlaka 27 za serikali za mitaa zilirekebisha ankara za kiasi cha shilingi bilioni 1.66 katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato bila maelezo na/au viambatisho toshelevu ili kuhalalisha mabadiliko ya ankara zinazohusika wakati baadhi ya Halmashauri zilifanya marekebisho bila idhini ya Wakurugenzi.

Kutokana na kukosekana kwa viambatisho hivyo, sikuweza kuthibitisha uhalali wa marekebisho yaliyofanywa. Kwa maoni yangu, mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika hazijatekeleza kikamilifu hatua za udhibiti kama inavyotakiwa na Agizo la 37(6) la Randama ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 na Aya ya 3.4 (vii) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019. Maelezo ya marekebisho hayo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 5-1**.

**Jedwali Na. 5-1: Ankara zilizorekebishwa bila viambatisho**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Rufiji | 656,820,563 | 15. | H/W Chamwino | 19,673,910 |
| 2. | H/W Mbozi | 201,359,728 | 16. | H/M Lindi | 17,195,983 |
| 3. | H/M Kinondoni | 135,994,090 | 17. | H/W Morogoro | 16,316,145 |
| 4. | H/W Mkuranga | 124,867,127 | 18. | H/W Bagamoyo | 13,663,932 |
| 5. | H/W Kilindi | 104,869,200 | 19. | H/W Nsimbo | 11,799,744 |
| 6. | H/M Iringa | 85,640,671 | 20. | H/W Serengeti | 9,875,644 |
| 7. | H/W Kibaha | 45,589,585 | 21. | H/Mji Nzega | 9,253,626 |
| 8. | H/W Kisarawe | 31,847,394 | 22. | H/Jiji Mwanza | 8,578,000 |
| 9. | H/W Rorya | 27,116,121 | 23. | H/W Bumbuli | 7,406,000 |
| 10. | H/W Kwimba | 25,563,641 | 24. | H/W Musoma | 5,476,000 |
| 11. | H/W Korogwe | 24,404,486 | 25. | H/W Nyasa | 4,956,250 |
| 12. | H/W Mpwapwa | 24,148,808 | 26. | H/W Kaliua | 4,301,700 |
| 13. | H/W Kiteto | 23,285,500 | 27. | H/W Simanjiro | 4,104,100 |
| 14. | H/W Mufindi | 20,716,628 | | **Jumla** | **1,664,824,576** |

Kwa maoni yangu, marekebisho bila kuwa na vielelezo vya kutosha na kibali yanaziweka halmashauri kwenye hatari ya ubadhirifu wa mapato yanayokusanywa.

**Ninatoa wito kwa mamlaka za serikali za mitaa kuweka udhibiti sahihi ili kusaidia utunzaji wa viambatisho vya ankara za mapato zinazorekebishwa au kufutwa kwa kuhuisha au kupakia nyaraka husika katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato kabla ya kuidhinishwa na mkurugenzi wa halmashauri.**

## 5.1 Kutowasilishwa Benki Shilingi Bilioni 17 za Mapato Yaliyokusanywa Kupitia POS

Kifungu cha 42 (2) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (iliyorejewa mwaka 2019) kinaelekeza kuwa, stakabadhi zote zinazohusiana na mamlaka ya serikali ya mitaa zitalipwa katika akaunti ya benki au akaunti iliyothibitishwa na mamlaka hiyo. Pia, kwa mujibu wa Aya ya 3.4 (v) ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuchukua hatua stahiki za udhibiti, ikijumuisha uwekaji wa mapato yanayokusanywa benki mara moja ili kuimarisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato.

Nilifanya tathmini ya taarifa za mapato kutoka mfumo wa ukusanyaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa na kupitia mapato

yatokanayo na vyanzo vingine vilivyokusanywa kupitia mashine za POS na kubaini kuwa, wakusanya mapato katika mamlaka 147 za serikali za mitaahawakuwasilisha jumla ya shilingi bilioni 17 katika akaunti husika za benki. Hii inatokana na kutofanyika kwa usuluhishi wa mara kwa mara wa hesabu (angalau kwa wiki) na kukosekana kwa ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha makusanyo ya mapato yanawekwa benki kwa wakati. Pia, kwa kuwa njia pekee inayotumika ni ya wakusanya mapato kuwasilisha wenyewe benki fedha zilizokusanywa, hali hii imesababisha kuongezeka kwa fedha zisizowasilishwa benki hasa kwa wakusanya mapato ambao wapo nje ya miji. Maelezo ya mapato ambayo hayajapelekwa benki yameoneshwa katika **Kiambatisho Na. 5-1**.

Ingawa kiasi cha fedha za mapato kisichowasilishwa benki kwa mwaka 2020/21 kimepungua ikilinganishwa na mwaka 2019/20; kiasi cha shilingi bilioni 17 bado ni kikubwa na hii inaashiria kuwa kunahitajika jitihada za ziada ili kuondosha uvujaji wa mapato katika mamlaka za serikali za mitaa. Mwenendo wa makusanyo ambayo hayajawekwa benki ni kama inavyooneshwa katika **Kielelezo Na. 5-2.**

**Kielelezo Na. 5-2: Mwenendo wa makusanyo yasiyowasilishwa benki**




Kutokuwasilishwa benki kwa makusanyo ya vyanzo hivyo, kunaweza kuzisababishia halmashauri husika hasara za upotevu ama ubadhirifu wa mapato hayo.

Ni maoni yangu kwamba, kuanzishwa na kutumika kwa njia za kielektroniki ikiwemo mitandao ya simu na benki, itawasaidia wateja

kuwasilisha moja kwa moja fedha katika akaunti, hii inaweza kupunguza kiasi kisichopelekwa benki kwani huduma hizi zinapatikana kwa urahisi na kwa maeneo mengi.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) ifanye mapitio ya utaratibu wa kupeleka fedha benki, ikijumuisha kuangalia uwezekano wa kutumia mifumo ya kimtandao ya simu na benki kupitia kampuni zinazotoa huduma hizo. (b) kuwe na sera zinazosimamia makubaliano ya muda wa kupeleka pesa benki na kutoza tozo kwa ucheleweshaji na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuimarisha taratibu zake za udhibiti wa ndani ili kuhakikisha fedha zinawasilishwa benki kwa wakati na kuhakikisha fedha ambazo hazikupelekwa benki zinarejeshwa.**

## 5.2 Mapato Shilingi Bilioni 14.3 Yasiyokusanywa Kutoka katika Vyanzo Muhimu vya Mapato

Nilikagua makusanyo ya mapato kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato katika mamlaka za serikali za mitaa na kubaini kuwa, jumla ya shilingi bilioni 14.30 hazikukusanywa katika mamlaka 120 za serikali za mitaa, zikijumuisha mapato ambayo hayajalipwa yaliyoorodheshwa katika rejista au ankara za madai zilizoorodheshwa katika taarifa ya wadaiwa katika Mfumo wa Ukusanyaji Mapato. Vyanzo vinavyohusishwa hasa ni pamoja na kodi za kupangisha maduka na nyumba vilivyopo katika stendi za mabasi na masoko, vibanda na vizimba vya masoko, uuzaji wa viwanja, ushuru wa mazao ya kilimo na leseni za vileo.

Hali hii ni kinyume na Agizo la 38 (1) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, linalomtaka mwekahazina kuwajibika kufanya taratibu stahiki za usimamizi wa fedha na uhasibu ili kuhakiki usahihi wa kumbukumbu za madai yote kwa kulinganisha na makusanyo; uhifadhi na uwekaji wa fedha hizo benki. Muhtasari wa vyanzo hivi unaelezewa katika **Jedwali Na. 5-2** na **Kiambatisho Na. 5-2** kinatoa muhtasari wa mapato ambayo hayajakusanywa.

**Jedwali Na. 5-2: Vyanzo vya mapato visivyokusanywa**

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mazao | 23 | 4,960,666,135 |
| 2. | Kodi za pango | 57 | 3,712,527,924 |
| 3. | Mauzo ya viwanja | 18 | 3,536,649,945 |
| 4. | Leseni za vileo | 47 | 961,863,718 |
| 5. | Vibanda/vizimba vya masoko | 13 | 852,199,103 |
| 6. | Ada ya machinjio/chanjo | 3 | 158,646,200 |
| 7. | Ushuru wa hoteli | 28 | 113,619,040 |
| | **Jumla** | | **14,296,172,065** |

Mapato ambayo hayajakusanywa na mamlaka za serikali za mitaa yanaweza kusababisha hasara kutokana na juhudi zisizoridhisha za kukusanya fedha hizo.

**Nanazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika (a) ziweke mifumo madhubuti ya utambuzi na ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyote vya mapato; na (b) zihakikishe ukusanyaji wa mapato ambayo hayajarejeshwa unafanyika.**

## 5.3 Tozo za Shilingi Bilioni 6.03 za Uchimbaji na Usafirishaji wa Madini ya Ujenzi ambazo Hazikukusanywa

Katika ukaguzi wa tozo nilibaini kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe inamdai kiasi cha shilingi bilioni 6.80 mkandarasi anayehusika na uchimbaji na usafirishaji wa madini ya ujenzi kutoka Kijiji cha Kibwemwenda ikiwa ni kwa mujibu wa Vifungu vya 56 (2) na 57 vya Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kijiji inayosomwa pamoja na Kiambatisho "E" vinavyoitaka halmashauri kukusanya shilingi 6,000 kwa tani moja ya mchanga, kokoto au mawe.

Kutofuatilia na kuhakikisha malipo hayo yanafanyika kunaweza kusababisha hasara kwa upotevu wa fedha hizo za mapato.

**Ninaishauri mamlaka husika ya serikali za mitaa (a) iingie mkataba na mlipakodi ili kuhakikisha tozo zinalipwa kwa wakati; na (b) ihakikishe tozo ambazo hazijalipwa zinarejeshwa na mkandarasi husika.**

## 5.4 Miamala ya Shilingi bilioni 8.36 ya Madai Mbalimbali ya Mapato Isiyosuluhishwa

Agizo la 38 (1) na (6) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009,

linamtaka mwekahazina kuwajibika kufanya taratibu stahiki za usimamizi wa fedha na uhasibu ili kuhakiki usahihi wa kumbukumbu za fedha zote zinazodaiwa na mamlaka kwa kulinganisha na makusanyo, uhifadhi na uwekaji wa fedha hizo benki. Kamati ya fedha na mipango inapaswa kubainisha kwa uwazi taratibu za kufuatilia madai ambayo bado hayajalipwa na mbinu za utekelezaji wa malipo. Pia, Aya ya 6.7 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 unataka utengenezaji wa hati za madai na usimamizi wa madai ya mapato ufanyike kupitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato. Kisha, walipakodi wenye madeni wafuatiliwe kupitia mfumo huo na kujulishwa kwa wakati ili kuhakikisha malipo yanafanyika kupitia benki au kielekitroniki na kuhuishwa katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato mara tu baada ya malipo kufanyika.

Ukaguzi katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ulibaini kuwa, kiasi cha shilingi bilioni 8.36 hakikukusanywa katika mamlaka 62 za serikali za mitaa kutoka vyanzo mbalimbali bila kubainisha sababu, kinyume na miongozo iliyotajwa hapo juu. Bila udhibiti na juhudi za kutosha, kuna uwezekano wa ukusanyaji wa mapato chini ya malengo. **Jedwali Na. 5-3** linaonesha wadaiwa wa mapato mbalimbali.

**Jedwali Na. 5-3: Wadaiwa wa mapato mbalimbali**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Simanjiro | 1,118,857,668 | 32. | H/W Bagamoyo | 57,054,073 |
| 2. | H/W Kongwa | 786,384,098 | 33. | H/W Nyasa | 55,268,844 |
| 3. | H/W Kilolo | 570,299,081 | 34. | H/W Monduli | 51,812,500 |
| 4. | H/W Madaba | 477,822,413 | 35. | H/Mji Bariadi | 49,235,333 |
| 5. | H/M Bukoba | 472,561,421 | 36. | H/W Iramba | 48,858,200 |
| 6. | H/W Siha | 438,400,535 | 37. | H/W Itilima | 43,878,674 |
| 7. | H/W Morogoro | 355,612,276 | 38. | H/W Ngara | 43,798,635 |
| 8. | H/W Busega | 319,433,118 | 39. | H/W Sengerema | 42,157,700 |
| 9. | H/Mji Geita | 256,184,930 | 40. | H/W Mvomero | 41,436,673 |
| 10. | H/M Singida | 219,142,375 | 41. | H/Mji Nanyamba | 41,324,805 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 11. | H/M Morogoro | 201,425,855 | 42. | H/W Kyerwa | 39,913,891 |
| 12. | H/W Kibaha | 195,315,502 | 43. | H/W Pangani | 33,124,511 |
| 13. | H/W Same | 189,886,012 | 44. | H/W Newala | 32,701,098 |
| 14. | H/M Shinyanga | 177,924,184 | 45. | H/W Ileje | 25,739,413 |
| 15. | H/W Bariadi | 169,551,904 | 46. | H/W Msalala | 24,322,532 |
| 16. | H/W Igunga | 161,702,608 | 47. | H/W Bukombe | 23,340,578 |
| 17. | H/Mji Kibaha | 143,330,146 | 48. | H/W Nsimbo | 20,795,459 |
| 18. | H/W Mpanda | 137,210,362 | 49. | H/W Songwe | 16,807,995 |
| 19. | H/W Meatu | 124,166,986 | 50. | H/Mji Newala | 15,420,000 |
| 20. | H/W Sikonge | 113,548,950 | 51. | H/M Moshi | 14,635,187 |
| 21. | H/Mji Korogwe | 108,900,500 | 52. | H/W Kilosa | 11,571,075 |
| 22. | H/W Ngorongoro | 107,102,071 | 53. | H/W Kishapu | 10,674,973 |
| 23. | H/W Meru | 90,679,096 | 54. | H/W Wanging'ombe | 8,678,000 |
| 24. | H/W Songea | 88,819,748 | 55. | H/W Namtumbo | 7,965,000 |
| 25. | H/M Tabora | 86,716,397 | 56. | H/W Buhigwe | 6,537,615 |
| 26. | H/W Kasulu | 83,472,753 | 57. | H/W Mkuranga | 6,400,000 |
| 27. | H/W Hai | 83,331,331 | 58. | H/W Itigi | 6,038,275 |
| 28. | H/M Mpanda | 80,467,018 | 59. | H/W Rombo | 3,939,780 |
| 29. | H/W Chalinze | 77,501,096 | 60. | H/W Chato | 3,757,687 |
| 30. | H/M Mtwara | 68,062,808 | 61. | H/W Maswa | 2,095,896 |
| 31. | H/W Tandahimba | 65,702,000 | 62. | H/W Singida | 547,230 |
| | **Jumla** | | | | **8,359,346,874** |

Ingawa mamlaka za serikali za mitaa zimefanya jitihada za kupunguza kiasi cha wadaiwa hawa kwa miaka mitatu mfululizo, kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 5-3** hapa chini; hata hivyo, kiasi cha shilingi bilioni 8.36 kinaonesha kuwa bado kuna haja ya jitihada zaidi kuchukuliwa ili kuondoa uwapo wa wadaiwa mbalimbali ambao hawajapatiwa ufumbuzi.

**Kielelezo Na. 5-3: Mwenendo wa madai**



**Ninapendekeza kwamba menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa (a) ziweke udhibiti ili kuhakikisha kwamba wadaiwa wote wanahakikiwa kabla ya kufanya marekebisho na hatimaye kukusanya mapato kwa madai yanayostahili; na (b) kuwe na utaratibu wa kufanya usuluhishi angalau kila mwezi kuhusiana na wadaiwa husika ili kupunguza vihatarishi vya upotevu na kuhakikisha usimamizi madhubuti katika mapato.**

## 5.5 Ukusanyaji hafifu wa mapato kutokana na kukosekana kwa ufanisi wa Sheria Ndogo

Sheria ndogo za Halmashauri zimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 89 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 (Iliyorejewa 2019) na Kifungu cha 153(1) na (2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sheria, Sura ya 287 (iliyorejewa 2019). Mapitio yangu yamebaini kuwa, mamlaka 12 za serikali za mitaahazikuwa na sheria ndogo zilizohuishwa ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali, pia Menejimenti za baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa hazijahuisha kwa wakati sheria zake ndogo, kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5-4**.

**Jedwali Na. 5-4: Halmashauri zisizohuisha sheria ndogo**

| Na. | Jina la Mamlaka za Serikali za Mitaa | Eneo | Uhalisia | Kiasi Kinachohusishwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Busega | Madini ya ujenzi | Hazijaanzishwa | 185,374,650 |
| 2. | H/M Kinondoni | Ukaguzi wa mabwawa ya kuogelea | Hazijaanzishwa | 250,800,000 |
| 3. | H/W Kongwa | Kodi ya Minara ya simu | Hazijaanzishwa | 14,834,700 |
| 4. | H/M Lindi | Ushuru wa mazao | Hazijahuishwa | Hakuna |
| 5. | H/W Lushoto | Vileo | Hazijaanzishwa | Hakuna |
| 6. | H/W Meru | Vibali vya biashara | Hazijahuishwa | Hakuna |
| 7. | H/M Musoma | Kodi ya nyumba | Hazijahuishwa | Hakuna |
| 8. | H/Jiji Mwanza | Uzoaji Taka | Hazijahuishwa | Hakuna |
| 9. | H/W Ngorongoro | Kambi na mageti | Hazijahuishwa | Hakuna |
| | | Uzoaji Taka | Hazijaanzishwa | Hakuna |
| 10. | H/M Songea | Mazao ya misitu, bustani na samaki | Hazijaanzishwa | 60,960,545 |

| Na. | Jina la Mamlaka za Serikali za Mitaa | Eneo | Uhalisia | Kiasi Kinachohusishwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| | | Madini ya ujenzi na kodi za nyumba | Hazijaidhinishwa | 91,981,100 |
| 11. | H/W Moshi | Madini ya ujenzi | Hazijaanzishwa | Hakuna |
| 12. | H/W Rombo | Magogo ya mitiki | Hazijaanzishwa | 97,743,225 |

Ukosefu wa sheria ndogo ambazo zimeboreshwa na kuidhinishwa katika usimamizi wa mapato, umekuwa kikwazo kwa Mamlaka za serikali za Mitaa husika katika kukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka husika za serikali za mitaa kuanzisha na kuboresha sheria zao ndogo ili kuendana na mabadiliko muhimu katika vyanzo vya mapato ili kukusanya ipasavyo katika maeneo yao.**

## 5.6 Kutohuishwa kwa Taarifa za Bajeti ya Mapato katika Mfumo wa Mapato Shilingi Bilioni 11.96

Aya ya 5.2 cha Mwongozo wa ukusanyaji mapato wa mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019, inazitaka Halmashauri kuweka malengo yanayoweza kufikiwa huku ikizingatia mfumuko wa bei, ongezeko la watu na mabadiliko ya sheria na kanuni katika mwaka wa bajeti. Pia, Kifungu cha 3.2.9.2 cha Mwongozo wa Mtumiaji (toleo la 0.1) la Mfumo wa taarifa za Ukusanyaji Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kinahitaji bajeti ya kila chanzo cha mapato kuingizwa katika Mfumo huo.

Nilipitia Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali wa Mitaa na kubaini kutokuwapo kwa taarifa za bajeti ya vyanzo vya mapato vyenye jumla ya shilingi bilioni 11.96 katika mamlaka nane za serikali za mitaa. Hali hii ni kinyume na miongozo iliyotajwa hapo juu. Maelezo ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo taarifa za bajeti hazijahuishwa katika Mfumo yameoneshwa katika **Jedwali Na. 5-5**.

**Jedwali Na. 5-5: Taarifa za bajeti zisizohuishwa katika mfumo wa mapato**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Mpwapwa | 2,671,600,000 |
| 2. | H/Mji Bariadi | 1,841,979,009 |
| 3. | H/W Bariadi | 1,665,360,650 |
| 4. | H/W Mtama | 1,607,651,487 |
| 5. | H/W Same | 1,483,611,630 |
| 6. | H/W Busega | 1,362,315,880 |
| 7. | H/W Itilima | 698,514,932 |
| 8. | H/W Simanjiro | 626,695,597 |
| | **Jumla** | **11,957,729,185** |

Kutohuisha taarifa za bajeti katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa huongeza hatari ya makosa ya kibinadamu na kukosa usahihi katika taarifa za fedha za taasisi husika, hasa wakati wa kutathmini ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo mbalimbali.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa bajeti kutoka vyanzo vyote vya mapato zinawekwa katika Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa ili kuimarisha udhibiti wa kibajeti katika makusanyo ya mapato na kutumika kama nyenzo ya mapitio ya utendaji.**

## 5.7 Fedha Shilingi Bilioni 3.31 Zilizowasilishwa na Mawakala wa Ukusanyaji Mapato chini ya Kiwango Kilichokubaliwa

Kifungu cha 26 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorejewa mwaka 2019) kinamtaka mtu anayestahili kuteuliwa na mamlaka za serikali za mitaa, kukusanya na kupokea kiasi stahiki kutoka kwa kila mlipakodi katika eneo ambalo amepangiwa; na kuhakikisha kiasi chote kilichokusanywa kinalipwa kwa mamlaka ya serikali ya mtaa inayohusika.

Nilipitia usimamizi wa mapato na kubaini kuwa, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa ziliingia mikataba 101 na mawakala wa kukusanya mapato katika vyanzo mbalimbali vyenye thamani ya shilingi bilioni 12.3. Mapitio zaidi ya Mfumo wa Taarifa za Ukusanyaji

wa Mapato ya Serikali za Mitaa yalibaini kuwa, ni shilingi bilioni 8.99 pekee ndizo zilizowasilishwa kwa mamlaka za serikali za mitaa, na hivyo kuacha shilingi bilioni 3.31 hazijawasilishwa kwa mujibu wa mikataba. **Jedwali Na. 5-6** linaonesha orodha ya halmashauri za wilaya ambazo makusanyo hayakuwasilishwa.

**Jedwali Na. 5-6: Kiasi kisichowasilishwa na mawakala kimkataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Mikataba | Kiasi (Sh.) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kimkataba | Kilichowasilishwa | Kinachodaiwa |
| 1. | H/Jiji Mwanza | 13 | 2,962,881,600 | 1,967,597,740 | 995,283,860 |
| 2. | H/Jiji Dar es Salaam | 13 | 3,453,699,114 | 2,903,908,659 | 549,790,455 |
| 3. | H/W Muheza | 3 | 1,224,000,000 | 790,737,934 | 433,262,066 |
| 4. | H/W Buchosa | 21 | 1,002,880,000 | 704,143,372 | 298,736,628 |
| 5. | H/W Ulanga | 2 | 1,530,421,000 | 1,260,611,085 | 269,809,915 |
| 6. | H/W Tarime | 2 | 297,000,000 | 91,610,000 | 205,390,000 |
| 7. | H/M Shinyanga | 2 | 504,000,000 | 327,905,114 | 176,094,886 |
| 8. | H/Jiji Arusha | 31 | 805,419,400 | 643,048,408 | 162,370,992 |
| 9. | H/W Bukombe | 5 | 268,285,000 | 177,921,310 | 90,363,690 |
| 10. | H/Jiji Tanga | 6 | 156,950,000 | 71,187,550 | 85,762,450 |
| 11. | H/W Rufiji | 1 | 57,000,000 | 27,000,000 | 30,000,000 |
| 12. | H/M Musoma | 2 | 35,280,000 | 22,520,000 | 12,760,000 |
| | **Jumla** | **101** | **12,297,816,114** | **8,988,191,172** | **3,309,624,942** |

Hakuna hatua zilizochukuliwa na mamlaka za serikali za mitaa kuhusiana na kiasi ambacho hakijakusanywa kwa mujibu wa mikataba. Hali hii ilitokana na kutokuwapo kwa kipengele katika mikataba iliyosainiwa kinachoelezea hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wakala atakayeshindwa kufikia malengo ya urejeshaji kwa mujibu wa mkataba.

Kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kupitia mawakala kunazuia utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninapendekeza menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa katika siku zijazo (a) zifanye upembuzi yakinifu unaoakisi uhalisia wa malengo ya makusanyo katika vyanzo vya mapato, huku zikihakikisha mikataba inaeleza wazi hatua zitakazochukuliwa dhidi ya mawakala watakaoshindwa kuwasilisha kiasi**

**kilichokubaliwa; na (b) kwa mikataba ambayo tayari ina vifungu vinavyoeleza hatua dhidi ya mawakala walioshindwa kuwasilisha makusanyo kulingana na makubaliano, ninashauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuchukua hatua stahiki dhidi mawakala hao ili wawasilishe mapato ambayo hayajarejeshwa.**

## 5.8 Hasara ya Mapato Shilingi Milioni 393.92 Kutokana na Kumtunuku Mzabuni Mwenye Kiasi Kidogo cha Mapato katika Zabuni

Kanuni ya 212 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inaitaka zabuni itakayofanikiwa katika makusanyo ya mapato iwe ni ile yenye bei ya juu kabisa miongoni mwa zabuni zilizotathminiwa.

Mapitio yangu ya nyaraka za mwenendo wa zabuni ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali yalibaini kuwa, timu ya tathmini ilipendekeza wazabuni wa bei ya chini badala ya wazabuni wa bei ya juu zaidi, hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya shilingi milioni 393.92 kinyume na kanuni iliyotajwa hapo juu. **Jedwali Na. 5-7** linaonesha orodha ya wazabuni waliotunukiwa kwa kiwango cha chini.

**Jedwali Na. 5-7: Wazabuni waliotunukiwa kwa kiwango cha chini**

| Na | Namba ya Mkataba | Maelezo ya Zabuni | Zabuni zilizotunukiwa (Sh.) | Zabuni ziliokataliwa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | LGA/076/R/2020/2021/09 | Ushuru wa mazao kwa Kata ya Mapogoro | 98,400,000 | 300,000,000 | 201,600,000 |
| 2. | LGA/076/R/2020/2021/12 | Ushuru wa mazao kwa Kata Utengule Usangu | 18,720,000 | 43,636,364 | 24,916,364 |
| 3. | LGA/076/R/2020/2021/14 | Ushuru wa mazao kwa Kata ya Mwatenga | 17,400,000 | 42,000,000 | 24,600,000 |
| 4. | LGA/076/R/2020/2021/16 | Ushuru wa mazao kwa Kata Ruiwa | 16,200,000 | 54,000,000 | 37,800,000 |

| Na | Namba ya Mkataba | Maelezo ya Zabuni | Zabuni zilizotunukiwa (Sh.) | Zabuni ziliokataliwa (Sh.) | Tofauti (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. | LGA/076/R/2020/2021/18 | Ushuru wa mazao kwa Kata Igurusi | 11,400,000 | 44,400,000 | 33,000,000 |
| 6. | LGA/076/R/2020/2021/20 | Mnada wa mifugo Imalilo Songwe | 24,000,000 | 48,000,000 | 24,000,000 |
| 7. | LGA/076/R/2020/2021/24 | Mnada wa mifugo Rujewa | 36,000,000 | 84,000,000 | 48,000,000 |
| | **Jumla** | | **222,120,000** | **616,036,364** | **393,916,364** |

Halmashauri ilipoteza shilingi milioni 393.92 kutokana na kutozingatiwa kwa taratibu za manunuzi kwa kutomtunuku mzabuni aliyetathminiwa kwa bei ya juu zaidi katika zabuni ya makusanyo ya mapato.

**Ninapendekeza kwamba menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa katika siku zijazo zihakikishe mzabuni wa bei ya juu zaidi katika ukusanyaji wa mapato ndiye anayepewa zabuni ya kukusanya mapato kama inavyotakiwa na Kanuni ya 212 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.**

## 5.9 Mapato ya Leseni za Biashara Kiasi cha Shilingi Bilioni 9.01 Ambayo Hayakukusanywa

Kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Leseni za Biashara, Sura ya 208 kinasema kwamba, hakuna mtu atakayeendesha biashara yoyote Tanzania bila kuwa na leseni halali ya biashara na biashara husika inapaswa kufanywa mahali palipotajwa katika leseni.

Kinyume na matakwa ya sheria, tathmini ya kumbukumbu za leseni za biashara ilibaini kuwa taasisi za biashara katika Halmashauri 94 zilifanya kazi na leseni za biashara zilizoisha muda wake zenye thamani ya shilingi bilioni 9.01. Maelezo yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 5-8**

### Jedwali Na. 5-8: Madai yasiyokusanywa kutoka leseni za biashara

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Mji Kibaha | 600,310,820 | 48. | H/W Itigi | 53,696,000 |
| 2. | H/W Manyoni | 461,511,000 | 49. | H/W Monduli | 52,217,500 |
| 3. | H/M Morogoro | 451,354,560 | 50. | H/W Hai | 46,743,000 |
| 4. | H/W Moshi | 445,627,500 | 51. | H/W Handeni | 45,324,000 |
| 5. | H/W Arusha | 439,454,550 | 52. | H/W Kwimba | 44,883,000 |
| 6. | H/W Urambo | 340,107,700 | 53. | H/W Mkuranga | 42,147,000 |
| 7. | H/W Chato | 296,079,400 | 54. | H/W Mlele | 39,500,000 |
| 8. | H/W Kaliua | 292,156,700 | 55. | H/W Mbinga | 37,487,000 |
| 9. | H/W Bukombe | 276,434,400 | 56. | H/Mji Makambako | 36,655,000 |
| 10. | H/W Karatu | 248,469,000 | 57. | H/W Biharamulo | 35,819,500 |
| 11. | H/W Meru | 225,288,500 | 58. | H/M Shinyanga | 35,418,500 |
| 12. | H/W Mpwapwa | 220,075,124 | 59. | H/W Nanyumbu | 34,394,000 |
| 13. | H/W Songea | 197,427,900 | 60. | H/W Kisarawe | 31,937,500 |
| 14. | H/W Mbozi | 185,543,000 | 61. | H/W Bumbuli | 31,697,000 |
| 15. | H/W Nzega | 178,520,800 | 62. | H/W Kalambo | 30,579,900 |
| 16. | H/Mji Handeni | 169,566,000 | 63. | H/Jiji Mwanza | 29,020,000 |
| 17. | H/W Mkinga | 158,207,060 | 64. | H/W Makete | 27,048,000 |
| 18. | H/M Mtwara | 147,780,000 | 65. | H/Mji Nzega | 27,047,480 |
| 19. | H/W Sengerema | 144,672,400 | 66. | H/W Kilolo | 26,747,000 |
| 20. | H/W Kongwa | 142,734,000 | 67. | H/W Karagwe | 26,587,000 |
| 21. | H/Mji Njombe | 116,327,000 | 68. | H/W Mpanda | 24,335,445 |
| 22. | H/W Mbarali | 116,289,900 | 69. | H/M Ilemela | 23,311,250 |
| 23. | H/W Kilosa | 112,199,900 | 70. | H/Mji Korogwe | 21,225,000 |
| 24. | H/W Korogwe | 109,149,461 | 71. | H/W Itilima | 20,252,000 |
| 25. | H/W Meatu | 108,367,000 | 72. | H/W Momba | 20,135,000 |
| 26. | H/M Tabora | 106455725 | 73. | H/W Newala | 18,920,000 |
| 27. | H/W Namtumbo | 106,396,000 | 74. | H/W Longido | 18,585,000 |
| 28. | H/W Kondoa | 103,448,917 | 75. | H/Jiji Dodoma | 18,093,550 |
| 29. | H/M Kahama | 103,288,000 | 76. | H/W Pangani | 18,068,000 |
| 30. | H/M Moshi | 96,904,000 | 77. | H/W Morogoro | 17,822,500 |
| 31. | H/Mji Bariadi | 94,917,000 | 78. | H/Mji Nanyamba | 16,385,000 |
| 32. | H/Mji Mbinga | 94,489,000 | 79. | H/W Kyerwa | 15,215,000 |
| 33. | H/Jiji Tanga | 84,004,000 | 80. | H/Mji Newala | 15,130,000 |
| 34. | H/W Nyasa | 81,955,980 | 81. | H/W Ushetu | 14,938,000 |
| 35. | H/Mji Kondoa | 77,349,920 | 82. | H/W Songwe | 14,697,500 |
| 36. | H/Mji Mafinga | 75,830,000 | 83. | H/W Kakonko | 14,505,000 |
| 37. | H/W Gairo | 73,596,931 | 84. | H/W Ludewa | 12,323,000 |
| 38. | H/M Kigoma/Ujiji | 72,700,000 | 85. | H/W Mkalama | 11,020,000 |
| 39. | H/Mji Geita | 70,803,000 | 86. | H/W Masasi | 9,600,000 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 40. | H/W Mbogwe | 67,000,000 | 87. | H/W Tandahimba | 9,250,000 |
| 41. | H/W Nkasi | 66,110,000 | 88. | H/W Same | 7,850,000 |
| 42. | H/W Kilindi | 63,814,000 | 89. | H/W Chalinze | 7,650,000 |
| 43. | H/W Mlimba | 61,133,000 | 90. | H/M Singida | 7,460,000 |
| 44. | H/Mji Mbulu | 59,040,000 | 91. | H/W Ikungi | 7,440,000 |
| 45. | H/W Ukerewe | 55,044,405 | 92. | H/Mji Tarime | 5,008,000 |
| 46. | H/W Simanjiro | 54,760,000 | 93. | H/W Serengeti | 2,900,000 |
| 47. | H/W Hanang | 54,118,000 | 94. | H/W Mtwara | 818,000 |
| | **Jumla** | | | | **9,014,697,178** |

Aidha, tathmini yangu katika mfumo wa taarifa wa usimamizi wa mapato imebaini kuwa, Halmashauri 14 zilitoa leseni za shilingi bilioni 1.93 wakati fedha zilizokusanywa kutokana na utoaji wa leseni hizo ni shilingi bilioni 2.64, ikimaanisha kuwa malipo ya shilingi milioni 718.28 yanahusika kwa biashara zinazofanywa bila leseni halali. **Jedwali Na. 5-9** linatoa maelezo zaidi.

**Jedwali Na. 5-9: Leseni za biashara zilizotolewa nje ya mfumo**

| Na. | Jina la Mamlaka za serikali za Mitaa | Kiasi kilichokusanywa (Sh.) | Leseni zilizotolewa (Sh.) | Leseni zisizotolewa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dodoma | 1,679,430,637 | 1,496,357,792 | 183,072,845 |
| 2. | H/Mji Bunda | 101,610,300 | 0 | 101,610,300 |
| 3. | H/W Kaliua | 118,909,220 | 59,313,700 | 59,595,520 |
| 4. | H/W Ngorongoro | 52,503,020 | 0 | 52,503,020 |
| 5. | H/W Shinyanga | 52,754,000 | 865,000 | 51,889,000 |
| 6. | H/W Karatu | 137,051,750 | 87,354,000 | 49,697,750 |
| 7. | H/W Kilosa | 193,179,760 | 145,697,700 | 47,482,060 |
| 8. | H/W Kigoma | 60,061,732 | 16,447,000 | 43,614,732 |
| 9. | H/W Mpanda | 50,830,000 | 15,161,000 | 35,669,000 |
| 10. | H/W Monduli | 100,577,000 | 78,129,800 | 22,447,200 |
| 11. | H/W Meatu | 22,317,400 | 0 | 22,317,400 |
| 12. | H/W Kondoa | 17,090,000 | 153,000 | 16,937,000 |
| 13. | H/W Serengeti | 23,529,000 | 6,978,000 | 16,551,000 |
| 14. | H/W Mlele | 33,790,000 | 18,895,000 | 14,895,000 |
| | **Jumla** | **2,643,633,819** | **1,925,351,992** | **718,281,827** |

Hali hiyo ilisababisha kutokusanywa kwa mapato yatokanayo na leseni za biashara; hivyo, mamlaka za serikali za mitaa husika hazikuweza kutekeleza shughuli zilizolengwa.

**Nazishauri Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kushirikiana na Ofisi za Kata na Vijiji ili kuanzisha kanzidata za wafanya biashara waliopo ndani ya maeneo yao na kuzihuisha katika mfumo wa LGRCIS na kuhakikisha usuluhishi wa kanzidata na wafanyabiashara wenye leseni unafanyika angalau kila mwezi ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa leseni za biashara.**

## 5.10 Ushuru wa Huduma wa shilingi bilioni 1.91 kutokusanywa kutokana na Ukosefu wa Mfumo wa kielektroniki wa kupeana taarifa za Mauzo ghafi kati ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na TRA

Aya ya 6.6.1(iii & iv) ya Mwongozo wa usimamizi wa Mapato ya mamlaka za serikali za mitaa wa mwaka 2019 inafafanua mkakati na taratibu za ukusanyaji wa ushuru wa huduma ukijumuisha utoaji wa fomu ya kukiri jumla ya mauzo ghafi ambayo hujazwa na mlipakodi na inaweza kutumika katika utozaji wa ushuru wa huduma.

Ukaguzi wa walipa ushuru wa huduma 15 katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ulibaini kuwa, jumla ya mauzo ghafi ya shilingi trilioni 1.33 yaliyohuishwa katika mfumo wa usimamizi wa mapato, yanatofautiana kwa shilingi bilioni 640 kutoka shilingi trilioni 1.97 zilizoandikwa katika majalada yanayohusiana na makadirio ya kodi ya ongezeko la thamani. Ushuru wa huduma unaotarajiwa kukusanywa kutokana na mauzo ya shilingi bilioni 640 ni shilingi bilioni 1.92. Kwa maoni yangu, kukosekana kwa fomu za kukiri mauzo ghafi kunazuia uthibitishaji wa uhalali wa kutoza ushuru wa huduma.

Hii inatokana na kukosekana kwa mfumo wa kielektroniki wa kubadilishana taarifa za mauzo ghafi kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kurahisisha tathmini katika ukokotoaji katika ushuru wa huduma.

Pia, nilibaini kuwa Halmashauri 43 zilikusanya ushuru wa huduma wenye jumla ya shilingi bilioni 9.01 bila kupata ushahidi wa taarifa za mauzo ghafi kutoka mamlaka husika au taasisi husika ili kuthibitisha kiasi kilichokusanywa. Maelezo zaidi ya ushuru wa huduma uliokusanywa bila vithibitisho vya mauzo ghafi yametolewa katika **Jedwali Na. 5-10.**

**Jedwali Na. 5-10: Makusanyo ya ushuru wa huduma bila uthibitisho**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Temeke | 2,389,435,326 | 23. | H/W Urambo | 76,270,252 |
| 2. | H/W Songwe | 872,694,259 | 24. | H/W Uvinza | 75,166,226 |
| 3. | H/W Kilwa | 749,369,267 | 25. | H/W Mtama | 73,647,756 |
| 4. | H/M Iringa | 554,956,920 | 26. | H/W Bahi | 55,379,724 |
| 5. | H/W Missenyi | 495,678,932 | 27. | H/W Busega | 54,867,923 |
| 6. | H/W Moshi | 434,274,721 | 28. | H/W Mufindi | 54,659,518 |
| 7. | H/W Kilosa | 408,996,984 | 29. | H/W Ngorongoro | 52,445,609 |
| 8. | H/M Songea | 306,516,591 | 30. | H/W Nzega | 51,589,270 |
| 9. | H/W Meru | 228,199,218 | 31. | H/W Lushoto | 50,123,163 |
| 10. | H/W Serengeti | 224,957,608 | 32. | H/W Iramba | 49,800,345 |
| 11. | H/W Hai | 199,776,983 | 33. | H/W Kwimba | 43,406,745 |
| 12. | H/W Mkuranga | 149,170,768 | 34. | H/M Morogoro | 37,296,117 |
| 13. | H/M Singida | 142,570,878 | 35. | H/W Kaliua | 34,011,454 |
| 14. | H/W Muheza | 142,310,981 | 36. | H/W Itilima | 31,171,455 |
| 15. | H/W Iringa | 134,686,893 | 37. | H/M Moshi | 27,316,290 |
| 16. | H/M Mpanda | 126,720,339 | 38. | H/M Nachingwea | 26,483,178 |
| 17. | H/W Rombo | 121,427,128 | 39. | H/W Ngara | 19,496,969 |
| 18. | H/M Kigamboni | 114,659,888 | 40. | H/W Butiama | 15,599,307 |
| 19. | H/W Uyui | 101,532,973 | 41. | H/W Nyasa | 12,593,685 |
| 20. | H/W Kishapu | 92,996,657 | 42. | H/W Liwale | 12,436,110 |
| 21. | H/W Kibaha | 84,844,445 | 43. | H/W Ukerewe | 3,379,093 |
| 22. | H/W Bunda | 76,571,554 | | **Jumla** | **9,009,489,502** |

Ushuru wa huduma unaweza kuwa haukukusanywa ipasavyo kutokana na kukosekana kwa taarifa za mauzo ghafi ambazo zingeweza kutumika katika kukokotoa kiasi stahiki cha ushuru wa huduma ambacho kinatakiwa kulipwa na mlipa kodi.

**Ninapendekeza kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika siku zijazo zihuishe mfumo wa kielektroniki utakaowezesha kupeana taarifa za mauzo ghafi au taarifa nyingine zitakazorahisisha ukokotoaji wa kiasi kinachostahili kulipwa kama ushuru wa huduma. Pia, nawasihi menejimenti ya mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kwa kutumia fomu za kukiri mauzo ghafi inayojazwa na mlipakodi kabla ya kumtoza.**

## 5.11 Kutokuwa na Ufanisi Katika Makadirio na Ukusanyaji wa Ushuru wa Huduma Shilingi Bilioni 4.57

Vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] kama iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha, 2020 (Sheria Na. 8 ya 2020) ambavyo vinaeleza kuwa chanzo cha mapato ni pamoja fedha zote zinazotokana na ushuru wa huduma zinazolipwa na taasisi au mtu binafsi anayeendesha biashara, na mwenye leseni halali ya biashara ambayo mauzo ghafi kwa mwaka yanazidi shilingi milioni nne, na utozaji ni kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya mauzo ghafi baada ya kupunguza kodi ya ongezeko la thamani na ushuru wa bidhaa: ili mradi, matawi ya taasisi husika yatalipa ushuru wa huduma katika maeneo ya Halmashauri.

Nimetathmini ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru wa huduma na kubaini kuwa, Halmashauri 31 hazikukusanya ushuru wa huduma wa kiasi cha shilingi bilioni 4.57 kutoka kwa wafanyabiashara wanaofanya kazi ndani ya mamlaka ya Halmashauri husika. Hii inatokana na kukosekana na udhibiti thabiti wa mapato ya ndani na kukosekana kwa kanzidata ya wafanyabiashara iliyohuishwa. Orodha ya Halmashauri ambazo hazikukusanya ushuru wa huduma imeoneshwa katika **Jedwali Na. 5-11.**

**Jedwali Na. 5-11: Ushuru wa huduma usiokusanywa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Rufiji | 1,384,598,310 | 17. | H/W Meatu | 28,042,350 |
| 2. | H/W Songwe | 485,557,289 | 18. | H/Jiji Tanga | 25,008,803 |
| 3. | H/W Mkuranga | 469,550,922 | 19. | H/W Moshi | 22,754,940 |
| 4. | H/W Msalala | 412,032,887 | 20. | H/Mji Korogwe | 21,254,266 |
| 5. | H/M Tabora | 381,973,273 | 21. | H/Mji Tunduma | 16,760,649 |
| 6. | H/W Rungwe | 380,608,080 | 22. | H/M Ubungo | 10,705,507 |
| 7. | H/Jiji Dar es Salaam | 181,885,286 | 23. | H/Mji Tarime | 10,597,950 |
| 8. | H/W Mbinga | 144,310,211 | 24. | H/W Hanang | 9,093,669 |
| 9. | H/W Karagwe | 113,172,969 | 25. | H/W Mbozi | 7,915,966 |
| 10. | H/M Ilemela | 91,717,531 | 26. | H/W Ruangwa | 7,137,267 |
| 11. | H/W Gairo | 87,082,454 | 27. | H/W Monduli | 5,904,688 |
| 12. | H/M Shinyanga | 77,323,407 | 28. | H/W Mpanda | 4,291,764 |
| 13. | H/W Kyela | 66,249,214 | 29. | H/W Mbarali | 3,621,630 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 14. | H/M Moshi | 40,922,790 | 30. | H/W Nzega | 1,544,199 |
| 15. | H/W Chalinze | 37,423,275 | 31. | H/W Kishapu | 1,249,351 |
| 16. | H/Mji Njombe | 35,301,217 | | **Jumla** | **4,565,592,114** |

Aidha, mapitio yangu ya usimamizi wa ushuru wa huduma katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe yalibaini kuwa, kikao cha kamati ya fedha cha tarehe 27 Novemba, 2016, kilipanga viwango vya makusanyo kuwa ni kuanzia shilingi 10,000 hadi 40,000 kwa mwaka kinyume na matakwa ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa iliyotajwa hapo juu.

Kwa maoni yangu, kiwango cha kodi mpaka chenye kuanzia asilimia 0 mpaka asilimia 0.3 kinaweza kutoa mwanya wa ukwepaji wa ushuru wa huduma.

Mamlaka za serikali za mitaa husika zimeshindwa kukusanya ushuru wa huduma kama chanzo cha mapato, hali ambayo inaathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.

**Ninapendekeza Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha kuwa, kanzidata za biashara zinahuishwa na ufuatiliaji wa kutosha unafanyika kupitia ngazi zote ikiwa ni pamoja na Kata na Vijiji ili kukusanya ushuru wa huduma kwa Halmashauri kulingana na matakwa ya vifungu vya 6(1) (u) na 7(1) (y) vya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] kama iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha, 2020 (Sheria Na. 8 ya 2020).**

## 5.12 Madai ya Ada ya Uzoaji Taka yasiyokuwa na Viambatisho Kiasi cha Shilingi Milioni 191.02

Agizo la 38 (1) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, linamtaka Mweka Hazina kuwajibika kufanya taratibu stahiki za usimamizi wa fedha na uhasibu ili kuhakiki usahihi wa kumbukumbu za fedha zote zinazodaiwa na Halmashauri kwa kulinganisha na makusanyo; uhifadhi na uwekaji wa fedha hizo benki.

Mapitio ya rejesta za mawakala zilizowasilishwa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam ili kuhakiki uhalali na ukamilifu wa ada za uzoaji wa taka zilizopo katika madai yaliyopo katika taarifa za fedha, yalibaini tofauti ya shilingi milioni 191.02 bila vielelezo vya kutanabaisha tofauti hizo. Hii ni kutokana na kutofanya usuluhishi wa mara kwa mara na kutohuisha kumbukumbu kati ya kiasi kilichooneshwa katika rejesta ya ada za uzoaji/ukusanyaji taka na mchanganuo unaoambatanishwa na taarifa za fedha. Maelezo ya tofauti katika takwimu zilizoripotiwa yameelezewa katika **Jedwali Na. 5-12**.

**Jedwali Na. 5-12: Madai ya ada za ukusanyaji wa taka**

| Na. | Namba ya mkataba | Madai yanayotofautiana na rejesta (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 18 | 14,976,000 |
| 2. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 16 | 5,443,200 |
| 3. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 17 | 11,120,000 |
| 4. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 41 | 111,684,000 |
| 5. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 29 | 26,000,000 |
| 6. | LGA/015/IMC/2019/2020/HQ/NCS/24 LOT 37 | 21,800,000 |
| | **Jumla** | **191,023,200** |

Kushindwa kusuluhisha na kuhuisha rejesta za mawakala na taarifa za madeni zinazohusiana na ada za ukusanyaji/uzoaji wa taka, kunapunguza usahihi wa taarifa za mapato yaliyokusanywa, kuwekwa benki na kiasi kinachodaiwa.

**Ninapendekeza kwamba Menejimenti katika siku zijazo, ifanye usuluhishi wa mara kwa mara kati ya rejesta za mawakala na nyaraka za makusanyo, taarifa za benki na kiasi ambacho bado hakijalipwa.**

## 5.13 Madai ya Muda Mrefu na Malipo Yaliyofanywa Kabla ya Kupokea Bidhaa na Huduma Shilingi Bilioni 176.28

Madai na malipo yaliyofanywa kabla ya kupokea bidhaa au huduma yanahusisha miamala iliyofanywa na Halmashauri kwa wateja wake waliopata huduma kwa mkopo, mapato ambayo hayajawasilishwa, masurufu ambayo hayajarejeshwa na watumishi, pamoja na mikopo

ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, na malipo ya awali yaliyofanywa na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya huduma au bidhaa ambazo hazijapokelewa.

Uzoefu unaonesha uwezekano wa Halmashauri kutopokea mapato ambayo hayajawasilishwa au huduma ambazo hazijatolewa unakuwa mkubwa kadri mdaiwa anapochelewa kulipa deni au kutoa huduma tarajiwa.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, taarifa za fedha pamoja na viambatisho vyake vilibainisha kuwa madai yenye thamani ya shilingi bilioni 176.28 katika mamlaka 135 za serikali za mitaa yalikuwa hayajalipwa na wadaiwa kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 5-3.**

Madai ya muda mrefu kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo yameongezeka kiasi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 176.28 kutoka shilingi bilioni 103.30 kwa Halmashauri 158 na shilingi bilioni 131.85 katika Halmashauri 170 zilizobainika kuwa na madai katika mwaka wa fedha 2018/19. Mwenendo wa madai ya muda mrefu na malipo yaliyofanywa kabla ya kupokea bidhaa au huduma kwa miaka ya fedha minne mfululizo ni kama ilivyo katika **Jedwali Na. 5-13**.

**Jedwali Na. 5 -13: Mwenendo wa madai ya muda mrefu**

| Mwaka wa fedha | Kiasi (Sh.) | Idadi ya Halmashauri |
|---|---|---|
| 2020/21 | 176,281,663,631 | 135 |
| 2019/20 | 103,304,511,810 | 158 |
| 2018/19 | 131,854,275,521 | 170 |
| 2017/18 | 143,045,745,088 | 166 |

Upatikanaji wa kiasi hiki cha madai unatia shaka kwani yamedumu kwa muda mrefu bila kukusanywa na hatimaye yanaweza kuwa madeni yasiyolipika. Hivyo, menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kufanya ufuatiliaji wa uhakika ili ziweze kujiridhisha iwapo madai haya yanaweza kurejeshwa na wadaiwa, vinginevyo yaorodheshwe kama madai yenye mashaka.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa husika kutathmini na kuhakiki madeni yote na kuweka mikakati thabiti itakayoboresha mchakato wa urejeshwaji wa madai yote.**

## SURA YA 6

## USIMAMIZI WA MATUMIZI

### 6.0 Utangulizi

Sura hii inajadili jinsi rasilimali za umma zinavyotolewa na kusimamiwa na mamlaka za serikali za mitaa kwa kufuata nidhamu ya fedha, kuweka vipaumbele vya kimkakati na thamani ya fedha. Usimamizi wa matumizi katika Halmashauri unahusisha taratibu zote zinazohitajika ili kuhakikisha kwamba malipo ya gharama za mamlaka za serikali za mitaa yanafanyika kwa usahihi, ufanisi na kwa wakati. Pia, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma unahakikisha kuwa rasilimali za umma zinazopokelewa na mamlaka za serikali za mitaa zinatumika kikamilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu, maagizo na kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

Matokeo ya ukaguzi wangu yanaonesha ukiukwaji mkubwa wa sheria, kanuni na maelekezo ya usimamizi wa fedha ambao ulisababisha matumizi mabaya katika mamlaka za serikali za mitaa. Sura hii inaeleza kwa muhtasari masuala muhimu ambayo yasiporekebishwa yanaweza kusababisha athari mbaya katika usimamizi wa fedha zilizokabidhiwa kwa Halmashauri. Barua za mapungufu kwa Menejimenti za Halmashauri husika zinaeleza kwa kina masuala yote ya kutokidhi sheria yaliyotolewa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

### 6.1 Matumizi yasiyo na Tija yenye Thamani ya Shilingi Milioni 664

Kulingana na Kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001, malipo yasiyokuwa na manufaa humaanisha malipo yanayoepukika ambayo hayatakuwa na faida. Matumizi yasiyo na tija ni yale yanayofanywa bila faida za kiuchumi. Matumizi hayo ni kama vile malipo yanayofanywa juu ya viwango vilivyoidhinishwa na riba na adhabu kwa kushindwa kutimiza wajibu wa kimkataba. Hujumuisha pia posho zinazolipwa kwa wafanyakazi kwa shughuli ambazo hazijatekelezwa.

Ukaguzi ulibaini kuwa mamlaka 24 za serikali za mitaa zilitumia jumla ya shilingi milioni 664 kwa matumizi yasiyo na faida kiuchumi. Hali hii iliathiri utekelezaji wa shughuli zingine zilizopangwa katika bajeti. **Kiambatisho Na. 6-1** kinaonesha mamlaka zilizofanya matumizi yasiyo na manufaa.

Matumizi yasiyo na manufaa yamesababishwa na kutowasilisha kwa wakati makato ya mishahara katika mifuko husika, usimamizi duni wa mikataba ya ujenzi, usuluhishi duni wa migogoro ya watumishi, na uwezo usioridhisha wa wanasheria katika kutafsiri baadhi ya vifungu vya sheria vinavyotumika katika mamlaka za serikali za mitaa husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-1.**

**Jedwali Na. 6-1: Mwenendo wa matumizi yasiyo na manufaa**

| Mwaka wa fedha | Idadai ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2020/21 | 24 | 664,001,836 |
| 2019/20 | 29 | 2,192,675,594 |
| 2018/19 | 14 | 417,097,179 |

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI ibuni mafunzo stahiki kwa lengo la kuwajengea uwezo wanasheria wa mamlaka za serikali za mitaa na kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa madai yote dhidi ya mamlaka za serikali za mitaa yanalipwa kwa wakati, malipo yanafanyika kwa shughuli halisi, na kuzingatia sheria na kanuni katika kufanya maamuzi ili kuepuka kujirudia kwa matumizi haya yasiyo na tija.**

## 6.2 Malipo ya Bidhaa na Huduma ambazo Hazikupokelewa Shilingi Bilioni 8.44

Agizo la 71(1) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaka malipo kufanywa wakati bidhaa, vifaa, huduma au kazi ambazo zinalipiwa ziwe zimepokelewa au zitakapokuwa zimepokelewa na ziwe katika hali nzuri.

Kinyume na agizo hilo, ilibainika kuwa mamlaka 61 za serikali za mitaa ziliagiza na kulipa shilingi bilioni 8.44 kwa ajili ya bidhaa, lakini bidhaa hizo hazikuwasilishwa na wazabuni husika kwa muda

wa hadi miezi 24. **Kiambatisho Na. 6-2** kinaonesha mamlaka ambazo zilifanya malipo kabla ya kupata huduma au kupokea bidhaa.

Pia, ilibanika kuwa, mara nyingi malipo ya bidhaa ambazo hazijapokelewa yanatokana na masharti yanayowekwa na wazabuni ambayo yanazitaka mamlaka za serikali za mitaa kulipa mapema kabla ya taratibu za kusambaza bidhaa. Pia, mamlaka zingine za serikali za mitaa zinalipa mapema karibu na mwisho wa mwaka ili kuepusha fedha zisizotumika kurejeshwa Hazina.

Hali hii inaziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari ya bidhaa au huduma zilizonunuliwa kutopokelewa kabisa au kupokelewa pungufu na kwa viwango duni.

**Ninapendekeza menejimenti za halmashauri husika (a) zihakikishe udhibiti wa ununuzi wa bidhaa na huduma unaimarishwa kwa kuhakikisha uzingatiaji wa Agizo la 71(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mmwaka 2009; (b) zifuatilie ili kuhakikisha kuwa bidhaa zilizolipiwa zinawasilishwa kwa kiasi na ubora unaohitajika; na (c) Hazina itoe fedha kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa wakati ili kupunguza shinikizo la matumizi ya fedha mwishoni mwa mwaka ambayo mara nyingi yanakiuka udhibiti uliowekwa ili kuepuka kurejeshwa kwa fedha.**

## 6.3 Kutokata Kodi ya Zuio Shilingi Millioni 338.06

Kifungu cha 83 A (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 (Iliyorejewa 2019) inalitaka shirika ambalo bajeti yake inafadhiliwa kikamilifu au kwa kiasi kikubwa na bajeti ya Serikali, kuzuia kodi ya mapato wakati wa kulipa bidhaa au huduma zinazotolewa na mkazi kwa kiwango kilichotolewa chini ya aya ya 4(c) ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 [Iliyorejewa 2019].

Nilibaini wakati wa ukaguzi kuwa, kodi ya zuio ya shilingi milioni 338.06 haikukatwa na Halmashauri 24 katika malipo yaliyofanywa kwa wazabuni kinyume na Kifungu cha 83 A (2) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332 [Iliyorejewa 2019] kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-2**.

**Jedwali Na. 6-2: Malipo yasiyokatwa kodi ya zuio**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Arusha | 10,666,954 | 14. | H/W Mpanda | 3,352,986 |
| 2. | H/Jiji Arusha | 12,426,204 | 15. | H/M Mpanda | 5,532,464 |
| 3. | H/W Chato | 141,139,943 | 16. | H/W Mpimbwe | 9,780,365 |
| 4. | H/Mji Handeni | 10,652,329 | 17. | H/W Mtwara | 1,435,604 |
| 5. | H/W Kaliua | 2,177,940 | 18. | H/W Nsimbo | 11,406,850 |
| 6. | H/W Kibiti | 2,179,600 | 19. | H/W Sikonge | 7,677,253 |
| 7. | H/M Kigamboni | 3,274,332 | 20. | H/M Singida | 1,732,680 |
| 8. | H/W Kishapu | 7,948,005 | 21. | H/M Tabora | 5,179,067 |
| 9. | H/W Kyerwa | 2,127,883 | 22. | H/W Tandahimba | 11,103,530 |
| 10. | H/W Masasi | 1,168,895 | 23. | H/Mji Tunduma | 6,574,554 |
| 11. | H/W Mbogwe | 4,967,716 | 24. | H/W Ulanga | 6,278,200 |
| 12. | H/W Monduli | 3,320,765 | | | |
| 13. | H/M Moshi | 65,955,048 | | **Jumla** | **338,059,167** |

Mapungufu yaliyobainika ni matokeo ya TRA kutofanya jitihada za kutosha katika kusimamia utekelezaji wa sheria za kodi, na baadhi ya menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kuisaidia Mamlaka hiyo na Serikali katika ukusanyaji wa mapato kwa vile jukumu hili walilokasimiwa halipewi uzito stahiki.

Kitendo cha kutokukata kodi ya zuio katika malipo ya wazabuni kinachochea ukwepaji wa kodi na hatimaye kuikosesha Serikali mapato. Pia, hii inaashiria kuwa Halmashauri hazitilii uzito katika kushughulikia mapendekezo yangu ya nyuma kwani hali hii imekua inajirudia.

**Natoa wito kwa Serikali kuiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania kuweka mkazo zaidi katika kusimamia uzingatiaji wa sheria za kodi kwa Halmashauri zote ili kuongeza ukusanyaji wa mapato. Pia, serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapaswa kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kuchukua hatua kwa dhati katika kutekeleza mapendekezo yangu ili kuzuia hali hiyo isijirudie tena.**

## 6.4 Malipo yasiyo na Risiti za EFD kiasi cha Shilingi Bilioni 6.07 na yenye Risit za EFD za Kughushi kiasi cha Shilingi Milioni 376.48

Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Utozaji wa Kodi, Sura ya 438 [Iliyorejewa 2019] kinamtaka mtu, ambaye anasambaza bidhaa,

anatoa huduma au anapokea malipo kuhusiana na usambazaji wa bidhaa au huduma aliyotoa, kutoa risiti au ankara kwa kutumia vifaa vya kielektroniki. Aidha, Kanuni ya 48 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za Mwaka 2016 zinasema kuwa, "Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anachezea au kusababisha kifaa cha kielektroniki kufanya kazi isivyostahili, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua pointi 100 za fedha au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja."

Nilibaini wakati wa ukaguzi kuwa, Halmashauri 71 zilifanya manunuzi na kulipa jumla ya shilingi bilioni 6.07 kwa wazabuni mbalimbali bila kudai risiti za kielektroniki kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 6-3**.

Wakati huo huo nilibaini kuwa, mamalaka tano za serikali za mitaa zilifanya malipo ya shilingi milioni 376.48 kwa wazabuni mbalimbali na zilipewa risiti za kielektroniki. Hata hivyo, uthibitisho wa uhalali wa stakabadhi za kielektroniki nilioufanya kupitia mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania ulibainisha kuwa stakabadhi hizo zilighushiwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-3**.

Pia, nilibaini kuwa, hali hiyo ilisababishwa na uelewa mdogo wa Menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuhusu jinsi ya kugundua risiti bandia na halisi kwa kutumia mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, wafanyabiashara wasio waaminifu na jitihada zisizotosheleza za Mamlaka ya Mapato Tanzania za kugundua na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika zilikuwa sababu nyingine.

**Jedwali Na. 6-3: Risiti za kielekitroniki zisizo halali**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Karatu | 22,765,818 |
| 2. | H/W Kilosa | 102,073,440 |
| 3. | H/M Kinondoni | 181,202,000 |
| 4. | H/M Morogoro | 21,382,132 |
| 5. | H/W Ruangwa | 49,056,500 |
| | **Jumla** | **376,479,890** |

**Naishauri Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoa elimu kwa mamlaka za serikali za mitaa jinsi ya kubaini risiti zisizo sahihi za**

kielektroniki ili kuepuka kujirudia kwa tatizo hilo. Pia, Mamlaka ya Mapato Tanzania iongeze ufuatiliaji wa kubaini wafanyabiashara wasiotoa risiti za kielektroniki na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za kodi. Aidha, Halmashauri zinapaswa kuripoti mara kwa mara matukio yote yaliyogunduliwa au yanayoshukiwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa hatua zinazostahili.**

## 6.5 Malipo ya Shilingi Bilioni 6.19 Yaliyofanywa kwa Fedha Taslimu

Kifungu cha 6.7.3 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 kinaitaka mamlaka ya serikali za mitaa kufanya malipo yote kwa njia ya kielekitroniki katika akaunti ya benki ya mlipwaji, na kwa hali yoyote ile mamlaka isilipe kwa hundi au fedha taslimu.

Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka 45 za serikali za mitaa zililipa kwa fedha taslimu shilingi bilioni 6.19 kinyume na matakwa ya kifungu tajwa hapo juu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-4.**

**Jedwali Na. 6-4: Malipo kwa fedha taslimu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 237,675,400 | 24. | H/Mji Kondoa | 6,680,000 |
| 2. | H/W Bariadi | 310,341,700 | 25. | H/W Kongwa | 23,044,000 |
| 3. | H/Mji Bariadi | 61,774,660 | 26. | H/W Korogwe | 9,747,000 |
| 4. | H/W Buhigwe | 168,941,030 | 27. | H/W Kyela | 10,252,000 |
| 5. | H/W Chamwino | 5,122,950 | 28. | H/M Lindi | 550,520,167 |
| 6. | H/W Chemba | 40,800,000 | 29. | H/W Manyoni | 91,511,500 |
| 7. | H/Mji Geita | 52,453,350 | 30. | H/W Maswa | 1,044,379,496 |
| 8. | H/W Hai | 18,839,936 | 31. | H/W Mbozi | 476,369,000 |
| 9. | H/Mji Handeni | 3,424,000 | 32. | H/W Mkalama | 142,185,098 |
| 10. | H/W Ikungi | 22,292,000 | 33. | H/W Monduli | 35,860,000 |
| 11. | H/W Iramba | 4,500,000 | 34. | H/W Mpanda | 42,029,938 |
| 12. | H/W Iringa | 847,374,272 | 35. | H/M Mpanda | 5,987,520 |
| 13. | H/M Iringa | 32,020,000 | 36. | H/M Musoma | 29,401,662 |
| 14. | H/W Kakonko | 9,542,400 | 37. | H/W Mvomero | 21,660,000 |
| 15. | H/W Karatu | 80,210,000 | 38. | H/W Namtumbo | 13,000,000 |
| 16. | H/W Kasulu | 168,941,030 | 39. | H/W Pangani | 3,371,500 |
| 17. | H/Mji Kibaha | 21,076,407 | 40. | H/W Shinyanga | 188,642,106 |
| 18. | H/M Kigamboni | 122,633,860 | 41. | H/M Shinyanga | 227,848,390 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | H/W Kigoma | 109,534,200 | 42. | H/M Singida | 10,500,000 |
| 20. | H/M Kigoma/Ujiji | 125,672,723 | 43. | H/M Sumbawanga | 89,000,000 |
| 21. | H/W Kilindi | 23,047,500 | 44. | H/M Tabora | 45,040,000 |
| 22. | H/W Kilolo | 32,746,000 | 45. | H/W Tunduru | 37,350,000 |
| 23. | H/M Kinondoni | 589,757,306 | | **Jumla** | **6,193,100,101** |

Kufanya malipo kwa fedha taslimu kunashawishi matumizi mabaya ya fedha za umma na kutolipwa kwa kodi stahiki.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe zinazingatia sheria zinazokataza matumizi ya fedha taslimu wakati wa kufanya malipo kwa wazabuni.**

## 6.6 Matumizi ya Kiasi cha Shilingi Bilioni 9.74 Yasiyosimamiwa Ipasavyo katika Akaunti za Amana

Akaunti ya amana hudhibiti fedha kutoka kwa waweka fedha tofauti ili zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Fedha zinazotumika kutoka katika Akaunti za Amana zinatarajiwa kuendana na madhumuni ya msingi ya amana hizo.

Nilibaini kuwa, mamlaka 81 za serikali za mitaa zilishindwa kusimamia fedha kikamilifu katika akaunti za amana kwani matumizi yalifanywa kutekeleza shughuli ambazo hazikuwa na fedha zilizowekwa katika akaunti za amana. Aidha, mikopo kutoka katika akaunti za amana haikurejeshwa kwa wakati ili kutekeleza shughuli kulingana na madhumuni ya fedha hizo. Jumla ya fedha zilizohusika zilikuwa shilingi bilioni 9.74.

Udhibiti duni wa fedha katika akaunti za amana na kutotunzwa vizuri kwa rejista ya amana ili kudhibiti mienendo ya fedha na uhaba wa fedha katika mamlaka za serikali za mitaa ni miongoni mwa sababu za usimamizi duni na ukopaji usioridhisha katika akaunti za amana.

Fedha zinazokopwa kutoka katika akaunti za amana zisiporudishwa husababisha madeni makubwa kwa mamlaka za serikali za mitaa na hatimaye kuiweka Serikali katika hatari ya kuwa na sifa mbaya

kutoka kwa wenye amana. Zaidi ya hayo, malipo yanayofanywa moja kwa moja kutoka katika akaunti za amana hayawi sehemu ya matumizi ya mamlaka za serikali za mitaa yanayoripotiwa katika taarifa zake za fedha na hivyo kusababisha makosa katika taarifa hizo.

Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizo na malipo yasiyosimamiwa kikamilifu na zenye mikopo isiyorejeshwa katika akaunti zao za amana zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 6-4**.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iziagize menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuweka udhibiti thabiti utakaoboresha usimamizi wa fedha za amana; na (b) ikilazimika fedha kukopwa kutoka katika akaunti za amana, marejesho yanapaswa kufanywa mara moja ili ukopaji huo usiathiri utekelezaji wa shughuli zilizokusudiwa.**

## 6.7 Matumizi ya Shilingi Bilioni 2.92 Yasiyokuwa katika Bajeti

Kifungu cha 46 (5) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] kinatamka, "pale ambapo Mamlaka ya Serikali za Mtaa itaidhinisha bajeti ya mwaka au bajeti ya ziada kwa ujumla wake, bajeti kama ilivyoidhinishwa itaibana hiyo, ambapo matumizi yake yatajikita katika vitu na kiasi kilichomo katika makadirio kama ilivyoidhinishwa".

Katika mwaka husika wa ukaguzi, nilibaini kuwa mamlaka 30 za serikali za mitaa zililipa shilingi bilioni 2.92 (**Jedwali Na. 6-5**) kutekeleza shughuli ambazo hazikuwa katika bajeti. Hali hii ilisababishwa na kupokea fedha nje ya bajeti na udhibiti duni wa kibajeti ndani ya mamlaka husika.

**Jedwali Na. 6-5: Mamlaka zenye matumizi nje ya bajeti**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | 158,085,000 | 17. | H/W Namtumbo | 85,215,000 |
| 2. | H/W Bagamoyo | 13,079,000 | 18. | H/W Nkasi | 17,770,200 |
| 3. | H/Mji Bariadi | 32,700,000 | 19. | H/W Nyang'hwale | 65,890,000 |
| 4. | H/W Bunda | 25,000,000 | 20. | H/W Nyasa | 12, 106,250 |
| 5. | H/W Chato | 65,325,277 | 21. | H/W Rombo | 30,667,872 |
| 6. | H/M Ilemela | 440,000,000 | 22. | H/W Sengerema | 35,355,806 |

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. | H/W Iringa | 17,199,401 | 23. | H/W Serengeti | 32,850,500 |
| 8. | H/M Iringa | 591,181,342 | 24. | H/W Songwe | 13,600,000 |
| 9. | H/W Kalambo | 8,000,000 | 25. | H/M Sumbawanga | 60,439,495 |
| 10. | H/W Kaliua | 13,469,700 | 26. | H/W Uyui | 25,568,159 |
| 11. | H/W Kilolo | 219,618,396 | 27. | H/W Tarime | 170,404,000 |
| 12. | H/W Kiteto | 144,067,375 | 28. | H/Mji Tunduma | 124,145,408 |
| 13. | H/W Mbogwe | 38,786,665 | 29. | H/W Tunduru | 163,910,000 |
| 14. | H/W Misungwi | 6,470,000 | 30. | H/W Ukerewe | 25,210,500 |
| 15. | H/W Mlele | 184,703,337 | | **Jumla** | **2,918,712,433** |
| 16. | H/W Mpanda | 110,000,000 | | | |

Matumizi yanayofanywa nje ya bajeti yanamaanisha kuwa baadhi ya shughuli zilizopangwa zinaweza kuwa zimetekelezwa kwa kiasi au hazijatekelezwa kabisa kutokana na fedha kufanya matumizi yasiyokusudiwa.

**Ninaishauri Hazina k(a) itoe fedha kwa mamlaka za serikali za mitaa kulingana na bajeti iliyoidhinishwa; (b) menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kutekeleza kikamilifu matakwa ya Kifungu cha 46(5) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] na kuimarisha udhibiti wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zilizopangwa; na (c) mamlaka husika za serikali za mitaa zinapaswa kuomba uidhinishaji wa matumizi ya awali ambayo hayakuwa katika bajeti iliyoidhinishwa.**

## 6.8 Malipo ya Shilingi Bilioni 3.87 Yasiyo na Viambatisho

Hati za malipo na viambatisho vyake zinatakiwa kutunzwa kwa umakini kwa muda usiopungua miaka mitano (5) kama inavyotakiwa na Agizo la 104(2) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. Pia, kwa mujibu wa Agizo la 34(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009, mwekahazina anatakiwa kuweka mfumo mzuri wa uhasibu na uhifadhi wa nyaraka zote muhimu.

Kinyume na matakwa yaliyotajwa hapo juu, nilibaini mamlaka 64 za serikali za mitaa hazikuwa na hati za malipo pamoja na viambatisho vyake yenye thamani ya shilingi bilioni 3.87 kama inavyooneshwa

katika **Jedwali Na. 6-6** na **Kiambatisho Na. 6-5**. Hali hii ilisababishwa na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani na utunzaji duni wa nyaraka katika mamlaka husika. Zaidi ya hayo, hali hii inaweza kuwa matokeo ya matumizi mabaya ya fedha na nyaraka kupotezwa/kufichwa ili kuficha ukweli.

**Jedwali Na. 6-6: Mwenendo wa malipo yasiyo na viambatisho**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2020/21 | 64 | 3,868,270,321 |
| 2019/20 | 102 | 4,346,845,180 |
| 2018/19 | 106 | 4,080,998,327 |

Kutokuwapo kwa hati za malipo na viambatisho husika kumepunguza wigo wa ukaguzi, hivyo kutoweza kuthibitisha uhalisia wa matumizi yaliyofanywa na mamlaka husika za serikali za mitaa.

**Kwa kuwa suala hili liliripotiwa pia katika ripoti zangu za miaka ya nyuma, ninapendekeza Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iziagize menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa kuchukua hatua za dhati ili kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani zitakazoimarisha utunzaji wa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake; na (b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichunguze na kutathmini ukubwa wa tatizo na kama linahusishwa na ubadhirifu, wahusika wachukuliwe hatua stahiki.**

## 6.9 Malipo Yenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.37 ya Madeni Yasiyooneshwa katika Hesabu za Mwaka Uliopita

Agizo la 22(1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka matumizi yanayostahili kulipwa yalipwe katika mwaka husika; na kama yasipolipwa yatakuwa deni ili kuepuka matumizi zaidi kwa mwaka unaofuata.

Kinyume na matakwa ya agizo tajwa hapo juu, ukaguzi ulibaini mamlaka 25 za serikali za mitaa zilitumia shilingi bilioni 1.37 kulipa madeni ya mwaka uliopita ambayo hayakuwa sehemu ya madeni ya mwaka uliopita yaliyowasilishwa katika taarifa zao za fedha. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ushahidi uliotolewa kuthibitisha iwapo kiasi kilicholipwa kilijumuishwa katika bajeti ya mwaka husika. Tatizo hili

lilitokana na usimamizi duni wa madeni katika mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-7**.

**Jedwali Na. 6-7: Madeni yasiyooneshwa katika taarifa za fedha**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Mji Babati | 18,990,000 | 14. | H/W Muheza | 21,500,000 |
| 2. | H/W Chamwino | 41,810,000 | 15. | H/Mji Njombe | 9,577,852 |
| 3. | H/Mji Handeni | 12,089,000 | 16. | H/W Nkasi | 23,393,000 |
| 4. | H/W Ikungi | 5,823,000 | 17. | H/W Nzega | 38,699,520 |
| 5. | H/M Iringa | 83,485,360 | 18. | H/W Pangani | 10,100,000 |
| 6. | H/W Kalambo | 14,735,000 | 19. | H/W Ruangwa | 67,325,972 |
| 7. | H/Mji Korogwe | 14,851,603 | 20. | H/W Sengerema | 37,882,600 |
| 8. | H/W Magu | 10,722,000 | 21. | H/Jiji Tanga | 64,831,900 |
| 9. | H/W Mbarali | 5,839,800 | 22. | H/M Temeke | 476,780,900 |
| 10. | H/W Mkinga | 41,392,922 | 23. | H/M Ubungo | 141,630,986 |
| 11. | H/W Momba | 30,011,580 | 24. | H/W Ukerewe | 132,692,930 |
| 12. | H/W Mpanda | 24,760,000 | 25. | H/W Wanging'ombe | 21,996,000 |
| 13. | H/W Mpwapwa | 21,356,858 | | **Jumla** | **1,372,278,783** |

Malipo ya madeni ya miaka ya nyuma ambayo hayakuoneshwa katika taarifa za fedha za mwaka uliopita na ambayo hayakujumuishwa katika bajeti ya mamlaka za serikali za mitaa yanazidisha matumizi ya mwaka unaokaguliwa. Zaidi ya hayo, hali hii inadhihirisha udhibiti dhaifu katika ufungaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka ambazo huficha ukweli wa taarifa za fedha zinazoandaliwa.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa (a) ziboreshe udhibiti wa usimamizi wa madeni na kuhakikisha yanajumuishwa katika vitabu vya hesabu za mwisho; kuingizwa katika bajeti za mamlaka za serikali za mitaa; na kuacha kulipa madeni ambayo hayamo katika orodha ya wadai iliyoidhinishwa; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zitafute uidhinishaji wa matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti iliyoidhinishwa.**

## 6.10 Madeni ya Shilingi Bilioni 279.46 Yasiyolipwa kwa Wakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14.1 cha Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, madeni ni madai

yanayotakiwa kulipwa na mamlaka za serikali za mitaa kutokana na bidhaa au huduma ambazo zimepokelewa na kuna ankara au makubaliano rasmi. Madai haya kwa ujumla yapo katika mfumo wa ankara zinazotolewa na wazabuni, madai ya watumishi, na wajibu mwingine wa mamlaka kwa wadau wao.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, mamlaka 141 za serikali za mitaa ziliripoti madeni ya shilingi bilioni 279.46 katika taarifa zao za fedha, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 6-6.** Madeni hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 88.51 ikilinganishwa na madeni ya shilingi bilioni 190.95 yaliyoripotiwa na mamlaka 72 za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2019/20. Mwenendo wa madeni ambayo hayajalipwa ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 6-8**.

Zaidi ya hayo, kati ya madeni ya shilingi bilioni 279.46, madeni ya shilingi bilioni 198.64 (asilimia 71) yalikuwa hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12 hali iliyosababishwa na uhaba wa fedha kutokana na kutopokea fedha za kutosha kutoka Hazina kulipa madeni, hasa yale yanayohusiana na madai ya wafanyakazi.

**Jedwali Na. 6-8: Mwenendo wa madeni yasiyolipwa**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 2020/21 | 141 | 279,458,170,718 |
| 2019/20 | 172 | 190,951,431,050 |
| 2018/19 | 169 | 207,235,717,133 |

Kutolipwa kwa madeni kama inavyotakiwa kunaweza kukatisha tamaa wauzaji kuuza bidhaa na huduma kwa mkopo kwa mamlaka za husika serikali za mitaa, na kunaweza kusababisha mashtaka na adhabu. Zaidi ya hayo, kutolipwa kwa madai ya wafanyakazi kwa wakati kunapunguza morari yao na kuathiri utendaji wao wa kazi.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Hazina (a) kutoa fedha kwa ajili ya malipo ya madai haya; (b) mamlaka zinapaswa kupitia upya sera zao za mikopo na kuhakikisha kuwa madeni yanalipwa kwa wakati ili kuepuka adhabu zisizo za lazima na kupoteza sifa.**

## 6.11 Uhamisho wa Fedha za Fidia ya Ardhi kiasi cha Shilingi Milioni 341.82 Bila ya Vielelezo vya Kuthibitisha Matumizi

Kifungu cha 41 (1) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 [iliyorejewa 2015] kinamtaka Ofisa Masuuli kuhamisha fedha kutoka katika matumizi yaliyopangwa kwenda kwa matumizi mengine baada ya kupata idhini ya Waziri mwenye dhamana.

Nilikagua matumizi na kubaini kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido aliwaagiza baadhi ya maofisa wa Halmashauri ya Wilaya na watendaji wa Vijiji kutoa benki kiasi cha shilingi milioni 341.82 ambapo shilingi milioni 90 zilitolewa kutoka katika akaunti ya Amana na shilingi milioni 251.82 kutoka katika akaunti za Vijiji, ili kusaidia shughuli Uchaguzi Mkuu uliofanyika Oktoba, 2020. Inavyoonekana, huu ulikuwa ni uchepushaji wa makusudi wa fedha za fidia kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa.

**Napendekeza Ofisi ya Rais -TAMISEMI ifanye uchunguzi ili kubaini kama fedha hizo hazikutumika kwa ubadhirifu.**

# SURA YA 7

# USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

## 7.0 Utangulizi

Usimamizi wa rasilimaliwatu ndani ya mamlaka za serikali za mitaa unalenga ajira, utawala, mafunzo na maendeleo ya watumishi ili kuhakikisha watumishi wa umma wana umahiri katika kutekeleza shughuli za Serikali. Hivyo, mifumo ya usimamizi wa rasilimaliwatu ndani ya mamlaka za serikali za mitaa huwezesha mazingira bora na yenye ufanisi wa kazi na ulipaji wa mishahara. Vilevile, huongeza utendaji kazi wa wafanyakazi wenye tija na utoaji huduma kwa mitazamo sahihi, uzoefu na ujuzi wa kutumikia maslahi ya umma.

Miongoni mwa mambo muhimu ya usimamizi wa rasilimaliwatu unaohusisha usimamizi wa mishahara ya wafanyakazi umejikita katika kutoa mafao, motisha na fidia kupitia tathmini ya utendaji kazi na ya mahitaji yanayoendana na sera na mifumo wezeshi ya taasasi ili kufikia malengo yaliopangwa. Katika ukaguzi nilioufanya, nimebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa rasilimaliwatu katika mamlaka za serikali za mitaa.

## 7.1 Hasara ya Shilingi Milioni 556.84 Kutokana na Malipo kwa Watumishi Wasiokuwapo Kazini

Agizo la 79(1) (a) na 79 (8) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linasema kuwa ofisa rasilimaliwatu pamoja na wakuu wa idara wanapaswa kutunza taarifa zilizohuishwa za watumishi wote. Aidha, wanapaswa kumpa mwekahazina taarifa za uhakiki za watumishi walio chini ya idara zao wanaopaswa kulipwa mishahara sambamba na uthibitisho wa mkaguzi wa ndani.

Nilibaini kuwa mamlaka 25 za serikali za mitaa zilifanya malipo ya shilingi milioni 556.84 kwa watumishi wasiokuwapo kazini. Kundi hili lilijumuisha watumishi waliowastaafu, waliofariki, watoro kazini, walioachishwa kazi, na watumishi waliokuwa na likizo bila malipo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-1** na **Kiambatisho Na. 7-1.**

**Jedwali Na. 7-1: Malipo kwa watumishi wasiokuwapo kazini**

| Kundi | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Watumishi waliostaafu | 18 | 343,431,106 |
| Watoro kazini | 6 | 81,376,793 |
| Watumishi waliofariki | 7 | 63,095,660 |
| Wengine | 6 | 68,932,717 |
| **Jumla** | | **556,836,276** |

***Chanzo:** Taarifa za Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma, 2021*

Hali hii imesababishwa na kutokuwa na mfumo madhubuti wa uhakiki na usafishaji wa taarifa za watumishi katika kanzidata za malipo kwa wakati stahiki. Vilevile, hali hii ilisababishwa na mawasiliano hafifu ya kuwaondoa watumishi wote wasiostahili katika orodha ya mishahara baina ya mamlaka za serikali za mitaa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Hazina.

Pia, mamlaka za serikali za mitaa hazina mifumo oainishi kati yao ya udhibiti wa malipo ambayo huwezesha udhibiti wa mishahara ya wafanyakazi inayoendana na usuluhishi na uboreshaji wa takwimu za malipo ya mifumo dhidi ya orodha ya malipo ya Hazina.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa kuweka mfumo wa uhakiki na usafishaji wa taarifa za watumishi kati yao na Hazina zinazohusu kustaafu, vifo, kufukuzwa kazi, utoro kazini na likizo bila malipo kwa hatua za haraka kufuta kwa wakati majina yao katika mfumo wa malipo.**

## 7.2 Makato ya Shilingi Bilioni 183.09 ya Watumishi ambayo Hayakupelekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Zingine Husika

Kifungu cha 18 (1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2018 kinasema kuwa mwajiri anapaswa kuchangia asilimia 20 ya mshahara wa mfanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Pia, Kifungu cha 19 (1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2018 kinasema kuwa mwajiri ambaye atashindwa kuchangia jumla ya

michango ndani ya muda uliopangwa atapewa adhabu ya kulipa faini zilizoainishwa kwa ongezeko la asilimia kulingana na muda wa uchelewasheji.

Kinyume na vifungu hivyo, wakati wa ukaguzi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021 nilibaini kuwa mamlaka 42 za serikali za mitaa zilishindwa kuwasilisha jumla ya shilingi bilioni 182.24 (shilingi milioni 888.97 kama michango ya mwajiri ya lazima na shilingi bilioni 181.35 kama adhabu ya fedha ambazo hazikuhamishwa) kwenda mifuko ya hifadhi ya jamii.

Vilevile, nilibaini kuwa makato mengine yasiyo ya mfuko wa hifadhi ya jamii ya thamani ya shilingi milioni 845.24 hayakupelekwa kwenye taasisi husika. Makato haya hutokana na mishahara ya wafanyakazi wa mamlaka za serikali za mitaa ambayo inatozwa makato ya kisheria na yasiyo ya kisheria ikiwa pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii, kodi ya mapato, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, na ulipaji wa mikopo kwa taasisi za kifedha, vyama vya akiba na mikopo, pamoja na michango kwenye vyama vya wafanyakazi na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-2** hapa chini na **Kiambatisho Na. 7-2**.

**Jedwali Na. 7-2: Michango ambayo haijapelekwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi zingine**

| Kundi | Idadi ya Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Michango kwa Mfuko ya Hifadhi ya Jamii ya Watumishi wa Umma | 33 | 888,967,644 |
| Adhabu Kutokana na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma | 21 | 181,354,927,774 |
| Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | 7 | 532,301,005 |
| Kodi ya mapato | 10 | 24,282,885 |
| Bima ya Afya ya Taifa | 12 | 23,754,200 |
| Taasisi zingine | 15 | 264,906,756 |
| **Jumla** | | **183,089,140,263** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Malipo ya Mishahara ya Watumishi wa Umma na Majalada ya Kiutumishi, 2021*

Hata hivyo, ilibainika kuwa deni la shilingi bilioni 180.70 lilihusisha adhabu zilizotolewa kwa mamlaka 5 za serikali za mtaa ambazo ni

Halmashauri ya Wilaya ya Chato: shilingi bilioni 1.83; Halmashauri ya Jiji la Dodoma: shilingi bilioni 56.81; Halmashauri ya Wilaya ya Meatu: shilingi milioni 578.74; Halmashauri ya Wilaya ya Nzega: shilingi bilioni 117; na Halmashauri ya Mji Nzega: shilingi bilioni 3.67 kwa madai ya kushindwa kuwasilisha/kulipa mafao ya wafanyakazi halali.

Kutowasilishwa kwa fedha hizo kunasababisha kucheleweshwa kwa uchakataji wa mafao ya wastaafu, na kunazigharimu mamlaka za serikali za mitaa kwa njia ya adhabu.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa kupeleka makato ya kisheria kwa wakati kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuepusha adhabu zisizo za lazima na kuokoa fedha za Serikali.**

## 7.3 Malimbikizo ya Muda Mrefu ya Mishahara yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 160 ambayo Hayakulipwa

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha ilioishia tarehe 30 Juni 2021, nilifanya mapitio ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma na kubaini kuwa, watumishi 33,405 hawakulipwa malimbikizo yao ya mishahara yenye thamani ya shilingi bilioni 63.83, yanayotokana na kupandishwa vyeo katika utumishi wa umma au kuteuliwa kushika nyadhifa za juu. Malimbikizo hayo ni ya zaidi ya mwaka mmoja. Hali hii ni kinyume na Kanuni ya E.23 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009.

Mamlaka za serikali za mitaa zimekuwa na tabia ya kutolipa kabisa madai jambo ambalo linahitaji Serikali kuingilia kati na kuwa na mtazamo tofauti ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza kwa watumishi wa umma. Hali hii imeleta changamoto kwa watumishi wa umma kupata tabu katika utumishi wao na kusababisha hali ya kukata tamaa, hivyo kuzuia ufanisi katika malengo na shabaha za Serikali kuelekea utoaji wa huduma kwa umma.

Aidha, nilibaini kuwa kiasi kikubwa cha madai mengine ya watumishi 71,670 yenye thamani ya shilingi bilioni 96.65 ambayo yalikuwa hayajalipwa yalikuwa posho za likizo, gharama za uhamisho, malimbikizo ya posho za simu, na malimbikizo ya gharama za

matibabu. Sambamba na hilo, ilibainika kuwa madai haya yamekuwa yakiongezeka kutokana na ukweli kuwa, mamlaka za serikali za mitaa zinashindwa kukusanya mapato yake ya ndani kwa mujibu wa bajeti yake. Serikali kuu imekuwa ikitoa fedha za matumizi ya kawaida chini ya bajeti ya kuwezesha kulipa madai hayo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7-3** na **Kiambatisho Na. 7-3**.

**Jedwali Na. 7-3: Madai ya wafanyakazi ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu**

| Kundi | Idadi ya Watumishi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| Malimbikizo ya mishahara | 33,405 | 63,832,478,393 |
| Posho za likizo | 34,648 | 12,671,181,149 |
| Gharama za uhamisho | 14,615 | 32,369,833,996 |
| Malimbikizo mengine | 22,407 | 51,606,982,612 |
| **Jumla** | | **160,480,476,150** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Hesabu za Mwisho, 2021*

**Ninapendekeza Serikali iweke muda maalumu wa kulipa madai yote ya watumishi wa umma.**

## 7.4 Wastaafu Kutolipwa Gharama za Usafirishaji Mizigo Zenye Thamani ya Shilingi 128.03 baada ya Kustaafu

Kanuni ya J.8 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 inaelezea stahiki za watumishi wanapokuwa wamekamilisha utumishi wao wa umma.

Nilifanya mapitio ya taarifa za wastaafu na kubaini kuwa wastaafu 160 wa kada ya uwalimu katika mamlaka mbili za serikali za mitaa hawakulipwa jumla ya shilingi milioni 128.03 fedha za gharama ya kusafirisha mizigo yao baada ya kufikia umri wa kustaafu na kuhitimisha utumishi wao wa uma kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 7- 4** hapa chini.

**Jedwali Na. 7- 4: Wastafu kutolipwa gharama za usafirishaji wa mizigo baada ya kustaafu**

| SN | Jina la Mamlaka ya Serikali za Mitaa | Idadi ya Watumishi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Chamwino DC | 144 | 117,868,897 |
| 2. | Chemba DC | 16 | 10,158,000 |
| **Jumla** | | **160** | **128,026,897** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Wastaafu wa Halmashauri, 2021*

Kutowalipa wastaafu haki zao kunaweza kuleta athari mbaya katika ustawi wa watumishi wa umma.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa ziwalipe gharama za usafirishaji wa mizigo watumishi waliostaafu mara tu baada ya kuhitimisha utumishi wao wa umma.**

## SURA YA 8

## UKAGUZI WA MIRADI YA KIMKAKATI, MAENDELEO NA MIRADI MINGINE

### 8.0 Utangulizi

Katika mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2020/21, mamlaka za serikali za mitaa zilitekeleza shughuli za miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha za makusanyo ya mapato ya ndani, fedha kutoka serikali kuu, wahisani, na michango ya wananchi. Baadhi ya vyanzo vya fedha hizo ni ruzuku ya maendeleo ya Serikali za mitaa (LGDG), ruzuku ya maendeleo ya sekta ya afya, mfuko wa kuchochea maendeleo ya jimbo na mpango wa kuboresha elimu (EQUIP-T).

Miradi mingine ya maendeleo iliyotekelezwa mwaka huu ilifadhiliwa kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii, Mradi wa Uimarishaji wa Serikali za Mitaa, Mradi wa Ariel Glaser wa Kutokomeza UKIMWI kwa Watoto na Familia (AGPAHI), Mfuko wa Elizabeth Glaser wa Kusaidia Afya ya Mtoto (EGPAF), Menejimenti na Maendeleo ya Afya (MDH), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mradi wa Ushirika wa Kilimwengu kwa ajili ya Elimu - II (GPE II), Mradi wa Ufadhili kwa Matokeo (RBF), Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni (SWASH), Uwajibikaji wa Taasisi kwa Jamii (CSR), na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Katika kuchambua na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi katika mamlaka za serikali za mitaa, nilibaini masuala mbalimbali kuhusiana na matokeo ya utekekelezaji wa miradi na taarifa za fedha kama inavyoainishwa hapa chini.

### 8.1 Miradi ambayo Haikukamilika yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 195.65

Katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mamlaka za serikali za mitaa, nilibaini miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 195.65 katika mamlaka 128 za serikali za mitaa ambayo hadi kufikia muda wa ukaguzi huu, ilikuwa haijakamilika. Kuchelewa kukamilika kwa miradi hii kulihusishwa na sababu

mbalimbali ikiwa pamoja na kukosekana kwa mipango madhubuti wakati wa kuanzishwa, kukosekana ufuatiliaji madhubuti wakati wa utekelezaji, kuchelewa au kutolewa fedha pungufu za utekelezaji wa miradi hiyo, na kukosekana kwa michango ya wananchi katika maeneo mengi. Miradi mingine imeibuliwa pasipo kushirikisha wananchi wa maeneo husika hivyo kusababisha mzigo mkubwa kwa Serikali kuu. Mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi ambayo haijakamilika na thamani zake imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-1**

Kuchelewesha ukamilishaji wa miradi ya maendeleo kunasababisha kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuongezeka kwa bei ya bidhaa za ujenzi kunakosababishwa na mfumuko wa bei. Pia, husababisha pia kuchelewa kwa manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii.

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa (a) zipitie makadirio ya gharama za ukamilishaji wa miradi hiyo na kuweka mikakati ya ukamilishaji; na (b) halmashauri hizo ziongeze umakini katika kupanga, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.**

## 8.2 Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 41.51 Iliyotelekezwa kwa Muda Mrefu bila Kukamilika

Nilibaini kuwa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 41.51 katika mamlaka 21 za serikali za mitaa iliyokuwa katika hatua mbalimbali za ukamilishaji ilitelekezwa kwa kipindi cha kati ya mwaka mmoja hadi miaka kumi na sita. Kutelekeza miradi ya maendeleo ambayo fedha zimewekezwa ni matumizi mabaya ya rasilimali ambayo yatasababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi iliyotelekezwa inaoneshwa katika K**iambatisho Na. 8-2.**

**Ninazishauri menejimenti za mamlaka husika za serikali za mitaa (a) kuja na mikakati ya kukamilisha miradi iliyotelekezwa, na katika siku zijazo, kuhakikisha upangaji na usanifu wa miradi unaandaliwa kwa namna ambayo itawezesha kukamilika kwa wakati na kufikia malengo yaliyokusudiwa; na (b) Serikali kupitia**

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI itoe fedha za kutosha kukamilisha miradi iliyotelekezwa.**

## 8.3 Miradi Iliyokamilika lakini Haitumiki yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 7.68

Nilifanya tathmini ya ufanisi wa utoaji wa huduma zilizokusudiwa kwa miradi iliyokamilika na nilibaini kuwa, katika Halmashauri 30, miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 7.68 ilikuwa imekamilika lakini haitumiki. Kuna sababu kadhaa zinazohusishwa na kutotumika kwa miradi iliyoainishwa ikiwa ni pamoja na ukosefu wa umeme, ukosefu wa wataalam wa kuendesha mifumo mbalimbali na idadi ndogo ya watumishi. Miradi kutotumika baada ya kukamilika kunamaanisha kutokuwapo kwa mipango thabiti na mahususi wakati wa uanzishwaji ili kuhakikisha miradi hiyo inatumika kikamilifu. Maelezo ya Halmashauri zenye miradi iliyokamilika lakini haijaanza kutumika zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 8-3**

**Ninazishauri Menejimenti za Halmashauri kuongeze umakini katika uandaaji wa mipango ya miradi, ili kuhakikisha miradi inayokamilika inatumika. Kwa upande wa miradi iliyoainishwa ninazishauri Halmashauri husika kuchukua hatua stahiki kama vile kuwasiliana na Mamlaka husika ili kutatua changamoto zinazozikabili na kuhakikisha miradi yote iliyokamilika inaanza kutumika na kuleta manufaa yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha.**

## 8.4 Fedha za Miradi ya Maendeleo Zilizorudishwa Hazina Shilingi Bilioni 14.76

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kiasi cha shilingi bilioni 14.76 zilizokuwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika Mamlaka za Selikali za Mitaa 80 zilirudishwa Hazina mwishoni mwa mwaka baada ya Halmashauri kushindwa kutumia fedha hizo ambapo shilingi bilioni 1.7 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 13.06 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, vyumba vya madarasa, zahanati, majengo ya utawala na majengo

mengineyo. Kati ya fedha zote zilizofungiwa, shilingi bilioni 1.21 zilirejeshwa kwa Halmashauri husika na kuacha shilingi bilioni 5.74 hazikurejeshwa. Hii ina maana kwamba miradi iliyopangwa yenye thamani ya shilingi bilioni 14.76 haikutekelezwa kutokana na fedha hizo kutorejeshwa kwa mamlaka za serikali za mitaa kama ilivyofafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 8-4**.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Hazina (a) ihakikishe inatoa fedha kwa wakati ili kutoa muda wa kutosha kwa mamlaka za serikali za mitaa kusimamia na kutumia fedha zinazotolewa; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuandaa mikakati ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa wakati ili kuepuka bakaa kurudishwa Hazina.**

## 8.5 Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Jimbo Iliyotekelezwa Pasipo Kuibuliwa na Jamii Shilingi Milioni 295.76

Kifungu cha 11(1) na (2) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Sura ya 16 ya Mwaka 2009 inaitaka Kamati ya Mfuko wa Jimbo kuidhinisha mapendekezo yote ya miradi kutoka kata zote za jimbo na miradi mingine yoyote ambayo Kamati inaona kuwa na manufaa kwa jimbo. Katika ukaguzi wangu, nilibaini mamlaka 7 za serikali za mitaa zilitumia fedha za Mfuko wa Jimbo jumla ya shilingi bilioni 295.76 kwa shughuli ambazo hazikuibuliwa na jamii. **Jedwali Na. 8-1** linaonesha mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi ambayo haikuibuliwa na jamii.

**Jedwali Na. 8-1: Fedha zilizotumika kwa shughuli ambazo hazikuibuliwa na jamii**

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi cha Fedha | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mlele | 33,423,000 | Fedha zilitumika kufadhili ujenzi wa Shule ya Sekondari Kwamsisi. |
| 2. | H/W Handeni | 6,866,077 | Fedha zimetumika kulipa posho kinyume na Kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo. |
| 3. | H/W Chalinze | 26,654,000 | Ununuzi wa mizinga 20 ya nyuki pamoja na ujenzi wa madarasa na wodi za wagonjwa. |
| 4. | H/W Kasulu | 61,400,000 | Fedha zimetekeleza shughuli zisizohusiana na Mfuko wa Jimbo |

| S/N | Jina la Halmashauri | Kiasi cha Fedha | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 5. | H/Mji Kasulu | 19,785,000 | Fedha zinazotumika kumlipa mkandarasi (Ngweruke) kwa ajili ya matengenezo ya barabara na ujenzi wa kalvati ikiwa pamoja na ununuzi wa dizeli kwa ajili ya greda na posho ya dereva wa greda. |
| | | 44,190,000 | Ununuzi wa madawati 100 ya Shule ya Msingi Kidyama na ujenzi wa barabara mbalimbali za kata. |
| 6. | H/M Lindi | 66,095,139 | Fedha zimetumika kwa shughuli ambazo hazikuidhinishwa na kamati ya mfuko wa jimbo. |
| 7. | H/W Liwale | 37,347,071 | Fedha zimetumika kwa ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa shughuli ambazo hazikuidhinishwa na amati ya mfuko wa jimbo. |
| **Jumla** | | **295,760,287** | |

***Chanzo:*** *Ripoti za menejimenti*

Utekelezaji wa miradi ambayo haikuibuliwa na jamii inainyima jamii husika manufaa yaliyokusudiwa kwani Mfuko huo uliundwa kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli zilizo katika kipaumbele cha jamii husika.

**Ninazishauri Halmashauri husika katika siku zijazo kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mfuko wa Jimbo kwa kutekeleza shughuli zilizo ibuliwa na wanajamii pia kuidhinishwa na Kamati za Mfuko wa Jimbo.**

## 8.6 Miradi Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 634.19 chini ya Mpango wa Wajibu wa Taasisi kwa Jamii ambayo Haikutekelezwa

Kifungu cha 105 (1), (2) na (4) cha Sheria ya Uchimbaji wa Madini, Sura ya 123 ya Mwaka 2019 kinamtaka mwenye leseni ya uchimbaji madini kuandaa na kuwasilisha katika mamlaka ya serikali za mitaa mpango mahususi wa miradi itakayotekelezwa chini ya Mpango wa Wajibu wa Taasisi kwa Jamii ikiwa na orodha ya miradi pamoja na shughuli zingine zitakazotekelezwa na mchimbaji huyo. Sheria hiyo pia inaitaka mamlaka ya serikali za mitaa kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

Nilibaini kampuni ya uchimbaji madini iliandaa mpangokazi wa mwaka wa Mpango wa Wajibu wa Taasisi kwa Jamii na kuuwasilisha katika Halmashauri ya Wilaya ya Songwe ikiorodhesha miradi itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21 yenye thamani ya shilingi bilioni 634.19.

Pia, nilipitia taarifa ya utekelezaji ya halmashauri na nilibaini kuwa hakukuwa na miradi iliyotekelezwa na kampuni kwa kutumia fedha za Mpango wa Wajibu wa Taasisi kwa Jamii au mchango uliotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi.

**Ninaishauri Halmashauri ya Wilaya Songwe kwa siku zijazo iingie mkataba wa makubaliano na kampuni unaoeleza kwa uwazi majukumu ya kila upande katika kuhakikisha miradi iliyopangwa imepatiwa fedha na imetekelezwa.**

## SURA YA 9

## USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

### 9.0 Utangulizi

Kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kinanitaka kueleza katika ripoti yangu ya ukaguzi ya mwaka iwapo taasisi nilizozikagua zimezingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Kufuatia ukaguzi wa utekelezaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa kazi, bidhaa, na huduma katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mwaka wa fedha 2020/21, thamani ya ununuzi uliofanyika katika mamlaka 127 za serikali za mitaa ni shilingi bilioni 509.65 zinazojumuisha kiasi cha shilingi bilioni 247.5 sawa na asilimia 49 kwa ajili ya bidhaa; shilingi bilioni 165.54 sawa na asilimia 33 kwa ajili ya kazi; shilingi bilioni 47.06 sawa na asilimia 9 kwa ajili ya huduma za ushauri; shilingi bilioni 43 sawa na asilimia 8 kwa ajili ya huduma zisizo za ushauri; na shilingi bilioni 6.08 sawa na asilimia 1 kwa ajili ya mauzo ya mali za serikali kwa njia ya zabuni.

Nilipitia taratibu na kanuni zilizoundwa ili kuhakikisha ufanisi katika kila hatua ya mzunguko wa ununuzi na kubaini udhaifu mbalimbali unaojadiliwa hapa chini.

### 9.1 Usimamizi wa Manunuzi

#### 9.1.1 Ununuzi Uliyofanyika Bila Idhini za Bodi za Zabuni Shilingi Bilioni 10.34

Kanuni ya 55 (2), 163 (4) na 185 (1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inakataza mamlaka za serikali za mitaa kutoa zabuni isipokuwa kama zabuni hiyo imeidhinishwa na bodi husika ya zabuni.

Kinyume na matakwa ya Kanuni, nilibaini kuwa mamlaka 42 zilifanya ununuzi wa bidhaa mbalimbali zenye thamani ya **shilingi bilioni 7.93** bila ya kuidhinishwa na bodi za zabuni za halmashauri husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-1.**

**Jedwali Na. 9-1: Ununuzi bila idhini ya bodi za zabuni**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dodoma | 2,496,261,055 | 22. | H/W Kasulu | 95,484,000 |
| 2. | H/W Kwimba | 553,587,970 | 23. | H/W Momba | 87,678,201 |
| 3. | H/W Muleba | 493, 004,859 | 24. | H/W Kondoa | 62,306,617 |
| 4. | H/W Ngorongoro | 477,083,770 | 25. | H/W Ludewa | 59,489,205 |
| 5. | H/Mji Njombe | 328,301,358 | 26. | H/W Shinyanga | 59,483,140 |
| 6. | H/W Nachingwea | 319,774,247 | 27. | H/W Geita | 50,252,547 |
| 7. | H/W Madaba | 314,698,500 | 28. | H/Mji Masasi | 48,568,650 |
| 8. | H/W Tarime | 305,307,924 | 29. | H/W Nsimbo | 42,489,500 |
| 9. | H/W Chato | 298,603,000 | 30. | H/W Nyang'hwale | 37,124,400 |
| 10. | H/M Kahama | 272,550,080 | 31. | H/W Nzega | 35,936,530 |
| 11. | H/M Kinondoni | 271,025,859 | 32. | H/M Tabora | 25,308,000 |
| 12. | H/W Msalala | 227,059,040 | 33. | H/W Meru | 23,981,966 |
| 13. | H/W Ukerewe | 206,638,848 | 34. | H/W Mpwapwa | 23,006,500 |
| 14. | H/M Lindi | 202,413,617 | 35. | H/W Meatu | 22,909,061 |
| 15. | H/W Mbozi | 166,090,000 | 36. | H/W Namtumbo | 21,210,420 |
| 16. | H/W Sengerema | 133,625,267 | 37. | H/W Moshi | 20,100,000 |
| 17. | H/W Mwanga | 129,476,135 | 38. | H/M Sumbawanga | 19,055,000 |
| 18. | H/Mji Makambako | 125,040,219 | 39. | H/W Igunga | 18,935,000 |
| 19. | H/W Bunda | 108,590,556 | 40. | H/W Urambo | 17,092,497 |
| 20. | H/W Kilosa | 103,665,912 | 41. | H/W Mpimbwe | 16,942,730 |
| 21. | H/W Makete | 98,489,044 | 42. | H/W Mbogwe | 5,550,000 |
| **Jumla** | | | | | **8,424,191,224** |

Pia, Kanuni ya 166 (7) (8) cha Kanuni ya Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kinataka ununuzi wote mdogo kutolewa taarifa katika bodi ya zabuni kila mwezi.

Katika ukaguzi nilioufanya kuhusu ununuzi mdogo katika mamlaka 17 za serikali za mitaa nilibaini kuwa ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 1.92 ulifanyika bila kuripotiwa kwa bodi za zabuni kila mwezi kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-2.**

**Jedwali Na. 9-2: Ununuzi ambao haukuripotiwa kwa bodi ya zabuni**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Muleba | 436,353,321 | 10. | H/Mji Kibaha | 46,080,200 |
| 2. | H/W Kasulu | 280,648,425 | 11. | H/W Msalala | 37,848,000 |
| 3. | H/W Kibondo | 267,078,231 | 12. | H/W Rungwe | 36,650,480 |
| 4. | H/W Urambo | 208,340,075 | 13. | H/W Nsimbo | 36,317,600 |
| 5. | H/M Shinyanga | 161,420,910 | 14. | H/Jiji Mwanza | 26,442,000 |
| 6. | Kigoma/Ujiji | 136,153,023 | 15. | H/W Mbogwe | 25,563,200 |
| 7. | H/W Meatu | 80,140,198 | 16. | H/W Mpimbwe | 20,204,604 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | H/W Buchosa | 55,836,400 | 17. | H/W Kishapu | 19,297,000 |
| 9. | H/M Kahama | 50,129,350 | | **Jumla** | **1,924,503,017** |

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua stahiki kwa mamlaka za serikali za mitaa zote zilizobainika kufanya ununuzi bila kuomba kibali cha bodi za zabuni.**

### 9.1.2 Ununuzi Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.84 Uliofanyika Nje ya Mpango wa Mwaka wa Halmashauri

Kanuni ya 69(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na marekebisho yake ya mwaka 2016 inaitaka taasisi inayofanya manunuzi kufanya makisio ya mahitaji yake ya bidhaa, huduma, na ujenzi kwa usahihi kadiri iwezekanavyo kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango kazi na kujumuishwa katika makadirio ya kila mwaka.

Katika ukaguzi wa ununuzi kwa kuyalinganisha na mpango wa ununuzi wa mwaka katika mamlaka 24 za serikali za mitaa nilibaini kuwa, ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 3.84 ulifanyika bila kuzingatia mpango wa ununuzi wa kila mamlaka husika ya serikali za mitaa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.9-3** hapa chini:

**Jedwali Na. 9-3: Ununuzi uliofanyika nje ya mpango wa ununuzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mbinga | 606,775,000 | 13. | H/W Kondoa | 88,328,580 |
| 2. | H/W Manyoni | 435,301,900 | 14. | H/W Misungwi | 84,999,000 |
| 3. | H/J Dodoma | 371,040,730 | 15. | H/W Karatu | 83,799,614 |
| 4. | H/M Sumbawanga | 368,588,589 | 16. | H/Mji Mbinga | 79,600,000 |
| 5. | H/Mji Kondoa | 339,789,788 | 17. | H/W Mbeya | 67,541,000 |
| 6. | H/Mji Bariadi | 253,661,093 | 18. | H/Mji Nanyamba | 42,900,000 |
| 7. | H/W Siha | 210,000,000 | 19. | H/W Monduli | 31,544,200 |
| 8. | H/W Ukerewe | 188,441,208 | 20. | H/M Iringa | 30,000,000 |
| 9. | H/W Nsimbo | 62,934,583 | 21. | H/W Kiteto | 25,201,797 |
| 10. | H/Jiji Arusha | 119,943,000 | 22. | H/W Sumbawanga | 18,800,000 |
| 11. | H/W Arusha | 119,943,000 | 23. | H/W Sengerema | 8,240,000 |
| 12. | H/W Mbulu | 98,897,350 | | **Jumla** | **3,836,270,432** |

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuzisisitizia mamlaka za serikali za mitaa kufanya ununuzi kwa kuzingatia mpango wa ununuzi wa mwaka.**

### 9.1.3 Ununuzi wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 5.37 Uliofanyika Bila Kushindanisha Wazabuni

Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 inaagiza taasisi inayofanya manunuzi kupata nukuu za bei kutoka kwa wazabuni/wauzaji wasiopungua watatu.

Mapitio ya ununuzi uliofanyika katika mamlaka 39 za serikali za mitaa yalibaini ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 5.37 ulifanyika bila kuitisha nukuu za bei za ushindani kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-4**.

**Jedwali Na. 9-4: Ununuzi uliofanyika bila ushindani**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Chalinze | 1,733,637,507 | 2. | H/W Kilolo | 60,252,690 |
| 3. | H/W Madaba | 446,309,400 | 4. | H/W Ushetu | 58,310,500 |
| 5. | H/W Chato | 377,789,672 | 6. | H/W Kilosa | 54,050,009 |
| 7. | H/W Nsimbo | 319,271,956 | 8. | H/W Tandahimba | 48,045,984 |
| 9. | H/W Geita | 241,538,805 | 10. | H/W Iringa | 41,899,200 |
| 11. | H/W Kishapu | 170,869,223 | 12. | H/W Mbogwe | 35,992,927 |
| 13. | H/W Songwe | 168,130,941 | 14. | H/W Tarime | 35,450,475 |
| 15. | H/W Butiama | 162,955,641 | 16. | H/W Itigi | 32,155,892 |
| 17. | H/M Sumbawanga | 143,243,851 | 18. | H/Mji Handeni | 31,410,750 |
| 19. | H/W Msalala | 139,044,404 | 20. | H/W Bahi | 29,456,065 |
| 21. | H/W Mlimba | 134,371,900 | 22. | H/W Makete | 28,221,080 |
| 23. | H/M Lindi | 126,859,509 | 24. | H/W Kyela | 22,302,000 |
| 25. | H/Mji Nzega | 110,000,000 | 26. | H/W Nyang'hwale | 20,953,960 |
| 27. | H/Mji Tunduma | 108,953,261 | 28. | H/W Ukerewe | 15,147,860 |
| 29. | H/W Sumbawanga | 103,172,600 | 30. | H/W Ileje | 13,153,351 |
| 31. | H/W Mwanga | 101,553,237 | 32. | H/W Mvomero | 12,853,633 |
| 33. | H/W Kilwa | 86,955,460 | 34. | H/W Kongwa | 12,339,287 |
| 35. | H/W Liwale | 86,052,055 | 36. | H/W Itilima | 11,510,000 |
| 37. | H/W Newala | 71,272,000 | 38. | H/W Mbinga | 9,243,000 |
| 39. | H/W Mufindi | 65,124,720 | | **Jumla** | **5,366,682,205** |

Kufanya ununuzi uliohusisha kiasi kikubwa cha fedha bila kupata nukuu za bei kutoka kwa wazabuni kunaminya mawanda ya ukaguzi

katika kutoa uhakika iwapo thamani ya fedha ilipatikana katika ununuzi uliofanyika.

**Ninaisisitizia Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) ihakikishe uzingatiaji wa sheria husika ili kupata thamani ya fedha na kuwapatia wazabuni fursa ya kushindana; na (b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ifanye uchunguzi zaidi kuhusu ununuzi huu.**

### 9.1.4 Ununuzi Uliyofanyika Bila Kutumia Hati ya Kuagiza Vifaa (LPO) Shilingi Bilioni 1.24

Kanuni ya 164 (2)(j) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013 inaeleza kwamba, barua ya mwaliko wa nukuu za bei na kiambatisho chochote kitakuwa na fomu ya mkataba au hati ya kuagiza vifaa (LPO) itakayojumuisha masharti yote ya malipo. Pia Agizo la 69 la Randama ya Fedha za mamlaka za serikali za mitaa ya Mwaka 2009 linataka bidhaa, huduma, na kazi zote zilizofanyika katika mamlaka za serikali za mitaa kuthibitishwa kwa hati ya kuagiza vifaa.

Ukaguzi wangu wa ununuzi ulibaini mamlaka 14 za serikali za mitaa zilifanya ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 1.24 bila kutumia hati ya kuagiza vifaa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-5.**

**Jedwali Na. 9-5: Ununuzi uliofanyika bila hati ya kuagiza vifaa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mtwara | 263,743,212 | 9. | H/W Bariadi | 30,864,188 |
| 2. | H/W Chamwino | 231,974,428 | 10. | H/Jiji Tanga | 26,480,000 |
| 3. | H/W Mufindi | 201,161,601 | 11. | H/W Kongwa | 22,035,090 |
| 4. | H/W Mbozi | 175,651,173 | 12. | H/W Moshi | 20,124,500 |
| 5. | H/W Sengerema | 90,402,000 | 13. | H/W Mpwapwa | 18,460,000 |
| 6. | H/W Makete | 51,406,849 | 14. | H/W Kyerwa | 18,248,000 |
| 7. | H/Mji Bariadi | 49,687,130 | | | |
| 8. | H/W Kilindi | 40,616,000 | | **Jumla** | **1,240,854,171** |

Udhaifu huu unaweza kusababisha upotevu mkubwa kama mkataba utavunjika kutokana na kutokuwapo na mkataba wowote wa kisheria kati ya pande za mkataba.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ishirikiane na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kuhakikisha mamlaka za serikali za**

**mitaa zinafuata kikamilifu matakwa ya sheria ya ununuzi na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika ambao hawatafuata sheria.**

### 9.1.5 Malipo ya Shilingi Bilioni 2.02 kwa Wazabuni wa Bidhaa na Huduma Bila Taarifa za Ukaguzi

Kanuni za 244(1) na 245 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 zinaelekeza taasisi nunuzi kukagua bidhaa zinazoletwa na wazabuni na kuzikubali iwapo tu zinakidhi vipimo vilivyowekwa katika mkataba. Kinyume na Kanuni hiyo nilibaini mamlaka 21 za serikali za mitaa zilifanya malipo ya ununuzi wa bidhaa na huduma yenye thamani ya shilingi bilioni 2.02 bila wazabuni kukaguliwa na kamati zilizoteuliwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-6** hapa chini.

**Jedwali Na. 9-6: Malipo ya bidhaa na huduma kabla ya ukaguzi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi Sh. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bunda | 641,439,137 | 12. | H/M Ubungo | 43,653,384 |
| 2. | H/W Chamwino | 242,399,798 | 13. | H/W Nsimbo | 39,337,700 |
| 3. | H/W Singida | 240,118,850 | 14. | H/W Kilolo | 34,553,080 |
| 4. | H/W Mbozi | 175,651,173 | 15. | H/W Momba | 31,429,195 |
| 5. | H/W Chemba | 98,976,978 | 16. | H/W Itilima | 24,110,200 |
| 6. | H/M Sumbawanga | 86,162,368 | 17. | H/Mji Nzega | 18,887,148 |
| 7. | H/W Mwanga | 66,566,764 | 18. | H/W Bukombe | 18,044,810 |
| 8. | H/W Tandahimba | 63,867,080 | 19. | H/W Iramba | 10,790,612 |
| 9. | H/W Ikungi | 61,770,400 | 20. | H/W Bariadi | 8,515,000 |
| 10. | H/W Songwe | 59,936,001 | 21. | H/W Handeni | 3,681,200 |
| 11. | H/W Kalambo | 53,714,388 | | **Jumla** | **2,023,605,266** |

Kufanya malipo ya ununuzi wa bidhaa na huduma bila mzabuni kukaguliwa na kamati husika kunaweza kuathiri ubora na utekelezaji wa matakwa ya mkataba na kunaweza kusababisha ununuzi wa bidhaa zisizo na ubora kwa taasisi nunuzi.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuhakikisha mamlaka zote za serikali za mitaa zinafuata sheria husika kwa kuhakiki ubora na kiasi cha bidhaa na huduma kabla hazijapokelewa na kufanya malipo kwa wazabuni.**

### 9.1.6 Kuanza kwa Miradi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 28.17 Kabla ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Kanuni ya 241(3) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi zinazofanya ununuzi kufanya tathmini ya athari kwa mazingira katika hatua ya maandalizi ya mradi kabla ya kuanza mchakato wa ununuzi. Aidha, Kifungu cha 81(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 kinataka utafiti wa tathmini ya athari za mazingira ufanyike kabla ya kuanza au kufadhili mradi.

Nimepitia majalada ya miradi na kubaini kuwa mamlaka 9 zilianza utekelezaji wa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 28.17 bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-7.**

**Jedwali Na. 9-7: Kuanza miradi bila tathmini ya athari kwa mazingira**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Bariadi | 10,310,795,917 | 6. | H/W Mbeya | 1,820,000,000 |
| 2. | H/W Itilima | 4,200,000,000 | 7. | H/W Mbogwe | 1,500,000,000 |
| 3. | H/W Rombo | 3,389,867,836 | 8. | H/W Kigoma | 1,494,826,301 |
| 4. | H/W Rufiji | 2,852,830,016 | 9. | H/W Mwanga | 600,000,000 |
| 5. | H/Jiji Mbeya | 2,000,000,000 | | **Jumla** | **28,168,320,070** |

Utekelezaji wa miradi bila kufanya tathmini ya athari za mazingira unaziweka mamlaka za serikali za mitaa katika hatari za kupata athari za mazingira ambazo zinaweza kuathiri jamii katika maeneo husika, na kusababisha hasara ya upotevu wa rasilimali.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe mamlaka zote za serikali za mitaa zinafanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wa ujenzi wa miradi ili kuhakikisha unafaa na ni endelevu na kuepuka madhara kwa mazingira.**

### 9.1.7 Mikataba Ambayo Haikuhakikiwa na Mwanasheria Halmashauri yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.59

Kanuni ya 60 ya Kanuni za Manunuzi wa Umma, 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 3 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016 [Tangazo la Serikali Na.121 la tarehe 22 Aprili, 2016] inataka mkataba unaotokana na utoaji wa zabuni ambayo thamani yake ni chini ya shilingi bilioni moja kuhakikiwa na Mwanasheria wa Taasisi nunuzi kabla ya kusainiwa na wahusika.

Nimekagua usimamizi wa mikataba, na kubaini mamlaka 12 za serikali za mitaa zilizosaini mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 1.59 kabla mikataba hiyo kupitiwa na mwanasheria wa halmashauri husika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-8** hapo chini.

**Jedwali Na. 9-8: Mikataba isiyohakikiwa na mwanasheria**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Kondoa | 89,125,500 | 8. | H/W Handeni | 202,212,392 |
| 2. | H/W Kongwa | 37,002,500 | 9. | H/Mji Handeni | 168,690,000 |
| 3. | H/W Muleba | 35,000,000 | 10. | H/W Kibondo | 286,604,800 |
| 4. | H/W Mpanda | 114,600,000 | 11. | H/W Maswa | 214,600,000 |
| 5. | H/W Bariadi | 221,533,690 | 12. | H/W Wang'ing'ombe | 150,000,000 |
| 6. | H/W Iramba | 21,500,000 | | | |
| 7. | H/W Sikonge | 52,950,000 | | **Jumla** | **1,593,818,882** |

Kwa maoni yangu, kusaini mkataba kabla ya kuhakiki na kujumuisha maoni ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwanasheria wa halmashauri kunaziweka halmashauri husika katika hatari za kisheria na kuhatarisha thamani ya fedha inayoweza kupatikana katika kutekeleza mikataba.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe mikataba ya mamlaka za serikali za mitaa inahakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au mwanasheria wa halmashauri kabla ya kusainiwa na kuanza kutumika ili kuepuka migogoro ya kisheria inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi.**

### 9.1.8 Ununuzi wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 4.61 Uliofanyika Kutoka kwa Wazabuni Ambao Hawakuwa na Mikataba na Wakala wa Ununuzi Serikalini

Wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa ununuzi na mikataba nilibaini Halmashauri 34 zilizofanya ununuzi wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 4.61 kwa wazabuni ambao hawakuwa na mkataba wa makubaliano na Wakala wa Ununuzi Serikalini kinyume na Kanuni ya 131 (4) (b) ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2013 kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Marekebisho) za 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la 30/12/2016). Halmashauri zilizonunua bidhaa kutoka kwa wazabuni wasiopitishwa na wakala wa Ununuzi zimeorodheshwa katika **Jedwali Na.9-9**.

**Jedwali Na. 9-9: Ununuzi kwa Wazabuni wasiokuwa na mikataba**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Chalinze | 449,365,049 | 19. | H/W Nzega | 69,591,980 |
| 2. | H/W Kisarawe | 430,986,655 | 20. | H/Mji Makambako | 69,266,900 |
| 3. | H/W Nyang'hwale | 376,073,380 | 21. | H/W Mkalama | 67,541,000 |
| 4. | H/W Ruangwa | 330,399,480 | 22. | H/W Urambo | 64,363,290 |
| 5. | H/W Chato | 308,756,637 | 23. | H/W Buchosa | 57,310,786 |
| 6. | H/W Rombo | 276,335,012 | 24. | H/Mji Masasi | 56,393,398 |
| 7. | H/Mji Tunduma | 251,427,344 | 25. | H/W Handeni | 54,875,300 |
| 8. | H/W Geita | 211,654,580 | 26. | H/Mji Njombe | 46,300,064 |
| 9. | H/W Mafia | 189,356,918 | 27. | H/W Moshi | 43,025,796 |
| 10. | H/W Bukombe | 169,464,500 | 28. | H/W Mufindi | 39,476,022 |
| 11. | H/W Ikungi | 163,410,772 | 29. | H/M Iringa | 38,945,582 |
| 12. | H/M Moshi | 152,195,713 | 30. | H/W Tarime | 27,326,718 |
| 13. | H/W Kasulu | 150,395,000 | 31. | H/Mji Kibaha | 16,989,051 |
| 14. | H/M Shinyanga | 107,708,570 | 32. | H/W Rungwe | 11,800,000 |
| 15. | H/Mji Korogwe | 103,911,441 | 33. | H/W Mbogwe | 11,655,000 |
| 16. | H/W Mbozi | 96,923,393 | 34. | H/W Iramba | 2,309,628 |
| 17. | H/W Makete | 87,761,858 | | **Jumla** | **4,606,133,517** |
| 18. | H/W Kishapu | 72,836,700 | | | |

Kwa maoni yangu, kufanya ununuzi kutoka kwa wazabuni wasiokuwa na mikataba ya makubaliano na Wakala wa Ununuzi Serikalini kunaleta wasiwasi iwapo bidhaa zilinunuliwa katika ubora na bei sahihi.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe ununuzi wowote wa bidhaa na huduma katika mamlaka zote za serikali za mitaa unafanywa kutoka kwa wazabuni walio na mikataba na Wakala wa Ununuzi Serikalini ili kutoa fursa sawa kwa wazabuni stahiki.**

## 9.2 Mapugufu katika Usimamizi wa Mikataba

Lengo kuu la ukaguzi wa usimamizi wa mikataba lilikuwa kutathmini iwapo kulikuwa na usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa mikataba ya miradi iliyotekelezwa katika mamlaka za serikali za mitaa nchini. Ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa yanayofafanuliwa hapa chini.

### 9.2.1 Kiasi cha Shilingi Milioni 310.42 Ambacho Hakikurudishwa na Wakandarasi Baada ya Kuvunjika kwa Mikataba Katika Halmashauri za Wilaya ya Madaba na Kibondo

Ukaguzi wa jalada la mkataba Na.LGA/182/HQ/W/HQ2018/2019/02 katika Halmashauri ya Wilaya Madaba kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi kwa gharama ya shilingi bilioni 2.29 ulibaini kuwa mkataba ulivunjwa tarehe 18 Juni 2020 baada ya mkandarasi kuvunja masharti ya mkataba. Pia, katika mapitio ya mkataba Na. LGA/041/HQ/AGRICO/2019/20/W/1 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kwa ajili ya ujenzi wa ghala la kukusanyia mazao katika Kijiji cha Kagezi kwa gharama ya shilingi milioni 286.27 nilibaini kuwa mkataba ulivunjwa kwa barua yenye kumbu Na. H/W A. 20/29/25 ya tarehe 2 Juni 2021 kufuatia mkandarasi kuvunja masharti ya mkataba.

Hata hivyo, Halmashauri za Wilaya ya Madaba na Kibondo hazikuweza kurejeshewa kiasi cha shilingi milioni 229.76 na shilingi milioni 51.43 mtawalia ikiwa ni asilimia 40 ya thamani ya kazi ambazo hazikufanyika kutoka kwa wakandarasi wawili hali iliyosababisha halmashauri hizo kuingia gharama za ziada katika kumalizia kazi.

Pia, katika kuvunja mkataba, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo haijarudishiwa jumla ya shilingi milioni 29.23 zilizohesabika kama gharama za uvunjaji wa mkataba ambazo zililipwa kwa mkandarasi

baada ya mkandarasi kuomba asikatwe fedha hizo hadi cheti cha mwisho.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwachukulia hatua stahiki maofisa masuuli pamoja na wakuu wa vitengo vya ununuzi wa Halmashauri hizi mbili kwa kushindwa kutekeleza vifungu vya sheria ya ununuzi.**

### 9.2.2 Malipo ya Shilingi Milioni 104.3 ya Mikataba ya Kukusanya Taka Yaliyofanyika Zaidi ya Viwango Vilivyoidhinishwa

Kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1) cha Sheria Ndogo za Halmashauri za tarehe 06/03/2020, Halmashauri itatoza ada ya ukusanyaji wa taka kutoka kwa kila kaya au jengo la biashara kwa kiwango cha shilingi 250,000 kwa safari kwa ajili ya kuzoa taka za soko.
Hata hivyo, nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliingia mikataba wa kununua huduma ya uzoaji taka kupitia mikataba na wazabuni watatu kwa viwango vya shilingi 450,000, shilingi 600,000 na shilingi 550,000 kwa kila safari badala ya shilingi 250,000 iliyoelezwa katika Sheria Ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Kutokana na kutotumia viwango vya soko vilivyopitishwa, halmashauri iliwalipa zaidi watoahuduma kiasi cha shilingi 104.3, hali inayothibitisha kutofuatwa kwa viwango vilivyopitishwa kulikosababisha ufujaji wa fedha za umma.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwachukulia hatua za kisheria maofisa waliohusika katika ununuzi wa huduma za kuzoa taka.**

### 9.2.3 Ukiukwaji wa Masharti ya Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wenye Thamani ya Shilingi Milioni 560.25

Tarehe 19 Mei 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ilisaini mkataba Na. LGA/021/2020-2021/HQC/W/02 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi kwa gharama ya shilingi milioni 560.25.

Kupitia ukaguzi nilioufanya pamoja na kutembelea mradi nilibaini kuwa hakukuwa na usimamizi madhubuti katika utekelezaji wa mradi kwa kuwa wasimamizi wa mradi hawakuwa na sifa stahiki. Msimamizi wa mradi kwa upande wa Halmashauri alikuwa mwalimu wa shule ya sekondari, na mtumishi aliyepo kama mhandisi hakuwa na vyeti vya taaluma hiyo.

Kwa ujumla, tathmini inaonesha kuwa mkandarasi alitumia vibarua wasio na sifa zilizoainishwa katika mkataba kwa kuzingatia elimu na ujuzi waliokuwa nao vibarua waliokuwapo eneo la mradi. Vibarua wote walishindwa kuwasilisha vyeti vinavyoonesha viwango vya elimu, ujuzi au uzoefu kwa ajili ya ukaguzi. Pia, kwa mujibu wa Kifungu cha 41 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, ofisa masuuli, bodi ya zabuni, kitengo cha usimamizi wa ununuzi, idara ya watumiaji na kamati ya tathmini inatakiwa kufanya kazi kwa uhuru bila kuwa na uhusiano binafsi katika kazi za mamlaka zao.

Kinyume chake, katika mwaka wa ukaguzi, nilibaini kuwa Ofisa Mipango wa Wilaya alihusika katika utiaji saini wa mkataba ambao uhitaji wa ununuzi huo ulitokea katika idara yake na ulithaminishwa na kamati ambayo yeye alikuwa mwenyekiti. Hali hii inaashiria mgongano wa maslahi na usimamizi hafifu wa mkataba.

**Ninasisitiza Ofisi ya Rais - TAMISEMI iweke usimamizi madhubuti wa ununuzi wa huduma za wakandarasi ikiwemo utekelezaji wa miradi ya ujenzi.**

### 9.2.4 Tuzo ya Mkataba kwa Mzabuni Mwenye Bei Kubwa Kulikosababisha Malipo Zaidi ya Shilingi Milioni 67 Katika Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro

Katika ukaguzi wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ufundi wa ujenzi wa jengo la utawala, Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro nilibaini wazabuni wawili walishiriki kuomba tuzo za mkataba ambapo nukuu zao za bei zilikuwa shilingi milioni 455.61 na shilingi milioni 810.5 bila kodi ya ongezeko la thamani.

Kwa mujibu wa taarifa ya timu ya tathmini, wazabuni wote wawili walikuwa na sifa kwa mujibu wa vigezo vilivyoainishwa katika nyaraka za maelekezo ya zabuni zilizotumwa kwa waombaji. Timu

ya tahmini ilipendekeza mkataba Na.LGA/005/2020/2021/ADB/W/1 utolewe kwa mzabuni wa pili kwa bei ya shilingi milioni 810 bila kodi ya ongezeko la thamani, kiasi ambacho baadaye kilipunguzwa na kufikia shilingi milioni 650 bila kodi ya ongezeko la thamani kufuatia majadiliano yaliyofanyika tarehe 27 Novemba 2020 badala ya tuzo hiyo kutolewa kwa mzabuni wa kwanza aliyeomba kufanya kazi hiyo kwa bei ya shilingi milioni 455.61 kinyume na Kanuni ya 212 (a) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

Hata hiyo, nilibaini kuwa mnamo tarehe 10 Machi 2021, Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro ilisaini mkataba Na. LGA/005/2020/2021/ADB/W/1 na mzabuni wa kwanza kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo kwa gharama ya shilingi milioni 522.62 wakati ambapo mkataba uliosainiwa awali na mzabuni wa pili bado ukiwa halali.

Halmashauri imeingia hasara ya shilingi milioni 67 kwa kutotoa zabuni kwa mzabuni wa kwanza katika bei ya awali ya shilingi 455.6 na hatimaye mradi ukatekelezwa na mzabuni huyohuyo kwa bei iliyoongezeka ya shilingi milioni 522.62

**Ninazishauri mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki maofisa waliohusika kwa kushindwa kufuata kanuni za ununuzi wa umma.**

### 9.2.5 Malipo Bila ya Vipimo vya Kazi Iliyofanyika Shilingi Bilioni 3.64

Kanuni ya 243(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, inazitaka taasisi zinazofanya manunuzi kuidhinisha malipo kulingana na vipimo na uthibitisho, katika vipindi au hatua zilizooneshwa katika mikataba na kwamba asilimia kadhaa ya thamani ya kazi zilizotekelezwa kutoka kila cheti cha malipo kinaweza kukatwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya matazamio endapo mkataba utaweka takwa hilo.

Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za serikali za mitaa 23 zililipa kiasi cha shilingi bilion 3.64 kwa kazi zilizotekelezwa bila uwapo wa nyaraka za vipimo za kazi zilizofanyika, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-10.**

**Jedwali Na. 9-10: Malipo bila ya vipimo vilivyoidhinishwa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Meru | 22,137,685 | 13. | H/W Mbeya | 45,185,375 |
| 2. | H/W Kibiti | 16,500,000 | 14. | H/W Makete | 33,390,500 |
| 3. | H/M Ubungo | 81,463,747 | 15. | H/W Kalambo | 348,700,678 |
| 4. | H/W Chemba | 30,200,000 | 16. | H/W Namtumbo | 43,796,250 |
| 5. | H/W Geita | 36,759,583 | 17. | H/M Shinyanga | 54,566,955 |
| 6. | H/W Mpanda | 4,270,000 | 18. | H/W Kaliua | 10,782,500 |
| 7. | H/W Mpimbwe | 55,635,000 | 19. | H/W Uyui | 3,026,145 |
| 8. | H/W Nsimbo | 8,490,000 | 20. | H/Mji Handeni | 6,650,000 |
| 9. | H/W Mwanga | 41,505,430 | 21. | H/W Mtama | 29,975,250 |
| 10. | H/W Rombo | 172,486,707 | 22. | H/W Mkinga | 11,059,790 |
| 11. | H/W Siha | 41,345,054 | 23. | H/Jiji Tanga | 69,337,889 |
| 12. | H/M Temeke | 2,470,000,000 | | **Jumla** | **3,637,264,538** |

**Chanzo:** Ripoti za mamlaka za serikali za mitaa

Kuidhinisha malipo bila kukagua na kujiridhisha kuwa kiasi cha fedha kinachopaswa kulipwa kinafanana na kazi zilizotekelezwa kunaweza kusababisha malipo ya ziada au malipo ya kazi ambazo hazijatekelezwa hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Napendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kuhakikisha serikali za mitaa zinapewa wahandisi wa kutosha wenye kiwango cha utaalamu kinachohitajika kufanya tathmini ya kazi zilizotekelezwa. Aidha, Maofisa Masuuli wa Halmashauri husika wanahimizwa kuweka udhibiti mathabuti wa ndani utakaohakikisha kazi zilizokamilika zinathibitishwa kabla ya kufanya malipo.**

### 9.2.6 Uwezekano wa Hasara kwa Kubadili Kazi Zilizoainishwa Katika Mkataba zenye Thamani ya Shilingi Milioni 365.58

Tarehe 3 Juni 2019, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke iliingia mkataba Na. LGA/016/2018-2019/W/DMDP/05 (chini ya Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam, Fungu Namba 10) kwa ajili ya ujenzi wa mradi katika Kata ya Mbagala (Bughudadi na Kizinga) kwa gharama ya shilingi bilioni 12.64.

Katika mapitio ya jalada la mikataba nilibaini kuwa, Halmashauri ilimuandikia mkandarasi barua yenye Kumb. Na.

TMC/DMDP/J.10/02/VOL. IV/73 ya tarehe 28 Oktoba 2021 kumtaarifu juu ya uamuzi wa kuondoa kipengele cha ujenzi wa soko la Zakhem kilichokuwa na gharama ya shilingi bilioni 2.26 sawa na asilimia 18 ya gharama ya mkataba.

Sababu ya kupunguza kazi hiyo kwenye mkataba ni kwamba Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam ulitakiwa kufunga utekelezaji wa mradi huo tarehe 31 Disemba 2021 na hivyo ilionekana mkandarasi asingemaliza ujenzi ndani ya muda wa utekelezaji.

Mkandarasi alijibu kwa barua yenye Kumb.Na. JCL/TMKE/DSM/MBG/474/2021 ya tarehe 12 Novemba 2021 akionesha kutokubaliana na Halmashauri kwa kudai fidia ya shilingi milioni 365.58 kwa ajili ya hasara ya rasilimali alizoelekeza katika mradi pamoja na faida ambayo angepata.

Kitendo cha mkandarasi kutoridhia mabadiliko ya mkataba kinaashiria kuwa Halmashauri inaweza kuingia hasara ya kulipa fidia na hivyo kusababisha uwapo wa matumizi yasiyo sahihi na kuongeza gharama ya mradi, hali itakayosababisha matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kiasi cha shilingi milioni 365.58

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua stahiki za kisheria kwa maofisa waliohusika katika mchakato wa ununuzi ikiwemo kuingia mkataba bila kuwa na mpangokazi sahihi hali inayoweza kusababisha Halmashauri kuingia hasara ya shilingi milioni 365.58 kwa kutofuata masharti ya mkataba na kusababisha halmashauri kuingia katika migogoro ya kisheria.**

### 9.2.7 Hasara Iliyotokana na Kutodai Fedha za Ukiukaji wa Mkataba Shilingi Milioni 593.24

Kifungu cha 20.1 cha Masharti ya Jumla ya Mikataba ya Hati ya Kawaida ya Zabuni (STD, 2018) kinawataka wakandarasi kuanza kazi kwa wakati na kutekeleza majukumu kwa mujibu wa mpangokazi ambao umehakikiwa na kuthibitishwa na msimamizi wa mradi na kumaliza kazi hizo katika muda uliopangwa.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilisaini mkataba Na. LGA/016/2019-2020/W/DMDP/01 kwa ajili ya ukarabati na

matengenezo ya barabara za ndani ya Halmashuri ya Temeke Fungu Na. 14 Nzasa – Kilungule - Buza na barabara za mitaa kwa mkataba wa shilingi bilioni 19.14

Katika ukaguzi wa jalada la mkataba, nilibaini kuwa mkandarasi aliongezewa muda wa kutekeleza mradi kwa siku 128 kwa barua yenye Kumbu Na. KCML/CRJE/PCKG9/19/202KJ na kusababisha muda wa kumaliza mradi kuwa tarehe 30 Juni 2021. Hata hivyo, hadi tarehe 1 Disemba 2021, mradi ulikuwa haujakamilika.

Nilibaini kuwa gharama za kutotimiza masharti ya mradi ambapo mkandarasi angepaswa kulipa kiasi cha shilingi milioni 593.24 sawa na asilimia 0.1 ya gharama ya mkataba kwa siku hazikujumuishwa katika madai ya ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mkataba kufuatia kutotekeleza Kifungu cha 47.1 cha masharti ya jumla ya mkataba.

**Ninasisitiza Ofisi ya Rais - TAMISEMI kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa kushirikiana na Ofisa Masuuli wa Halmashauri na kuhakikisha kuwa kiasi cha gharama za uvunjaji wa masharti ya mkataba cha shilingi milioni 593.24 kinakatwa kutoka vyeti vya malipo vya mkandarasi.**

## 9.3 Udhaifu Uliobainika katika Usimamizi wa Mikataba, Usimamizi wa Kazi, na Ununuzi wa Vifaa vya Ujenzi kwa Utaratibu wa Nguvukazi

Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imetoa miongozo inayopaswa kuzingatiwa katika kujenga na kukarabati miundombinu ya umma kama vile shule, hospitali, vituo vya afya, zahanati na majengo mengine ya umma kwa kutumia njia ya nguvukazi.

Katika kufanya tathmini ya matumizi ya nguvukazi, nilibaini kuwa mamlaka 135 za serikali za mitaa zilitumia jumla ya shilingi bilioni 350.95 kununua vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa shule, hospitali, vituo vya afya, zahanati na majengo mengine ya umma yaliyotekelezwa kwa njia ya nguvukazi kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.9-1**.

Pamoja na kwamba ninathamini na kutambua juhudi na hatua kubwa iliyofikiwa na Serikali katika kutimiza malengo yake kupitia njia ya nguvukazi, nilibaini kuwapo kwa mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kuangaliwa upya. Mapungufu yaliyobainika yanafafanuliwa hapa chini.

### 9.3.1 Ukiukaji wa Masharti Yaliyowekwa Ili Kuweza Kutumia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Nguvukazi Shilingi Bilioni 11.65

Kanuni ya 167(2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka, 2013 (kama ilivyorekebishwa na Kanuni ya 64 (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2016 (Tangazo la Serikali Na. 333 la 30.12.2016) inaelekeza muktadha na mazingira ambapo utarartibu wa utekelezaji wa miradi unaweza kufanywa na Taasisi nunuzi kwa mfumo wa ununuzi wa nguvukazi.

Katika kufanya tathmini ya uzingatiaji wa sheria, nilibaini mamlaka 16 za serikali za mitaa zilitekeleza miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 11.65 kwa njia ya nguvukazi bila kukidhi masharti yaliyoainishwa katika kanuni hizo. Mamlaka hizo ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 9-11** hapa chini.

**Jedwali Na. 9-11: Miradi iliyotekelezwa bila kuzingatia sheria**

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miradi | Thamani ya Miradi (Sh.) | Kigezo Kilichokiukwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Muleba | N/A | 493, 004,859 | Hakukuwa na uthibitisho endapo Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kiliwasilisha ombi la kutaka kutumia nguvukazi na endapo ombi hilo liliridhiwa na bodi ya zabuni |
| 2. | H/W Mpanda | 2 | 220,000,000 | |
| 3. | H/W Sengerema | 1 | 70,120,267 | |
| 4. | H/W Itilima | 1 | 500,000,000 | |
| 5. | H/W Sumbawanga | 1 | 43,000,000 | |
| 6. | H/W Rombo | 2 | 30,000,000 | Uteuzi wa mafundi bila ushindanishi |

| Na | Jina la Halmashauri | Idadi ya Miradi | Thamani ya Miradi (Sh.) | Kigezo Kilichokiukwa |
|---|---|---|---|---|
| 7. | H/W Kakonko | 6 | 2,171,019,000 | Kukosekana kwa wafanyakazi wenye sifa zinazohitajika kutekeleza na kusimamia kazi hizi |
| 8. | H/W Bariadi | 50 | 2,034,399,522 | |
| 9. | H/W Ileje | 1 | 20,000,000 | |
| 10. | H/W Chamwino | 1 | 3,726,820,679 | |
| 11. | H/W Chemba | 11 | 50,000,000 | |
| 12. | H/W Mufindi | 11 | 1,163,000,000 | |
| 13. | H/W Kyela | 6 | 195,000,000 | |
| 14. | H/W Kwimba | N/A | 220,000,000 | |
| 15. | H/W Kalambo | 1 | 500,000,000 | |
| 16. | H/W Uyui | 5 | 220,000,000 | |
| Jumla | | | **11,656,364,327** | |

**Chanzo: Ripoti Husika za mamlaka za serikali za mitaa, 2021**

Mapungufu yaliyobainika yalichangiwa na kukinzana kwa maelekezo ya mamlaka mbalimbali kama vile wizara, viongozi wa mikoa na wilaya, na viongozi wa kisiasa.

**Ninapendekeza kwamba Serikali ianzishe mfumo utakaohusika na kuratibu maelekezo yote yanayotolewa kwa mamlaka za serikali za mitaa, ambao maagizo yoyote kutoka kwa mamlaka na viongozi wengine yapitishwe kupitia mfumo huo ulioidhinishwa ili kuepuka kupokea maelekezo kutoka vyanzo mbalimbali yanayokinzana na mengine kutozingatia matakwa ya sheria.**

### 9.3.2 Miradi Isiyokidhi Ubora yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 6.06 Iliyotekelezwa kwa Njia ya Nguvukazi

Katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi iliyokamilika na inayoendelea katika mamlaka za serikali za mitaa, nilibaini kuwa mamlaka 10 za serikali za mitaa zilitekeleza miradi ya ujenzi yenye viwango duni vya ubora. Kasoro hizi zilibainika katika baadhi ya miradi kuanzia katika ujenzi wa msingi wa majengo hadi kumalizika kwa miradi. Baadhi ya mapungufu niliyoyabaini ni nyufa kwenye majengo na majengo mengine kuwa na misingi iliyotitia. Pia, kulikuwa na mamlaka zinazotumia mbao ambazo hazikuwekwa dawa ya kuzilinda zisishambuliwe na wadudu wakati wa kupaua majengo.

Pamoja na mapungufu hayo, nilibaini pia kukulikuwa na mamlaka za serikali za mitaa amabazo zilitumia mbao mbichi (mbao ambazo hazijakauka) katika milango na madirisha hivyo kusababisha kusinyaa, kuvimba au kupinda kwa milango na madirisha. Mamlaka ambazo zilikuwa na miradi yenye viwango duni zinaoneshwa katika **Jedwali Na. 9-12.**

**Jedwali Na. 9-12: Miradi iliyotekelezwa bila kuzingatia ubora**

| Na. | Jina la Halmashauri | Thamani ya mradi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Mkuranga | 153,200,000 |
| 2. | H/W Chamwino | 4,430,721,498 |
| 3. | H/W Mpimbwe | 281,345,000 |
| 4. | H/W Kigoma | 114,529,513 |
| 5. | H/W Rombo | 118,635,300 |
| 6. | H/W Sengerema | 713,729,289 |
| 7. | H/W Kishapu | 93,472,080 |
| 8. | H/Mji Bariadi | 60,000,000 |
| 9. | H/Mji Nzega | 40,000,000 |
| 10. | H/Mji Handeni | 51,658,250 |
| **Jumla** | | **6,057,290,930** |

**Chanzo:** Ripoti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2021

Mamlaka za serikali za mitaa kushindwa kupima vifaa vya ujenzi na kushindwa kuchukua hatua za tahadhari kunaiweka Serikali katika hatari ya kujenga upya au kufanyia ukarabati miradi iliyobainika kutokidhi viwango kwa kipindi kifupi kijacho hivyo kusababisha upotevu wa fedha za Serikali bila sababu za msingi.

**Ninapendekeza kwa maofisa masuuli wa mamlaka za serikali za mitaa husika (a) waimarishe usimamizi wa mikataba ili kuepusha kazi zisizokidhi viwango; na (b) halmashauri zinasisitizwa kuweka kipengele katika mikataba ya ujenzi na ununuzi wa vifaa kitachotaka mafundi kurudia kazi walizozifanya chini ya kiwango na wazabuni kuleta tena vifaa vyenye ubora uliokuwa umeagizwa bila ongezeko la malipo.**

### 9.3.3 Kutoandaliwa kwa Mchanganuo wa Vifaa kwa Miradi ya Ujenzi yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.78

Kipengele cha 11.1 cha Mwongozo wa Nguvukazi kwa Taasisi Nunuzi Nchini Tanzania uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kinazitaka idara tumizi kueleza kazi za ujenzi au matengenezo zinazotakiwa kutekelezwa.

Halikadhalika, kipengele cha 11.2 cha mwongozo huohuo kinaelekeza kuwa "Ikiwa idara ya watumiaji ni tofauti na idara yenye ujuzi wa kitaalamu, basi idara ya watumiaji itapaswa kuomba wataalamu kutoka idara hiyo (au mtumishi mwenye taaluma stahiki ndani ya taasisi nunuzi au kwa ushirika na taasisi nyingine nunuzi) ili kubainisha upeo wa kazi kwa kuandaa michoro, vipimo, na mchanganuo wa idadi ya bidhaa kwa ajili ya kutekeleza kazi husika".

Katika kufanya tathmini ya mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa nguvukazi, nilibaini kuwa mamlaka 17 za serikali za mitaa zilikuwa zinatekeleza miradi ya maendeleo bila kuwa na mchangunuo wa vifaa vinavyohitajika katika ujenzi. Na kwasababu hiyo niligundua kuwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.78 vilinunuliwa bila ya kuwapo kwa makisio sahihi ya vifaa vya ujenzi. Mamlaka za serikali za mitaa zilizotekeleza miradi ya ujenzi kwa nguvukazi na kufanya ununuzi bila kuandaa makisio na mchanganuo wa vifaa ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-13**.

**Jedwali Na. 9-13: Miradi iliyotekelezwa bila mchangunuo wa vifaa**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 419,726,419 | 10. | H/W Kalambo | 500,000,000 |
| 2. | H/W Mufindi | 1,163,000,000 | 11. | H/W Nkasi | N/A |
| 3. | H/W Hai | 17,714,106 | 12. | H/W Kishapu | 55,046,500 |
| 4. | H/W Rombo | 150,000,000 | 13. | H/M Shinyanga | 23,824,500 |
| 5. | H/M Lindi | 1,824,993,550 | 14. | H/W Ikungi | 200,000,000 |
| 6. | H/W Babati | N/A | 15. | H/W Kaliua | 83,791,891 |
| 7. | H/M Tarime | 48,895,677 | 16. | H/Mji Nzega | 40,000,000 |
| 8. | H/W Mbeya | 145,000,000 | 17. | H/W Mkinga | N/A |
| 9. | H/W Mvomero | 114,296,102 | | **Jumla** | **4,786,288,744** |

**Chanzo: Ripoti za mamlaka za serikali za mitaa**

Mapungufu yaliyobainika yalisababishwa na idadi ndogo ya wahandisi na mafundi mchundo katika mamlaka za serikali za mitaa. Upungufu wa wataalamu hao ulitokana na kuhamishwa kwa watumishi kutoka katika mamlaka za serikali za mitaa kwenda Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini na Mijini (RUWASA).

Ununuzi wa vifaa vya ujenzi bila vipimo vilivyoainishwa na makadirio ya mchanganuo wa vifaa vinavyohitajika katika ujenzi unaweza si tu kusababisha ununuzi wa vitu visivyo na viwango, bali pia unaweza kusababisha ununuzi wa vifaa zaidi ya mahitaji halisi katika miradi na hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma.

**Ninapendekeza mamlaka za serikali za mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zihakikishe zinapewa wahandisi na wakadiriaji majenzi wa kutosha ili kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

### 9.3.4 Utunzaji Mbovu wa Vifaa vya Ujenzi Vilivyotumika katika Ujenzi wa Miradi kwa Njia ya Nguvukazi yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.48

Agizo la 58 (1) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linataka bidhaa zilizowasilishwa kukaguliwa ili kuhakikisha kuwa zinaendana na viwango na vipimo vilivyobainishwa kabla hazijakubaliwa. Pia, Agizo la 59 (1) na (2) la Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linaeleza kuwa baada ya bidhaa kuchunguzwa na/au kupimwa, pale inapobidi, na wanaohusika na upimaji kuwa wamesaini na kuthibitisha usahihi wa bidhaa husika, ofisa wa stoo atapaswa kuingiza bidhaa hizo katika daftari la bidhaa husika. Kisha, kila ingizo katika daftari la vifaa linapaswa kuwa na hati inayoweza kufuatiliwa kama vile hati ya madai kutoka kwa mzabuni, au hati za kurejeshea bidhaa kwa mzabuni.

Hali kadhalika, Agizo la 54(3) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 linazitaka taasisi nunuzi kuhifadhi kumbukumbu kila inapopokea bidhaa, kutoa bidhaa na kuandika idadi ya kila bidhaa iliyoko katika stoo katika ukurasa tofauti na daftari la vifaa.

Kinyume na maagizo yaliyotajwa, nilibaini mamlaka 26 za serikali za mitaazililipia vifaa mbalimbali vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi bilioni 3.37 bila kuzingatia matakwa ya maagizo yaliyotajwa hapo juu. **Jedwali Na. 9-14** linaonesha mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikuzingatia maagizo ya hapo juu.

**Jedwali Na. 9-14: Utunzaji usiofaa wa vifaa vya ujenzi**

| Na | Jina la Halmshauri | Thamani ya mradi (Sh.) | Na | Jina la Halmshauri | Thamani ya mradi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Kigamboni | 20,899,976 | 15. | H/W Kishapu | 120,320,970 |
| 2. | H/M Kinondoni | 898,470,016 | 16. | H/W Msalala | 275,283,100 |
| 3. | H/W Chato | 140,792,500 | 17. | H/W Bariadi | 8,515,000 |
| 4. | H/W Iringa | 116,976,028 | 18. | H/W Itilima | 4,547,000 |
| 5. | H/W Mpanda | 74,092,800 | 19. | H/W Ikungi | 32,237,500 |
| 6. | H/W Hai | 57,204,096 | 20. | H/W Manyoni | 306,256,688 |
| 7. | H/W Babati | 19,389,642 | 21. | H/W Kaliua | 65,056,826 |
| 8. | H/W Kiteto | 7,819,500 | 22. | H/Mji Nzega | 17,000,000 |
| 9. | H/Mji Nanyamba | 220,278,500 | 23. | H/W Sikonge | 93,793,104 |
| 10. | H/W Ukerewe | 57,975,000 | 24. | H/W Handeni | 63,169,573 |
| 11. | H/W Madaba | 242,823,968 | 25. | H/Mji Handeni | 213,421,885 |
| 12. | H/W Mbinga | 21,290,000 | 26. | H/W Korogwe | 4,200,000 |
| 13. | H/W Songea | 182,614,130 | **Jumla** | | **3,375,539,192** |
| 14. | H/M Kahama | 111,111,390 | | | |

***Chanzo**: Chanzo: Ripoti mahususi za Mamlaka za Serikali za mitaa*

Katika hali ambayo haikutarajiwa, nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama iliandaa ripoti ya ukaguzi wa vifaa na mapokezi ya vifaa vya thamani ya shilingi milioni 107.76 kabla vifaa hivyo havijapokelewa. Kutokana na dosari hizo nimeshindwa kuthibitisha uhalali wa manunuzi na matumizi ya vifaa husika katika miradi.

Kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa katika madaftari husika ya kuhifadhia kumbukumbu za vifaa hivyo kulinifanya nishindwe kuthibitisha matumizi ya vifaa hivyo.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa husika (a) kuzingatia udhibiti uliowekwa wa uwajibikaji kwa bidhaa zilizonunuliwa na kuhakikisha bidhaa zote zilizopokelewa zimeingizwa katika leja ya vifaa; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zinashauriwa kuandaa taarifa za kukiri kupokea mizigo katika ubora na idadi iliyoagizwa kabla ya mapokezi ya bidhaa husika.**

### 9.3.5 Kazi na malipo yaliyofanywa kwa mafundi bila kuwapo kwa mikataba yenye thamani ya shilingi milioni 947.92

Kifungu cha 60(7) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kinataka pale zabuni, tuzo au pendekezo linapokuwa limekubaliwa na ofisa masuuli, taasisi nunuzi na mtu ambaye zabuni, tuzo au pendekezo lake limekubaliwa, kuingia katika mkataba rasmi wa usambazaji wa bidhaa, utoaji wa huduma au kufanya kazi.

Vivyo hivyo, Vipengele vya 25.1 na 25.2 vya Mwongozo wa Kufanya Kazi kwa Kutumia Nguvukazi kwa Taasisi Nunuzi Nchini iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma tarehe 22 Mei 2020 vinasema kuwa "Malipo kwa taasisi zinazotumia utaratibu wa nguvukazi yanaweza kufanyika kwa utaratibu wa malipo kwa kazi zilizofanyika kwa kuzingatia viwango vya malipo vilivyopo kwenye mkataba na kwamba taasisi au chombo kinachotekeleza kazi kitawasilisha madai ya malipo kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika mkataba".

Katika kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi nilibaini kuwa mamlaka 12 za serikali za mitaa zilitumia mafundi kwenye ujenzi wa majengo bila kuwa na mikataba nao ya kisheria. Kwa hali hiyo, nilishindwa kuthibitisha uhalali wa malipo kwa mafundi hao. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizowalipa mafunzi wa mtaani bila kuwa na mikataba ya kisheria ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-15**.

**Jedwali Na. 9-15: Malipo bila kuwapo kwa mikataba na mafundi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Nsimbo | 13,358,000 | 8. | H/M Shinyanga | 32,803,688 |
| 2. | H/W Mwanga | 27,940,333 | 9. | H/W Bariadi | 221,533,690 |
| 3. | H/W Newala | 22,120,000 | 10. | H/W Itilima | 64,350,000 |
| 4. | H/W Buchosa | 83,800,000 | 11. | H/W Bumbuli | 150,000,000 |
| 5. | H/W Sengerema | 90,402,000 | 12. | H/W Handeni | 30,157,250 |
| 6. | H/W Kishapu | 22,258,600 | | **Jumla** | **947,923,561** |
| 7. | H/W Msalala | 189,200,000 | | | |

Chanzo: Chanzo: Ripoti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, 2021

Mapungufu yaliyobainika yalitokana na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mikataba ya ujenzi katika mamlaka husika za serikali za mitaa.

**Ninashauri mamlaka za serikali za mitaa husika (a) zizingatie sheria na kanuni katika usimamizi wa mikataba ya ujenzi kwa kuhakikisha kuna mikataba ya kisheria na mafundi wa mtaani; na (b) ninashauri mamlaka za serikali za mitaa husika kuanzisha mfumo wa udhibiti wa ndani ambao utatoa tathmini ya mara kwa mara ya mikataba.**

### 9.3.6 Bidhaa zenye Thamani ya Shilingi Milioni 239.16 Zilizonunuliwa Zaidi ya Mahitaji

Kipengele cha 11.1 cha Mwongozo wa Kufanya Kazi kwa Kutumia Nguvukazi kwa Taasisi Nunuzi Nchini iliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kinaitaka idara tumizi au idara ya ufundi kueleza kazi ya ujenzi au matengenezo inayohitajika kutekelezwa.

Katika tathmini ya vifaa vya ujenzi vilivyonunuliwa na uhakiki wa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi nilibaini mamlaka 10 za serikali za mitaa zilinunua vifaa vingi vya ujenzi kuliko mahitaji halisi. Ununuzi wa ziada ya vifaa yaligharimu shilingi milioni 239.16 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 9-16.**

**Jedwali Na. 9-16: Bidhaa zilizonunuliwa zaidi ya mahitaji halisi**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Longido | 23,093,000 | 7. | H/W Manyoni | 154,718,580 |
| 2. | H/W Kakonko | 6,144,000 | 8. | H/W Ileje | 20,299,948 |
| 3. | H/W Mwanga | 14,844,430 | 9. | H/W Kaliua | 2,172,000 |
| 4. | H/Mji Tarime | 10,315,742 | 10. | H/M Tabora | 2,036,500 |
| 5. | H/W Kwimba | 4,436,000 | | | |
| 6. | H/M Kahama | 1,100,000 | | **Jumla** | **239,160,200** |

***Chanzo:*** *Chanzo: Ripoti za mamlaka za serikali za mitaa*

Wakati wa kutembelea miradi, nilibaini kuwa vifaa hivi vya ujenzi vilikuwa vimeachwa katika vituo vilivyokuwa vikitekeleza miradi hiyo huku ujenzi ukiwa umeshakalika.

Kununua vifaa vya ujenzi ambavyo havikutumika katika miradi iliyokusudiwa kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma iwapo bidhaa hizo zitatumika kwa manufaa binafsi ama kutumika kinyume na malengo yaliyowekwa.

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe michanganuo ya mahitaji wa vifaa vya ujenzi vinavyohitajika inaandaliwa kwa usahihi ili kukwepa kununua zaidi ya vifaa vya ujenzi vinavyotakiwa. Pia, mamlaka za serikali za mitaa husika zinahimizwa kuhakikisha vifaa vilivyobaki vinahamishwa na kutumika katika miradi mingine ya ujenzi yenye uhitaji wa vifaa hivyo.**

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

## SURA YA 10

## UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA ELIMU

### 10.0 Utangulizi

Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina jukumu la kusimamia ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari, watu wazima na elimu isiyo rasmi Tanzania Bara kwa kuhakikisha kuwa shule zote zinasimamiwa vyema ikiwa pamoja na kuwa na walimu wa kutosha na wenye uwezo, miundombinu ya kutosha, vitendeakazi, na vifaa vya shule.

Tangu mwaka 1997, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yenye dhamana ya elimu imekuwa ikiandaa Mipango ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (ESDP). Mipango hii imejengwa katika vipaumbele vya Serikali kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya Mwaka 2025 na kuweka vigezo vya maendeleo ya sekta ya elimu katika kipindi cha miaka mitano kupitia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa utendaji na ufanisi wa serikali za mitaa katika usimamizi wa shule zilizo chini ya mamlaka yake kama ilivyoanishwa hapa chini:-

### 10.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupeleka shuleni vitabu vya kiada pungufu Shilingi Bilioni 19.42

Aya ya 1 & 2 za Waraka wa Ruzuku kwa Shule za Msingi za Serikali (elimu bila malipo) wenye Kumb.Na.DC.297/507/01/39 ya tarehe 28 Desemba, 2015 unataka Serikali kutoa fidia ya shilingi 10,000 na shilingi 25,000 kwa mwaka kwa kila mwanafunzi katika shule za msingi na sekondari mtawalia; ambapo wizara itatumia asilimia 40 kununua vitabu na kusambaza shuleni.

Nilifanya ukaguzi katika mamlaka 22 za serikali za mitaa kuhusu utekelezaji wa waraka ulionukuliwa na kubaini kuwa, ili kukidhi mahitaji ya vitabu kwa wanafunzi katika shule za msingi za Serikali vilihitajika vitabu 6,323,566. Hata hivyo, ni vitabu vya kiada 1,467,829 (sawa asilimia 23) vilisambazwa katika mwaka huo,

ikionesha upungufu wa vitabu 4,855,737 vyenye thamani ya shilingi bilioni 19.42 kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 10-1** hapa chini.

**Jedwali Na.10-1: Vitabu vya kiada vilivyotolewa pungufu**

| Na. | Jina la Halmashauri | Mahitaji | Vilivyoletwa | Pungufu | Kiasi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Babati | 130,488 | 0 | 130,488 | 4,000 | 521,952,000 |
| 2. | H/Mji Bariadi | 7,168 | 4,342 | 2,826 | 4,000 | 11,304,000 |
| 3. | H/W Buchosa | 767,564 | 50,391 | 717,173 | 4,000 | 2,868,692,000 |
| 4. | H/W Bumbuli | 194,221 | 49,740 | 144,481 | 4,000 | 577,924,000 |
| 5. | H/W Bunda | 165,839 | 54,571 | 111,268 | 4,000 | 445,072,000 |
| 6. | H/Jiji Dodoma | 653,835 | 208,596 | 445,239 | 4,000 | 1,780,956,000 |
| 7. | H/W Karatu | 91,798 | 24,517 | 67,281 | 4,000 | 269,124,000 |
| 8. | H/MKinondoni | 538,652 | 37,315 | 501,337 | 4,000 | 2,005,348,000 |
| 9. | H/W Ludewa | 630,189 | 218,624 | 411,565 | 4,000 | 1,646,260,000 |
| 10. | H/W Mlele | 95,196 | 26,586 | 68,610 | 4,000 | 274,440,000 |
| 11. | H/W Mpanda | 345,126 | 2,753 | 342,373 | 4,000 | 1,369,492,000 |
| 12. | H/MMpanda | 362,810 | 113,874 | 248,936 | 4,000 | 995,744,000 |
| 13. | H/W Mpimbwe | 222,496 | 23,375 | 199,121 | 4,000 | 796,484,000 |
| 14. | H/W Muheza | 315,656 | 112,573 | 203,083 | 4,000 | 812,332,000 |
| 15. | H/W Mwanga | 24,715 | 17,546 | 7,169 | 4,000 | 28,676,000 |
| 16. | H/W Nsimbo | 43,044 | 38,538 | 4,506 | 4,000 | 18,024,000 |
| 17. | H/W Nyanghw'ale | 275,586 | 79,380 | 196,206 | 4,000 | 784,824,000 |
| 18. | H/W Pangani | 80,291 | 22,157 | 58,134 | 4,000 | 232,536,000 |
| 19. | H/W Rombo | 41,132 | 18,792 | 22,340 | 4,000 | 89,360,000 |
| 20. | H/W Rorya | 16,627 | 4,899 | 11,728 | 4,000 | 46,912,000 |
| 21. | H/W Tarime | 762,280 | 116,928 | 645,352 | 4,000 | 2,581,408,000 |
| 22. | H/M Ubungo | 558,853 | 242,332 | 316,521 | 4,000 | 1,266,084,000 |
| **Jumla** | | **5,975,665** | **6,323,566** | **1,467,829** | | **19,422,948,000** |

Chanzo: Ripoti za Elimu ya Shule za Msingi, 2021

Utoaji wa vitabu pungufu vya kiada unachangiwa na jitihada duni za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, katika kuhakikisha kiasi cha asilimia 40 ya fidia ya Serikali inatumika kununua vitabu vya kiada na kusambazwa kwa shule za Serikali, kwa kuzingatia viwango vya uwiano wa mwanafunzi kwa kitabu. Kutofuata waraka uliotajwa kunaathiri matokeo ya kitaaluma kwa wanafunzi.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika siku zijazo, izingatie Aya ya 1 & 2 za Waraka wa Ruzuku kwa Wanafunzi kwa kuhakikisha asilimia 40 ya fedha za fidia ya Serikali zinatumika kununua vitabu vya kiada na kusambazwa**

**katika shule za msingi za Serikali ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi kwa uwiano wa mwanafunzi mmoja kitabu kimoja.**

## 10.2 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Kutoa Fedha Pungufu Shilingi Bilioni 4.25 kwa ajili ya Ada ya Ruzuku ya Elimu bila Malipo

Aya ya 1 & 2 za Waraka wa Ruzuku kwa Wanafunzi kwa Shule za Serikali (elimu bila malipo) wenye Kumb. Na. DC.297/507/01/39 (Shule za Msingi) na Kumb. Na. DC.297/507/01/40 wa tarehe 28 Desemba 2015 (Shule za Sekondari) ziliitaka Serikali kulipa fidia ya shilingi 10,000 na 25,000 mtawalia kwa mwaka kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Nilifanya ukaguzi wa fedha zilizotolewa kwa ajili ya elimu bila malipo katika mamlaka 25 za serikali za mitaa na kubaini kuwa katika mwaka wa fedha 2020/21, fedha za ruzuku kwa shule za msingi na sekondari zilitolewa pungufu kwa kiasi cha Sh. 4,252,600,723 kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 10-1.**

Upungufu wa fedha unaotokana na ufinyu wa bajeti unaweza kuathiri taaluma kwani shule nyingi zinakosa mahitaji muhimu ya kuwezesha kutoa elimu bora kama vile ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na nyenzo za kujifunzia.

**Ili kuimarisha ubora wa elimu nchini, ninapendekeza Hazina na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupanga bajeti toshelevu kwa ajili ya elimu bila malipo na ruzuku itolewe kulingana na bajeti iliyoidhinishwa.**

## 10.3 Upungufu wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari

Aya ya 4.3.1 ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia 2016/17 hadi 2020/21 umeonesha vitu vinavyoboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia ni vyumba vya madarasa, madawati, vitabu vya kiada, vyoo/uwiano wa vyoo na kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu wa ngazi zote, (kutoa malipo linganifu, makazi kuwa karibu na eneo kazi).

Pamoja na Serikali hivi karibuni kuongeza jitihada katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa miundombinu mfano vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, ofisi, viti na meza katika shule za msingi na

sekondari, tathmini yangu kuhusu upatikanaji wa miundombinu hiyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 77 imebaini uwapo wa upungufu wa miundombinu, 516,642 katika Shule za Msingi na 136,278 katika shule za sekondari kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10-2.**

**Jedwali Na. 10- 2: Uhaba wa miundombinu ya shule**

| Shule za Msingi | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Vifaa** | **Mahitaji** | **Vilivyopo** | **Upungufu** |
| 1. | Madarasa | 124,268 | 49,533 | 74,735 |
| 2. | Nyumba za Walimu | 90,742 | 17,607 | 73,135 |
| 3. | Ofisi za Walimu | 9,730 | 4,618 | 5,112 |
| 4. | Viti | 150,833 | 84,944 | 65,889 |
| 5. | Meza | 632,062 | 446,222 | 185,840 |
| 6. | Matundu ya Vyoo | 178,547 | 66,616 | 111,931 |
| **Jumla** | | **1,186,182** | **669,540** | **516,642** |
| **Shule za Sekondari** | | | | |
| **Na.** | **Vifaa** | **Mahitaji** | **Vilivyopo** | **Upungufu** |
| 1. | Madarasa | 16,319 | 13,250 | 3,069 |
| 2. | Nyumba za Walimu | 22,103 | 4,011 | 18,092 |
| 3. | Ofisi za Walimu | 2,044 | 637 | 1,407 |
| 4. | Viti | 249,274 | 204,437 | 44,837 |
| 5. | Meza | 359,324 | 302,161 | 57,163 |
| 6. | Matundu ya Vyoo - Wanafunzi | 29,096 | 17,600 | 11,496 |
| 7. | Matundu ya Vyoo - Walimu | 762 | 548 | 214 |
| **Jumla** | | **678,922** | **542,644** | **136,278** |

Ufaulu wa kitaaluma unategemea mazingira mazuri ya kujifunzia, kuingilia kati kushughulikia uhaba wa miundombinu ya shule unapotokea.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoa fedha kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na kuweka mikakati inayotekelezeka ya kutokomeza au kupunguza tatizo la miundombinu kwa ajili ya kuimarisha ubora wa elimu.**

## 10.4 Upungufu wa Walimu katika Shule za Msingi

Aya ya 3.4.1 ya Sera ya Taifa ya Elimu ya Mwaka 2014 inataka kuwapo usimamizi wa rasilimaliwatu kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu na mafunzo. Moja ya malengo ya Sera hiyo ni kuhakikisha

ifikapo mwisho wa mwaka 2022, lengo la uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi la 1:45 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45) linatimia.

Nilitathmini uwiano wa walimu na wanafunzi katika mamlaka 48 za serikali za mitaa na nilibaini kati ya walimu 40,458 wanaohitajika kwa shule za msingi walikuwa 23,881 tu ikimaanisha upungufu wa walimu 16,571 sawa na asilimia 41 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 10-2**. Hali hii imechangiwa na walimu wapya kutoripoti katika maeneo ya vijijini; na kutokana na mazingira ya kazi yasiyoridhisha kusababisha walimu walioajiriwa kutafuta uhamisho wa kwenda mijini.

Kwa maoni yangu, upungufu niliubaini katika mamlaka 48 za serikali za mitaa nilizozibainisha zinatoa taswira kuwa hali hii inaweza kuwaathiri kwa kiwango kikubwa wanafunzi kitaaluma nchini.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Hazina (a) itoe fedha za kutosha na kuweka mikakati inayotekelezeka ili kukabiliana na upungufu uliobainika kwa kuboresha uwezo wa waalimu kitaaluma na kuinua ari yao kwa kuboresha mazingira ya kufundishia; na (b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI itafute kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuziba pengo lililopo.**

## 10.5 Idadi Kubwa ya Wanafunzi Kukatisha Masomo kabla ya Kumaliza Darasa la Saba

Kifungu cha 4.3.1 cha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kiliweka kiwango halisi cha uwiano wa uandikishaji wa elimu ya msingi kuwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2022. Uwekezaji unaoendelea wa serikali katika elimu umesababisha kuongeza uandikishaji ambao unachangiwa zaidi na kuanzishwa kwa elimu ya msingi bila ada. Nilichukua sampuli za mamlaka 27 za serikali za mitaa na kubaini kuwa kati ya mwaka 2018 na 2021, wanafunzi 18,670 walishindwa kuhitimu elimu ya msingi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 10-3** hapa chini.

**Jedwali Na. 10-3: Idadi ya wanafunzi waliokatisha masomo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Walioandikishwa | Waliomaliza | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mbozi | 13,524 | 11,733 | 1,791 |
| 2. | H/Mji Tunduma | 3,786 | 3,527 | 259 |
| 3. | H/W Kakonko | 4,050 | 2,957 | 1,093 |
| 4. | H/W Kishapu | 7,605 | 6,490 | 1,115 |
| 5. | H/W Mbogwe | 7,505 | 5,397 | 2,108 |
| 6. | H/W Mlele | 887 | 668 | 219 |
| 7. | H/W Mpanda | 5,587 | 3,675 | 1,912 |
| 8. | H/W Mpimbwe | 2,316 | 1,732 | 584 |
| 9. | H/W Nsimbo | 4,618 | 2,594 | 2,024 |
| 10. | H/W Songwe | 3,263 | 2,315 | 948 |
| 11. | H/W Tabora | 6,245 | 5,768 | 477 |
| 12. | H/M Tarime | 3,162 | 2,872 | 290 |
| 13. | H/W Urambo | 8,137 | 3,729 | 4,408 |
| 14. | H/Mji Babati | 3,810 | 2,368 | 1,442 |
| 15. | H/W Kiteto | 5,194 | 3,770 | 1,424 |
| 16. | H/W Bunda | 13,625 | 6,060 | 7,565 |
| 17. | H/W Magu | 12,424 | 9,645 | 2,779 |
| 18. | H/W Mbogwe | 7,505 | 5,397 | 2,108 |
| 19. | H/W Musoma | 7,232 | 5,560 | 1,672 |
| 20. | H/W Shinyanga | 6,835 | 6,814 | 21 |
| 21. | H/M Shinyanga | 4,983 | 2,294 | 2,689 |
| 22. | Tarime H/W | 12,775 | 8,289 | 4,486 |
| 23. | H/W Ushetu | 9,219 | 5,945 | 3,274 |
| 24. | H/W Biharamulo | 9,511 | 5,579 | 3,932 |
| 25. | H/W Songea | 3,560 | 3,164 | 396 |
| 26. | H/W Babati | 14,569 | 10,669 | 3,900 |
| 27. | H/Mji Mbulu | 2,224 | 1,385 | 839 |
| **Jumla** | | **74,495** | **55,825** | **18,670** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Elimu ya Shule za Msingi, 2021*

Mwenendo wa kuacha shule umekuwa ukipungua katika miaka ya hivi karibuni kutokana na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa elimu na mpango wa serikali wa elimu bila malipo kama inavyofafanuliwa katika **Kielelezo Na. 10-1** hapa chini.

**Kielelezo Na. 10-1: Mwenendo wa kukatisha masomo kwa wanafunzi wa shule za msingi**




Tathmini yangu ilibainisha kuwa sababu kuu za kuacha shule kwa wasichana zilihusiana na matukio ya ujauzito ambayo zilizotokana na umbali mrefu kutoka nyumbani hadi shule, asili ya familia, na masuala ya binafsi.

**Ninapendekeza kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iandae programu za kuifikia jamii ili kutoa ushauri kwa wazazi kuwaandikisha watoto wao katika shule zilizo karibu; na mazingira ya kufundishia na kujifunzia yanatakiwa kuwa rafiki na ya kuvutia kwa kujumuisha nyenzo stahiki za kufundishia, pamoja na kutoa elimu ya taaluma na ufundi stadi.**

## 10.6 Upungufu wa Uandikishaji wa Wanafunzi Shule za Msingi

Nilifanya tathmini ya hali ya mpango wa uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi za Serikali kati ya mwaka 2018 na 2021 katika mamlaka 16 za serikali za mitaa na kubaini kuwa kulikuwa na tofauti ya wanafunzi 9,427 kama inavyofafanuliwa katika **Jedwali Na. 10-4.**

**Jedwali Na. 10-4: Kiwango cha chini cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi**

| Na. | Mamlaka ya Serikali ya Mtaa | Makadirio ya Uandikishaji | Uandikishaji Halisi | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/M Mpanda | 8,317 | 7,357 | 960 |
| 2. | H/W Nyangwale | 8,460 | 7,692 | 768 |
| 3. | H/W Tabora | 115,670 | 115,558 | 112 |

| Na. | Mamlaka ya Serikali ya Mtaa | Makadirio ya Uandikishaji | Uandikishaji Halisi | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| 4. | H/Mji Kibaha | 3,384 | 3,377 | 7 |
| 5. | H/W Buchosa | 14,682 | 14,466 | 216 |
| 6. | H/W Mlele | 2,827 | 2,353 | 474 |
| 7. | H/W Mpanda | 14,169 | 11,729 | 2,440 |
| 8. | H/M Tabora | 4,395 | 4,176 | 219 |
| 9. | H/W Ulanga | 5,439 | 5,089 | 350 |
| 10. | H/W Urambo | 7,715 | 7,167 | 548 |
| 11. | H/W Bunda | 10,156 | 10,025 | 131 |
| 12. | H/W Tarime | 12,144 | 12,125 | 19 |
| 13. | H/W Kilwa | 8,901 | 7,671 | 1,230 |
| 14. | H/M Lindi | 2,242 | 2,110 | 132 |
| 15. | H/W Morogoro | 11,022 | 10,619 | 403 |
| 16. | H/W Mtama | 5,778 | 4,360 | 1,418 |
| **Jumla** | | **23,5301** | **22,5874** | **9,427** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Elimu ya Shule za Msingi, 2021*

Ingawa kuna upungufu wa idadi ya wanafunzu walioandikishwa kwa mwaka, mwenendo wa uandikishaji umekuwa ukiongezeka kwa kiasi ikilinganishwa na wakati mpango ulipoanza mwaka 2019. Rejea **kielelezo Na. 10- 2**

**Kielelezo Na. 10- 2: Mwenendo wa Uandikishaji wa Wanafunzi wa Shule za Msingi kwa Miaka Mitatu**




***Chanzo:*** *Taarifa za Elimu ya Shule za Msingi, 2021*

Zaidi ya hayo, nimebaini changamoto kuu zinazochangia kuandikisha wanafunzi pungufu ni kuwapo kwa shule binafsi katika maeneo ya mjini. Kwa upande wa vijijini, sababu ni pamoja na kuhamahama

kwa familia zinazojishughulisha na ufugaji, maeneo ya kijiografia, na uelewa mdogo wa umuhimu wa elimu kwa baadhi ya jamii ambapo sehemu kubwa ya wazazi wanapendelea watoto wao kulima na kuchunga mifugo kuliko kwenda shule.

**Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wadau wengine kuwezesha uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu na kuboresha mazingira ya shule hususani vijijini.**

# SURA YA 11

# UFANISI WA KIUTENDAJI KATIKA SEKTA YA AFYA

## 11.0 Utangulizi

Afya njema ni muhimu katika kukuza ustawi wa watu na maendeleo ya taifa. Kutokana na matokeo ya ukaguzi yaliyooneshwa katika ripoti yangu ya serikali za mitaa, sekta ya afya bado ina changamoto mbalimbali za upungufu wa rasilimali zikiwemo wafanyakazi wasio na mafunzo, bajeti ndogo, mazingira duni ya kazi, uhaba wa dawa na vifaatiba na upungufu wa miundombinu.

Kupitia ukaguzi wa mwenendo wa utoaji wa huduma za afya katika kipindi cha miaka mitatu nilibaini kuwa, licha ya jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali katika kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma za msingi za afya, bado kuna changamoto zinazoathiri upatikanaji wa huduma bora za afya hasa kwa wananchi wa kawaida.

Sura hii inatoa baadhi ya changamoto katika sekta ya afya, kwa kuonesha maeneo muhimu ambayo yanahitaji usimamizi makini, na kushauri hatua ambazo serikali na wadau wengine wanaweza kuchukua ili kutatua changamoto hizo, ambazo baadhi zimeanishwa hapa chini: -

## 11.1 Kuchelewa Kukamilika kwa Ujenzi wa Vituo vya Afya

Katika kufanya tathmini ya utendaji wa kazi katika miradi iliyotekelezwa, nilibaini kulikuwa na mamlaka 54 za serikali za mitaa zilizopokea kiasi cha shilingi bilioni 31.10 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa majengo, ikiwemo hospitali za wilaya, vituo vya afya na zahanati.

Wakati wa mapitio ya mikataba na taarifa za utekelezaji wa miradi na kutembelea miradi nilibaini kuchelewa kukamilika kwa ujenzi kwa kipindi cha kati ya miezi mitatu hadi miaka mitatu. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye miradi iliyochelewa kukamilika imeoneshwa katika **Jedwali Na. 11-1** hapo chini.

**Jedwali Na. 11-1: Miradi ya majengo yaliyochelewa kukamilika**

| Na. | Jina la Halmashauri | Gharama ya Mradi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Gharama ya Mradi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | H/W Geita | 4,106,000,000 | 29 | H/W Ngara | 400,000,000 |
| 2 | H/W Moshi | 2,500,000,000 | 30 | H/W Nachingwea | 400,000,000 |
| 3 | H/Mji Kondoa | 1,977,660,749 | 31 | H/W Kilindi | 400,000,000 |
| 4 | H/W Sengerema | 1,417,797,820 | 32 | H/W Rombo | 387,543,766 |
| 5 | H/W Madaba | 1,150,000,000 | 33 | H/W Tarime | 384,575,150 |
| 6 | H/W Mpanda | 1,090,000,000 | 34 | H/W Msalala | 357,550,250 |
| 7 | H/W Wang'ing'ombe | 1,000,000,000 | 35 | H/W Muleba | 347,362,400 |
| 8 | H/W Kigoma | 996,004,020 | 36 | H/W Magu | 298,598,250 |
| 9 | H/W Mufindi | 950,000,000 | 37 | H/W Chemba | 295,000,000 |
| 10 | H/M Sumbawanga | 897,002,420 | 38 | H/M Morogoro | 281,569,575 |
| 11 | H/W Mtama | 720,000,000 | 39 | H/W Manyoni | 220,000,000 |
| 12 | H/W Lushoto | 694,467,322 | 40 | H/W Nzega | 220,000,000 |
| 13 | H/W Gairo | 650,000,000 | 41 | H/W Ikungi | 200,000,000 |
| 14 | H/Mji Kibaha | 605,000,000 | 42 | H/W Busega | 184,400,000 |
| 15 | H/W Bariadi | 596,870,574 | 43 | H/Mji Mafinga | 150000000 |
| 16 | H/W Handeni | 580,327,070 | 44 | H/W Bumbuli | 150,000,000 |
| 17 | H/W Kalambo | 545,000,000 | 45 | H/W Momba | 141,580,388 |
| 18 | H/W Mafia | 500,000,000 | 46 | H/Mji Nzega | 120,000,000 |
| 19 | H/W Ruangwa | 500,000,000 | 47 | H/W Karagwe | 75,840,000 |
| 20 | H/W Mbeya | 500,000,000 | 48 | H/Jiji Arusha | 52,427,900 |
| 21 | H/Mji Nanyamba | 500,000,000 | 49 | H/W Arusha | 50,000,000 |
| 22 | H/W Newala | 500,000,000 | 50 | H/W Chamwino | 50,000,000 |
| 23 | H/W Mbinga | 500,000,000 | 51 | H/W Nyang'hwale | 50,000,000 |
| 24 | H/W Itilima | 500,000,000 | 52 | H/Mji Makambako | 50,000,000 |
| 25 | H/M Iringa | 460,773,698 | 53 | H/W Mbozi | 50,000,000 |
| 26 | H/Jiji Tanga | 453,373,990 | 54 | H/W Korogwe | 50,000,000 |
| 27 | H/W Tandahimba | 445,000,000 | Jumla | | **31,101,725,342** |
| 28 | H/W Monduli | 400,000,000 | | | |

Sababu za ucheleweshaji ni kuchelewa kutolewa kwa fedha za mradi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwenda katika mamlaka za serikali za mitaa; ucheleweshaji wa usambazaji wa vifaa vya ujenzi kutoka kwa wazabuni; upungufu wa watumishi wataalamu; ufinyu wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya vituo vya afya; na athari za hali mbaya ya hewa.

Kwa upande mwingine, muda unaotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hakuwa na uhalisia kwa kuwa wakati mwingine hauhusishi muda wa maandalizi ya vifaa vya ujenzi na muda wa kusubiri kukauka kwa zege kabla ya kuendelea na hatua zingine za ujenzi.

Aidha, mamlaka 41 za serikali za mitaa zilipewa jumla ya shilingi bilioni 32.65 kwa ajili ya kukamilisha vituo vya afya ambavyo havikuwa vimekamilika kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 11-2**.

Kwa mtazamo wangu, kuna hatari kubwa ya Serikali kutokufikia malengo ya kuanzisha vituo vya afya katika kila wilaya kama ilivyokusudiwa katika Dira ya Mpango wa Maendeleo wa Tanzania, 2025.

**Ninapendekeza kwa mamlaka zinazohusika katika usimamizi na ujenzi wa majengo ya afya nchini kuyafanyia kazi mapungufu yaliyoainishwa kwa kuweka mikakati ambayo itahakikisha miradi inatekelezwa na kukamilika ndani ya muda uliopangwa ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.**

## 11.2 Mamlaka za Serikali za Mitaa Zilizochelewa Kuanza Ujenzi wa Majengo ya Vituo vya Afya

Nilibaini mamlaka 8 za serikali za mitaa zilichelewa kuanza ujenzi wa miradi ya majengo ya vituo vya afya ambavyo baadhi yake ujenzi ulichelewa kuanza kwa takribani miezi 6 tangu fedha zilipopokelewa.

Sababu kubwa ya kuchelewa kuanza kwa ujenzi na ukamilishaji wa majengo ya miradi ya vituo vya afya ni pamoja na kamati za usimamizi wa ujenzi kukosa uelewa wa namna ya miradi inavyotekelezwa kwa kutumia nguvukazi; mchakato wa ununuzi kutumia muda mrefu kablya ya kuanza ujenzi wa vituo vya afya; na kuchelewa kuhamisha fedha kutoka mamlaka za serikali za mitaa kwenda ngazi za chini kunakotekelezwa miradi. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zilizochelewa kuanza ujenzi imeoneshwa katika **Jedwali Na. 11-2**.

**Jedwali Na. 11-2: Halmashauri zenye miradi iliyochelewa kuanza ujenzi wa vituo vya afya**

| Na. | Jina la Halmashauri | Thamani (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Mbarali | 500,000,000 |
| 2. | H/W Malinyi | 500,000,000 |
| 3. | H/W Wang'ing'ombe | 500,000,000 |
| 4. | H/W Kasulu | 400,000,000 |
| 5. | H/W Buchosa | 250,000,000 |
| 6. | H/W Mbozi | 200,000,000 |
| 7. | H/W Iringa | 150,000,000 |
| 8. | H/W Rorya | 150,000,000 |
| **Jumla** | | **2,650,000,000** |

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI na mamlaka za serikali za mitaa kuandaa mipango ya kazi yenye uhalisia na ratiba za ununuzi wa vifaa vya ujenzi zitakazozingatiwa wakati wa utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya afya. Utekelezaji wa miradi unapaswa kuzingatia muda wa usanifu unaohitajika, uandaaji wa vitendeakazi, mchakato wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi ikiwa pamoja na kipindi cha kusubiri kukauka kwa zege kabla ya kuendelea na hatua zinazofuata za ujenzi ili kuhakikisha miradi inakamilika ndani ya muda uliopangwa.**

## 11.3 Miradi ya Afya Yenye Thamani ya Shilingi Bilioni 3.98 Iliyokamilika lakini Haitumiki

Nilibaini miradi ya majengo ya afya iliyokamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 3.98 katika mamlaka 20 za serikali za mitaa ambayo haikuwa ikitumika kama ilivyokusudiwa. Miradi hii inajumuisha vyumba vya upasuaji, vyumba vya kuhifadhi maiti, wodi, zahanati, na vituo vya afya. Hali hii inamaanisha kuwa thamani ya fedha kwenye miradi husika haikupatikana na kuna athari ya kupungua thamani kwa miradi ya vituo vya afya kutokana na uchakavu. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye majengo yaliyokamilika lakini hayatumiki zimeoneshwa katika **Jedwali Na. 11-3**.

**Jedwali Na. 11-3: Vituo vya afya viliyokamilika lakini havitumiki**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Iramba | 199,000,000 | 12. | H/W Kilolo | 120,000,000 |
| 2. | H/W Busega | 543,879,085 | 13. | H/W Kyerwa | 100,000,000 |
| 3. | H/W Songea | 450,000,000 | 14. | H/Mji Kasulu | 100,000,000 |
| 4. | H/W Namtumbo | 433,745,800 | 15. | H/Mji Handeni | 99,746,174 |
| 5. | H/W Morogoro | 383,704,516 | 16. | H/Mji Kibaha | 75,000,000 |
| 6. | H/Mji Newala | 346,667,590 | 17. | H/M Kigoma Ujiji | 70,000,000 |
| 7. | H/W Maswa | 280,082,579 | 18. | H/W Mkuranga | 66,500,000 |
| 8. | H/W Igunga | 154,000,000 | 19. | H/W Kibondo | 60,722,050 |
| 9. | H/W Kibaha | 150,000,000 | 20. | H/W Kaliua | 50,000,000 |
| 10. | H/W Buchosa | 150,000,000 | | **Jumla** | **3,983,047,794** |
| 11. | H/W Kalambo | 150,000,000 | | | |

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa husika zichukue hatua stahiki katika kuhakikisha miradi yote iliyokamilika inatumika ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa pamoja na kupata thamani ya fedha zilizotumika katika miradi hiyo ya vituo vya afya.**

## 11.4 Hasara ya Shilingi Bilioni 3.49 Iliyotokana na Dawa Zilizokwisha Muda wa Matumizi

Aya ya 4.11 na 4.14 za Randama ya Maelewano kati ya Bohadi Kuu ya Dawa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto unaitaka Bohari Kuu ya Dawa kupanga namna ya kuteketeza dawa na bidhaa za afya zilizokwisha muda wake, na kutoa taarifa kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya kuwapo kwa dawa na bidhaa za afya zilizokwisha muda wa matumizi (zaidi ya miezi kumi).

Katika ukaguzi wa rejista ya dawa, nilibaini kuwapo kwa dawa ambazo muda wa matumizi umepita katika mamlaka 46 za serikali za mitaa. Dawa hizo ambazo zimeendelea kuwapo kwa kipindi cha kati ya miezi mitatu hadi miaka 20 zina thamani ya shilingi bilioni 3.49. Kuwapo kwa dawa zilizokwisha muda wake kunasababishwa na kupokea dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa zenye muda mfupi wa matumizi na kukosekana kwa mfumo wa upokeaji na utoaji wa dawa unaohakikisha dawa zilizonunuliwa kwanza ndizo zinazoanza kutumika.

Kuendelea kutunza dawa zilizomaliza muda wa matumizi bila kuziteketeza kunaweza kusababisha madhara kwa umma ikiwa kwa bahati mbaya zitatumika au kuangukia mikononi mwa watu wasiokuwa na maadili. Mwenendo wa mamlaka za serikali za mitaa zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi kwa miaka mitatu mfululizo umeoneshwa katika **Jedwali Na. 11-4** hapa chini.

**Jedwali Na. 11-4: Mwenendo wa halmashauri zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi**

| Mwa wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kipindi (Miaka) | Thamani ya Dawa (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 46 | 0-20 | 3,490,306,860 |
| 2019/20 | 31 | 0-20 | 1,537,713,125 |
| 2018/19 | 14 | 0-19 | 7,334,114,927 |

Mwelekeo hapo juu unaonesha idadi ya mamlaka za serikali za mitaa zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi imeongezeka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/20. Hali hii inamaanisha kuwa mapendekezo yangu ya ukaguzi kwa miaka iliyopita hayajazingatiwa na mamlaka za serikali za mitaa husika. Mamlaka hizo za serikali za mitaa zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 11-2.**

**Ninatoa wito kwa mamlaka za serikali za mitaa zenye dawa zilizokwisha muda wa matumizi (a) ziteketeze dawa hizo kwa mujibu wa sheria; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zenye mapungufu yaliyobainishwa zinashauriwa kufanyia kazi mapungufu hayo kabla ya kuagiza dawa zingine na kuzingatia kiwango cha juu cha kuagiza dawa.**

## 11.5 Changamoto Zilizobainishwa katika Utekelezaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulianza mwaka 1996 ukiwa na matarajio ya kuenea nchi nzima. Mpango huo ulitambuliwa kama utaratibu wa kutoa fursa ya upatikanaji wa huduma za msingi za afya kwa idadi kubwa ya watu katika maeneo ya vijijini na sekta isiyo rasmi. Lengo lake kuu halikuwa kuongeza fedha za ziada bali kuboresha makundi maskini na yaliyo katika mazingira magumu kupata huduma za afya.

Serikali ilianzisha mpango wa afya ya jamii ulioboreshwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii ya Mwaka 2001 kwa lengo la kuwezesha utoaji wa huduma za afya zenye ubora, usawa, zinazopatikana, nafuu, endelevu, na zinazozingatia jinsia kwa jamii ili kufikia malengo ya kitaifa ya sekta ya afya.

Mpango huu unafanikiwa kwa kukusanya rasilimalifedha kutoka kwa jamii (kaya) kwa kila mwaka, na Serikali inachangia kiasi sawa na kinacholipwa na kaya. Mfuko wa Afya ya Jamii una utaratibu wa kutoa ankara za madai kwa huduma kama zinavyotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Mfuko wa Afya ya Jamii una malengo ya kufuatilia makusanyo ya mapato, utoaji wa huduma bora za afya kwa bei nafuu, na uboreshaji wa huduma za afya kwa jamii.

Aya ya 3.3 ya Usimamizi wa Fedha za Afya ya Jamii na Mwongozo wa Uendeshaji wa Mwaka 2014 unasema "Timu ya Menejimenti ya Mfuko wa Afya ya Jamii inapaswa kukamilisha na kuomba kwa wakati msaada linganifu". Wakati wa ukaguzi, nilibaini mapungufu yanayoelezwa hapa chini.

### 11.5.1 Madai Yenye Thamani ya Milioni 220.86 ya Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa ambayo Hayakulipwa

Aya ya 4.5 ya Usimamizi wa Fedha za Afya ya Jamii na Mwongozo wa Uendeshaji wa Mwaka 2014 inaeleza kuwa "Watoa huduma za afya (hospitali, vituo vya afya na zahanati) wanapaswa kulipwa kila mwezi moja kwa moja kwenye akaunti za vituo". Aya inaeleza zaidi kwamba "kiasi cha fedha kinachopaswa kulipwa kwa kila kituo kinapatikana kwa kutumia fomula kulingana na mambo matatu, ambapo kwa zahanati na kituo cha afya), malipo hufanywa kwa kuzingatia (i) huduma iliyotolewa kwa mwanachama wa Mfuko (idadi ya ujio), (ii) idadi ya jamii kwenye kituo, na iii) idadi ya jamii wenye bima (wanachama hai)".

Kinyume na matakwa ya aya tajwa, katika kipindi cha mwaka unaokaguliwa, mamlaka nane za serikali za mitaa kupitia vituo vya afya zilidai jumla ya shilingi milioni 220.86 ambazo hazijalipwa kama ilivyoonekana katika **Jedwali Na. 11-5** hapa chini.

**Jedwali Na. 11-5: Madai ambayo hayakulipwa na mfuko wa afya ya jamii**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Kalambo | 23,665,544 |
| 2. | H/W Mtama | 110,875,000 |
| 3. | H/Mji Korogwe | 16,292,673 |
| 4. | H/W Ludewa | 15,618,600 |
| 5. | H/M Singida | 15,228,438 |
| 6. | H/W Misungwi | 15,063,840 |
| 7. | H/W Sengerema | 14,677,200 |
| 8. | H/W Kibondo | 9,437,829 |
| **Jumla** | | **220,859,124** |

**Ninazishauri mamlaka za serikali za mitaa husika (a) ziweke utaratibu madhubuti wa kupitia madai ya Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa kabla ya kuyawasilisha kwa ajili ya marejesho; na (b) kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba madai ambayo hayajalipwa na Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa yanalipwa.**

### 11.5.2 Uendeshaji Duni wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa (iCHF)

Tathmini yangu ya ufanisi wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa katika kufikia mipango na malengo yaliyokusudiwa ilibaini mapungufu yafuatayo:

(i) Baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa zilishindwa kufikia malengo yaliyowekwa ya kusajili kaya hivyo kukosa makusanyo ya shilingi milioni 667.29 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 11-6** hapo chini.

(ii) Kuwapo kwa mawasiliano yasiyoridhisha kati ya mamlaka za serikali za mitaa na sekretarieti za mikoa juu ya usimamizi wa fedha zilizokusanywa na ulipaji wa marejesho. Hakukuwa na usuluhishi uliofanywa kwa kiasi kilichodaiwa na mamlaka za serikali za mitaa husika.

(iii) Hali ya madai ya Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa yaliyofanyiwa kazi haioneshwi katika mfumo; na taarifa za kaya zilizochangia zinatofautiana kati ya mfumo mmoja na mwingine.

(iv) Kuchelewa kutuma marejesho ya fedha kwenye vituo kwa madai ya huduma zilizotolewa; pia, fomula maalumu ya kufanya hesabu ya kiasi kinachopaswa kurejeshwa vituoni haikuweza kufahamika.

(v) Mafunzo duni hutolewa kwa maofisa wasajili, hivyo kusababisha matumizi yasiyoridhisha ya Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Bima (IMIS) wakati wa usajili wa wanakaya.

(vi) Uhaba wa fedha kwa ajili ya kuwezesha usafiri kwa ajili ya shughuli za usajili na shughuli za usimamizi.

**Jedwali Na. 11-6: Halmashauri zenye mfuko wa afya ya jamii ulioboreshwa zisizokuwa na ufanisi**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Mji Njombe | 271,260,000 |
| 2. | H/W Sikonge | 101,940,000 |
| 3. | H/W Itilima | 82,680,913 |
| 4. | H/W Handeni | 59,971,961 |
| 5. | H/W Igunga | 52,260,000 |
| 6. | H/M Tabora | 45,330,000 |
| 7. | H/Mji Kasulu | 39,640,500 |
| 8. | H/W Mbogwe | 8,510,000 |
| 9. | H/W Bariadi | 5,698,110 |
| **Jumla** | | **667,291,484** |

**Ninapendekeza uongozi wa mamlaka za serikali za mitaa kuzingatia mwongozo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Kifedha wa Mfuko wa Afya ya Jamii Ulioboreshwa ili kupata manufaa na malengo ya Mfuko.**

## 11.6 Malipo ya Shilingi Bilioni 1.17 kwa Dawa na Vifaatiba ambavyo Havikupokelewa

Katika mapitio ya malipo yaliyofanywa na mamlaka za serikali za mitaa kwa ajili ya dawa na vifaatiba katika vituo vya afya, nilibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2021, Bohari Kuu ya Dawa haikupeleka dawa na vifaatiba vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.17 kwa mamlaka 9 za serikali za mitaa. Kutopeleka bidhaa hizo kunaathiri

uwezo na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na watendaji na wahudumu wa sekta ya afya kwa jamii. Orodha la mamlaka za serikali za mitaa zenye mapungufu yaliyobainishwa imeoneshwa katika **Jedwali Na. 11-7** hapa chini.

**Jedwali Na. 11-7: Dawa na Vifaatiba ambavyo Havikupokelewa**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) | Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Mbinga | 422,558,996 | 6. | H/M Kahama | 31,646,500 |
| 2. | H/Mji Mbinga | 304,793,554 | 7. | H/W Mpanda | 24,468,700 |
| 3. | H/W Longido | 184,593,204 | 8. | H/Mji Handeni | 15,739,700 |
| 4. | H/M Songea | 113,110,672 | 9. | H/W Mkinga | 1,334,690 |
| 5. | H/Jiji Mwanza | 70,231,600 | | **Jumla** | **1,168,477,616** |

**Ninapendekeza kuwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Dawa ibuni mikakati itakayohakikisha inawasilisha dawa na vifaatiba kwa mamlaka za serikali za mitaa husika ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa vituo vya afya.**

## 11.7 Hasara ya Shilingi Bilioni 2.34 Itokanayo na Madai Kukataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Tathmini yangu katika hospitali, vituo vya afya na zahanati ilibaini kuwapo kwa madai ya gharama za huduma kwa wagonjwa wanaostahili kupata huduma za afya kwa njia ya bima yaliyowasilishwa na mamlaka 111 za serikali za mitaa katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Hata hivyo, madai ya jumla ya shilingi bilioni 2.34 yalikataliwa kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 11-3.**

Hali hii ilichangiwa na madai hayo kutofuata taratibu pamoja na makosa kama vile idhini batili, kanuni za magonjwa zisizofaa, kutofuata miongozo ya kawaida ya matibabu, kutoonesha kipimo cha uchunguzi, na kutoa huduma ambazo hazikuainishwa katika mkataba na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Nilibaini kuwa madai yaliyokataliwa yaliongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita kwa zaidi ya shilingi milioni 520 ikimaanisha kwamba mapendekezo yangu ya awali kuhusu suala hili hayakutekelezwa ipasavyo.

Madai yaliyokataliwa ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yanaathiri uthabiti wa vituo vya kutoa huduma za afya kwa jamii kwani kunaweza kusababisha uhaba wa rasilimalifedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa vya matibabu.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI iandae na itoe mafunzo stahiki ili kuwajengea uwezo watumishi wa afya kuhusu ujazaji sahihi wa fomu za madai ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuzuia tatizo kujirudia.**

## SURA YA 12

## UFANISI WA MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU

### 12.0 Utangulizi

Mwaka 1993, Serikali kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilianzisha Mfuko wa fedha wa Maendeleo kwa Wanawake na Vijana ili kuwainua wanawake na vijana wasiojiweza kiuchumi ambapo wengi wao hawakidhi vigezo vya mikopo inayotolewa na taasisi za fedha kutokana na ukosefu wa dhamana. Kwa wakati huo, mikopo hiyo ya uwezeshaji ilitolewa asilimia 5 kwa wanawake na asilimia 5kwa vijana.

Mnamo mwaka 2019, Serikali kupitia Bunge lilirekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290 [Iliyorejewa 2019] kwa kuongeza kifungu cha 37A mahususi kwa ajili ya kuwezesha mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kifungu cha 37A(1) cha Sheria hii kinazitaka Halmashauri zote kutenga asilimia 10 ya mapato yao ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu vilivyosajiliwa. Vile vile, Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye Ulemavu, 2019 (Tangazo la Serikali Na. 286 la 5/04/2019) zinataka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vilivyosajiliwa vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.

Madhumuni ya Mfuko huu ni kuongeza uwezeshaji kiuchumi kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu, kwa kufanya shughuli za kiuchumi ili kuboresha kiwango chao cha maisha. Ili kuwezesha Mfuko uwe hai, mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuhakikisha kuwa fedha zinazokopeshwa kwa vikundi zinarejeshwa kwa mujibu wa makubaliano kati ya mamlaka za serikali za mitaa na vikundi vinavyonufaika na mkopo huo.

Katika kufuatilia uzingatiaji wa matakwa ya sheria iliyopo nilibaini kuwa, wanufaika wa vikundi katika mamlaka 155 za serikali za mitaa

hawakurejesha shilingi bilioni 47.01 kama marejesho ya mkopo. Aidha, mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia shilingi bilioni 6.68 katika Mfuko kama inavyotakiwa kisheria, jambo ambalo linazuia azma ya serikali ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kupunguza umaskini.

Pia, nilibaini mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 178.61 ilitolewa kwa vikundi visivyokuwa na sifa, na shilingi bilioni 1.24 hazikuhamishwa kutoka akaunti za amana za mamlaka 11 za serikali za mitaa kwenda akaunti maalum ya Mfuko, kinyume na Kanuni ya 22 (1) na (2) ya Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

### 12.1 Halmashauri kushindwa kukusanya shilingi bilioni 47.01 za marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi

Tathmini ya utendaji kazi wa Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu katika mamlaka 185 za serikali za mitaa imebaini kuwa, mamlaka 155 za serikali za mitaa hazikukusanya kiasi kikubwa cha marejesho ya mikopo ya shilingi bilioni 47.01 iliyotolewa kwenye vikundi vinavyodaiwa. Hali hii ni kutokana na kutokuwa na udhibiti mzuri wa usimamizi wa mikopo.

Tatizo lililobainika linamaanisha kwamba, mamlaka za serikali za mitaa husika zilitoa mikopo kabla ya kufanya uchambuzi wa kina wa historia ya ulipaji wa kikundi na kupitia mapendekezo ya mradi husika ili kuhakikisha kuwa kikundi kina uwezo wa kurejesha mkopo kwa wakati. Aidha, hakuna ufuatiliaji wa karibu wa kukusanya marejesho ya mikopo ambayo bado haijalipwa kutoka kwenye vikundi. Ni dhahiri kuwa kutorejeshwa mikopo kunaweza kuathiri Mfuko, hivyo kuufanya usiwe endelevu. **Kiambatisho Na. 12-1** kinaonesha orodha ya mamlaka za serikali za mitaa zenye mikopo ambayo haikurejeshwa.

**Jedwali Na. 12-1** linaonesha kiwango cha mikopo isiyorejeshwa ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa miaka mitano mfululizo.

Jedwali Na. 12- 1: Mikopo isiyorejeshwa

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi ambacho Hakijarejeshwa (Sh.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 155 | 47,006,024,260 | 70 |
| 2019/20 | 130 | 27,790,189,049 | 65 |
| 2018/19 | 111 | 13,794,359,981 | 59 |
| 2017/18 | 90 | 10,044,453,656 | 59 |
| 2016/17 | 84 | 5,809,326,477 | 63 |

**Ili kufikia lengo na uendelevu wa Mfuko, ninasisitiza mamlaka za serikali za mitaa kufanya tathmini kabla ya kutoa mikopo na kuweka juhudi zaidi katika kukusanya madeni ambayo bado hayajalipwa. Aidha, ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI ianzishe hatua madhubuti za kurejesha mikopo kwa kuhusisha wataalamu wa usimamizi wa mikopo ambao watahimiza uzingatiaji wa urejeshaji wa mikopo kwa hiari ili kufikia ukuaji endelevu wa Mfuko.**

## 12.2 Fedha Shilingi Bilioni 1.24 Ambazo Hazikuhamishwa Kutoka Akaunti ya Amana Kwenda Katika Akaunti ya Mfuko

Kanuni ya 22(1) na (2) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kufungua na kuendesha akaunti maalumu za mikopo na kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mikopo na fedha za marejesho ya mikopo hiyo zinaingizwa katika akaunti hiyo maalumu.

Ukaguzi nilioufanya katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu na akaunti za benki zilizofunguliwa umebaini kuwa, mamlaka 11 za serikali za mitaa hazikuwa zimehamisha kiasi cha shilingi bilioni 1.24 kutoka katika akaunti za amana kwenda akaunti maalumu za mikopo ya Mfuko ambazo zimefunguliwa ili kurahisisha shughuli za mikopo. Nina shaka kuwa fedha hizo zinaweza kutumika kutekeleza shughuli zisizokusudiwa na hivyo kuchelewesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanufaika. Orodha ya mamlaka za serikali za mitaa ambazo hazikuhamisha fedha kwenda akaunti maalumu za mikopo zinaoneshwa katika **Jedwali Na.12-2.**

**Jedwali Na. 12-2: Halmashauri ambazo hazikuhamishia fedha katika akaunti maalumu za mikopo**

| Na | Jina la Halmashauri | Kiasi Kisichohamishwa (Sh.) | Na | Jina la Halmashauri | Kiasi Kisichohamishwa (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/W Ushetu | 308,528,550 | 7. | H/W Bahi | 54,222,488 |
| 2. | H/W Iringa | 236,486,588 | 8. | H/W Busega | 49,090,000 |
| 3. | H/W Nanyumbu | 179,268,173 | 9. | H/W Momba | 41,795,000 |
| 4. | H/W Kilolo | 122,596,622 | 10. | H/W Gairo | 38,679,672 |
| 5. | H/W Rungwe | 115,777,111 | 11. | H/W Ileje | 32,043,700 |
| 6. | H/W Sengerema | 59,511,900 | | **Jumla** | **1,237,999,804** |

Aidha, tathmini niliyoifanya katika akaunti za Benki za Biashara ambako mamlaka za serikali za mitaa hutunza fedha za Mfuko ilibainisha kuwa, shilingi milioni 156.23 za Mfuko zililimbikizwa katika akaunti kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kukopeshwa kwa wanufaika pasipokuwa na sababu za msingi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 12-3**.

**Jedwali Na. 12-3: Halmashauri zilizokuwa na bakaa ya muda mrefu katika benki za biashara**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/W Mpwapwa | 108,703,450 |
| 2. | H/W Nyasa | 47,530,700 |
| | **Jumla** | **156,234,150** |

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iziagize mamlaka za serikali za mitaa zenye salio katika akaunti za benki za amana na benki za biashara kuhamishia fedha hizo katika akaunti za Mfuko wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.**

## 12.3 Mikopo ya Shilingi Bilioni 3.26 Iliyotolewa Bila Kuzingatia Uwiano wa Utoaji Mikopo

Kanuni ya 5 (2) (a) - (c) ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2019 inazitaka mamlaka za serikali za mitaa kutoa mikopo kwa kuzingatia uwiano wa asilimia 40 ya fedha kwa vikundi vya wanawake, asilimia 40 kwa vikundi vya vijana, na asilimia 20 kwa watu wenye ulemavu.

Ukaguzi nilioufanya kuhusu mikopo iliyotolewa kwa vikundi ulibaini kuwa, mamlaka 17 za serikali za mitaa zilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.26 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu bila kuzingatia uwiano ulioainishwa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.12-4**.

**Jedwali Na.12-4: Halmashauri zilizotoa mikopo bila kuzingatia uwiano wa utoaji wa mikopo**

| Na. | Jina la Halmashauri | Kiasi cha Mkopo (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | H/Mji Geita | 952,500,000 |
| 2. | H/W Chato | 300,000,000 |
| 3. | H/W Songwe | 292,500,000 |
| 4. | H/W Shinyanga | 230,244,000 |
| 5. | H/W Same | 229,000,000 |
| 6. | H/Mji Kasulu | 184,423,061 |
| 7. | H/W Kakonko | 145,031,130 |
| 8. | H/W Nanyumbu | 136,000,000 |
| 9. | H/W Mbogwe | 117,213,883 |
| 10. | H/W Kondoa | 116,000,000 |
| 11. | H/Mji Newala | 110,114,000 |
| 12. | H/W Rorya | 104,800,000 |
| 13. | H/Mji Bunda | 104,000,000 |
| 14. | H/W Mpwapwa | 98,590,000 |
| 15. | H/W Korogwe | 87,500,000 |
| 16. | H/W Manyoni | 37,180,000 |
| 17. | H/W Ikungi | 19,220,000 |
| | **Jumla** | **3,264,316,074** |

Kutozingatiwa kwa uwiano wa utoaji mikopo kunazuia juhudi za Serikali za kutenga rasilimali zake kulingana na vipaumbele.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zizingatie Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za Mwaka 2019 kwa kuhakikisha kuwa uwiano wa utoaji mikopo uliowekwa unazingatiwa wakati wa kutoa mikopo.**

## 12.4 Halmashauri Kutochangia Shilingi Bilioni 6.68 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu

Kifungu cha 37(A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinazitaka mamlaka za serikali za mitaa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kwa madhumuni ya kufadhili vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.

Nilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matakwa haya na kubaini kuwa, mamlaka 83 za serikali za mitaa hazikuchangia jumla ya shilingi bilioni 6.68 kwenye Mfuko kutoka kwenye mapato yake ya ndani kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.12-2**.

**Jedwali Na.12-5** linaonesha mwenendo wa uchangiaji kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu kwa miaka mitatu mfululizo.

**Jedwali Na.12-5: Kiasi kisichochangwa kwenye mfuko wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri | Kiasi Kisichochangwa (Sh.) |
|---|---|---|
| 2020/21 | 83 | 6,684,257,317 |
| 2019/20 | 82 | 5,720,140,159 |
| 2018/19 | 115 | 9,930,902,514 |

**Ninapendekeza kwamba, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na vyombo husika vya usimamizi kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2019 viimarishe usimamizi na vizifuatilie kwa karibu mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikisha zinachangia kikamilifu kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kulingana na matakwa ya sheria.**

## 12.5 Kutoshirikishwa kwa Wataalam wa Usimamizi wa Mikopo katika Mchakato wa Utoaji na Urejeshwaji wa Mikopo

Kanuni ya 8 ya Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu za mwaka 2019 [Tangazo

la Serikali Na. 286 la 05/04/2019] inataka taratibu zote za wa mikopo zisimamiwe na mamlaka za serikali za mitaa.

Tathmini niliyoifanya ya taratibu zinazopaswa kuzingatiwa wakati wa utoaji wa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa, ilibaini changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na uwezo duni wa Idara za Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Halmashauri katika kutoa, kufuatilia na kusimamia urejeshwaji wa mikopo hiyo na kutoa huduma za maendeleo ya kibiashara kwa wanufaika, jambo ambalo linapunguza uwezo wa Mfuko kufanya kazi ipasavyo.

Pia, nilibaini kuwa uhakiki wa vikundi vilivyoomba mikopo ulikuwa haufanyiki kabisa kabla ya mikopo kutolewa. Hii ni kutokana na ukosefu wa utaalamu wa kufanya uhakiki unaostahili katika mikopo. Aidha, kukosekana kwa usaidizi wa kisheria kutoka katika vitengo vya sheria kuhusu masuala ya bima hasa kwa mikopo inayotolewa kwa vijana, ambao mara nyingi walikuwa wakinunua pikipiki na bajaji. Pia, Mfuko hauna sera ya jinsi ya kushughulikia mikopo isiyolipika (NPL).

Kutokana na hali hii, mfuko umeongeza madeni yanayofikia kiasi cha Sh. Bilioni 47 kama ilivyoelezwa kwa kina katika aya ya 12.1 ya taarifa hii, kati ya madeni hayo yanaweza kushindwa kulipika kutokana na kuwa ni chechefu au madeni hewa na hivyo kuendelea kuudhoofisha mfuko.

**Ninapendekeza kuwa OR-TAMISEMI itumie benki za serikali au wataalamu wa usimamizi wa dhamana na uwekezaji kama vile Benki ya Maendeleo TIB (TIB Development Bank) na Benki ya biashara Tanzania (TCB) katika kuongeza ufanisi katika kutoa, kufuatilia na kusimamia urejeshwaji wa mikopo na kwa kuzingatia gharama nafuu ya uendeshaji. Zaidi ya hayo, OR-TAMISEMI inashauriwa kuandaa sera ya mikopo isiyolipika (NPL) ili kusimamia mikopo inayotolewa kwa vikundi husika.**

# SURA YA 13

# UFANISI KATIKA USIMAMIZI WA MASOKO NA VITUO VYA MABASI

## 13.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa kanuni za uanzishaji wa serikali za mitaa, mamlaka za serikali za mitaa zinatakiwa kudhibiti na kusimamia masoko na vituo vyote vya mabasi. Kama inavyoonekana katika dhana ya upembuzi yakinifu na nyaraka za miradi ya kimkakati, masoko na vituo vya mabasi ni vyanzo vya mapato katika mamlaka za serikali za mitaa hivyo hutoa rasilimali kwa ajili ya uwekezaji na kuimarisha utoaji wa huduma kwa jamii.

Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa masoko na vituo vya mabasi nilibaini changamoto zikiwemo kukosekana kwa umakini wakati wa kufanya upembuzi yakinifu; mazingira yasiyoridhisha ya utendaji kazi; na ukosefu wa ofisi za wasimamizi wa masoko na kutokuwapo kwa mikataba ya upangaji. Chanagmoto zingine nilizozibaini ni migogoro ya ardhi iliyochangiwa na ukosefu wa hatimiliki; na kuwapo kwa viongozi wa umma ambao hawafanyi kazi kwa manufaa ya umma hivyo kuchangia usimamizi hafifu katika uendeshaji wa masoko na vituo vya mabasi.

Katika sura hii, nitajadili kwa kina ufanisi wa utendaji katika usimamizi wa masoko na vituo vya mabasi katika mamlaka za serikali za mitaa na kutoa mapendekezo yatakayohitaji Serikali kuchukua hatua za muda mfupi na mrefu ili kupunguza mapungufu yaliyobainika.

## 13.1 Kutoonekana kwa Faida ya Uwekezaji Katika Masoko na Vituo vya Mabasi Visivyotumika wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 533.68

Wakati wa ukaguzi nilifanya ziara kwenye masoko na vituo mbalimbali vya mabasi na nilibaini kuna baadhi vilikuwa hazitumiki kikamilifu.

## (a) Soko la Chuno, Soko la Skoya na Soko la Chiyangu, na Kituo cha Mabasi cha Chipuputa katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani

Soko la Chuno lilijengwa chini ya Mradi wa Miji ya Kimkakati Tanzania kwa gharama ya shilingi bilioni 5.54 na makadirio ya makusanyo ya mwaka yalikuwa shilingi milioni 138.10. Hata hivyo, nilibaini kuwa soko lilikuwa na vibanda 237 vilivyokuwa wazi kwa zaidi ya miezi minne na kusababisha hasara ya mapato ya shilingi milioni 32.11.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini pia kuwa Masoko ya Skoya na Chiyangu, na Kituo cha Mabasi cha Chipuputa katika Manispaa hiyohiyo ya Mtwara-Mikindani kilikuwa wazi kwa kipindi cha mwaka mzima na kusababisha hasara ya jumla ya mapato ya shilingi milioni 131.10 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.13-1**.

**Jedwali 13-1: Masoko na vituo vya mabasi yaliyo wazi**

| Jina la Soko / Stendi | Vibanda vilivyokodishwa | Vibanda vilivyo wazi | Kiwango (Sh.) | Kipindi (Miezi) | Hasara (Sh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| Kituo cha Basi Chipuputa | 173 | 130 | 50,000 | 12 | 78,000,000 |
| Soko la Skoya | 84 | 81 | 40,000 | 12 | 38,880,000 |
| Soko la Magomeni (A) | 08 | 59 | 10,000 | 12 | 7,080,000 |
| Soko la Magomeni (B) | 07 | 22 | 10,000 | 12 | 2,640,000 |
| Soko la Chiyangu | 16 | 15 | 25,000 | 12 | 4,500,000 |
| **Jumla** | | | | | **131,100,000** |

Katika Halmashauri ya Mji wa Masasi, nilikuta soko la Mkuti likiwa na vibanda 68 ambavyo havijakodishwa ambavyo vingeweza kuingiza mapato ya shilingi milioni 12.84 kwa mwaka.

Aidha, katika halmashauri nyingine sikuweza kupata taarifa katika baadhi ya masoko na stendi za mabasi zilizokuwa wazi kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu sahihi. Sehemu hizo ni pamoja na

kituo cha mabasi katika Mji wa Mangaka, soko la Mbagala-Kuu, soko la Kijichi na maduka makubwa ya Kijichi.

Katika Mji wa Mangaka ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kulikuwa na kituo cha mabasi kilichokamilika kinachojumuisha majengo ya biashara kwa ajili ya kupangisha kama vile maduka, maduka ya dawa, migahawa, maduka makubwa na baa. Hata hivyo, ni vyumba 14 tu ndivyo vilivyokuwa vimekodiwa na kuacha 31 vikiwa wazi.

Soko la Mbagala-kuu, soko la Kijichi na maduka makubwa ya Kijichi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke vilifadhiliwa na Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam (DMDP). Nilibaini kuwa Soko la Mbagala-kuu lililogharimu shilingi bilioni 1.19, lilikuwa na vibanda vitupu 141 kati ya vibanda 180 (sawa na asilimia 78). Pia, niligundua fremu 8 sawa na asilimia 88 zilikuwa wazi.

Soko la Kijichi lililogharimu shilingi milioni 765.01 lote lilikuwa wazi. Maduka makubwa ya Kijichi yaliyogharimu shilingi bilioni 1.73 yalikuwa wazi na katika soko la Makangarawe, maduka 147 kati ya 186 (sawa na asilimia 79), fremu 14 kati ya 19 (sawa na asilimia 74), maduka wawili ya nyama na duka moja kubwa vyote vilikuwa wazi.

Wakati Ukaguzi maalumu katika kituo cha mabasi cha Kilole kilichopo Halmashauri ya Mji wa Korogwe kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na 2019/20 nilibaini idadi kubwa ya vibanda vilivyokuwa wazi hali iliyosababisha upotevu wa mapato unaokadiriwa kufikia shilingi milioni 357.63. Hali bado haijabadilika kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.13-2**.

**Jedwali Na.13-2: Orodha vibanda visivyo na wapangaji**

| Maelezo | Vilivyopo | Vilivyokodishwa | |
|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 |
| Vibanda | 56 | 19 | 1 |
| Bucha za Samaki | 3 | 0 | 0 |
| Bucha za Nyama | 3 | 0 | 0 |
| Vibanda vya wamachinga | 4 | 0 | 0 |
| Soko la kuku | 1 | 0 | 0 |
| Choo | 1 | 0 | 0 |

| Maelezo | Vilivyopo | Vilivyokodishwa | |
|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 |
| Ghala | 1 | 0 | 0 |
| Wauza chakula | 4 | 0 | 0 |

**(b) Kituo cha Mabasi cha Mangaka katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu**

Kituo hiki kilichopo katika Mji wa Mangaka katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kimekamilika na kinajumuisha majengo ya biashara kwa ajili ya kupangisha kama vile maduka, maduka ya dawa, migahawa, maduka makubwa na baa. Hata hivyo, ni vyumba 14 tu kati ya 31 ndivyo vilikuwa vimekodishwa.

**(c) Soko la Mbagala Kuu, Soko la Kijichi na Maduka Makubwa ya Kijichi katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke**

Wakati wa ukaguzi wangu nilitembelea miradi hii iliyofadhiliwa na Mradi wa Maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam na nilibaini kuwa Soko la Mbagala Kuu lililogharimu shilingi bilioni 1.19 lilikuwa na vibanda 141 vilivyokuwa wazi kati ya vibanda 180 (sawa na asilimia 78). Pia, niligundua fremu 8 sawa na asilimia 88 zilikuwa wazi. Soko la Kijichi lililogharimu shilingi milioni 765.01 lote lilikuwa wazi; na Maduka Makubwa ya Kijichi yaliyogharimu shilingi bilioni 1.73 yalikuwa wazi na katika Soko la Makangarawe, maduka 147 kati ya 186 (sawa na asilimia 79), fremu 14 kati ya 19 (sawa na asilimia 74), na maduka wawili ya nyama na duka moja kubwa yote yalikuwa wazi.

Hata hivyo, hasara iliyotolewa hapo juu si timilifu kwa vile sikuweza kupata taarifa katika baadhi ya masoko na stendi za mabasi zilizokuwa wazi kutokana na kumbukumbu kutokamilika. Vituo hivyo ni pamoja na Kituo cha Mabasi katika Mji wa Mangaka, Soko la Mbagala Kuu, Soko la Kijichi, na Maduka Makubwa ya Kijichi.

Ninakubaliana na menejimenti ya Halmashauri ya Mji wa Masasi ambayo ina mpango wa kupunguza viwango vya kodi ilivyoweka ili kuvutia wapangaji wengi wakiwemo wafanyabiashara wadogo. Pia, ninapongeza hatua zinazochukuliwa na uongozi wa Manispaa ya Temeke za kuruhusu kuwapo kwa gulio na huduma kama vile

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Wakala wa Sajili, Ufilisi na Udhamini, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na huduma za ushuru wa huduma na utoaji wa leseni za biashara katika masoko yake ili kuongeza mzunguko wa watu na hatimaye kuwavutia kupanga katika majengo yaliyo wazi.

Suala la kutotumika kwa masoko na vituo vya mabasi vilivyojengwa lisiposhughulikiwa ipasavyo na kwa wakati, linaweza kuchelewesha kupatikana wa faida itokanayo na uwekezaji mkubwa uliofanywa; na kutotumika kwa miundombinu hii kutasababisha uchakavu hivyo kushusha thamani yake.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iwasiliane na menejimenti za mamlaka za serikali za mitaa ili kuimarisha usimamizi wa mfumo wa masoko na vituo vya mabasi kwa kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wote wanatumia masoko na vituo vya mabasi vilivyojengwa badala ya kutumia maeneo yasiyo rasmi ili kupata thamani ya fedha za miundombinu iliyojengwa; na (b) ihakikishe upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kama vile umeme, maji, idadi ya watu, makazi na mengine yanayofanana na hayo unahitaji kuzingatiwa wakati wa upembuzi yakinifu kwa kuwa kuwapo kwake kunatengeneza mazingira mazuri ya biashara.**

## 13.2 Ghala la Soko la Mpunga Lililotelekezwa lenye Thamani ya Shilingi Milioni 677.42

Wakati wa ukaguzi wangu nilitembelea ghala la kuhifadhia mpunga katika Kijiji cha Mahiga kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba lililokamilika tangu tarehe 7 Mei 2017. Mradi huo ulifadhiliwa na MIVAR kwa gharama ya shilingi milioni 617.42. Mwaka 2018, Halmashauri ilifunga mashine ya kukoboa mpunga yenye thamani ya shilingi milioni 60 hivyo gharama ya uwekezaji kufikia jumla ya shilingi milioni 677.42. Lengo la mradi lilikuwa kuwezesha uhifadhi wa mpunga kwa lengo la kuuza kwa bei ya soko ili kuboresha mapato ya Halmashauri na ya jamii.

Licha ya kiasi kikubwa cha fedha kilichowekezwa, nilibaini wakati wa ukaguzi kuwa miundombinu ya soko ikiwa pamoja na ghala ilitelekezwa kwa muda mrefu kutokana na kukosekana kwa nishati

ya umeme kwa ajili ya kuendeshea mashine ya kukoboa mpunga. Katika mahojiano ya timu ya ukaguzi na menejimenti ilielezwa kuwa upembuzi yakinifu wa mradi ulifanyika kwa kuwashirikisha wadau kadhaa likiwemo Shirika la Umeme Tanzania kupitia barua yenye kumbukumbu namba MZA/KDC/M.20/5/58 ya tarehe 18/07/2017 kwa ajili ya kusaidia maendeleo ya jamii ya vijijini. Halmashauri ilichagua kuweka mradi katika eneo la Mahiga kwa nia ya kuiongezea thamani skimu ya umwagiliaji ambapo uzalishaji wa mazao ulikuwa mkubwa.

Nina wasiwasi na hali ya miundombinu ya ghala la mpunga iliyotelekezwa. Ni dhahiri kwamba, ikikaa muda mrefu bila kufanya kazi, thamani yake itapungua kutokana na uchakavu.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Shirika la Umeme Tanzania na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kuchukulia ukosefu wa umeme katika ghala hilo kama jambo la dharura ambalo linahitaji hatua za haraka ili mradi uliotelekezwa uweze kufanya kazi na thamani ya fedha ipatikane.**

## 13.3 Upotevu wa Mapato Kiasi cha Shilingi Milioni 900 Kutokana na Kubomolewa kwa Soko la Tarime

Soko la Tarime ni miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyoidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Mkataba wa utekelezaji wa mradi huo ulisainiwa tarehe 5 Februari 2019 kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na timu ya Halmashauri ya Mji wa Tarime ikiongozwa na Sekretarieti ya Mkoa wa Mara.

Kufuatia makubaliano hayo, soko lililokuwapo lilivunjwa wakati wa uandaaji wa eneo ili kuruhusu ujenzi wa soko la kisasa. Tarehe 14 Mei 2019, Halmashauri iliingia mkataba Na. LGA /165/2018/2019/S/02 wenye thamani ya shilingi bilioni 8.07.

Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa mradi huo, Serikali ilisitisha miradi yote ya kimkakati katika Halmashauri zilizochaguliwa ambayo ilikuwa haijaanza kutekelezwa ukiwemo mradi wa Soko la Tarime. Katika mapitio ya kumbukumbu za mapato nilibaini Halmashauri ilikuwa na makusanyo ya wastani wa shilingi milioni 300 kwa mwaka

kutoka katika soko lililobomolewa (au shilingi milioni 900 kwa miaka mitatu).

Katika mahojiano, uongozi ulieleza kuwa shilingi bilioni 300 zimetengwa katika bajeti ya Halmashauri ya mwaka 2021/22 na mchakato wa zabuni ya ujenzi wa Soko la Kisasa la Tarime umeanza upya.

Kwa maoni yangu, agizo la Serikali la kusitisha ujenzi wa Soko la Kisasa la Tarime lilisababisha upotevu wa shilingi milioni 900 ambazo zingeweza kukusanywa kutoka katika Soko Kuu la zamani la Tarime.

**Ninaishauri menejimenti ya Halmashauri ya Mji wa Tarime (a) iwasiliane na Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ili kuhakikisha fedha zilizotengwa zinatolewa kwa wakati na utekelezaji wa mradi unaaza ili kuepusha upotevu zaidi wa mapato, na (b) muhimu zaidi, watendaji wa Serikali waliopewa dhamana ya usimamizi wa rasilimali za umma wahakikishe wanakuwa makini wakati wa kufanya maamuzi ili kuepusha upotevu mkubwa wa fedha za umma.**

## 13.4 Mazingira na Usafi Usioridhisha katika Masoko na Stendi za Mabasi

Nilibaini kuwa katika masoko ya Temeke Stereo, Tazara, Mbagala Rangitatu, Mbande na Kisewe yalikuwa na miundombinu chini ya viwango, mifumo duni ya mifereji ya maji, uvujaji wa mapaa usiodhibitiwa, mrundikano wa taka ngumu, miundombinu duni ya usafi ikiwa pamoja na hali isiyoridhisha ya vyoo, mabafu, vifaa vya kunawia mikono, kuta, na sakafu, pamoja na vibanda vilivyokuwa havijakarabatiwa kwa muda mrefu.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Menejimenti ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilinieleza kuwa shilingi milioni 230 zimetengwa katika bajeti ya Halmashauri ya mwaka wa fedha 2021/2022 ili kurekebisha kasoro hizo.

Kwa ujumla, mamlaka nyingi za serikali za mitaa zimepunguza kutoa ushauri wa njia salama za kujikinga na maradhi katika masoko na vituo vya mabasi bila sababu za msingi. Idadi kubwa ya masoko na vituo vya mabasi havitekelezi tena hatua za usalama wa afya ikiwa pamoja na udhibiti wa taka. Nina wasiwasi kwamba, hali hii inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa kama vile kipindupindu; pia

ukosefu wa vifaa vya kunawia mikono sokoni na katika vituo vya mabasi kunaweza kuzidisha kuenea kwa janga la UVIKO-19 ikiwa hatua stahili hazitachukuliwa kwa wakati.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI na mamlaka za serikali za mitaa (a) kuwasiliana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na mamlaka zingine zinazohusika ili kuimarisha hatua za usalama wa afya kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji salama, usafi wa mazingira, na udhibiti wa taka na hali ya usafi katika masoko na vituo vya mabasi ili kudhibiti magonjwa ya milipuko; na (b) ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI itoe waraka kwa mamlaka za serikali za mitaa zote kutenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya masoko na vituo vya mabasi vilivyochakaa na kuhakikisha kuwa kuna ofisi za wasimamizi wa masoko na vituo vya mabasi kwa ajili ya kudhibiti na kusimamia shughuli za kila siku.**

## 13.5 Ukodishaji bila Mikataba wa Vibanda katika Masoko na Stendi za Mabasi

Nilibaini kuwa idadi kubwa ya wapangaji katika masoko na vituo mbalimbali vya mabasi walikuwa wakifanya shughuli zao bila mikataba. Nilifanya ukaguzi wa sampuli katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani na tathmini katika masoko matatu na kituo kimoja cha mabasi na kubaini kulikuwa na wapangaji 347 kati ya 737 (sawa na asilimia 47) ambao hawakuwa na makubaliano yoyote yaliyotiwa saini kati yao na halmashauri. Pia, katika Kituo cha Mabasi cha Lindi, Uwanja wa Michezo wa Ilulu, na Soko Kuu la Lindi katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kulikuwa na wapangaji 248 ambao hawakuwa na mikataba.

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma, licha ya mapendekezo yangu katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuhusu Soko Kuu, Soko la Nyasho, Soko la Nyasho Mlango, Soko la Kamnyonge, na Kituo cha Mabasi cha Bweri kwa mwaka huu ni mikataba 99 tu kati ya 715 ndiyo ilitolewa kwa ajili ya uhakiki ikimaanisha maduka 616 bado yalikuwa yamekodishwa bila mikataba.

Ufafanuzi uliotolewa na menejimenti kuhusu kukosekana kwa mikataba ya upangishaji sokoni ni kwamba kuna migogoro ya umiliki

wa vibanda tajwa kati ya Halmashauri na wafanyabiashara ambao siku za nyuma walijenga katika viwanja vya Halmashauri bila makubaliano ya maandishi.

Katika mfululizo wa kaguzi nilizofanya kwa miaka mingi, Halmashauri nyingi zimekuwa na migogoro ya umiliki wa vibanda vya masoko. Tathmini yangu ilibaini kuwa, mamlaka za serikali za mitaa zinapata matokeo hasi kutokana na maamuzi ya siku za nyuma kuruhusu watu kujenga vibanda katika maeneo ya masoko bila masharti na makubaliano ya kimaandishi.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuwasiliana na mamlaka za serikali za mitaa husika ili kuhakikisha migogoro iliyotokana na makubalino mabovu inashughulikiwa; kisha baada ya makubaliano, kila mpangaji apewe mkataba.**

## 13.6 Uvamizi wa Maeneo ya Masoko na Ukosefu wa Hatimiliki katika Ardhi za Masoko

Nilipitia kesi namba 196/2021, 188/2021, 191/2021, 193/2021 na 195/2021 zilizofunguliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke katika Mahakama ya Wilaya ya Ardhi na Nyumba dhidi ya walalamikiwa kuiomba mahakama hiyo kuchunguza uhalali wa umiliki wa eneo ambalo lilijengwa maduka katika Soko la Madenge ambalo Manispaa inadai kuwa mmiliki halali.

Hali hii pia iko katika Jiji la Mwanza na katika iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambazo ardhi zake zenye thamani ya shilingi bilioni 199.02 na shilingi bilioni 199.77 mtawalia hazina hatimiliki, huku Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (zamani H/M Ilala), asilimia 93 ya ardhi yenye thamani ya shilingi bilioni 925 haina hatimiliki. Hali hii inasababisha uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya masoko ya halmashauri, vituo vya mabasi na kwa madhumuni mengine.

Uvamizi wa eneo katika Soko la Madenge ni mfano tu ambao umeenea katika mamlaka nyingi za serikali za mitaa Tanzania Bara. Ardhi zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya umma kama ujenzi wa masoko na vituo vya mabasi huvamiwa na kusababisha migogoro ambayo baadhi yake hufikishwa katika mahakama na mabaraza mbalimbali bila mafanikio.

Kwa maoni yangu, hali hii inachangiwa na maeneo kukosa hatimiliki, uuzaji wa ardhi usiofuata taratibu unaochochewa na kukithiri kwa vitendo vya rushwa na usimamizi usioridhisha wa watendaji wa serikali za mitaa na viongozi wa kisiasa wakiwemo madiwani wenye dhamana na wajibu wa kulinda mali za mamlaka za serikali za mitaa.

**Ninatoa wito kwa mamlaka za serikali za mitaa (a) zishughulikie migogoro ya ardhi iliyotokana na mapungufu ya kisheria na kuchukua hatua ya kuzuia rushwa na ushawishi wa kisiasa unaosababisha uvamizi wa viwanja vyake hususani vilivyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa masoko, vituo vya mabasi, na huduma zingine za umma; na (b) ninatoa wito kwa mamlaka za serikali za mitaa kupima na kupata hati za hakikumiliki ya ardhi kama inavyotakiwa na Kifungu cha 29(1) (b) cha Sheria ya Ardhi, Sura ya 334.**

## SURA YA 14

## MAPITIO YA UFANISI KATIKA UWEKEZAJI

### 14.0 Utangulizi

Katika nia ya kuongeza mapato ya vyanzo vyake vya ndani na kuwa na mtiririko madhubuti wa fedha ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya huduma bora, baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa zimewekeza katika mifuko mbalimbali ili kupata faida. Uwekezaji huo ni pamoja na hisa, hoteli, mali za uwekezaji, na ubia mwingine wa kibiashara. Katika kuhakikisha ufanisi katika usimamizi wa uwekezaji, baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa zimeanzisha kampuni tanzu na ubia ili kutekeleza shughuli za taasisi mpya zilizoanzishwa.

Katika sura hii, ninatathmini mwenendo wa ufanisi wa miradi ya uwekezaji unaofanywa na mamlaka za serikali za mitaa. Ninachambua zaidi ufanisi wa mamlaka husika katika kusimamia miradi yake ya uwekezaji. Pia, ninajadili kwa kina sheria, kanuni, sera, miongozo na mifumo mingine iliyopo ambayo inaboresha maamuzi yote ya uwekezaji wa mamlaka za serikali za mitaa ili kuhakikish

### 14.1 Uwekezaji Katika Hisa

Ukaguzi wangu katika eneo hili umebaini udhaifu wa aina mbili ambao ni uwekezaji wa mamlaka za serikali za mitaa katika benki ya biashara yenye utendaji usioridhisha; na ukosefu wa watumishi waliobobea katika kusimamia uwekezaji katika hisa kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### 14.1.1 Uwekezaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa Katika Benki ya Biashara Yenye Utendaji Usioridhisha

Tathmini yangu ya utendaji katika benki moja ya biashara iliyotokana na taarifa za fedha zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2020 ulibaini kuwa benki hiyo ilitambua faida ya shilingi bilioni 0.45 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.04 kufikia tarehe 31 Desemba 2019. Asilimia 96 ya mapato yake yanatumika kwenye

gharama za uendeshaji, hivyo kumaanisha kuwa benki haitoi faida ya kutosha kwa wanahisa wake. Licha ya utendaji mbaya wa kifedha na kiuchumi, baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa zimeendelea kuwekeza katika Benki hii, hivyo kuhatarisha fedha za umma kupitia uwekezaji huo usio na faida.

Kwa mfano, asilimia ya mapato yake na mali (ROA) kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 ilikuwa asilimia 0.3, ambayo ni chini ya asilimia 5 iliyoonekana kuwa nzuri. Hali hii inamaanisha kuwa benki hii haikuwa na uwezo wa kupata mapato kutoka kwenye rasilimali zake za uwekezaji licha ya ukuaji wa mali kwa asilimia 22 ikilinganishwa na asilimia 7 ya mwaka uliotangulia.

Aidha, uwiano wa mapato yanayotokana na mtaji wa wanahisa (rejesho la mtaji) wa asilimia 2 ulikuwa mdogo sana ikilinganishwa na wastani wa sekta wa kati ya asilimia 15 na 20. Vilevile, mapitio yangu ya taarifa za fedha zilizokaguliwa za Benki hiyo kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2020 yalibaini kuwa, mapato kwa kila hisa yalishuka kutoka shilingi 22 hadi shilingi 5.

Tarehe 23 Julai 2018, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilitoa agizo lenye Kumb. Na.DB.59/184/01/81 lililozitaka baadhi ya mamlaka za serikali za mitaa kuongeza mtaji wa Benki kwa kununua hisa zaidi. Hata hivyo, katika kutekeleza maagizo hayo, mamlaka za serikali za mitaa hazikushauriwa au kupewa fursa ya kutathmini mwenendo wa uwekezaji utakaofanywa katika benki.

Matokeo yake, kwa kuitikia maagizo ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, iliyokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilinunua hisa 3,103,448 za ziada kutoka Benki hiyo zenye thamani ya shilingi milioni 900 licha ya viashiria vya utendaji mbaya wa Benki.

**Hali katika benki si nzuri kwa mwekezaji makini. Hivyo, ninazishauri mamlaka husika za serikali za mitaa kuja na mkakati wa kina na madhubuti wa kuinusuru benki hiyo ili kuongeza faida na ufanisi.**

Vilevile, mapitio yangu yalibaini kuwa mamlaka 6 za serikali za mitaa zilikuwa zinamiliki hisa 24,036,348 katika Benki hiyo ambazo

thamani yake ilikuwa shilingi bilioni 6.97 (au shilingi 290/hisa) hadi tarehe 30 Juni 2020. Hata hivyo, mamlaka hizi zilipata hasara ya shilingi bilioni 1.20 kwa pamoja ndani ya miezi 12 tu baada ya kushuka kwa bei ya hisa kutoka shilingi 290 hadi shilingi 240 kwa kila hisa kufikia tarehe 30 Juni 2021.

Kwa mujibu wa ripoti zilizochapishwa za soko la hisa la Dar es Salaam, hisa za Benki hiyo ziliuzwa kwa thamani ya soko ya shilingi 170 kwa kila hisa tarehe 10 Februari 2022 kutoka shilingi 240 kwa kila hisa iliyorekodiwa tarehe 30 Juni 2021. Hali hii inamaanisha kwamba mamlaka husika zinaweza kupata hasara zaidi ya shilingi bilioni 1.68 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2021/22 ikiwa bei ya hisa haitatengemaa kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.14-1.**

**Jedwali Na.14-1: Mwenendo wa bei ya soko kwa kila Hisa**

| Na. | Jina | Idadi ya Hisa | Upungufu wa Thamani (290-240) -Sh. | Upungufu wa Thamani (240-170) -Sh. |
|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Dar es Salaam | 10,207,566 | 510,378,300 | 714,529,620 |
| 2. | H/M Kinondoni | 5,625,019 | 281,250,950 | 393,751,330 |
| 3. | H/M Temeke | 3,422,252 | 171,112,600 | 239,557,640 |
| 4. | H/M Ubungo | 2,500,009 | 125,000,450 | 175,000,630 |
| 5. | H/M Kigamboni | 2,281,502 | 114,075,100 | 159,705,140 |
| | **JUMLA** | **24,036,348** | **1,201,817,400** | **1,682,544,360** |

**Ninatoa wito kwa menejimenti za mamlaka husika za serikali za mitaa kufanya ufuatiliaji wa karibu juu ya mwenendo wa thamani ya hisa na kuja na mkakati wa uwekezaji utakaohakikisha bei za hisa zinakuwa imara.**

### 14.1.2 Ukosefu wa Watumishi Waliobobea katika Kusimamia Uwekezaji Katika Hisa

Nilitathmini muundo wa mamlaka za serikali za mitaa na mipango ya kitaasisi na kubaini kuwa hazina vitengo au wafanyakazi maalumu wa kusimamia uwekezaji hasa katika hisa.

Kwa mujibu wa miundo iliyopo ya mamlaka za serikali za mitaa, programu za uwekezaji zipo chini ya maofisa mipango na vifaa ambao pia wana jukumu la kusimamia, kuratibu na kuandaa taarifa

za miradi ya maendeleo, idadi ya watu, rasilimaliwatu, maendeleo ya jamii, mazingira endelevu, maliasili, na bajeti.

Katika tathmini yangu, mbali na upungufu mkubwa wa watumishi wenye sifa na weledi katika idara za mipango, maofisa mipango na vifaa wa mamlaka za serikali za mitaa kwa sasa wamezidiwa na miradi mingi inayotekelezwa na halmashauri kwa utaratibu wa nguvukazi na baadhi ina uhitaji wa haraka wa ukamilishaji. Katika hali hii, haiwezekani kwa maofisa mipango hasa katika manispaa na majiji kuchunguza kwa ufanisi fursa za uwekezaji hasa katika hisa kwa kufuatilia na kutathmini hasara na faida zinazohusiana na uwekezaji.

**Ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iwasiliane na mamlaka za serikali za mitaa zenye idadi kubwa ya miradi ya uwekezaji katika masoko ya hisa na vitegauchumi vingine ili kuangalia upya na kuanzisha utaratibu wa kitaasisi ambao utafaa kwa usimamizi madhubuti wa uwekezaji; na (b) mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kushirikiana kwa karibu na Benki Kuu ya Tanzania na wawekezaji wengine katika kuongeza ufanisi wa usimamizi, kupunguza vihatarishi na kubadilishana taarifa muhimu kama sehemu ya mpango wao wa uwekezaji ili kuongeza ufanisi na faida katika uwekezaji wao.**

## 14.2 Uwekezaji katika Mali na Kampuni Tanzu

### 14.2.1 Uwekezaji Usio na Tija Katika Soko la Kisasa Mwanjelwa Shillingi Bilioni 49.20

Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipata mkopo kutoka benki moja ya biashara wa shilingi bilioni 19.56 kati ya mwaka 2008 na 2015 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Kisasa la Mwanjelwa. Masharti ya awali ya mkopo yalibaini kuwa jumla ya fedha zilizotakiwa kulipwa kufikia mwaka 2030 zilikuwa shilingi bilioni 61.55 ikimaanisha kuwa riba ya mkopo ilikuwa shilingi bilioni 41.99.

Kufuatia juhudi nyingi zilizofanywa na Serikali, Benki ilikubali kurekebisha masharti ya mkopo hadi kufikia shilingi bilioni 41.20 ambazo zinatakiwa kuwa zimelipwa ifikapo mwaka 2033.

Halmashauri iliweza kulipa jumla ya shilingi bilioni 6.55 pekee, hivyo, shilingi bilioni 35.44 zilikuwa hazijalipwa hadi mwezi Desemba 2021.

Kiuhalisia, ili Halmashauri iweze kukidhi masharti ya mkopo ifikapo mwaka 2033, ni lazima ilipe awamu za shilingi bilioni 2.95 kila mwaka kwa miaka 12 mfululizo. Hata hivyo, niliarifiwa na uongozi kuwa jumla ya makusanyo ya mapato kutoka sokoni hapo ni kati ya shilingi milioni 750 hadi 850 kwa mwaka. Menejimenti ilizidi kunifahamisha kuwa benki iko tayari kusamehe riba yote ya mkopo ikiwa Halmashauri italipa mkupuo wa shilingi bilioni 13 za mkopo mkuu mbali na shilingi bilioni 6.55 zilizokwishalipwa.

Kushindwa kurejesha malipo ya awamu iliyokubaliwa kwa wakati kutasababisha ongezeko kubwa la riba ya mkopo. Kama Halmashauri haitatekeleza chaguo ambalo linaondoa riba ya mkopo, marejesho yanayotarajiwa ya uwekezaji katika soko la kisasa la Mwanjelwa hayatekelezeki.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) kuchukua hatua zitakazoinusuru Halmashauri na hasara zaidi katika Soko la Kisasa la Mwanjelwa; (b) menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuanzia mwaka ujao wa fedha kuandaa ripoti tofauti za mara kwa mara za fedha za soko zitakazoainisha pamoja na mambo mengine hasara iliyopatikana katika uwekezaji.**

### 14.2.2 Gharama ya Shilingi Bilioni 6.16 za Uwekezaji Isiyojulikana Katika Kampuni ya Mwanza City Commercial Complex

Kampuni ya Mwanza City Commercial Complex ilianzishwa tarehe 11 Machi 2010. Hivi sasa kampuni iko chini ya ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Kampuni inamiliki na kuendesha Mwanza Rock City Mall iliyopo Manispaa ya Ilemela.

Kwa mujibu wa mkataba wa makubaliano uliosainiwa tarehe 28 Januari 2009, Halmashauri ya Jiji la Mwanza iliingia makubaliano na uliokuwa Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (sasa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma) kuanzisha uwekezaji wa Kampuni ya Mwanza City Commercial Complex wenye thamani ya

shilingi bilioni 20 kwa mtaji wa uwiano wa 40:60 kwa mfuatano kwa masharti kwamba Halmashauri ya Jiji la Mwanza itatoa ardhi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kugharamia ujenzi na kulipia gharama zingine za mradi.

Katika mwaka unaoangaziwa, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma iliripoti katika taarifa zake za fedha umiliki wa Kampuni kwa asilimia 93 sawa na shilingi bilioni 83.97, huku Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zikiripoti uwekezaji katika Kampuni hiyo wa shilingi bilioni 3.7 na bilioni 2.46 mtawalia. Hii inamaanisha kwamba mtaji wa hisa za Halmashauri umepunguzwa kutoka asilimia 40 mwaka 2010 hadi 7.

Kutokana na hali hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ilirekebisha muundo wa hisa za Kampuni kutoka uwiano wa 40:60 hadi 20:80 kwa kuupendelea Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma. Zaidi ya hayo, Bodi ilipendekeza kuwa ili Halmashauri ziendelee kuwa na hisa katika Kampuni kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Mkataba na Kifungu cha Ushirika, pamoja na thamani ya ardhi, inatakiwa kuongeza kiwango cha uwekezaji hadi asilimia 20 kwa kununua hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 10 zinazolipwa kwa uwiano wa 40:60 kwa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Halmashauri ya Jiji la Mwanza mtawalia.

Hata hivyo, hapakuwa na ushahidi wa kuhalalisha uwekezaji wa ziada ulioripotiwa kufanywa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kutoka shilingi bilioni 20 wakati wa kuanzishwa hadi shilingi bilioni 83.97 kufikia tarehe 30 Juni 2021. Kukosekana kwa ushahidi huo, kuna uwezekano wa gharama ya uwekezaji inayodaiwa kufanywa kuwa si sahihi na yenye lengo la kufifisha mtaji wa hisa za Halmashauri chini ya uwiano uliokubaliwa.

Kutokana na utata wa gharama za uwekezaji zinazoongezeka mara kwa mara, Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela hawajapata faida yoyote kutokana na uwekezaji uliofanyika katika Kampuni ya Mwanza City Commercial Complex kwa zaidi ya miaka 11 kutokana na hasara inayoripotiwa mara kwa mara na kampuni tangu kuanzishwa kwake.

**Ninasisitiza agizo lililotolewa wakati wa kikao cha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kilichofanyika tarehe 20 Oktoba 2021 kwa Mkurugenzi wa Jiji kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Katibu Tawala wa Mkoa (a) kuwasiliana na wadau wote ili kujadili muundo wa hisa za Kampuni na mipango ya usimamizi wa mradi kwa manufaa ya pande zote zinazohusika; na (b) kuundwe kamati ya pamoja itakayoundwa na wataalamu wenye ujuzi wa kutosha kuchunguza gharama za uwekezaji zilizoripotiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ili kupata uhalali wa muundo wa hisa ulioripotiwa.**

### 14.2.3 Uwekezaji Usio na Tija Katika Soko la Machinga Complex Shilingi Bilioni 16.27

Mwezi Julai 2007, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliingia mkataba wa muda mrefu wa kukopa kutoka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya ujenzi wa eneo la biashara Jijini Dar es Salaam (Machinga Complex). Mkopo wa awali ulikuwa shilingi bilioni 13.50 huku riba ya mtaji ya shilingi bilioni 2.77 ikilipwa kwa miaka 11, ingawa mwaka 2016, masharti ya mkopo yalipingwa na Halmashauri. Kutokana na hali hiyo, kamati ya pamoja kati ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, na Wizara ya Fedha na Mipango iliundwa ili kupitia mgogoro huo.

Ukaguzi wangu wa taarifa za fedha kwa mwaka unaoangaziwa ulibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii haikutambua deni lililotolewa kwa ajili ya ujenzi wa soko la Machinga Complex, na hali kama hiyo ilibainika katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020. Masuala ya malipo na utambuzi wa mkopo wa ujenzi wa soko la Machinga Complex yanatia shaka juu ya utaratibu mzima wa uwekezaji uliofanywa katika mradi huo kwa pande zote mbili.

Kwa kuzingatia ukweli kwamba muda wa mkopo uliisha tangu Julai 2018 bila taarifa zaidi kutoka Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii au kamati ya pamoja kuhusu hali ya mkopo, nimeshindwa kuthibitisha kiasi kilichoripotiwa katika taarifa za fedha za Halmashauri kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2021.

Kwa kuwa kiasi kikubwa cha mkopo kimebaki bila kulipwa kwa zaidi ya miaka 13 na hakuna maelezo ya kutosha katika taarifa za fedha za pande zote mbili kuhusiana na mkopo na mapato yaliyopatikana kutoka Machinga Complex, kuna uwezekano kwamba mapato ya uwekezaji huu yanatumika vibaya badala ya kutumika kulipia mkopo.

**Ninatoa wito kwa Serikali (a) kuifuta kazi kamati iliyoteuliwa kwa vile miaka sita imepita bila Kamati kukamilisha taarifa yake kuhusu suala hilo bila sababu za msingi; (b) Serikali ifikirie kufanya uchunguzi maalumu kuhusu mkopo usiolipwa kwa muda mrefu na kutoa maagizo kuhusu usimamizi na uendeshaji sahihi wa Machinga Complex; na (c) Ofisi ya Rais - TAMISEMI iielekeze menejimenti ya Halmashauri kuandaa ripoti tofauti za fedha za Machinga Complex ikiwa pamoja na taarifa ya mapato tangu kuanzishwa kwake na kuwasilisha kwangu pamoja na nyaraka zote kwa ajili ya ukaguzi.**

### 14.2.4 Taarifa Zisizotosheleza za Uwekezaji Katika Kampuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi

Kampuni hii (MDCC Ltd ilizinduliwa tarehe 21 Novemba 2019 na hivi sasa inaendesha mradi wa matofali, duka la dawa, na kiwanda cha maziwa. Mtaji wa hisa za Kampuni ni shilingi bilioni moja na hadi wakati wa ukaguzi (mwezi Agosti,2021) ni hisa zenye thamani ya shilingi milioni 24.55 pekee ndizo zililipwa kama uwekezaji wa awali kutoka Halmashauri.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Kampuni haikuwa na bodi ya wakurugenzi kwa hiyo hakuna mikutano mikuu ya bodi iliyofanyika tangu kuanzishwa kwake kinyume na malengo na katiba ya kampuni. Aidha, Kampuni haikuwa inatunza vitabu vya hesabu au kuandaa taarifa za fedha na hakuna mkaguzi yeyote aliyeteuliwa kukagua kumbukumbu zake za fedha kama ilivyoainishwa katika malengo na katiba ya Kampuni.

Nina maoni kwamba udhibiti usiofaa wa uendeshaji wa Kampuni unaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha na kushindwa kwa Kampuni kuzalisha faida.

**Uongozi wa Halmashauri unahimizwa (a) kuhakikisha kwamba bodi ya wakurugenzi ya Kampuni inaanzishwa; na (b) hesabu za Kampuni zinatayarishwe na kukaguliwa kama ilivyoainishwa kwenye malengo na katiba ya kampuni.**

### 14.2.5 Migogoro ya Uwekezaji Isiyotatuliwa na Upungufu wa Kiutendaji Katika Kampuni ya Nyama ya Arusha

Katika ripoti yangu ya miaka ya nyuma, nilitoa wito kwa hatua zinazofaa kuchukuliwa dhidi ya viongozi wanaodaiwa kuhusika katika utata wa uwekezaji wa pamoja kati ya Halmashauri ya Jiji la Arusha na Kampuni moja na kuunda Kampuni ya Nyama Arusha na uhamisho wa umiliki wa kiwanja cha Halmashauri Na.2 kilichopo Kitalu FF kwenda katika Kampuni ya zamani. Hata hivyo, sijaona maendeleo yoyote kuhusu hatua nilizopendekeza kuhusu uhamishaji haramu wa umiliki wa Kiwanja cha Halmashauri.

Katika tathmini yangu ya mwaka huu kwenye uwekezaji, niliendelea kubaini mapungufu mengi katika uendeshaji wa Kampuni ya Nyama Arusha. Kwa mfano, mapitio yangu ya makusanyo ya kila siku ya benki kutokana na mauzo dhidi ya taarifa za benki yalibainisha kuwa mauzo ya fedha taslimu ya shilingi milioni 54.4 hayakuwekwa benki kwa wakati na hivyo kusababisha kucheleweshwa kwa kipindi cha kati ya siku 4 hadi 59.

Pia, nililinganisha kati ya bidhaa zilizopo stoo na taarifa za mauzo na nilibaini utofauti ambapo kiasi kilichouzwa kilikuwa kikubwa kuliko kiasi kilichokuwapo kwa ajili ya mauzo ambacho, kimsingi, kinapaswa kuwa sawa. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa kilo 974 kati ya kilo 1,716 za nyama zilizokatwa zilikutwa katika maduka ya Kampuni na sehemu za mauzo mwishoni mwa mwaka. Hali hii inamaanisha kwamba kilo 741 zenye thamani ya shilingi milioni 9.52 hazikuhesabiwa au fedha zake zilitumika vibaya.

Nilipitia taratibu za ununuzi na usambazaji wa vifaa vya ujenzi na nilibaini kuwa mara nyingi fomu za ushindani mdogo zilitolewa mara kwa mara kwa wasambazaji walewale kwa kila agizo la bidhaa a huduma lililofanywa bila kujali upatikanaji wa wasambazaji wengine

walioteuliwa. Pia, mwaliko wa wasambazaji kwa usambazaji wa bidhaa na huduma ulifanywa kupitia ubao wa matangazo wa Kampuni badala ya kutumia jukwaa la mawasiliano lililoenea sehemu kubwa kama ilivyoainishwa katika kanuni za ununuzi.

**Kwa kuzingatia hayo, ninarudia pendekezo langu la mwaka uliopita kwamba Halmashauri ya Jiji la Arusha (a) ifuatilie kiwanja kilichohamishwa kinyume cha sheria na kuchukua hatua stahiki dhidi ya watendaji wote waliohusika katika mkataba huo wenye shaka; na (b) Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni inashauriwa zaidi kuimarisha uzingatiaji wa sheria na kanuni kuhusu usimamizi wa fedha na ununuzi na kuhakikisha mapato ya pesa taslimu yanapelekwa benki kwa wakati ikijumuisha usimamizi wa bidhaa zilizopo stoo, uzalishaji, na mauzo.**

### 14.2.6 Ukosefu wa Ufanisi wa Uwekezaji katika Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam

Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam lilianzishwa mwaka 1971 chini ya Sheria ya Maendeleo ya Wilaya, Sura ya 382 toleo lililorekebishwa mwaka 2002. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inamiliki Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam kwa asilimia 100. Shirika lilianzishwa kwa madhumuni ya kufanya shughuli za kibiashara au kiviwanda au biashara ambayo inaweza kuainishwa katika hati iliyolianzisha.

Katika mwaka huu wa ukaguzi nilibaini upotevu mkubwa wa mapato kutokana na kuchagua uwekezaji usiofaa. Nilibaini wakati wa kutembelea vitegauchumi mbalimbali vya Shirika kuwa mali zake zilizopo katika maeneo yenye thamani ya juu kama Keko, Mlimani, Kariakoo na Magomeni zimechakaa hivyo viwango vya kodi vinavyotozwa kwa wapangaji ni vya chini hivyo kusababisha upotevu wa mapato.

Katika eneo la DDC Mlimani, bei ya soko ya kodi ni karibu shilingi 23,000 hadi shilingi 113,000 kwa mita moja ya mraba, wakati Shirika linatoza shilingi 10,000 tu kwa mita ya mraba.

Katika eneo la Mlimani Mlalakuwa, Shirika lilipanga kujenga hosteli na pendekezo la mradi liliwasilishwa kwa Bodi mwezi Februari 2019.

Hata hivyo, nilibaini kuwa kuanza kwa mradi kumechelewa na kusababisha upotevu wa mapato. Pia, kuna nafasi ya wazi iliyokodishwa kama yadi inayolipiwa milioni 12 pekee kwa mwaka ambayo ni ndogo sana ikilinganishwa na viwango vya soko vilivyopo.

Vilevile, niliona nafasi iliyoachwa katika eneo la DDC Magomeni. Hata hivyo, mpangaji ametumia nafasi hiyo kama yadi akilipa shilingi milioni 36 kwa mwaka. Eneo hili liko katika hali mbaya na ikiwa Shirika litaendeleza nafasi hii, itapata mapato zaidi kuliko kuwa nayo kama yadi.

Katika eneo la Keko, nilibaini kuwa Shirika lilijenga maduka, ukumbi na baa tangu mwaka wa 2020. Hata hivyo, baa bado iko wazi, na ukumbi si wa kisasa kama kumbi zingine za kijamii. Kwa hiyo, mradi hautoi kiwango cha faida ya uwekezaji kinachotarajiwa.

**Ninapendekeza kwamba (a) Shirika la Maendeleo la Dar es Salaam libuni mkakati wa kina wa uwekezaji ikiwa pamoja na kukarabati mali zote linazomiliki ambazo zinaonekana kuingiza mapato chini ya uwezo wake baada ya kuachwa zikichakaa kwa muda mrefu. Hali hii italiwezesha Shirika kunufaika na viwango vya ushindani ili kuongeza faida ya uwekezaji wa mali zake.**

### 14.2.7 Amana za Shilingi Bilioni 4.88 katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa Zisizo na Tija

Kifungu cha 56 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2019 kilianzisha Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa ambayo ina mjumbe mmoja aliyeteuliwa na waziri mwenye dhamana ya fedha, na wajumbe wengine ambao waziri atawateua. Majukumu ya Bodi ni pamoja na kupokea, kusimamia na kuwekeza fedha za Bodi; kuzikopesha mamlaka za serikali za mitaa kutoka kwenye fedha za Bodi kwa ajili ya utoaji wa huduma na kufanya maendeleo; kutoa msaada wa kifedha kwa mamlaka za serikali za mitaa iwe kwa njia ya ruzuku, kutoa dhamana au kwa njia nyingine yoyote; na kutoa na kuendesha huduma kwa niaba au kwa manufaa ya mamlaka za serikali za mitaa.

Fedha na rasilimali za Bodi ni pamoja na fedha zilizowekwa na halmashauri na mamlaka za serikali za mitaa, mapato mengine ya Bodi iwe kwa riba ya uwekezaji wa Bodi au vinginevyo na michango, ruzuku, na mikopo kadri Bodi inavyoweza, mara kwa mara, kupokea kutoka kwa mtu yeyote au kundi la watu. Bodi inatakiwa kulipa riba kwa mamlaka za serikali za mitaa kuhusiana na fedha zilizowekwa kwenye Bodi kwa kiwango ambacho kitaidhinishwa na waziri mwenye dhamana ya fedha.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 20.3 (b) cha Mwongozo wa Fedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 "mamlaka ya serikali za mitaa itadumisha akiba kwa asilimia iliyowekwa ya mapato ya kawaida ya mwaka uliopita kabla ya ruzuku kujumuishwa na itatofautiana mwaka hadi mwaka". Kwa mujibu wa Kifungu cha 20.4 (b) cha Mwongozo wa Fedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, amana zinatakiwa kuwa sehemu ya mali za mamlaka ya serikali za mitaa.

Katika sampuli ya mamlaka 81 za serikali za mitaa zilizofanyiwa tathmini kati ya 185 zilizopo, nilibaini kuwa shilingi bilioni 4.88 zilichangwa kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa hadi tarehe 30 Juni 2021. Ingawa, amana hizi zinazochukuliwa katika Mwongozo wa Fedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama uwekezaji, hazijatoa faida yoyote kwa mamlaka husika za serikali za mitaa. Mchanganuo wa kina umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 14-1**.

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inachukulia kiasi ilichoweka katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kama fedha isiyoweza kurejeshwa kwa sababu haitaraji kuwa fedha hizo zitarejeshewa.

Aidha, uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa haukuwa na masharti yoyote ya kutoa gawio kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa fedha zilizowekwa. Tangu mwaka 2000, Halmashauri iliweza kukopa milioni 20 tu mara moja kati ya michango yake yote ya shilingi milioni 942.

Inaonekana kwamba malengo ya uanzishwaji wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa hayajafikiwa ipasavyo kwani idadi kubwa ya

mamlaka za serikali za mitaa zinatafuta mikopo kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na benki za biashara. Kwa kufanya hivyo, mamlaka za serikali za mitaa zinakabiliwa na viwango vya juu vya riba ambavyo vinaathiri kwa kiasi kikubwa uwekezaji wao.

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na Wizara ya Fedha na Mipango ili kuangalia upya Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kubainisha maeneo yote muhimu yanayohitaji maboresho ili kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kunufaika na fedha walizoweka ambazo zinaonekana kukaa katika akaunti ya Bodi bila kutoa faida yoyote ya maana.**

### 14.2.8 Taarifa Zisizotosheleza za Uwekezaji wa Shilingi Bilioni 2.95 katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza

Nimebaini kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza tangu mwaka 2019/20 imekuwa ikijenga Jengo la Uwanja wa Ndege wa Mwanza kwa gharama inayokadiriwa kufikia shilingi bilioni 5.4. Kiasi hiki kilitakiwa kuchangiwa na halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela ambapo Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilitakiwa kuchangia shilingi bilioni 2.2 na Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela shilingi bilioni 1.8.

Katika miaka ya 2019/2020 na 2020/21, kulikuwa na uhamisho wa fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.95 kutoka Halmashauri za Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela kwenda Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza katika akaunti maalumu ya benki namba 31110064751 yenye jina la Mwanza Airport Terminal kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na.14-2.**

**Jedwali Na.14-2 Fedha za ujenzi wa uwanja wa ndege**

| Mwaka | H/Jiji Mwanza (Sh.) | H/W Ilemela (Sh.) | Jumla (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 2020/21 | 617,000,000 | 470,000,000 | 1,087,000,000 |
| 2019/20 | 882,708,316 | 980,000,000 | 1,862,708,316 |
| **TOTAL** | **1,499,708,316** | **1,450,000,000** | **2,949,708,316** |

Hakukuwa na uthibitisho wowote uliotolewa kuhalalisha uhamishaji wa fedha hizo kwenda Uwanja wa Ndege wa Mwanza. Zaidi ya hayo,

hakukuwa na uhakika iwapo fedha hizo zilikuwa sehemu ya uwekezaji uliofanywa na Halmashauri hizo mbili au mkopo uliotolewa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania.

Pia nilibaini kuwa fedha zilizohamishwa hazikuidhinishwa katika bajeti za Halmashauri wala kupitishwa na Waziri mwenye dhamana kinyume na Kifungu cha 41 (1) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 (Kama ilivyorekebishwa mwaka 2015).

**Ninatoa wito kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) kuandaa sera ya uwekezaji kwa mamlaka za serikali za mitaa na kuanzisha mkataba wa maelewano na taasisi zinazotafuta usaidizi wa kifedha kutokana na fedha zilizoidhinishwa katika bajeti za mamlaka za serikali za mitaa; na (b) ninaishauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI izielekeze mamlaka za serikali za mitaa zote ziombe vibali kutoka ngazi zote kama ilivyoelezwa katika mfumo wa udhibiti kabla ya kufanya malipo yoyote kwa taasisi zingine au kufanya uwekezaji.**

NATIONAL AUDIT OFFICE NAOT

# SURA YA 15

# MATOKEO YA UKAGUZI MAALUMU

## 15.0 Utangulizi

Kifungu Na. 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 (Iliyorekebishwa 2021) pamoja na Kanuni za 78 na 79 (1) za Kanuni za Ukaguzi wa Umma za Mwaka 2009 zinampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalumu pale anapoona inafaa au kwa ombi maalumu la maandishi kutoka kwa ofisa masuuli, au mtu yeyote, taasisi, mamlaka ya umma, wizara, idara inayojitegemea, wakala, mamlaka ya serikali za mitaa, au chombo kingine chochote.

Katika kipindi ninachotolea taarifa nilifanya kaguzi maalumu 37 katika mamlaka 36 za serikali za mitaa, ambazo zinajumuisha ziliombwa na wadau mbalimbali na nilizozianzisha. Matokeo ya kaguzi hizi yameelezwa kwa kina katika ripoti zinazojitegemea zilizowasilishwa kwa taasisi zilizoomba kaguzi hizo, na kwa Katibu Mkuu Kiongozi kwa ukaguzi nilizozianzisha.

Sura hii inatoa muhtasari wa mapungufu yaliyobainika wakati wa ukaguzi maalumu uliofanyika mwaka 2021 kuhusiana na utendaji na miamala katika mwaka wa fedha kuanzia mwaka 2009/10 hadi 2020/21.

Makundi ya kaguzi hizi maalumu yameainishwa kwa muhtasari hapa chini.

**Ukaguzi Maalumu Uliofanyika kwa Maombi ya Watu au Taasisi**

Ombi la kufanya kaguzi hizo liliwasilishwa kwangu na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Mbunge wa Jimbo la Sengerema. Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema.

**Kaguzi maalumu zilizofanyika kwa maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

Kaguzi hizi zimefanyika katika katika mamlaka 34 za serikali za mitaa kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na 15-1.**

**Jedwali Na 15 -1: Kaguzi maalumu zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Mwaka wa Fedha Uliokaguliwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | H/W Longido | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 2. | | H/W Arusha | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 3. | Dar es Salaam | H/M Kigamboni | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 4. | | H/M Ubungo | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 5. | | H/M Temeke | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 6. | | H/M Kinondoni | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 7. | | H/M Dar es Salaam | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 8. | Dodoma | H/MJI Mpwapwa | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 9. | Geita | H/W Mbogwe | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 10. | | H/Mji Geita | 2013/14 hadi 2020/21 |
| 11. | Iringa | H/W Iringa | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 12. | Kagera | H/W Kyerwa | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 13. | | H/W Biharamulo | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 14. | Katavi | H/W Mpanda | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 15. | Kigoma | H/W Kakonko | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 16. | Kilimanjaro | H/W Moshi | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 17. | Lindi | H/W Nachingwea | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 18. | Manyara | H/Mji Babati | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 19. | Mara | H/W Bunda | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 20. | Mbeya | H/W Chunya | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 21. | Morogoro | H/W Ifakara | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 22. | Mtwara | H/W Masasi | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 23. | Mwanza | H/W Ilemela | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 24. | Njombe | H/W Ludewa | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 25. | Pwani | H/W Rufiji | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 26. | Rukwa | H/W Kalambo | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 27. | Ruvuma | H/W Tunduru | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 28. | Shinyanga | H/W Shinyanga | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 29. | Simiyu | H/W Bariadi | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 30. | Singida | H/W Singida | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 31. | Songwe | H/W Songwe | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 32. | Tabora | H/W Igunga | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 33. | | H/W Urambo | 2018/19 hadi 2020/21 |
| 34. | Tanga | H/W Kilindi | 2018/19 hadi 2020/21 |

Masuala muhimu ambayo yalibainishwa katika ripoti za ukaguzi maalumu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yameainishwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

## 15.1 Ukaguzi Maalumu Ulioombwa na TAKUKURU na Mbunge

### 15.1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema

**i. Makusanyo ya Fedha Taslimu Shilingi Milioni 645.24 kwa Njia ya POS Yasiyowasilishwa Benki**

Nilibaini kuwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 01 Julai 2015 hadi 15 Februari 2021, Halmashauri kwa kutumia namba za utambulisho wa mlipaji 87 kupitia Mfumo wa Kukusanya Mapato (LGRCIS) ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 3.03 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2.38 kiliwasilishwa benki, na kiasi cha shilingi milioni 645.24 hakikuwasilishwa benki. Hali hii ni kinyume na Kifungu Na. 42(2) cha Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019) ikisomwa pamoja na Agizo la 50(5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

**Serikali kupitia Katibu Mkuu (Ofisi ya Rais - TAMISEMI) (a) ihakikishe kuwa hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya waliohusika na kutokuwasilisha mapato yaliyokusanywa benki; na (b) ihakikishe kiasi cha shilingi milioni 645.24 kinawasilishwa benki mara moja.**

**ii. Hasara ya Shilingi Milioni 681.10 Kutokana na Kutelekezwa kwa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Katika Kijiji cha Katunguru**

Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ilisaini mkataba Na. LGA/094/HQ/IRR/2009-2010/44 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Katunguru kwa thamani ya shilingi milioni 883.80 ulioanza tarehe 10 Agosti 2011 na kukamilika tarehe 10 Aprili 2012. Nilibaini ongezeko la wigo wa kazi wenye jumla ya shilingi bilioni 1.01 lililosababisha thamani ya mkataba kuongezeka kutoka shilingi milioni 883.80 hadi shilingi bilioni 1.89 sawa na asilimia 114.

Kutokana na mapungufu katika usanifu wa mradi, hadi kufikia mwezi Aprili 2021 wakati wa ukaguzi huu, mradi ulikuwa haujakamilika na mkandarasi alikuwa ametelekeza eneo la mradi akiwa tayari ameshalipwa shilingi milioni 681.1 kupitia cheti cha malipo Na. 1-3. Kiasi kilicholipwa kwa mkandarasi ni hasara kwa Halmashauri.

**Ninaishauri Serikali ihakikishe inakamilisha mradi wa ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Kijiji cha Katunguru ili thamani ya fedha za mradi huo iweze kupatikana.**

**iii. Hasara ya Shilingi Milioni 354.59 Iliyotokana na Malipo kwa Wakandarasi kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika**

Kanuni ya 243 (1-2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inataka taasisi inayofanya ununuzi kupima na kuthibitisha kazi katika vipindi vilivyoainishwa katika mkataba kabla ya kuidhinisha malipo. Katika mapitio ya mikataba mitatu yenye thamani ya shilingi bilioni 3.93 (bila kodi ya ongezeko la thamani), nilibaini kuwa malipo ya shilingi milioni 354.59 yalilipwa kwa wakandarasi kwa kazi ambazo hazikufanyika.

Miongoni mwa kiasi hicho ni shilingi milioni 31.76 kwa kazi ambazo hazikufanyika katika Mradi wa Maji Buyagu-Kalangalala-Bitoto; shilingi milioni 89.88 kwa ujenzi wa Mradi wa Maji Katunguru-Nyamtelela; shilingi milioni 73.76 kwa kukarabati na kuboresha miundombinu ya Mradi wa Maji Busisi; na shilingi milioni 159.19 kwa kazi ambazo hazikufanyika katika Mradi wa Maji wa Vijiji vya Chamabanda, Nyantakubwa na Kasungamile

Ni wazi kuwa Halmashauri na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) haikuwa makini kupima kazi zilizofanyika kabla ya kuidhinisha malipo.

**Ninapendekeza kwamba Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili wachunguze malipo yaliyofanywa kwa kazi ambazo hazikutekelezwa na kuwachukulia hatua maofisa wote waliohusika.**

### iv. Mradi wa Maji (LVWATSAN II) Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 1.08 Uliotelekezwa na Kutofanya Kazi

Mkataba Na. MWAUWASA/LVWATSAN II/EAC/2014/001 uliingiwa baina ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na mkandarasi kwa ajili ya kutekeleza awamu ya pili ya Mradi wa Maji LVWATSAN II katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kuanzia tarehe 7 Oktoba 2014 hadi tarehe 31 Machi 2017 kwa thamani ya shilingi bilioni 24.76.

Hadi ninahitimisha ukaguzi huu tarehe 30 Aprili 2021, miundombinu ya usafi wa mazingira na majitaka iliyogharimu shilingi bilioni 1.08 haikuwa ikifanya kazi kutokana na kujengwa bila usanifu. Miundombinu hiyo inajumuisha dampo la taka lililojengwa eneo la Ibondo kwa thamani ya shilingi milioni 931.96 na makontena 29 ya kuhifadhia taka kati ya 37 yenye thamani ya shilingi milioni 152.95.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji na Umwagiliaji (a) iwachukulie hatua stahiki mshauri mwelekezi, mkandarasi na mratibu wa mradi wa MWAUWASA LVWATSAN II kwa kuisababishia Serikali hasara ya shilingi milioni 931.96 zilizotumika kujenga dampo ambalo halitumiki; na (b) Katibu Mkuu (Ofisi ya Rais - TAMISEMI) kwa kushirikiana na menejimenti ya Halmashauri ichukue hatua stahiki kuhakikisha miundombinu ya mradi huo inafanya kazi kama ilivyopangwa, ikiwa pamoja na kujenga kingo kuzunguka dampo ili kulikinga eneo hilo dhidi ya mafuriko.**

### 15.1.2 Ujenzi na Ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Ihungo Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba

#### i. Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Kiasi Cha Shilingi Milioni 393.64 Iliyojumuishwa Katika Cheti Cha Malipo Kinyume Na Mkataba

Tarehe 22 Desemba 2016, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliingia mkataba namba ME-024/CTR/HQ/2016-17/10 wenye thamani ya shilingi bilioni 10.49 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Ihungo. Kulikuwa na

ongezeko la gharama za mradi kwa kiasi cha shilingi milioni 463.60 na hivyo kusababisha gharama za mradi kufika shilingi bilioni 10.95.

Hadi kufikia mwezi Machi 2021, mkandarasi alikuwa amelipwa kiasi cha shilingi bilioni 10.69 kupitia cheti Na. 1-7. Hata hivyo, cheti Na. 2 chenye thamani ya shilingi bilioni 2.58 kilijumuisha kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha shilingi milioni 393.64 ambayo kimsingi mkandarasi hakupaswa kulipwa kwa kuwa mkataba huo haukuainisha kama bei hiyo inajumuisha kodi ya ongezeko la thamani.

Kwa maoni yangu, kiasi cha shilingi milioni 393.64 hakikupaswa kulipwa kulingana na matakwa ya mkataba.

**Ninashauri Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia awasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza kiasi cha shilingi milioni 393.64 zilizolipwa kama kodi ya ongezeko la thamani katika cheti cha malipo awamu ya 2 na hatua stahiki zichukuliwe kwa maofisa wote waliohusika kuidhinisha malipo hayo.**

**ii. Matumizi ya Vifaa vya Ujenzi Visivyokidhi Ubora vya Thamani Shilingi Milioni 518.2**

Mkandarasi alinunua nondo za 10mm zenye thamani ya shilingi milioni 387.73 kutoka kwa wazabuni mbalimbali zisizokidhi ubora kwa mujibu matakwa ya mkataba. Vilevile, nilibaini kuwa mkandarasi alinunua rangi zenye thamani ya shilingi milioni 130.47 kutoka kampuni isiyopendekezwa katika mkataba, na rangi hizo zilinunuliwa pasipo kuzingatia viwango vya ubora vilivyoainishwa katika Kipengele cha 13.2 cha masharti maalumu ya mkataba kilichomtaka mkandarasi kutumia rangi zilizochanganywa na kuwa tayari kwa matumizi kwa ubora wa vipimo vilivyoanishwa katika mkataba ambavyo ni BS 2521-2524.

Kitendo cha Mkandarasi kutumia nondo na rangi zisizokidhi viwango vya ubora kunaweza kuathiri ubora wa majengo ya shule hiyo.

**Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI awasiliane na Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi ili kuwachukulia hatua stahiki watumishi wa Wakala wa Majengo Tanzania waliohusika kununua nondo na rangi zisizokidhi ubora katika ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihungo.**

### 15.1.3 Ukaguzi Maalumu wa Barabara ya Kijichi - Toangoma (km 5.5) na Kijichi - Mwanamtoti (km 1.8) katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Zilizojengwa Chini ya Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam

#### i. Malipo ya Shilingi Milioni 120 Zaidi ya Kazi Zilizofanyika

Nimebaini katika Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kijichi – Toangoma kupitia mkataba LGA//016/2015-2016/W/DMDP/01 wenye thamani ya shilingi bilioni 21.67, mkandarasi alipaswa kulipwa kiasi cha shilingi bilioni 13.46 kulingana na kazi zilizohakikiwa badala ya shilingi bilioni 13.50 alizolipwa hivyo kulipwa zaidi shilingi milioni 40. Kadhalika, katika Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kijichi – Mwanamtoti, mkandarsi alipaswa kulipwa kiasi cha shilingi bilioni 5.15 badala ya shilingi bilioni 5.23 alizolipwa kwa kazi alizofanya na kusababisha malipo ya ziada ya shilingi milioni 80 kwa mkandarasi.

**Ninamshauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) achukue hatua stahiki kwa watumishi waliohusika kuandaa na kuidhinisha malipo ya kazi ambazo hazijafanyika; na (b) ahakikishe kuwa mkandarasi anarejesha kiasi cha shilingi milioni 120 walizolipwa kwa kazi ambazo hazikutekelezwa.**

#### ii. Hasara ya Shilingi Bilioni 1.22 Iliyosababishwa na Kumuondoa Mzabuni Mwenye Gharama Ndogo

Katika ukaguzi wangu, kinyume na Kifungu cha 72 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, Kanuni ya 203 (2) na Kanuni ya 17 (2-4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, nilibaini kuwa mkandarasi mwenye bei ya chini ya shilingi bilioni 20.45 (bila kodi ya ongezeko la thamani) aliondolewa wakati wa kufanyika tathmini bila sababu za msingi na kumpa kazi mkandarasi mwingine kwa gharama ya shilingi bilioni 21.67 (bila kodi ya ongezeko la thamani) hivyo kusababisha hasara ya shilingi bilioni 1.22.

Maamuzi ya Bodi ya Zabuni na Kamati ya Tathmini kumwondoa mkandarasi mwenye gharama ya chini kumetokana na Kamati ya Tathmini kutumia kigezo kisichostahili na kusababisha gharama ya mradi kuongezeka kwa shilingi bilioni 1.22 ambayo ni hasara kwa Serikali.

**Ninashauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI achukue hatua stahiki kwa waliohusika kuisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 1.22 kwa kutompa tenda mzabuni mwenye gharama ya chini.**

## 15.2 Kaguzi Maalumu Zilizofanyika kwa Maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

### 15.2.1 Hoja zenye Mwelekeo Unaofanana Katika Halmashauri Nyingi Zilizokaguliwa

#### i. Makusanyo ya Shilingi Bilioni 9.60 ambayo Hayakuwasilishwa Benki

Matokeo ya ukaguzi maalumu uliofanyika katika mamlaka 31 za serikali za mitaa yanaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, makusanyo ya jumla ya shilingi bilioni 9.60 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani hayakuwasilishwa benki kutokana na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani. Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 242.36 kilitokana na mapato yatokanayo na huduma za afya.

Kutowasilisha mapato benki kulichangiwa zaidi na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani katika mamlaka katika ukusanyaji na uwasilishaji wa mapato benki; na ni kinyume na Agizo la 50 (5) la Randama ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009 ambayo inaelekeza makusanyo yote kuwasilishwa benki siku hiyohiyo au siku inayofuata.

Mchanganuo wa mapato taslimu ambayo hayakuwasilishwa benki kwa kila halmashauri ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 15-2** hapa chini.

**Jedwali Na 15 -2:** Mapato ambayo hayakuwasilishwa benki

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | H/W Longido | 298,781,938 |
| 2. | | H/W Arusha | 117,865,762 |
| 3. | Dar es Salaam | H/M Ubungo | 563,076,800 |
| 4. | | H/M Kigamboni | 127,673,100 |
| 5. | | H/M Kinondoni | 1,265,668,160 |
| 6. | Dodoma | H/W Mpwapwa | 301,700,393 |
| 7. | Geita | H/W Mbogwe | 179,822,016 |
| 8. | Iringa | H/W Iringa | 35,575,031 |
| 9. | Kagera | H/W Kyerwa | 19,749,683 |
| 10. | Kagera | H/W Biharamulo | 482,544,529 |
| 11. | Katavi | H/W Mpanda | 334,755,218 |
| 12. | Kigoma | H/W Kakonko | 217,251,755 |
| 13. | Kilimanjaro | H/W Moshi | 154,731,663 |
| 14. | Lindi | H/W Nachingwea | 4,960,395 |
| 15. | Manyara | H/M Babati | 93,891,092 |
| 16. | Mara | H/W Bunda | 144,011,399 |
| 17. | Mbeya | H/W Chunya | 259,280,247 |
| 18. | Morogoro | H/Mji Ifakara | 236,638,459 |
| 19. | Mtwara | H/M Masasi | 44,337,100 |
| 20. | Mwanza | H/M Ilemela | 627,856,616 |
| 21. | Njombe | H/W Ludewa | 150,096,454 |
| 22. | Pwani | H/W Rufiji | 1,962,855,526 |
| 23. | Rukwa | H/W Kalambo | 97,918,150 |
| 24. | Ruvuma | H/W Tunduru | 300,420,128 |
| 25. | Shinyanga | H/W Shinyanga | 999,240,060 |
| 26. | Simiyu | H/M Bariadi | 151,124,348 |
| 27. | Singida | H/W Singida | 15,039,326 |
| 28. | Songwe | H/W Songwe | 218,772,736 |
| 29. | Tabora | H/W Urambo | 25,620,000 |
| 30. | Tabora | H/W Igunga | 48,442,460 |
| 31. | Tanga | H/W Kilindi | 118,153,195 |
| **Jumla** | | | **9,597,853,739** |

**Ninashauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI awasiliane na vyombo vya uchunguzi ikiwa pamoja na TAKUKURU na Jeshi la Polisi kuhakikisha vinafanya uchunguzi na kuchukua hatua stahiki dhidi ya maofisa waliohusika.**

**ii. Marekebisho ya miamala ya thamani ya shilingi bilioni 28.33 ambayo hayakuidhinishwa**

Katika kipindi cha miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, nilibaini kwamba mamlaka 16 za serikali za mitaa zilifanya marekebisho ya ankara na ufutaji wa miamala katika Mfumo wa Makusanyo ya Mapato (LGRCIS) yenye thamani ya shilingi bilioni 28.33 bila kufuata taratibu zilizowekwa. Marekebisho hayo hayakuidhinishwa na maofisa masuuli husika na hayakuwa na

ushahidi wowote wa maandishi. Hali hii imesababishwa na uwapo wa mfumo dhaifu wa udhibiti wa makusanyo ya mapato ya ndani. Muhutasari wa halmashauri zilizobainika kufanya marekebisho ya miamala yasiyoidhinishwa ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 15-3** hapa chini.

**Jedwali Na 15 -3: Marekebisho ya miamala katika Mfumo wa Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuidhinishwa**

| Na. | Mkoa | Jina La Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | H/W Longido | 23,122,895 |
| 2. | | H/W Arusha | 32,239,000 |
| 3. | Dar es Salaam | H/M Ubungo | 156,900,936 |
| 4. | Dar es Salaam | H/M Kinondoni | 10,857,780,242 |
| 5. | Dodoma | H/W Mpwapwa | 129,265,756 |
| 6. | Kagera | H/W Biharamulo | 466,857,403 |
| 7. | Kilimanjaro | H/W Moshi | 508,551,089 |
| 8. | Lindi | H/W Nachingwea | 2,626,096,232 |
| 9. | Manyara | H/M Babati | 1,524,857,685 |
| 10. | Mara | H/W Bunda | 36,040,721 |
| 11. | Mwanza | H/M Ilemela | 8,724,331,077 |
| 12. | Njombe | H/W Ludewa | 168,007,444 |
| 13. | Rukwa | H/W Kalambo | 1,236,658,523 |
| 14. | Ruvuma | H/W Tunduru | 1,466,155,022 |
| 15. | Shinyanga | H/W Shinyanga | 131,248,516 |
| 16. | Simiyu | H/Mji Bariadi | 243,000,669 |
| **Jumla** | | | **28,331,113,210** |

Kwa maoni yangu, marekebisho yasiyo na idhini yalifanyika ili kuficha ubadhirifu wa fedha za mapato ya ndani. Aidha, kufuta au kurekebisha taarifa za mapato katika Mfumo bila idhini kunachangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa fedha za Serikali.

**Ninazishauri Mamlaka husika (a) zichukue hatua stahiki dhidi ya wote waliofanya marekebisho ya miamala ya mapato iliyokosewa bila kufuata utaratibu na bila kuzingatia matakwa ya mfumo wa udhibiti wa mapato ya ndani; na (b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe kuwa Mfumo wa Makusanyo ya Mapato unatoa nafasi kwa mwidhinishaji kutoa kibali na zuio la kufanya marekebisho bila idhini.**

### iii. Hati za Malipo ya Shilingi Bilioni 1.37 Ambazo Hazikuwasilishwa kwa Ajili ya Ukaguzi

Wakati wa ukaguzi maalumu, mamlaka 7 za serikali za mitaa hazikuwasilisha kwangu hati za malipo zenye thamani ya jumla ya

shilingi bilioni 1.37 kwa malipo yaliyofanyika kati ya miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, hivyo sikuweza kujiridhisha na uhalali wa malipo yaliyofanyika. Hali hii ni kinyume na Kifungu cha 15(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008, pamoja na Agizo la 8 (2) (c) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

Mchanganuo wa nyaraka za malipo ambazo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kwa kila halmashauri ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na 15-4** hapa chini.

**Jedwali Na 15 -4: Hati ambazo hazikuwasilishwa kwa ukaguzi**

| Na. | Mkoa | Jina La Halmashauri | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | H/W Arusha | 49,507,236 |
| 2. | Dodoma | H/W Mpwapwa | 185,689,454 |
| 3. | Iringa | H/W Iringa | 21,977,000 |
| 4. | Manyara | H/M Babati | 401,802,862 |
| 5. | Mara | H/W Bunda | 233,931,243 |
| 6. | Rukwa | H/W Kalambo | 432,519,015 |
| 7. | Shinyanga | H/W Shinyanga | 43,862,800 |
| **Jumla** | | | **1,369,289,610** |

**Ninapendekeza kuwa mamlaka husika zichukue hatua stahiki dhidi ya wafanyakazi wa halmashauri waliotajwa katika taarifa maalumu za ukaguzi kwa upotevu wa hati za malipo.**

### iv. Ujumuishwaji wa Madeni Hewa ya Thamani ya Bilioni 1.52 Katika Taarifa za Fedha

Ukaguzi maalumu katika mamlaka 20 za serikali za mitaa ulibaini uwapo wa madeni ya jumla ya shilingi bilioni 1.52 ambayo yalishalipwa na hayakustahili kujumuishwa katika orodha ya madeni kinyume na Agizo 8(2) (c) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009. Hali hii inaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za umma endapo madeni hayo yatalipwa. Muhtasari wa halmashauri zilizobainika kujumuisha madeni hewa ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na 15-5** hapa chini.

**Jedwali Na 15 -5: Madeni hewa katika taarifa za fedha**

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | H/W Arusha | 100,469,222 |
| 2. | | H/W Longido | 120,258,007 |
| 3. | Dodoma | H/W Mpwapwa | 37,023,123 |
| 4. | Geita | H/W Mbogwe | 47,848,740 |

| Na. | Mkoa | Jina la Halmashauri | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 5. | Iringa | H/W Iringa | 127,261,363 |
| 6. | Kagera | H/W Kyerwa | 14,892,232 |
| 7. | Kigoma | H/W Kakonko | 107,438,685 |
| 8. | Kilimanjaro | H/W Moshi | 57,015,400 |
| 9. | Mara | H/W Bunda | 105,160,181 |
| 10. | Mbeya | H/W Chunya | 22,590,520 |
| 11. | Morogoro | H/Mji Ifakara | 29,449,602 |
| 12. | Mwanza | H/M Ilemela | 200,519,659 |
| 13. | Njombe | H/W Ludewa | 192,381,080 |
| 14. | Pwani | H/W Rufiji | 122,171,822 |
| 15. | Rukwa | H/W Kalambo | 9,229,471 |
| 16. | Ruvuma | H/W Tunduru | 13,784,000 |
| 17. | Shinyanga | H/W Shinyanga | 62,949,405 |
| 18. | Simiyu | H/Mji Bariadi | 16,882,353 |
| 19. | Tabora | H/W Urambo | 112,662,196 |
| 20. | | H/W Igunga | 19,985,865 |
| **Jumla** | | | **1,519,972,926** |

**Ninapendekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI aziagize halmashauri husika kuhakikisha madeni halali pekee ndiyo yanaingizwa katika taarifa za fedha za mwaka.**

### 15.2.2 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Zamani Halmashauri ya Manispaa ya Ilala)

Baada ya kuona viashiria vya upotevu wa fedha za makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Manispaa ya Ilala), mnamo tarehe 1 Novemba 2021 niliamua kufanya Ukaguzi Maalumu katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 ili kubaini iwapo fedha zilizokusanywa katika vyanzo mbalimbali zilikusanywa kikamilifu na kuwasilishwa Halmashauri; pia kuhakiki iwapo kulikuwa na ubadhirifu wa fedha zilizokusanywa. Ukaguzi wangu ulibaini masuala yafuatayo:

#### (i) Ubadhirifu wa Mapato ya Shilingi Bilioni 10.13 ya Halmashauri Yaliyokusanywa na Mawakala 10 na Watumishi 19

Kwa mujibu wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani na uwasilishaji wake Halmashauri, ilinilazimu kuhakiki taarifa za Mfumo wa Mapato wa Serikali za Mitaa na taarifa za akaunti za mapato za Halmashauri katika Benki za NMB, CRDB, NBC na DCB kwa kipindi kilichoanzia mwezi Julai 2019 hadi Juni 2021 na kubaini kuwa mawakala 10 na watumishi 19 walikusanya mapato ya Halmashauri

ya jumla kiasi cha shilingi bilioni 9.07 na shilingi bilioni 7.29 mtawalia. Mawakala hao walipaswa kuwasilisha Halmashauri jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 5.62 kati ya walichokusanya, huku kiasi chote kilichokusanywa na watumishi kikipaswa kuwasilishwa Halmashauri.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mawakala na watumishi hao waliwasilisha Halmashauri jumla ya kiasi cha shilingi milioni 987.76 na shilingi bilioni 1.8 pekee, na kutowasilishisha kiasi cha jumla ya shilingi bilioni 4.64 na shilingi bilioni 5.49 mtawalia. Ukaguzi wangu ulithibitisha vitendo vya ubadhirifu wa fedha zilizokusanywa na mawakala na watumishi husika ambazo hazikuwasilishwa Halmashauri kwa mbinu mbalimbali za udanganyifu zikiwemo kubadili taarifa za Mfumo na kutoa stakabadhi za mapokezi ya fedha zenye udanganyifu hivyo kuisababishia Halmashauri hasara ya jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 10.13.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi na mawakala waliosababisha hasara hiyo na kuhakikisha kiasi hicho kinarejeshwa.**

**(ii) Ubadhirfu wa Mapato ya Shilingi Milioni 495.57 ya Halmashauri Yaliyokusanywa na Wakala**

Pia, ukaguzi wangu ulihakiki usimamizi wa Halmashauri katika utekelezaji wa mikataba iliyoingia na mawakala kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato yake ya ndani na kubaini udhaifu. Mathalani, ilibainika kuwa licha ya muda wa mkataba wa Wakala Pick Trading Ltd kwisha tarehe 30 Novemba 2019, aliendelea kukusanya mapato ya Halmashauri bila mkataba kwa miezi 11 kuanzia tarehe 01 Desemba 2019 hadi 30 Oktoba 2020, ambapo alikusanya kiasi cha jumla ya shilingi milioni 496.47 na kuwasilisha Halmashauri kiasi cha shilingi 900,000 pekee, huku kiasi cha shilingi milioni 495.57 kikibakia kwa wakala isivyostahili.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi na mawakala waliosababisha hasara hiyo.**

### (iii) Udanganyifu Katika Matumizi ya Mashine Za POS Zilizotumika Kukusanya Mapato ya Shilingi Milioni 131.35

Kadhalika, ukaguzi wangu ulibaini udanganyifu wa taarifa za makusanyo kwa mawakala kurudisha nyuma muda halisi wa makusanyo husika ili kupotosha taarifa hiyo katika Mfumo wa Kukusanya Mapato. Katika kipindi cha miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21 mawakala Pick Trading Ltd. na Workers General Supply walikusanya kwa kutumia mashine za POS kiasi cha shilingi milioni 131.07 na 289,500 mtawalia.

Hata hivyo, nilibaini kuwa mawakala hao walirejesha nyuma muda katika mashine za POS kwa kuonesha makusanyo hayo yalifanyika kati ya mwaka 2008 na 2017, kipindi ambacho hata namba za utambulisho zilizotumika hazikuwa zimesajiliwa katika Mfumo wa Makusanya ya Mapato. Nilithibitisha kuwa hatua hiyo ililenga kupotosha kiasi halisi cha makusanyo kilichopaswa kuwasilishwa Halmashauri katika kipindi husika kwa kuficha miamala halisi katika muda huo.

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi na mawakala waliosababisha hasara hiyo.**

## 15.2.3 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke

Katika mwaka wa fedha 2020/21 nilifanya kaguzi maalumu tatu katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ambazo ni uzoaji taka, mkopo kutoka benki ya CRDB uliotumika kulipa fidia ili kupisha Utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji La Dar es Salaam na miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Masuala ya msingi yaliyojitokeza na kupewa umuhimu mkubwa katika taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

### (a) Ukaguzi Maalumu wa Uzoaji Taka

**i. Mapato ya Shilingi Milioni 719.77 ya Uzoaji wa Taka Ambayo Hayakuwasilishwa**

Katika ukaguzi maalumu wa miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21, nilibaini Halmashauri ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 3.60 kutokana na ushuru wa uzoaji taka. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2.09 kilikusanywa na watendaji na shilingi bilioni 1.51 kilikusanywa na wakandarasi.

Vipengele vya 3 na 6 (iii) vya mkataba kati ya Halmashauri na wakandarasi wa uzoaji wa taka kinawataka wakandarasi wote kurejesha Halmashauri asilimia 20 ya makusanyo yake yanayotokana na ushuru wa uzoaji wa taka. Hata hivyo, nilibaini kuwa kiasi cha shilingi milioni 719.77 (sawa na asilimia 20) ya makusanyo yote hakikuwasilishwa katika Halmashauri.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichukue hatua stahiki dhidi ya maofisa wa Halmashauri walioshindwa kusimamia utekelezaji wa mikataba na kusababisha kutowasilishwa kwa mapato ya shilingi milioni 719.77.**

**ii. Malipo Hewa Kiasi cha Shilingi Milioni 114.45 za Ukodishaji wa Magari ya Uzoaji Taka**

Nilibaini kuwa Halmashauri ililipa masurufu yenye jumla ya shilingi milioni 298.40 kwa watumishi mbalimbali wa kitengo cha usafi na mazingira kwa ajili ya gharama za kukodi magari 43 kwa ajili ya kusafirisha taka kwenda dampo la Pugu Kinyamwezi. Hata hivyo, nilifanya uhakiki wa magari haya kwa Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mkoa wa Kariakoo na kubaini miongoni mwa vyombo hivyo ni pikipiki za matairi mawili, pikipiki za matairi matatu, magari madogo, na vyombo vingine ambavyo havikuwa vimesajiliwa.

Kati ya kiasi kilicholipwa, shilingi milioni 183.95 kililipwa kwa magari halali na shilingi milioni 114.45 yalikuwa malipo hewa ya magari ya uzoaji taka. Pia, nilibaini kuwa Halmashauri haikuwa na mikataba ya

kukodi magari hayo kinyume na Kifungu cha 60(7) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichukue hatua stahiki dhidi ya watendaji wa Halmashauri waliowasilisha nyaraka za kughushi kwa ajili ya malipo ya uzoaji taka kiasi cha shilingi milioni 114.45.**

**iii. Malipo ya Kiasi Cha Shilingi Milioni 373.67 ya Uzoaji Taka na Ununuzi wa Vifaa vya Usafi Kupitia Stakabadhi za Kielekitroniki Zilizoghushiwa**

Nilibaini kiasi cha shilingi milioni 410.42 kililipwa kwa njia ya masurufu kwa watumishi wa halmashauri katika idara ya usafi na mazingira kwa ajili ya uzoaji taka. Hata hivyo, nilifanya uhakiki wa uhalali wa stakabadhi za kielekitroniki zilizotumika kama sehemu ya nyaraka za marejesho ya masurufu kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania na nilibaini stakabadhi zilizoambatishwa zenye kiasi cha shilingi milioni 373.67 hazikutambuliwa na Mamlaka hiyo. Hali hii inamaanisha kwamba watumishi wa Halmashauri waliochukua masurufu na kuwasilisha stakabadhi za kughushi wamesababishia serikali hasara ya shilingi milioni 373.67

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichukue hatua stahiki dhidi ya watendaji wa Halmashauri waliohusika katika kuambatisha stakabadhi za kielekitroniki zilizoghushiwa zenye thamani ya shilingi milioni 373.67.**

**(b) Ukaguzi wa Miradi ya Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam Iliyotekelezwa kwa Ufadhili wa Benki ya Dunia**

**i. Malipo Zaidi ya Gharama Halisi ya Bima Yaliyosababisha Hasara ya Shilingi Bilioni 2.02**

Kipengele cha 3(a) (Jedwali la Tatu) cha Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 kinataka malipo yatakayofanywa kwa wakala au mhusika wa tatu iwe fidia inayoendana na huduma halali. Halmashauri ililipa jumla ya shilingi bilioni 2.38 kwa wakandarasi kwa ajili ya gharama za bima wakati wa kutekeleza miradi ya

Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam. Hata hivyo, nilibaini kuwa gharama ya bima kwa wakandarasi wote ni shilingi milioni 376.55 tu, hivyo kusababisha malipo ya ziada kwa shilingi bilioni 2.02 kinyume na Kanuni tajwa hapo juu.

Ni maoni yangu kwamba, malipo ya ziada ya shilingi bilioni 2.02 kwa ajili ya bima yameongeza gharama za utekelezaji wa mradi na kuisababishia hasara Halmashauri.

**Ninashauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI achukue hatua stahiki kwa maofisa ambao kwa namna moja au nyingine walihusika katika dosari hizo.**

**ii. Ongezeko la Gharama za Mradi kwa Shilingi Bilioni 1.23 Kutokana na Kazi Moja Kuingizwa Mara Mbili Katika Hati ya Makadirio ya Gharama za Ujenzi**

Katika ukaguzi wa mradi wa ukarabati na utengenezaji wa Daraja la Kijichi-Tuangoma na barabara zake (km 3) pamoja na Barabara ya Mwanamtoti (km 1.8) kwa awamu ya kwanza uliotekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, nilibaini kazi katika kipengele Na. 23.08(a) kinachosomeka "cast in situ concrete lining grade 25 to drains, rate inxlussive of formwork" kiliingizwa mara mbili na kusababisha gharama za mradi kuongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.23

**Ninapendekeza, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) awachukulie hatua watumishi wote ambao hawakutimiza majukumu yao na kusababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa shilingi bilioni 1.23 kutokana na kazi iliyojirudia katika mkataba; na (b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI iangalie namna ya kuongeza udhibiti katika ulipaji wa fedha za miradi ya maendeleo ikiwemo Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam ili kuondoa uwezekano wa Serikali kupata hasara.**

iii. **Malipo Hewa Kiasi cha Shilingi Milioni 219.05 kwa Ajili ya Kuhamisha Miundombinu ya Maji na Mawasiliano**

Halmashauri ililipa jumla ya shilingi milioni 219.05 kwa wakandarasi kwa kazi za kuhamisha miundombinu ya maji na mawasiliano.

Nilibaini kuwa, kati ya kiasi kilicholipwa kupitia cheti Na. 7 cha mkataba Na. LGA/016/2018-2019/W/DMDP/05 (Package 10) Mkandarasi alilipwa shilingi milioni 67.65 kwa ajili ya kuhamisha miundombinu ya maji katika eneo la Barabara ya Msikitini, Kizinga na Baghdadi. Aidha, kupitia cheti Na. 4 cha mkataba Na. LGA/016/2018-2019/W/DMDP/04 (Package 9), Mkandarasi alilipwa jumla ya shilingi milioni 151.39 kwa ajili ya kuhamisha miundombinu ya mawasiliano mali ya Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania.

Kupitia uthibitisho wa barua zenye Kumb. Na.DAWASA/TMK/CAG/2021/01 ya tarehe 28 Aprili 2021 kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Kumb. Na. DF 4120/DG ya tarehe 5 Mei 2021 kutoka Kampuni ya Mawasiliano ya Simu Tanzania zilithibitisha kutokuwapo kwa mkataba kati yao na Halmashauri na kati yao na wakandarasi kwa ajili ya kazi hizo. Aidha, taasisi hizi zilithibitisha kutotekeleza kazi ya namna hiyo ndani ya Manispaa ya Temeke.

Ni wazi kuwa malipo ya jumla ya shilingi milioni 219.05 kwa wakandarasi hao yanaashiria kufanyika kwa njia ya ubadhirifu.

**Ninashauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI achukue hatua stahiki ili wakandarasi hao warejeshe jumla ya shilingi milioni 219.05 walizolipwa bila kufanya kazi.**

iv. **Kukosekana kwa Nyaraka za Malipo ya Kiasi cha Shilingi Bilioni 4.11 ya Kuhamisha Miundombinu ya Umeme**

Halmashauri ya Manispaa Temeke ilisaini mikataba na wakandarasi mbalimbali kwa ajili ya kazi ya miradi ya Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam ikijumuisha gharama za kuhamisha miundombinu ya umeme zenye jumla ya shilingi bilioni 4.11. Mikataba inaeleza kuwa, malipo ya gharama zilizotajwa za kuhamisha miundombinu

yangezingatia gharama halisi kama zitakavyowasilishwa na taasisi zinazohusika na miundombinu hiyo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hakukuwa na nyaraka za matumizi ya shilingi bilioni 4.11 ambazo zilihusu malipo ya uhamishaji wa miundombinu yaliyofanywa kwa wakandarasi kwa taasisi mbalimbali.

**Ninashauri Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kushirikiana na vyombo vya uchunguzi kuthibisha uhalali wa malipo ya shilingi bilioni 4.11, ikiwa pamoja na kuwachukulia hatua watumishi waliosababisha upotevu wa nyaraka za matumizi ya fedha za mradi.**

**(c) Ukaguzi Maalumu wa Mkopo kutoka CRDB kwa ajili ya Kulipa Fidia Ili Kupisha Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam**

**i. Ongezeko la Gharama za Mkopo Shilingi Bilioni 5.33 Kutokana na Makosa ya Ukokotoaji wa Deni**

Tarehe 18 Februari 2016, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ilisaini mkataba na CRDB wenye thamani ya shilingi bilioni 29.28 ukijumuisha msingi na riba. Mkopo huo utarejeshwa ndani ya miezi 72 baada ya miezi 6 ya matazamio tangu tarehe ya kusaini mkataba, kwa marejesho ya shilingi bilioni 1.22 kwa kila robo ya mwaka kwa awamu 24 na kumalizika 30 Septemba 2022.

Ukokotoaji mpya nilioufanya katika jedwali la urejeshaji wa mkopo katika kipengele Na. 7 cha mkataba nilibaini ukokotoaji wa deni na marejesho usio sahihi unaosababisha ziada ya shilingi bilioni 5.34. Ziada hiyo ni jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 2.17 na shilingi bilioni 3.16 inayotokana na makosa ya ukokotoaji wa kiasi cha msingi na riba mtawalia.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iwasiliane na vyombo vya uchunguzi juu ya ukokotoaji usio sahihi wa mkopo kiasi cha shilingi bilioni 5.33; na (b) ipitie upya mtiririko wa marejesho ya mkopo ili kupata kiasi kilicho sahihi.**

ii. **Malipo ya Fidia ya Shilingi Bilioni 2.16 kwa Watu Wasiotambuliwa na Viongozi wa Serikali za Mitaa**

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia kampuni ya uthamini, ilifanya uthamini wa maeneo kwa ajili ya fidia kwa ajili ya ujenzi wa miradi inayofadhiliwa kwa fedha za Benki ya Dunia. Kufikia tarehe 24 Aprili 2021, jumla ya shilingi bilioni 18.79 zilikuwa zimelipwa na Halmashauri. Nilibaini kuwa wakazi 94 waliolipwa jumla ya shilingi bilioni 2.16 hawakuwa wanatambulika na viongozi wa serikali za mitaa yao.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ifanye ufuatililaji zaidi juu ya uhalali wa malipo ya shilingi bilioni 2.16 kwa wakazi wasiotambulika.**

### 15.2.4 Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo

i. **Upotevu wa Shilingi Bilioni 4.64 Kutokana na Usimamizi Dhaifu wa Ukusanyaji wa Mapato**

Nilifanya ukaguzi maalumu wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo kwa miaka ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/2021 na kubaini mapungufu katika ukusanyaji wa mapato na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 4.64 kama ifuatavyo.

- Nilibaini kuwapo kwa maeneo ya wazi yenye ukubwa wa mita za mraba 69,020 yaliyokuwa yamevamiwa ambayo yengeweza kuiingizia Halmashauri kiasi cha shilingi bilioni 2.96 endapo yangekuwa yamepangishwa kwa kutoza shilingi 15,552 kwa mita moja ya mraba kama ilivyokuwa imeazimiwa kwenye kikao cha Kamati ya Fedha cha tarehe 12 Februari 2019.

- Katika zabuni Na. LGA/180/2018-2019/NCS/53 LOT 2 na LGA/180/2018-2019/NCS/53 LOT 1 ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada za choo katika Kituo cha Mabasi cha Simu 2000 na Soko la Mabibo, Halmashauri ilitunuku zabuni kwa mawakala walionukuu kiasi cha chini cha mapato shilingi milioni 131.96 na kuwaacha wa kiasi cha juu shilingi milioni 207

na kusababisha upotevu wa shilingi milioni 75.04 bila sababu za msingi.

- Nimebaini Halmashauri imepoteza mapato ya shilingi milioni 373.39 katika ushuru wa vibanda na vizimba vilivyopo katika masoko ya Halmashauri kutokana na kukusanya ushuru kwa kutumia viwango vya chini vya shilingi 500 kwa siku kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo Na. 226 ya tarehe 22 Machi 2019.

- Baada ya kugawanywa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni mnamo mwezi Julai 2016, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ilipata mgawo wa vyumba 7 vya kupangisha vilivyoko Oysterbay Villa, Mitaa ya Mawenzi na Ruvu. Nimebaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo haikuwahi kukusanya kodi ya pango katika vyumba hivyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu kuanzia mwaka 2017/18 hivyo kupoteza mapato ya shilingi milioni 720.

- Nimebaini kuwa Halmashauri inadai ushuru wa huduma kutoka kwa wafanyabiashara 38 wakubwa kati ya biashara 6,270 na kuikosesha Halmashauri mapato ya shilingi milioni 507.52 kinyume na Kifungu cha 6(1) (u) na 7(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019).

**ii. Hasara ya Shilingi Milioni 284.31 Iliyotokana na Kutokatwa kwa Asilimia 10 ya Kazi Zilizosalia Wakati wa Kusitisha Mkataba wa Ujenzi wa Jengo la Utawala**

Tarehe 23 Juni 2020, Halmashauri ilisitisha mkataba wa ujenzi wa jengo la utawala na mkandarasi kutokana na ukiukaji wa masharti ya mkataba uliofanywa na mkandarasi. Nimebaini Halmashauri haikumkata mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 384.31 ikiwa ni tozo ya asilimia 10 ya kazi zilizosalia zenye thamani ya shilingi bilioni 2.84 kinyume na Kipengele cha 68.1 cha Masharti Maalumu ya Mkataba namba LGA/180/2017-2018/W/11 wenye thamani ya shilingi bilioni 6.30.

**Ninapendekeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam (a) akishirikiana na mamlaka husika kuwachukulia hatua stahiki waliotajwa katika taarifa maalumu kwa kuisababishia Halmashauri hasara kutokana na kutofuata sheria na taratibu na vipengele vya mkataba; na (b) mawasiliano yafanyike na mkandarasi ili kuhakikisha kuwa shilingi milioni 284.31 zinarejeshwa kwa Halmashauri.**

### 15.2.5 Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni

Katika mwaka wa fedha 2020/21, nilifanya kaguzi maalumu mbili katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni, ambazo ni ukaguzi wa Mfumo wa Kukusanya Mapato (LGRCIS) na Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi (MOLIS); pamoja na ukaguzi wa mapato, miradi na madeni. Masuala ya msingi yaliyojitokeza katika kaguzi hizi ni kama ifuatavyo:

#### a) Ukaguzi Maalumu wa Mfumo wa Kukusanya Mapato na Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi

##### i. Hasara Kutokana Kughushi Risiti za Mapato Zenye Thamani ya Shilingi Milioni 264.75

Kupitia ukaguzi wa kiuchunguzi nilioufanya kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2017 hadi Julai 2020, nilibaini udanganyifu katika risiti 825 zenye thamani ya shilingi milioni 264.75. Kati ya hizo, ni risiti 92 tu zenye thamani ya shilingi milioni 59.77 ndizo zilithibitishwa kuwapo kwake, na risiti 733 zenye thamani ya shilingi milioni 204.98 zilizotokana na utoaji wa vibali vya ujenzi, ambazo taarifa zake zilitokana na Muhtasari wa Kamati ya Vibali vya Ujenzi.

Ulinganifu wa taarifa za risiti halisi 825 na taarifa za risiti hizo katika Mfumo wa Makusanyo ya Mapato, na Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi ulibaini utofauti wa taarifa zinazohusiana na majina ya walipaji, anwani, kiasi cha fedha kilicholipwa na aina ya huduma iliyolipiwa.

Utofauti wa taarifa za risiti 825 ulisababishwa na mfumo kuwa na uwezekano wa kupakua risiti, kulikosababisha watumishi wasio waaminifu kutumia nafasi hiyo kupakua risiti, kuweka katika

kompyuta katika mfumo wa "excel and pdf", kisha kuzihariri ili kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, na kuisababishia Serikali hasara ya shilingi milioni 264.75.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) idhibiti matumizi ya Mfumo wa Makusanyo ya Mapato yanayoruhusu mtumiaji wa Mfumo kupakua risiti katika muundo unaoweza kuhaririwa ili kuepuka matumizi mabaya kwa wafanyakazi wasio waaminifu; (b) Ofisi ya Rais - TAMISEMI inashauriwa pia kuhakikisha matumizi kamili ya mfumo wa Mfumo wa Usimamizi wa Ardhi katika huduma zote zinazohusiana na ardhi; na (c) ihakikishe hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya watumishi wa Halmashauri waliohusika katika kutoa risiti za kughushi na kusababisha hasara ya shilingi milioni 264.75.**

**b) Ukaguzi Maalumu wa Mapato, Miradi na Madeni**

**ii. Hasara ya Shilingi Milioni 229.84 Iliyosababishwa na Uuzaji wa Viwanja Chini ya Bei Iliyopitishwa na Kamati ya Ugawaji Ardhi**

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kupitia kikao cha kamati ya kugawa ardhi iliridhia viwanja katika eneo la Gezaulole kuuzwa mita moja ya mraba kwa bei ya kati ya shilingi 1,000 na shilingi 10,000. Nilibaini viwanja sitini na tisa (69) vyenye jumla ya shilingi milioni 229.84 vilivyo katika maeneo yaliyoainishwa hapo juu viliuzwa kwa bei ya ulinganifu ya shilingi 1,000 kwa mita ya mraba kinyume na bei elekezi na kusababisha hasara ya shilingi milioni 229.84.

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza upotevu wa shilingi milioni 229.84 na ubadhirifu wa shilingi milioni 63.16 za mapato ya ndani na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika.**

**iii. Ubadhirifu wa Mapato Kiasi cha Shilingi Milioni 63.16 Yaliyoingizwa Katika Mfumo wa Makusanyo ya Mapato Kupitia Dirisha la Nyuma la Mfumo**

Nilibaini ubadhirifu wa jumla ya shilingi milioni 63.16 za mapato ya Halmashauri katika miaka mitatu ya fedha kuanzia 2018/19 hadi

2020/21 uliofanywa na watumishi wasio waaminifu kupitia dirisha la nyuma la mfumo wa mapato, kwa kuhariri taarifa za mapato, kasma, chanzo, namba ya malipo na kiasi cha malipo katika stakabadhi. Kati ya kiasi hicho, shilingi milioni 61.98 kilitokana na mauzo ya viwanja na utoaji wa vibali vya ujenzi kilichoingizwa katika Mfumo kwa stakabadhi za kughushi; na shilingi milioni 1.18 kilitokana na mapato mbalimbali kilichoingizwa katika Mfumo kwa kukatiwa stakabadhi halali bila kuwasilishwa benki.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza ubadhirifu wa shilingi milioni 63.16 na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika waliosababisha hasara hiyo.**

### 15.2.6 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni

#### i. Hasara ya Shilingi Milioni 196.65 Kutokana na Udanganyifu wa Nyaraka za Magari ya Uzoaji Taka

Wakati wa ukaguzi maalumu wa uzoaji taka, nilibaini kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ililipa jumla ya shilingi milioni 196.65 ikiwa ni gharama ya uwakala wa uzoaji taka kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha kuanzia 2018/2019 hadi 2020/2021. Nilibaini nyaraka za magari zilizowasilishwa ni za magari madogo ambayo hayana uwezo wa kubeba taka.

Aidha, nilibaini kuwa magari yaliyotumika kuzoa taka katika masoko ya Magomeni, Tandale na Tegeta Nyuki ni magari yenye usajili wa Serikali za Mitaa (SM) na si magari yenye usajili binafsi kama nyaraka za malipo zilivyoonesha.

Malipo ya madai yasiyo na nyaraka za kutosha yanaweza kusababisha matumizi yasiyo na tija na Halmashauri.

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza uhalali wa malipo yaliyofanywa kwa wakala wa uzoaji taka yenye jumla ya shilingi milioni 196.65 kutokana na kughushi nyaraka za magari.**

ii. **Malipo ya Shilingi Milioni 278.7 kwa Wakala wa Kuzoa Taka Pasipo Uthibitisho wa Kiwango cha Taka Zilizokusanywa**

Halmashauri ilimlipa wakala wa uzoaji taka jumla ya shilingi milioni 278.78 bila kuwapo kumbukumbu za uthibitisho wa umwagaji taka katika Dampo la Pugu Kinyamwezi, hali inayoashiria kutokuwapo udhibiti katika usimamizi wa matumizi na kusababisha malipo yasiyo halali kiasi cha shilingi milioni 278.78.

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza uhalali wa malipo ya jumla ya shilingi milioni 278.7 yaliyofanywa kwa wakala wa uzoaji taka bila kuwapo uthibitisho wa kazi zilizofanyika.**

### 15.2.7 Halmashauri ya Mji Masasi

i. **Mkandarasi Kutorejesha Malipo ya Awali ya Shilingi Milioni 172.35**

Nilibaini kuwa tarehe 24 Juni 2019 Halmashauri iliingia mkataba Na. LGA/135/2018/2019/W/NCT/02 na mkandarasi wenye thamani ya shilingi bilioni 1.15 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili.

Tarehe 26 Juni 2019 kupitia hati ya malipo Na. 802031V1902335, mkandarasi alilipwa asilimia 15 ya thamani ya mkataba sawa na shilingi milioni 172.35 ikiwa ni gharama ya malipo ya awali.

Hadi kufikia tarehe 10 Februari 2021, nimebaini mkandarasi alikuwa ameshalipwa asilimia 72 ya thamani ya mkataba bila kukatwa marejesho ya malipo ya awali kinyume na sharti la 24 ya masharti maalumu ya mkataba kinachohitaji malipo ya awali kurejeshwa kwa kukata asilimia 25 ya kiasi cha kila cheti cha madai ya mkandarasi, baada ya mkandarasi kufikisha malipo ya asilimia 20 ya kiasi cha mkataba.

**Ninashauri hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maofisa wote waliohusika kufanya malipo ya kazi ambazo hazijatekelezwa na**

**kushindwa kukata kiasi hicho kutoka katika malipo ya awali ya asilimia 5 kutoka kwa vyeti vya malipo vya mkandarasi.**

**ii. Fedha Shilingi Milioni 146.18 za Matazamio ya Mradi Kutumika kwa Shughuli Zisizokusudiwa**

Halmashauri ya Mji Masasi ilisaini mkataba Na. LGA/135/2015/2016/W/01 na mkataba Na. LGA/135/2018/2019/W/NCT/02 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri katika mwaka wa fedha 2015/16.

Nimebaini kuwa kwa vipindi tofauti jumla ya shilingi milioni 146.18 zilikatwa kama fedha za matazamio kutoka katika malipo ya wakandarasi na kuhifadhiwa katka akaunti ya amana. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 128.37 zilitokana na malipo ya mkandarasi mwenye mkataba Na. LGA/135/2015/2016/W/01, na shilingi milioni 17.81 zilitokana na mkandarasi mwenye mkataba LGA/135/2018/2019/W/NCT/02.

Hata hivyo, nimebaini kuwa kiasi hicho kimetumika kwa shughuli zisizokusudiwa hali inayoweza kusababisha Halmashauri kushindwa kulipa wakandarasi hao fedha zao muda wa matazamio utakapomalizika na kusababisha Halmashauri kushitakiwa.

**Ninapendekeza kuwa Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara kwa kushirikiana na mamlaka zinazohusika kuhakikisha kuwa Halmashauri inarejesha kiasi cha shilingi milioni 146.18 kilichotumika kwa shughuli zisizotarajiwa ikiwa pamoja na kuchukua hatua stahiki kwa waliohusika na uchepushaji wa fedha za muda wa matazamio.**

**iii. Malipo ya Shilingi Milioni 105.99 kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika**

Nimebaini kuwa Halmashauri kupitia cheti cha malipo Na. 3 ilimlipa mkandarasi mwenye mkataba LGA/135/2018/2019/W/NCT/02 jumla ya shilingi milioni 105.99 kwa ajili ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri kwa kazi ambazo hazikufanyika.

Malipo hayo yanajumuisha kiasi cha shilingi milioni 17.02 kilicholipwa zaidi ya kazi halisi zilizofanyika na kiasi cha shilingi milioni 88.97 kilicholipwa kwa mkandarasi kwa mkupuo kama malipo ya halisi na fedha za dharura bila kuainisha kazi zilizofanyika kwenye cheti cha malipo kinyume na Kifungu cha 45.2 cha Masharti ya Jumla ya mkataba kinachotaka mkandarasi kulipwa kulingana na kiasi cha kazi zilizofanyika kwa bei iliyoainishwa katika hati ya makadirio ya gharama za ujenzi.

**Ninapendekeza kuwa, menejimenti ya Halmashauri ihakikishe kuwa hatua stahiki zinachukuliwa ili kurejesha malipo ya awali ya shilingi milioni 278.34 kutoka kwa wakandarasi kwa malipo ya kazi ambazo hazijatekelezwa.**

### 15.2.8 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa

#### i. Kukosekana kwa Nyaraka za Matumizi ya Shilingi Milioni 400 Katika Ujenzi wa Kituo cha Afya Kibakwe

Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilipokea jumla ya shilingi milioni 400 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kibakwe. Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha matumizi ya fedha hizo kutokana na kutopatiwa nyaraka licha ya kuziomba kwa barua yenye Kumb. Na.NAO/SA/MPD/2021/50 ya tarehe 23 Juni 2021.

Kutowasilishwa kwa nyaraka za matumizi kumenizuia kuthibitisha uhalali wa malipo yanayohusiana na ujenzi huo, hivyo kuashiria kuwapo kwa matumizi mabaya ya fedha hizo.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza uhalali wa shilingi milioni 400 zilizolipwa kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kibakwe ili kubaini iwapo fedha hizo zilitumika kwa malengo yaliyokusudiwa.**

ii. **Hasara ya Shilingi Milioni 150.03 Kutokana na Wakandarasi/Mafundi Kulipwa Zaidi ya Kazi Walizofanya**

Kwa mujibu wa Kipengele cha 39.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba, mkandarasi hulipwa kulingana na ukubwa wa kazi iliyofanyika kwa kiwango kilichokubaliwa katika hati ya makadirio ya gharama za ujenzi kwa kila kazi. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa ililipa wakandarasi bila kupima ukubwa wa kazi na kusababisha kulipa shilingi milioni 150.03 zaidi ya kiasi kilichostahili.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ishirikiane na uongozi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa kiasi cha shilingi milioni 150.03 kinarejeshwa kutoka wa wakandarasi/mafundi waliolipwa zaidi ya kazi walizofanya ili fedha hizo zitumike kutekeleza shughuli zingine zilizopangwa.**

### 15.2.9 Halmashauri ya Mji wa Geita

i. **Hasara ya Shilingi Bilioni 1.70 Kutokana na Kuvunjwa kwa Mkataba**

Wakati wa ukaguzi maalumu wa Machinjio ya Kisasa Mpomvu nilibaini kuwa tarehe 14 Machi 2017, Halmashauri ya Mji Geita iliingia mkataba Na. Na.LGA/160/ULGSP/W/2016/2017/01 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.71 uliotakiwa kukamilika tarehe 11 Disemba 2018.

Mkataba huo ulivunjwa tarehe 22 Februari 2019, kisha Halmashauri kusaini mkataba mwingine wenye Na. LGA/160/2019-2020/HQ/ULGSP/06 wa tarehe 20 Januari 2020 na kusababisha hasara ya shilingi bilioni 1.70. Hasara hiyo inatokana na malipo ya mhandisi mshauri kwa ajili ya mkataba wa pili wa shilingi milioni 150.72; shilingi milioni 80.95 za gharama za awali ambazo zilikwishalipwa kwa mkandarasi wa kwanza; shilingi bilioni 1.40 za gharama zilizoongezeka kwa kuingia mkataba mpya; pamoja na shilingi milioni 75.83 za gharama za uendeshaji wa shauri baina ya Halmashauri na mkandarasi aliyevunjiwa mkataba.

Mapungufu haya yanaweza kusababishwa na wanasheria wa Halmashauri kushindwa kusimamia kikamilifu mikataba.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kufanya uchunguzi juu ya hasara ya shilingi bilioni 1.70 iliyopatikana baada ya Halmashauri kuvunja mkataba na kuona iwapo kiasi hicho cha fedha kilistahili kulipwa kwa mkandarasi aliyepewa mkataba huo.**

**ii. Malipo Mara Mbili ya Kiasi cha Shilingi Milioni 44.14 kwa Kazi ya Utafiti wa Udongo**

Katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa, nilibaini Halmashauri ya Mji Geita ilifanya malipo yenye jumla ya shilingi milioni 44.14 ikiwa ni gharama ya utafiti wa udongo. Gharama hizo zililipwa kwa mkandarasi mshauri ambaye alifanya kazi ya utafiti wa kitopografia kwa gharama ya shilingi milioni 21.4 na mkandarasi aliyefanya kazi ya utafiti wa udongo kwa gharama ya shilingi milioni 22.74 .

**Ninashauri kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ahakikishe mkandarasi mwelekezi anarejesha shilingi milioni 44.14 zilizolipwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli za upimaji wa ardhi ambazo hazikufanyika.**

### 15.2.10 Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa

**i. Shilingi Milioni 281.87 Zilizolipwa Mara Mbili kwa Kazi ya Ujenzi wa Jengo la Utawala**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa iliingia mkataba Na. LGA/137/2016-2017SS/ADM/BLOCK/W/01 wenye thamani ya shilingi milioni 717.21 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala awamu ya kwanza ambao ulipaswa kutekelezwa kuanzia tarehe 5 Mei 2017 hadi 5 Septemba 2017. Halmashauri ilivunja mkataba kwa barua yenye Kumb. Na.CE.3/992/03/37 ya tarehe 4 Julai 2018, na kuingia mkataba mwingine wenye namba LGA/137/2017/2018/ADM BLOCK/W/04 wenye thamani ya shilingi bilioni 1.44 na mkandarasi mwingine kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la utawala awamu ya kwanza.

Nilibaini kuwa kazi zenye thamani ya shilingi milioni 281.87 zilizotekelezwa na kulipwa kwa mkandarasi wa kwanza zilijumuishwa na kulipwa tena kwa mkandarasi mwingine.

**Mamlaka husika ichukue hatua stahiki kwa watumishi wote waliotajwa katika ripoti ya ukaguzi maalumu waliohusika kuidhinisha na kulipa shilingi bilioni 281.87 kwa kazi iliyokwishalipwa.**

**ii. Kutorejeshwa Kwa Malipo ya Awali ya Shilingi Milioni 62.41 Kutoka kwa Mkandarasi**

Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa ilimlipa mkandarasi malipo ya awali ya jumla ya shilingi milioni 156.02 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na ukumbi, ambapo kiasi cha shilingi milioni 93.61 zilikatwa katika vyeti vya malipo na kubaki kiasi cha shilingi milioni 62.41 ambazo zilikuwa ziendelee kukatwa katika malipo yanayofuata.

Hata hivyo, tarehe 6 Disemba 2020 Halmashauri ilivunja mkataba na mkandarasi kuondoka eneo la mradi bila kurejeshwa kwa kiasi kilichosalia cha shilingi milioni 62.41.

**Mamlaka husika iwachukulie hatua stahiki waliotajwa katika taarifa maalumu kwa kufanya malipo ya shilingi milioni 281.87 mara mbili kwa kazi moja.Vilevile, menejimenti ya Halmashauri inashauriwa kuhakikisha mkandarasi wa pili anarejesha fedha kiasi cha shilingi milioni 62.41 zilizosalia katika fedha za malipo ya awali katika ujenzi wa jengo la utawala.**

### 15.2.11 Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo

**i. Wadaiwa wa POS Kiasi cha Shilingi Milioni 44.57 Waliosajiliwa kwa Majina ya Uongo**

Nimebaini POS 9 zenye madeni ya kiasi cha shilingi milioni 44.57 zilisajiliwa kwa majina yasiyo halisi, hivyo kuwa ngumu kutambua uhalali wa ukusanyaji wa mapato hayo ambayo hayakupelekwa benki.

Hali hii ni kinyume na Mwongozo wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI uliotolewa kwa barua yenye Kumb. Na.EB.151/297/01/79 ya tarehe 6 Oktoba 2017 ukielekezea kuwa kila POS isajiliwe na kujulikana kwa jina la mtumiaji, kituo anapofanyia kazi na mawasiliano kwa ajili ya ufuatiliaji.

Ukiukaji huu wa mwongozo umechangiwa na udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa mapato na kusababisha hasara ya shilingi milioni 44.57.

**Ninapendekeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI awasiliane na TAKUKURU ili kufanya uchunguzi kuhusiana na wakusanyaji mapato wenye POS zilizo na majina na anuani feki.**

### 15.2.12 Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

#### i. Malipo ya Shilingi Milioni 231.17 kwa Vifaa Ambavyo Havikupokelewa

Tarehe 27 Februari 2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala awamu ya pili. Nilibaini kuwa Halmashauri ilifanya malipo ya shilingi milioni 231.17 kwa wazabuni mbalimbali kwa ajili ya kununua vifaa vya ujenzi ambapo hadi tarehe 30 Juni 2021, vifaa hivyo havikuwa vimepokelewa katika eneo la mradi.

Hali hii ni kinyume na Kanuni Na. 242 na 248 za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 inayotaka bidhaa kukaguliwa na kukubalika kabla ya kupokelewa. Malipo kufanyika kwa vifaa ambavyo havijapokelewa kunatokana na udhibiti hafifu wa manunuzi.

**Uongozi wa Halmashauri unashauriwa kuhakikisha kuwa shilingi milioni 231.17 zilizolipwa kwa ajili ya vifaa vya ujenzi ambavyo havijawasilishwa zinarejeshwa kutoka kwa wazabuni husika.**

ii. **Malipo Zaidi ya Gharama Halisi ya Bima Yaliyosababisha Hasara ya Shilingi Bilioni 160.96**

Tarehe 31 Mei 2019 Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko iliingia mkataba namba LGA/139/HQ/2018-2019/W/02 kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kakonko kwa thamani ya shilingi bilioni 2.15. Muda wa mkataba ulikuwa kuanzia tarehe 14 Juni 2019 hadi 14 Juni 2020 na hadi kufikia 30 Juni 2021.

Nimebaini kuwa Halmashauri kupitia hati ya malipo namba 743110V2001023 ya tarehe 14 Februari 2020 Halmashauri ilimlipa mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 239.24 ikiwa ni malipo ya cheti namba 1 cha mkataba huo. Miongoni mwa kiasi hicho shilingi milioni 165.26 kilikuwa ni gharama za mkandarasi kwa ajili ya kutafuta dhamana ya kazi.

Hata hivyo, gharama halisi alizotumia kuipata dhamana ya utendaji kazi zilikuwa shilingi milioni 4.29 hivyo kusababisha hasara ya kiasi cha shilingi milioni 160.96 kwa kumlipa mkandarasi gharama ambazo hakuzitumia.

**Ninashauri menejimenti ya Halmashauri kuhakikisha mkandarasi anarejesha kiasi cha shilingi milioni 160.96 alicholipwa isivyostahili.**

### 15.2.13 Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea

i. **Uwekezaji Usio na Faida wa Shilingi Milioni 209.91 Katika Kituo cha Redio na Ujenzi wa Vibanda Katika Kituo cha Mabasi Nachingwea**

Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea iliingia mikataba ya ujenzi wa majengo ya maduka na ofisi za kukatia tiketi yenye vyumba 12 katika kituo kipya cha mabasi; na ununuzi na ufungaji wa vifaa vya kituo cha redio kwa gharama ya kiasi cha shilingi milioni 209.91.

Hata hivyo, nilipotembelea eneo la mradi wa kituo kipya cha mabasi na kituo cha redio Nachingwea nilibaini vyumba 12 kutokuwa na wapangaji kwa muda mrefu tangu kukamilika. Aidha, vyumba 26

vilivyofikia hatua ya boma vimesimama na vibanda hivi kukosa wapangaji wa kuvikamilisha. Pia, nimebaini kuwa kituo cha redio kimesajiliwa kama redio ya kijamii ambapo lengo kuu ni kutoa huduma kwa jamii na si kupata faida. Hali hii imeipa mzigo mkubwa Halmashauri wa kuihudumia kutokana na mradi huu kutegemea kuendeshwa kwa kutumia mapato ya vyanzo vingine vya ndani.

Hali hii imechangiwa na kutofanya upembuzi yakinifu na kuandaa mpango wa kibiashara kabla ya kuanza kutekeleza miradi.

**Menejimenti ya Halmashauri inashauriwa (a) iboreshe mazingira ya biashara katika kituo kipya cha mabasi ili kuvutia wafanyabiashara; na (b) ikigeuze Kituo cha Radio Nachingwea kuwa redio ya kibiashara ili iweze kufanya kazi bila kutegemea ruzuku ya Halmashauri.**

**ii. Upotevu wa Mapato ya Kiasi cha Shilingi Milioni 69.91 Yatakonayo na Ushuru wa Huduma**

Nilifanya ulinganifu wa taarifa za mauzo ya madini kutoka Tume ya Madini na Mamlaka ya Mapato Wilaya ya Nachingwea mtawalia kwa kipindi cha miaka ya fedha mitatu kuanzia 2018/19 hadi 2020/2021 na nilibaini kuwa kampuni au biashara 103 zilizofanya shughuli zake katika Halmashauri zilitoa ushuru pungufu wa huduma kwa kiasi cha shilingi milioni 69.91 kinyume na Kifungu cha 6(1) (u) na 7(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019).

**Menejimenti ya Halmashauri inapaswa kufanya jitihada za kurejesha shilingi milioni 69.91 kutoka kwa kampuni au biashara ambazo zililipa ushuru wa huduma pungufu.**

### 15.2.14 Halmashauri ya Mji wa Babati

**i. Malipo ya Fidia ya Shilingi Milioni 367.81 ya Viwanja kwa Wanufaika Ambao Hawakuthibitika**

Mapitio yangu ya orodha ya wadai kwa miaka mitatu ya fedha kuanzia 2018/19 hadi 2020/21 yamebaini kuwa Halmashauri ililipa

shilingi milioni 367.81 kwa ajili ya fidia ya ardhi kwa wanufaika ambao hawakuwamo katika orodha ya waliofanyiwa tathmini.

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI inashauriwa kuwasiliana na TAKUKURU ili kuchunguza uhalali wa fedha za fidia zenye jumla ya shilingi milioni 367.81 kwa wanufaika ambao hawakutambuliwa awali.**

**ii. Fedha Shilingi Milioni 167.43 za Mauzo ya Viwanja Zilizowekwa katika Akaunti Binafsi za Watumishi**

Nimebaini viwanja vyenye thamani ya shilingi milioni 167.43 viliuzwa kwa wanunuzi 58 na malipo yake kufanyika katika akaunti binafsi za watumishi wa Halmashauri. Hadi ninakamilisha ukaguzi wangu, hapakuwa na uthibitisho wa fedha hizo kuhamishiwa katika akaunti ya Halmashauri.

**Ofisi ya Rais - TAMISEMI inashauriwa kuwasiliana na TAKUKURU ili ichunguze uhalali wa mapato ya shilingi milioni 167.43 zilizowekwa katika akaunti za binafsi za watumishi.**

### 15.2.15 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda

**i. Kukosekana kwa Nyaraka za Shilingi Milioni 255.85 za Mchakato wa Ununuzi ili Kuwapata Mafundi wa Ujenzi**

Katika ukaguzi maalumu nilishindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi ya shilingi milioni 255.85 kutokana na kutowasilishwa kwa nyaraka za mchakato wa upatikanaji wa mafundi wa ujenzi wa miradi ya Vituo vya Afya vya Kisorya na Kasahunga na Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya awamu ya kwanza.

Hali hii ni kinyume na Aya ya 7 ya Mwongozo wa TAMISEMI wa matumizi ya nguvukazi wa tarehe 21 Septemba 2017 na wenye Kumb. Na. AD. 296/303/01/I/82 uliotoa maelekezo ya matumizi ya nguvukazi katika ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya.

Kukosekana kwa nyaraka za zabuni kuliathiri mawanda ya ukaguzi wangu.

**Menejimenti ya Halmashauri ifanye jitihada za makusudi ili nyaraka zinazohusiana na miradi ya ujenzi wa vituo vya afya na hospitali ya wilaya zenye thamani ya shilingi milioni 255.85 zipatikane na kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki.**

### 15.2.16 Halmashauri ya Mji Chunya

**i. Hasara ya Shilingi Milioni 281.14 ya Ushuru Wa Huduma Kutokana Na Mauzo ya Madini**

Nilifanya ulinganifu wa taarifa za mauzo ya madini kutoka Tume ya Madini na taarifa za ushuru wa huduma zilizotolewa na Halmashauri kwa kipindi cha miaka ya fedha mitatu kuanzia 2018/19 hadi tarehe 30 Mei 2021 zilizoonyesha ushuru wa huduma wa madini usiokusanywa kiasi cha shilingi milioni 281.14.

Hali hii ni kinyume na Kifungu Na. 4(2) cha Sheria Ndogo (Ushuru wa Huduma) ya Halmashauri ya Mji Chunya ya Mwaka 2019 iliyotungwa chini Kifungu cha 6(1) (u) na 7(1) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (iliyorekebishwa mwaka 2019).

Kutokusanywa kwa mapato ya Halmashauri kunaathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa kwa miaka husika.

**ii. Hasara ya Shilingi Milioni 328.56 Iliyosababishwa na Zabuni Kupewa Mkandarasi Mwenye Gharama Kubwa**

Wakati wa kukagua mchakato wa kumpata mzabuni kwa zabuni Na. LGA/075/W/BLD/2016-2017/01 ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri nimebaini kwamba, Halmashauri ilimuacha mkandarasi aliyekuwa na bei ya chini ambaye aliomba zabuni kwa bei ya chini ya shilingi bilioni 1.86 na kumchukua mkandarasi aliyeshinda kwa bei ya shilingi bilioni 2.194 na kusababisha ziada ya shilingi milioni 328.56.

Kuachwa kwa mzabuni mwenye bei ya chini kwa vigezo ambavyo havikuainishwa katika nyaraka za zabuni kumeisababishia Halmashauri ya Wilaya ya Chunya hasara ya shilingi milioni 328.56.

**Ninapendekeza menejimenti ya Halmashauri iwachukulie hatua stahiki watendaji wote waliohusika kutoa zabuni kwa mzabuni mwenye bei ya juu.**

### 15.2.17 Halmashauri ya Mji Ifakara

#### i. Hasara ya Shilingi Milioni 172.58 Iliyotokana na Uzembe na Uwezo Mdogo wa Mkandarasi

Mapitio ya matokeo ya uchunguzi wa udongo wa eneo la mradi wa jengo la utawala la Halmashauri yalibaini kuwa jamvi la msingi lilojengwa lisingeweza kuhimili uzito wa jengo kutokana na aina ya udongo uliopo eneo la mradi. Kutokana na matokeo hayo, iliamuliwa ujengwe msingi mwingine wa zege na kufukia msingi wa awali hivyo kuisababishia Serikali kupoteza shilingi milioni 172.58.

Aidha, nilibaini kuwa maboksi ya zege yaliyofungwa kabla ya ujenzi kusimama kuanzia tarehe 20 Oktoba 2018 hadi 9 July 2019 kutokana na zoezi la kupima udongo hayataweza kutumika tena kwa kazi iliyokusudiwa kwa kuwa yameharibika na kukauka baada ya kunyeshewa mvua na kupigwa jua.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na menejimenti ya Wakala wa Majengo Tanzania ili kuhakikisha kuwa shilingi milioni 172.58 zilizolipwa zaidi zinarejeshwa.**

#### ii. Malipo ya Shilingi Milioni 221.04 Zaidi ya Kazi Zilizofanyika

Ukaguzi wangu wa vyeti vya malipo ya muda pamoja na taarifa za vipimo vya kazi zilizofanyika katika eneo la mradi wa jengo la utawala la Halmashauri ulibaini kuwa katika vyeti vya malipo namba 2 na 3, Wakala wa Majengo Tanzania ililipwa shilingi bilioni 221.04 zaidi ya kazi halisi iliyotekelezwa kinyume na Kanuni ya 243 (2) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013.

**Katibu Mkuu, ofisi ya Rais – TAMISEMI ahakikishe menejimenti ya Halmashauri inarejesha shilingi milioni 221.04 kutoka katika vyeti vya malipo ya wakandarasi yanayofuata na kuhakikisha kuwa mkandarasi anarejea katika kazi kwa muda uliokubaliwa.**

### 15.2.18 Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela

**i. Hasara ya Mapato ya Shilingi Milioni 40.40 Yaliyokusanywa Bila Kutumia POS**

Halmashauri ilimtumia wakala mmoja wa mapato ambaye alitumia vifaa vingine kukusanya mapato badala ya kutumia mashine za POS zilizotolewa na Halmashauri hivyo kusababisha hasara ya shilingi milioni 40.40 ambazo hazikuwekwa benki.

Hali hii ni kinyume na Aya ya 6 ya barua ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye Kumb. Na.EB.110/ 156/01/26 ya tarehe 11 Julai 2016 inayotaka mamlaka za serikali za mitaa kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia njia ya kielekitroniki na kuwasilisha mapato benki. Hali hii imetokana na udhaifu wa mifumo ya udhibiti wa ndani katika usimamizi wa mawakala wa kukusanya mapato.

**Ninapendekeza Katibu Tawala wa Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na Halmashauri na mamlaka husika kuchukua hatua stahiki kurejesha shilingi milioni 40.40 kutoka kwa wakala wa ukusanyaji wa upakiaji na upakuaji.**

**ii. Malipo ya Shilingi Milioni 161.27 kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika**

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Halmashauri iliwalipa baadhi ya wakandarasi shilingi milioni 161.27 kwa kwa kazi ambazo hazikufanyika. Kati ya fedha zilizolipwa, shilingi milioni 22.51 zililipwa kwa mkandarasi wa maegesho ya malori eneo la Nyamhongolo kupitia mkataba Na. LGA/1592/018/2019/W/2 wa tarehe 17 Julai 2019 na shilingi milioni 138.76 zililipwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala kupitia mkataba Na. LGA/159/2017/2018/W/03 wa tarehe 26 Machi 2018.

Menejimenti ya Halmashauri kutokuwa makini katika usimamizi kumeisababishia Serikali hasara ya shilingi milioni 161.27.

**Ninapendekeza Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na menejimenti ya Halmashauri ahakikishe**

**mkandarasi anarejesha fedha kiasi cha shilingi milioni 161.27 ambazo amelipwa kwa kazi ambazo hakuzifanya.**

### 15.2.19 Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa

#### i. Utengenezaji wa Boti Usio na Tija Uliosababisha Hasara ya Shilingi Milioni 20.84

Tarehe 24 Agosti 2018 Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ilipokea shilingi milioni 200 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya utengenezaji wa boti ya kutoa huduma katika kata zote zilizopo katika mwambao wa Ziwa Nyasa.

Tarehe 13 Machi 2019 Halmashauri ilisaini mkataba Na. LGA/030/2018-2019/G/01 wenye thamani shilingi milioni 169.92 kwa ajili ya kuunda boti katika kipindi cha miezi mitatu.

Nibaini kuwa tarehe 27 Agosti 2019 mkandarasi alikabidhi boti kwa Halmashauri na tarehe 2 Desemba 2019 lilirudishwa tena kwa mkandarasi kwa ajili ya matengenezo, na hadi ninakamilisha ukaguzi wangu mwezi Juni 2021, mkandarasi alishalipwa jumla ya shilingi milioni 101.95 na boti hiyo ilikuwa haijarejeshwa katika mamlaka ya Halmashauri ikiwa ni zaidi ya mwaka mmoja tangu irejeshwe kwa mkandarasi kwa ajili ya matengenezo.

Pia, nilibaini kuwa katika kipindi hicho cha kuanzia tarehe 2 Desemba hadi Juni 2021, kiasi cha shilingi milioni 20.84 zilitumika kukodi boti, jambo ambalo lingeweza kuepukika iwapo boti ya Halmashauri ingefanya kazi.

Hali hii imesababisha matumizi yasiyo na tija ya shilingi milioni 169.92 kama tozo za kukodi kutokana na boti kutofanya kazi.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inamfuatilia kwa karibu mkandarasi ili kuhakikisha boti inarudishwa kwa Halmashauri.**

### 15.2.20 Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo

**i. Hasara ya Shilingi Milioni 91.22 Iliyosababishwa na Kumuacha Mzabuni Mwenye Gharama Ndogo**

Ukaguzi wangu wa mchakato wa ununuzi wa kazi za mfumo wa umeme na TEHAMA kuhusiana na ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ulibaini kuwa Baraza liliidhinisha mkandarasi mwenye bei ya zabuni ya shilingi milioni 907.41 na kumuacha aliyenukuu shilingi milioni 816.20 kinyume na Kifungu cha 72 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011, Kanuni ya 203 (2), na Kanuni ya 76 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (zilizorekebishwa mwaka 2016).

Hali hii imeisababishia Halmashauri hasara ya shilingi milioni 91.22.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI na menejimenti ya Halmashauri kuhakikisha kuwa hatua stahiki zinachukuliwa kwa wale wote waliohusika katika mchakato wa ununuzi kuanzia hatua ya tathmini hadi kutoa zabuni.**

### 15.2.21 Halmashauri ya Mji Bariadi

**i. Hasara ya Shilingi Milioni 112.05 Kutokana na Kuondolewa kwa Mzabuni Bila Sababu**

Halmashauri ya Mji Bariadi iliingia mkataba Na. LGA/158/2018/2019/HQ/C/01 wa tarehe 20 Mei 2019 kwa ajili ya usimamizi wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya malori kwa thamani ya shilingi milioni 496.80.

Kinyume na Kanuni za 203 (2) na 17 (2-4) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013, nilibaini mkandarasi aliyekuwa na bei ya chini ya shilingi milioni 384.75 aliondolewa bila sababu za msingi kwa kupewa alama ndogo katika vipengele vya watendaji, uelewa wa hadidu za rejea, na viwango vya utendaji ikilinganishwa na alama alizopewa mzabuni aliyekuwa na bei ya shilingi milioni 522.80 na baadaye kupunguzwa hadi shilingi milioni 496.80.

Hata hivyo, vigezo hivi vya tathmini havikuweza kuthibitishwa katika ripoti ya tathmini iliyowasilishwa kwa ajili ya mapitio yangu na hapakuwa na maelezo dhidi ya alama alizopewa mzabuni aliyekataliwa kinyume na Kipengele vya 11.3 na 19.4 vya Mwongozo wa Tathmini ya Zabuni wa Mwaka 2014 uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, ambao unawataka wajumbe wa kamati ya tathmini kutoa maoni yao dhidi ya alama walizotoa kwa kila mzabuni.

Kutozingatia sheria kumeisababishia Halmashauri kukosa nafasi ya kuokoa shilingi milioni 112.05.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichukue hatua stahiki kwa wale wote waliohusika katika kuondolewa kwa mzabuni wa chini kabisa bila sababu za msingi na kusababisha hasara ya shilingi milioni 112.05.**

**ii. Hasara ya Shilingi Milioni 116.89 Kutokana na Malipo ya Fidia ya Umeme Ambayo Hayakustahili**

Halmashauri ya Mji Bariadi ilifanya malipo ya jumla ya shilingi milioni 116.89 ikiwa ni fidia ya eneo lililokuwa limepitiwa na njia ya umeme mkubwa kwa viwanja vya wananchi 7 wa eneo la Sesele I na Sesele II. Nilibaini mnamo tarehe 4 Februari 2019 Shirika la Umeme Tanzania kupitia barua yenye Kumb.Na.RM/SMY/MVL/1 ilimjulisha ofisa masuuli wa Halmashauri kwamba ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa 33KV umelenga kuwapatia wananchi wa Bariadi huduma ya umeme hivyo waruhusu ujenzi wa njia hiyo uendelee.

Aidha, Shirika la Umeme Tanzania Mkoa wa Simiyu lilinithibitishia kwa barua yenye Kumb.Na.RM/SMY/GC/24/2021 ya tarehe 10 Juni 2021 kuwa wananchi wa maeneo yaliyopitiwa na mradi huo walitoa maeneo yao kwa hiari na hivyo hawakustahili kulipwa fidia.

**iii. Malipo ya Shilingi Milioni 114 kwa Kazi Ambazo Hazikufanyika**

Halmashauri ya Mji Bariadi iliingia mkataba Na. LGA/158/2016/2017/C/02 wa tarehe 29 Mei 2017 kwa ajili ya usimamizi wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Kisasa

Somanda na barabara za kiwango cha lami za kilomita 1.5 kwa gharama ya shilingi milioni 691.95. Pia, Halmashauri iliingia mkataba Na. LGA/158/2018/2019/C/01 na Kampuni hiyo kwa ajili ya usimamizi wa mradi wa ujenzi wa kituo cha maegesho ya malori kwa shilingi milioni 496.80.

Nilibaini kuwa kutokana na mkataba wenye Na. LGA/158/2016/2017/C/02, Halmashauri ilimlipa mkandarasi jumla ya shilingi milioni 532.03. Kati ya malipo hayo, shilingi milioni 95 zililipwa kwa mishahara ya mhandisi wa mitaro, mhandisi wa jengo, na mpimaji wa topografia. Vilevile, ilifanya malipo ya shilingi milioni 400.20 kwa jili ya mkataba Na. LGA/158/2018/2019/C/01 ikijumisha shilingi milioni 19 za mishahara ya mpimaji wa topografia na mkurugenzi wa mradi.

**Ninapendekeza Ofisi ya Rais - TAMISEMI ichukue hatua stahiki dhidi ya maofisa walioshiriki kulipa shilingi milioni 114 kwa wakandarasi washauri kwa kazi ambazo hazikufanyika hivyo kusababisha upotevu wa fedha.**

**iv. Fedha za ULGSP Zilizochepushwa Shilingi Milioni 704.11**

Halmashauri ya Mji Bariadi ilipokea jumla ya shilingi bilioni 22.82 kwa kipindi cha miaka mitano kwa ajili ya mradi wa maendeleo uliotekelezwa chini ya ufadhili wa Programu ya Kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mijini, na hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Halmashauri ilikuwa imetumia jumla ya shilingi bilioni 22.12 hivyo kusalia kiasi cha shilingi milioni 704.11.

Nilibaini kuwa tarehe 26 Juni 2020 Halmashauri kupitia hati ya malipo Na. 472036v2003099 ilihamisha shilingi milioni 471.01 kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya amana. Pia, nilibaini jumla ya shilingi milioni 290.14 zilikatwa kutoka katika malipo ya mkandarasi mwenye mkataba Na. LGA/158/ULGSP/2017/2018/W/02 na kuwekwa katika akaunti ya amana kama fedha za matazamio.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 22 Mei 2021, akaunti ya amana ilikuwa na shilingi milioni 111.49 ikimaanisha fedha ya Programu ya

Kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mijini zilizosalia jumla ya shilingi milioni 704.11 zilikuwa zimetumika kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa.

Hali hii ni kinyume na mkataba uliongiwa tarehe 11 Disemba 2012 kati ya Shirika la Kimataifa la Maendeleo (International Development Association) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliotaka taasisi nufaika kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha, uwazi na uwajibikaji.

**Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI anashauriwa kuhakikisha kuwa menejimenti ya Halmashauri ya Mji inarejesha kiasi cha shilingi milioni 704.11 za mradi wa Programu ya Kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mijini.**

### 15.2.22 Halmashauri ya Wilaya ya Songwe

**i. Ubadhirifu na upotevu wa fedha za mapato shilingi milioni 65.16**

Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa kukusanyia mapato kwa mwaka wa fedha 2018/2019, 2019/2020, na 2020/2021 nilibaini miamala ya madeni ya wakusanyaji mapato yenye jumla ya shilingi milioni 19.76 yaliyofutwa katika Mfumo wa Kukusanya Mapato kupitia dirisha la nyuma kwa kuingiza namba za risiti zisizo halali. Kadhalika, kiasi cha shilingi milioni 33.59 zilikabidhiwa kwa watumishi wa Halmashauri na wakusanyaji mapato bila kupelekwa benki. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 11.80 za makusanyo ya ada za leseni hazikupelekwa benki.

Ubadhirifu wa mapato kiasi cha shilingi milioni 65.16 ulichangiwa na udhibiti hafifu wa miamala iliyofanyika kupitia dirisha la nyuma kinyume na Agizo la 50(5) la Randama ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI (a) iwasiliane na TAKUKURU ili kufanya uchunguzi na kubaini uhalali wa miamala ya mapato iliyofutwa kupitia dirisha la nyuma la mfumo wa mapato; kuchukua hatua stahiki kwa watumishi waliohusika ili warejeshe**

**kiasi hicho cha shilingi milioni 65.16 kilichopotea; Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kuchunguza na kuthibitisha uhalali wa miamala ya mapato iliyofutwa kupitia dirisha la nyuma la Mfumo wa Kukusanya Mapato, na kuchukua hatua stahiki dhidi ya watumishi wote waliohusika na upotevu wa shilingi milioni 65.16.**

### 15.2.23 Halmashauri ya Wilaya ya Igunga

**i. Usajili Wenye Shaka wa Mashine Mbili za POS Zilizokusanya Shilingi Milioni 130.99**

Kupitia taarifa za Mfumo wa Kukusanyia Mapato kutoka katika kanzidata nilibaini kuwapo kwa mashine 2 za kukusanyia mapato (POS) zilizosajiliwa kwa namba zenye shaka, kwa mfano 'NULL' zilizokusanya jumla ya shilingi milioni 130.99.

Kutoonekana kwa namba za usajili wa mashine za POS kunatokana na udhibiti hafifu wa mfumo wa ukusanyaji mapato hali inayosababisha kushindwa kuzuia upotevu wa fedha za umma; na kunaweza kutoa mwanya kwa watumishi wasio waaminifu kutumia nafasi hiyo kujinufaisha binafsi.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na mamlaka zingine za uchunguzi ili zifuatilie kwa kina ubadhirifu wa fedha za umma kiasi cha shilingi milioni 130.99 zilizokusanywa kupitia mashine za kukusanya mapato zilizosajiliwa kwa namba zenye shaka na kuwachukulia hatua stahiki wote waliohusika na mapungufu hayo.**

**ii. Stakabadhi za Kielekitoniki Zilizoghushiwa Zenye Thamani ya Shilingi Milioni 190.12**

Wakati wa ujenzi wa Kituo cha Afya cha Simbo, jumla ya shilingi milioni 192.48 zililipwa kwa wazabuni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. Wakati wa ukaguzi nilibaini risiti za kielekitroniki zenye thamani ya shilingi milioni 190.13 zilizowasilishwa na wazabuni hao hazikuwa halisi kwa mujibu wa uthibitisho uliotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kupitia barua yenye Kumb. Na. TRA/DM/IG/GC/VOL.2/86 ya tarehe 15 Juni 2021.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania ichukue hatua stahiki dhidi ya wazabuni waliotoa stakabadhi za kielekitroniki za kughushi za jumla ya shilingi milioni 190.13.**

### 15.2.24 Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi

#### i. Makusanyo ya Shilingi Milioni 360.23 ya Mawakala Waliositishiwa Mikataba Ambayo Hayakupelekwa Benki

Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi iliingia mikataba na kampuni mbili kwa ajili ya uwakala wa ukusanyaji wa mapato kwa vipindi tofauti. Kampuni hizo zilitakiwa kurejesha shilingi milioni 183.33 na shilingi milioni 45 kwa mwezi mtawalia.

Mzabuni wa kwanza aliingia mkataba wa kukusanya mapato kuanzia tarehe 5 Oktoba 2017 hadi tarehe 5 Aprili 2018 kwa kutumia mashine za kukusanyia mapato (POS); na mzabuni wa pili aliingia mkataba wa kukusanya mapato kwa kuanzia tarehe 1 Agosti 2015 hadi tarehe 30 Juni 2016 kwa kutumia vitabu vya kukusanyia mapato (HW5). Kwa mujibu wa mikataba hiyo, wazabuni hao walipaswa kukusanya mapato na kuyawasilisha katika akaunti ya benki ya Halmashauri ndani ya siku 15 baada ya kukusanya, kisha halmashauri kuwalipa kamisheni, na endapo watachelewesha mzabuni atatozwa asilimia 20 ya kiasi cha makusanyo kama adhabu.

Mawakala hao wawili hawakutii masharti ya kimkataba yaliyokubaliwa na kusababisha mikataba yao kusitishwa.

Pamoja na Halmashauri kusitisha mikataba na wazabuni hao, kufungua kesi mahakamani ambayo baadaye iliondolewa na kisha kuingia Mkataba Na. LGA/127/2019/2020/NC/02 na kampuni ya ufirisi ya Mjini Tanga tarehe 1 Agosti 2020 kwa ajili ya kuuza mali za wazabuni ili kurejesha jumla ya shilingi milioni 360.23 ambazo hazikupatikana kwa kuwa mali za wazabuni katika soko zina thamani ya chini ikilinganishwa na madeni yao.

**Ninashauri Ofisi ya Rais - TAMISEMI iwasiliane na TAKUKURU ili kufanya uchunguzi kuhusu mapato hayo kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki dhidi ya mawakala hao.**

**ii. Hasara ya shilingi milioni 547.59 iliyotokana na udanganyifu wa marekebisho ya miamala katika mfumo wa mapato**

Nimebaini kuwa kati ya mwaka 2018/19 na 2020/21 watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi walifuta miamala ili kuficha jumla ya shilingi milioni 547.59 ambazo walizifanyia ubadhirifu.

Ninapendekeza **Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI ihakikishe hatua stahiki zinachukuliwa kwa watumishi wote waliohusika katika upotevu wa mapato ya Halmashauri kwa kutumia mapato bila kupelekwa benki na kufuta miamala isivyostahili ndani ya Mfumo wa Kukusanya Malipo.**

# MAPENDEKEZO YA JUMLA NA HITIMISHO

## Mapendekezo ya Jumla

Ni matarajio yangu kwamba, Serikali itaandaa mpangokazi endelevu ili kuwezesha utekelezaji wa mapendekezo yanayojirudia kwa wakati, huku ikihusisha mikakati inayotekelezeka ya kutekeleza mapendekezo ya muda mrefu. Zaidi ya hayo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapaswa kuanzisha na kuimarisha udhibiti wa ndani uliopo na ulioanzishwa hivi karibuni ikiwa pamoja na mifumo ya kielekitroniki ili kupunguza hatari zinazohusiana na ukusanyaji wa mapato; na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na taratibu zilizowekwa.

## Hitimisho la Jumla

Ninashukuru sana kwa ushirikiano wa karibu wa wadau wetu wakiwemo Serikali, Bunge na mamlaka za serikali za mitaa, watunga sera na wataalamu kwa juhudi zao zilizoniwezesha kutoa ripoti inayofikisha taarifa kwa umma. Ni imani yangu kwamba mtanipa ushirikiano kama huu katika miaka ijayo ya ukaguzi.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Na.1-1: Hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | H/Jiji Arusha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 2. | H/W Arusha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 3. | H/W Babati | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 4. | H/Mji Babati | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 5. | H/W Bagamoyo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 6. | H/W Bahi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 7. | H/W Bariadi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 8. | H/Mji Bariadi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 9. | H/W Biharamulo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 10. | H/W Buchosa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 11. | H/W Buhigwe | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 12. | H/W Bukoba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 13. | H/M Bukoba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 14. | H/W Bukombe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 15. | H/W Bumbuli | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 16. | H/W Bunda | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati mbaya |
| 17. | H/Mji Bunda | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 18. | H/W Busega | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 19. | H/W Busokelo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 20. | H/W Butiama | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 21. | H/W Chalinze | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 22. | H/W Chamwino | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 23. | H/W Chato | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 24. | H/W Chemba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 25. | H/W Chunya | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 26. | H/Jiji Dar es Salaam (Zamani H/M Ilala) | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 27. | Iliyokuwa H/Jiji Dar es Salaam | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati yenye shaka |
| 28. | H/Jiji Dodoma | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 29. | H/W Gairo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 30. | H/W Geita | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 31. | H/Mji Geita | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 32. | H/W Hai | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 33. | H/W Hanang | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 34. | H/W Handeni | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 35. | H/Mji Handeni | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 36. | H/Mji Ifakara | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 37. | H/W Igunga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 38. | H/W Ikungi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 39. | H/W Ileje | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 40. | H/M Ilemela | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 41. | H/W Iramba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 42. | H/W Iringa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 43. | H/M Iringa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 44. | H/W Itigi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 45. | H/W Itilima | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 46. | H/M Kahama | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 47. | H/W Kakonko | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 48. | H/W Kalambo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 49. | H/W Kaliua | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 50. | H/W Karagwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 51. | H/W Karatu | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 52. | H/W Kasulu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 53. | H/Mji Kasulu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 54. | H/W Kibaha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 55. | H/Mji Kibaha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 56. | H/W Kibiti | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 57. | H/W Kibondo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 58. | H/M Kigamboni | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 59. | H/W Kigoma | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 60. | H/M Kigoma/Ujiji | Hati mbaya | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 61. | H/W Kilindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 62. | H/W Kilolo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 63. | H/W Kilosa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 64. | H/W Kilwa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 65. | H/M Kinondoni | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 66. | H/W Kisarawe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 67. | H/W Kishapu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 68. | H/W Kiteto | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 69. | H/W Kondoa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 70. | H/Mji Kondoa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 71. | H/W Kongwa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 72. | H/W Korogwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 73. | H/Mji Korogwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 74. | H/W Kwimba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 75. | H/W Kyela | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 76. | H/W Kyerwa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 77. | H/M Lindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 78. | H/W Liwale | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 79. | H/W Longido | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 80. | H/W Ludewa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 81. | H/W Lushoto | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 82. | H/W Madaba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 83. | H/W Mafia | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 84. | H/Mji Mafinga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 85. | H/W Magu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 86. | H/Mji Makambako | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 87. | H/W Makete | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 88. | H/W Malinyi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 89. | H/W Manyoni | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 90. | H/W Masasi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 91. | H/Mji Masasi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 92. | H/W Maswa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 93. | H/W Mbarali | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 94. | H/Jiji Mbeya | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 95. | H/W Mbeya | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 96. | H/W Mbinga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 97. | H/Mji Mbinga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 98. | H/W Mbogwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 99. | H/W Mbozi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 100. | H/W Mbulu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 101. | H/Mji Mbulu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 102. | H/W Meatu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 103. | H/W Meru | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 104. | H/W Missenyi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 105. | H/W Misungwi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 106. | H/W Mkalama | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 107. | H/W Mkinga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 108. | H/W Mkuranga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 109. | H/W Mlele | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 110. | H/W Mlimba | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 111. | H/W Momba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 112. | H/W Monduli | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 113. | H/W Morogoro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 114. | H/M Morogoro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 115. | H/W Moshi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 116. | H/M Moshi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 117. | H/W Mpanda | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 118. | H/M Mpanda | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 119. | H/W Mpimbwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 120. | H/W Mpwapwa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 121. | H/W Msalala | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 122. | H/W Mtama (Iliyokuwa H/W Lindi) | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 123. | H/W Mtwara | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 124. | H/M Mtwara | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 125. | H/W Mufindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 126. | H/W Muheza | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 127. | H/W Muleba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 128. | H/W Musoma | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka |
| 129. | H/M Musoma | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 130. | H/W Mvomero | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 131. | H/W Mwanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 132. | H/Jiji Mwanza | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 133. | H/W Nachingwea | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 134. | H/W Namtumbo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 135. | H/Mji Nanyamba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 136. | H/W Nanyumbu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 137. | H/W Newala | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 138. | H/Mji Newala | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 139. | H/W Ngara | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 140. | H/W Ngorongoro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 141. | H/W Njombe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 142. | H/Mji Njombe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 143. | H/W Nkasi | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 144. | H/W Nsimbo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 145. | H/W Nyanghw'ale | Kushindwa kutoa maoni | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 146. | H/W Nyasa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 147. | H/W Nzega | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 148. | H/Mji Nzega | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 149. | H/W Pangani | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 150. | H/W Rombo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 151. | H/W Rorya | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 152. | H/W Ruangwa | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 153. | H/W Rufiji | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 154. | H/W Rungwe | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 155. | H/W Same | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 156. | H/W Sengerema | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka |
| 157. | H/W Serengeti | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 158. | H/W Shinyanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 159. | H/M Shinyanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 160. | H/W Siha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 161. | H/W Sikonge | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 162. | H/W Simanjiro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 163. | H/W Singida | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 164. | H/M Singida | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 165. | H/W Songea | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 166. | H/M Songea | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 167. | H/W Songwe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
|---|---|---|---|---|---|
| 168. | H/W Sumbawanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 169. | H/M Sumbawanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 170. | H/M Tabora | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 171. | H/W Tandahimba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 172. | H/Jiji Tanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 173. | H/W Tarime | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 174. | H/Mji Tarime | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 175. | H/M Temeke | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 176. | H/Mji Tunduma | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 177. | H/W Tunduru | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 178. | H/M Ubungo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 179. | H/W Ukerewe | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 180. | H/W Ulanga | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 181. | H/W Urambo | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati mbaya | Hati inayoridhisha |
| 182. | H/W Ushetu | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 183. | H/W Uvinza | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha |
| 184. | H/W Uyui | Hati yenye shaka | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 185. | H/W Wanging'ombe | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |

## Kiambatisho Na.2 - 1: Mapendekezo ya ukaguzi yasiyotekelezwa

| Na. | Jina la Halmashauri | Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | | Na. | Jina la Halmashauri | Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | | | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
| 1. | H/W Bariadi | 2 | 1 | 1 | 59. | H/W Kilolo | 1 | 2 | 1 |
| 2. | H/Mji Bariadi | 1 | 3 | 1 | 60. | H/W Kyela | | 4 | |
| 3. | H/W Bukombe | 1 | 1 | | 61. | H/W Namtumbo | | | 5 |
| 4. | H/W Bumbuli | 2 | 4 | 5 | 62. | H/W Nkasi | 4 | 6 | 3 |
| 5. | H/W Busega | 3 | 5 | 5 | 63. | H/W Nzega | 5 | 10 | 5 |
| 6. | H/W Handeni | | | 4 | 64. | H/M Sumbawanga | 2 | 4 | 4 |
| 7. | H/W Igunga | 2 | 2 | 4 | 65. | H/M Iringa | 2 | | |
| 8. | H/W Ikungi | 1 | | 1 | 66. | H/W Geita | 1 | 2 | 2 |
| 9. | H/W Itilima | 2 | 4 | | 67. | H/W Misungwi | | 1 | 1 |
| 10. | H/W Kaliua | 1 | 4 | 3 | 68. | H/W Muleba | 1 | 6 | 1 |
| 11. | H/W Kibondo | 1 | | 2 | 69. | H/Jiji Mwanza | 3 | | 4 |
| 12. | H/W Kilosa | | 1 | 1 | 70. | H/W Sengerema | | | 3 |
| 13. | H/M Kinondoni | | | 1 | 71. | H/W Siha | 1 | 1 | 4 |
| 14. | H/W Kishapu | | 3 | 6 | 72. | H/W Chamwino | 2 | 3 | 1 |
| 15. | H/W Kondoa | 4 | 2 | 2 | 73. | H/W Chemba | 1 | 1 | |
| 16. | H/W Kongwa | 1 | 2 | | 74. | H/Jiji Dodoma | 1 | 2 | |
| 17. | H/Mji Korogwe | 1 | | 3 | 75. | H/W Kalambo | 3 | 2 | 1 |
| 18. | H/W Kyerwa | 3 | | 6 | 76. | H/W Kwimba | 3 | 6 | 1 |
| 19. | H/W Lushoto | 2 | | 1 | 77. | H/Mji Kondoa | | | 2 |
| 20. | H/W Mbogwe | 1 | 6 | 9 | 78. | H/W Arusha | | 1 | 2 |
| 21. | H/W Meru | 1 | 4 | 7 | 79. | H/W Bukoba | 9 | 4 | 4 |
| 22. | H/W Mlele | | 4 | 4 | 80. | H/M Bukoba | | | 2 |
| 23. | H/W Mpanda | 2 | | 3 | 81. | H/W Bunda | 2 | 1 | 4 |
| 24. | H/W Mpwapwa | | 2 | | 82. | H/W Busekelo | 4 | 2 | 2 |
| 25. | H/W Msalala | 1 | 6 | 4 | 83. | H/W Butiama | | 6 | 4 |
| 26. | H/W Muheza | 2 | 7 | 4 | 84. | H/W Chunya | | | 1 |
| 27. | H/W Mwanga | 3 | 13 | 6 | 85. | H/W Karagwe | 2 | 1 | 2 |
| 28. | H/W Ngara | 2 | 6 | 4 | 86. | H/W Magu | | 2 | 2 |
| 29. | H/W Ngorongoro | 2 | | 3 | 87. | H/Jiji Mbeya | | | 1 |
| 30. | H/W Nsimbo | 1 | 3 | 1 | 88. | H/W Mbogwe | 1 | | 15 |
| 31. | H/W Shinyanga | 3 | 5 | 4 | 89. | H/M Moshi | 2 | 8 | 3 |

| Na. | Jina la Halmashauri | Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | | Na. | Jina la Halmashauri | Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 | | | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
| 32. | H/M Shinyanga | | 1 | | 90. | H/W Moshi | 2 | 2 | 1 |
| 33. | H/W Sikonge | 2 | 1 | | 91. | H/M Musoma | | | 3 |
| 34. | H/W Singida | 1 | 2 | | 92. | H/W Rorya | 1 | 2 | 2 |
| 35. | H/M Tabora | 1 | 2 | | 93. | H/W Same | | 2 | 1 |
| 36. | H/Jiji Tanga | 1 | 5 | 3 | 94. | H/W Serengeti | | 3 | 4 |
| 37. | H/W Tarime | 1 | 2 | | 95. | H/W Shinyanga | 3 | 4 | 4 |
| 38. | H/W Ukerwe | 4 | 2 | 11 | 96. | H/M Shinyanga | | 1 | |
| 39. | H/W Urambo | 3 | 10 | 6 | 97. | H/W Tarime | 2 | | 2 |
| 40. | H/W Mbeya | | 2 | | 98. | H/W Ukerewe | 4 | 2 | 4 |
| 41. | H/W Mufindi | 1 | | 1 | 99. | H/W Ushetu | 1 | | 4 |
| 42. | H/Mji Muheza | 3 | 8 | 3 | 100. | H/W Kilwa | 1 | 1 | |
| 43. | H/W Nyang'hwale | 1 | 1 | 2 | 101. | H/Mji Masasi | 3 | | |
| 44. | H/W Nyasa | 1 | 1 | 1 | 102. | H/W Mkuranga | | 1 | 3 |
| 45. | H/W Sumbawanga | 4 | 2 | 3 | 103. | H/W Mlimba | | 1 | |
| 46. | H/W Uyui | | | 1 | 104. | H/W Morogor | | 2 | |
| 47. | H/W Meatu | 5 | 2 | 1 | 105. | H/M Morogor | | 1 | |
| 48. | H/M Moshi | 8 | 7 | 3 | 106. | H/M Mtwara | | 1 | |
| 49. | H/W Kiteto | | | 4 | 107. | H/W Mvomero | | 2 | |
| 50. | H/W Longido | 8 | 19 | 3 | 108. | H/W Nachingea | | 2 | |
| 51. | H/W Hanang' | 1 | | 1 | 109. | H/W Newala | | | 1 |
| 52. | H/Mji Handeni | | 4 | 3 | 110. | H/W Ruangwa | 1 | 1 | 1 |
| 53. | H/W Korogwe | 10 | 5 | 6 | 111. | H/M Temeke | | | 1 |
| 54. | H/W Mkinga | 2 | 1 | 4 | 112. | H/W Biharamulo | | 5 | 3 |
| 55. | H/W Pangani | 4 | 4 | 6 | 113. | H/W Chato | | | 4 |
| 56. | H/W Rombo | | 5 | 5 | 114. | H/Mji Nanyamba | | | 1 |
| 57. | H/W Iramba | 3 | | 1 | | | | | |
| 58. | H/W Bahi | 1 | 3 | 1 | | **Jumla** | **178** | **285** | **283** |

## Kiambatisho Na.2-2: Halmashauri zenye mapendekezo yasiyotekelezwa kwa muda mrefu

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | | | Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Mapendekezo Yasiyotekelezwa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | | | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 |
| 1. | H/W Bariadi | | | | 1 | 32. | H/W Kyela | | | 1 | 4 |
| 2. | H/Mji Bariadi | | | | 3 | 33. | H/W Nkasi | | 1 | 3 | |
| 3. | H/W Bumbuli | | | | 2 | 34. | H/W Nzega | | | | 2 |
| 4. | H/W Gairo | | | | 2 | 35. | H/M Sumbawanga | | | 1 | |
| 5. | H/W Handeni | | | 2 | 1 | 36. | H/W Tandahimba | | | | 1 |
| 6. | H/W Itilima | | | | 1 | 37. | H/M Iringa | | | | 1 |
| 7. | H/W Kakonko | | | | 4 | 38. | H/W Geita | 1 | | 1 | 1 |
| 8. | H/W Kibondo | | | 1 | | 39. | H/W Misungwi | | | | 1 |
| 9. | H/Mji Korogwe | | | 1 | 1 | 40. | H/Jiji Mwanza | | | 1 | |
| 10. | H/W Lushoto | | | | 1 | 41. | H/W Sengerema | | 1 | | |
| 11. | H/W Mbogwe | | | | 1 | 42. | H/W Siha | | | | 1 |
| 12. | H/W Mpanda | | | | 2 | 43. | H/Jiji Dodoma | 2 | 1 | | |
| 13. | H/W Muheza | | | | 3 | 44. | H/W Kalambo | | | | 2 |
| 14. | H/W Mwanga | | | | 1 | 45. | H/W Kwimba | | | 1 | 3 |
| 15. | H/W Ngara | | | 3 | | 46. | H/W Bukoba | | | | 1 |
| 16. | H/W Shinyanga | | | | 1 | 47. | H/M Bukoba | 1 | | 4 | 1 |
| 17. | H/M Shinyanga | 1 | | | | 48. | H/W Bunda | | | 1 | 1 |
| 18. | H/M Tabora | | | 2 | | 49. | H/W Busekelo | | | | 1 |
| 19. | H/W Ukerwe | | 2 | 2 | 1 | 50. | H/W Karagwe | | 2 | 3 | |
| 20. | H/W Mufindi | | | | 3 | 51. | H/W Magu | | | 1 | |
| 21. | H/Mji Muheza | | | | 3 | 52. | H/W Mbogwe | | | | 1 |
| 22. | H/W Nyang'hwale | | | | 3 | 53. | H/M Moshi | | | 1 | |
| 23. | H/W Sumbawanga | | | 1 | 4 | 54. | H/W Moshi | | | 1 | |
| 24. | H/W Uyui | | 1 | | | 55. | H/W Same | | | | 2 |
| 25. | H/W Meatu | | | 1 | 4 | 56. | H/W Serengeti | | | | 1 |
| 26. | H/W Kiteto | | | 1 | | 57. | H/W Shinyanga | | | | 1 |
| 27. | H/W Longido | | | | 4 | 58. | H/M Shinyanga | | 1 | | |
| 28. | H/W Mkinga | 1 | 1 | 2 | 2 | 59. | H/W Ukerewe | | 2 | 2 | |
| 29. | H/W Pangani | 1 | | 5 | 1 | 60. | H/Mji Masasi | | | | 1 |
| 30. | H/W Iramba | 1 | 1 | 2 | 4 | 61. | H/W Chato | 1 | | | |
| 31. | H/W Rungwe | | | 1 | 1 | | **Jumla** | **9** | **13** | **45** | **80** |

## Kiambatisho Na.2-3: Hali ya utekelezaji wa maagizo ya kamati ya LAAC

| Na. | Jina la Halmashauri | 2016/17 | | | 2017/18 | | | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa |
| 1. | H/W Chamwino | | | | | | | | | | | | |
| 2. | H/W Chemba | | | | | | | | | | | | |
| 3. | H/Jiji Dodoma | | | | | | | | | | | | 3 |
| 4. | H/W Kalambo | 4 | 2 | | | | | | | | | | |
| 5. | H/W Kwimba | 6 | | | | | | | | | | | |
| 6. | H/W Mafia | | | | | | | | | | 9 | | |
| 7. | H/W Mbeya | | | | 2 | | 2 | | | | | | |
| 8. | H/W Mkalama | | | | | | | | | | | | 3 |
| 9. | H/M Mpanda | | | | | | | | | | | | |
| 10. | H/W Mufindi | | | | | | | | | | 8 | 4 | |
| 11. | H/W Muheza | | 1 | | | 1 | | | 1 | | | 1 | |
| 12. | H/M Songea | | | | | | | | | | | | |
| 13. | H/W Sumbawanga | | 3 | | | 3 | | | 3 | | 2 | 3 | 3 |
| 14. | H/W Nyasa | | 2 | | | 2 | | | 2 | | | 2 | |
| 15. | H/W Uvinza | | 3 | | | 3 | | | 3 | | | 3 | |
| 16. | H/W Uyui | | 6 | | | 6 | | | 6 | | | 6 | |
| 17. | H/W Geita | | 2 | | | 2 | | | 2 | | | 2 | |
| 18. | H/M Iringa | | 5 | | | 5 | | | 5 | | | 5 | |
| 19. | H/M Kahama | | 1 | | | 1 | | | 1 | | | 1 | |
| 20. | H/Mji Kibaha | | 2 | | | 2 | | | 2 | | | 2 | |
| 21. | H/W Makete | | | | | | | | | | 4 | 2 | |
| 22. | H/W Misungwi | | 3 | | | 3 | | | 3 | | | 3 | |
| 23. | H/W Muleba | | | | | | | 2 | 3 | | | | |
| 24. | H/W Sengerema | | | | | | | | | | 2 | 1 | |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2016/17 | | | 2017/18 | | | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyote kelezwa | Yasiyotekelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa |
| 25. | H/W Siha | | | | | | | | | | 2 | 1 | 1 |
| 26. | H/W Iramba | | 4 | 3 | | | | | | | | | |
| 27. | H/W Bahi | | 1 | 3 | | | | | | | | | |
| 28. | H/W Ileje | | | | | | | | | | | | 3 |
| 29. | H/W Iringa | | | | 2 | 3 | | | | | | | |
| 30. | H/W Kigoma | | 7 | | | 2 | | | 7 | | | 7 | |
| 31. | H/W Kilolo | | | | 5 | 3 | | | | | | | |
| 32. | H/W Kyela | | | | 2 | 7 | | | | | | | |
| 33. | H/W Ludewa | | | | | 1 | | | | | | | |
| 34. | H/Mji Makambako | | | | | | | | | | | 5 | |
| 35. | H/W Mbinga | | | | 3 | 2 | | | | | | | |
| 36. | H/W Mbozi | 5 | 2 | | | | | | | | | | |
| 37. | H/W Namtumbo | | 6 | | | | | | | | | | |
| 38. | H/Mji Njombe | 3 | | | | | | | | | | | |
| 39. | H/W Nzega | | | | | | 3 | | | | | | |
| 40. | H/W Rungwe | | | | | 2 | 3 | | | | | | |
| 41. | H/M Sumbawanga | | 1 | | | | | | | | | | |
| 42. | H/W Tandahimba | | 6 | | | | | | | | | | |
| 43. | H/M Ubungo | | 3 | | | | | | | | | | |
| 44. | H/W Wang'ing'ombe | | | | | | | | | | 2 | 2 | |
| 45. | H/W Bariadi | 2 | 2 | | | | | | | | | | |
| 46. | H/Mji Bariadi | | | | | | | | | | | | 3 |
| 47. | H/W Buchosa | | | | | 1 | 1 | | | | | | |
| 48. | H/W Bukombe | 3 | | 3 | | | | | | | | | |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2016/17 | | | 2017/18 | | | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyote kelezwa | Yasiyotekelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayo endelea Kutekelezwa |
| 49. | H/W Bumbuli | | | | | | | 3 | 1 | | | | |
| 50. | H/W Busega | | | | | | | | | | 5 | | 3 |
| 51. | H/W Gairo | 2 | | 2 | | | | | | | | | |
| 52. | H/W Handeni | | | | 1 | | 4 | | | | | | |
| 53. | H/W Igunga | | | | | | 3 | | | | | | |
| 54. | H/W Ilemela | | | | | | | 5 | | | | | |
| 55. | H/W Itigi | | | | 2 | | 1 | | | | | | |
| 56. | H/W Itilima | 1 | 3 | 1 | | | | | | | | | |
| 57. | H/W Kaliua | 2 | 2 | | | | | | | | | | |
| 58. | H/W Kibondo | | | | | | | | | | | | 7 |
| 59. | H/W Kilosa | | | | 2 | 2 | | | | | | | |
| 60. | H/M Kinondoni | | | | | | | | | | 2 | 2 | |
| 61. | H/W Kondoa | | | | 3 | | | | | | | | |
| 62. | H/W Kongwa | | | | | | | | | 2 | | | |
| 63. | H/Mji Korogwe | 7 | | 1 | | | | 1 | | 1 | 4 | | 1 |
| 64. | H/W Kyerwa | | | | | | | | | 4 | | | |
| 65. | H/W Lushoto | | | | 15 | 1 | 4 | | | | | | |
| 66. | H/W Maswa | 2 | | 2 | | | | | | | | | |
| 67. | H/W Mbarali | 2 | | 4 | | | | | | | | | |
| 68. | H/W Mbogwe | 1 | | 3 | | | | | | | | | |
| 69. | H/W Meru | | | | | | | | | | 3 | 1 | |
| 70. | H/W Mlele | 6 | | 2 | | | | | | | | | |
| 71. | H/W Mpanda | | | | | | | 2 | | 1 | | | |
| 72. | H/W Muheza | 7 | 1 | | | | | | | | | | |
| 73. | H/W Ngara | | | | | | | 3 | | 2 | | | |
| 74. | H/W Nsimbo | 4 | | 2 | | | | | | | | | |
| 75. | H/Mji Nzega | | | | | | | 2 | | 1 | | | |
| 76. | H/W Serengeti | 1 | 1 | | | | | | | | | | |

| Na. | Jina la Halmashauri | 2016/17 | | | 2017/18 | | | 2018/19 | | | 2019/20 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Yaliyote kelezwa | Yasiyotekelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa | Yaliyote kelezwa | Yasiyote kelezwa | Yanayoendelea Kutekelezwa |
| 77. | H/W Sikonge | 9 | 1 | 2 | | | | | | | | | |
| 78. | H/W Nyang'hwale | | | | | | 5 | | | | | | |
| 79. | H/W Singida | | | | | | | | | | 2 | 8 | |
| 80. | H/M Tabora | 9 | 4 | | | | | | | | | | |
| 81. | H/Jiji Tanga | | 1 | 5 | | | | | | | | | |
| 82. | H/Mji Tarime | | | | | | | 4 | 1 | 1 | | | |
| 83. | H/W Ukerewe | | | | | | | 12 | 3 | | | | |
| 84. | H/W Ulanga | 5 | | | | | | | | | | | |
| 85. | H/W Urambo | | | | 1 | 2 | 1 | | | | | | |
| 86. | H/W Meatu | | | | | | | | | | 2 | 6 | |
| 87. | H/Mji Mbulu | | | | | | | | | | 2 | 2 | |
| 88. | H/Mji Babati | | | | | | | | | | | 2 | |
| 89. | H/W Karatu | | | | | | | | | | | 2 | |
| 90. | H/W Kiteto | 4 | | 2 | | | | | | | | | |
| 91. | H/W Longido | | | | 6 | | 8 | | | | | | |
| 92. | H/W Hanang | | | | 2 | | 4 | | | | | | |
| 93. | H/W Korogwe | 7 | | 1 | 3 | | | | | | | | |
| 94. | H/W Kyerwa | 4 | 3 | 1 | | | | | | | | | |
| 95. | H/W Lushoto | 2 | 6 | | | | | | | | | | |
| 96. | H/W Mkinga | | | | | | | | | 3 | | | |
| 97. | H/W Pangani | 2 | 5 | 3 | | | | | | | | | |
| 98. | H/W Monduli | | | | | | | | | | | 3 | 1 |
| 99. | H/W Rombo | | | | | | | | 2 | 1 | | | |
| Jumla | | 102 | 89 | 43 | 49 | 55 | 40 | 34 | 45 | 16 | 49 | 76 | 28 |

## Kiambatisho Na. 3-1: Mapungufu katika vitengo vya ukaguzi wa ndani

| Jina la Halmashauri | Upungufu wa Wakaguzi wa Ndani | Kutotolewa kwa fedha za kutosha kulingana na bajeti | 100% ya bajeti kutoka mapato ya ndani haikutolewa | Upungufu wa vitendea kazi (Magari, Kompyuta na Samani) | Kutokamilishwa kwa kazi kulingana na mpango kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| H/W Arusha | 2 | | | X | |
| H/W Babati | 3 | | | | X |
| H/Mji Babati | 2 | X | | | |
| H/W Bagamoyo | 2 | X | | | x |
| H/W Bahi | 3 | | | x | x |
| H/W Bariadi | 3 | | | X | |
| H/Mji Bariadi | 2 | X | | X | |
| H/W Buchosa | 3 | x | | | |
| H/W Buhigwe | 4 | x | | | |
| H/W Bukoba | 2 | X | | X | |
| H/M Bukoba | | X | | | X |
| H/W Bumbuli | 1 | x | | x | x |
| H/W Busega | 2 | x | | | x |
| H/W Chalinze | 2 | | | | |
| H/W Chamwino | 2 | x | | x | |
| H/W Chemba | X | | | X | X |
| H/W Hanang | 3 | x | | | x |
| H/W Handeni | 2 | | | X | |
| H/Mji Handeni | 2 | x | | X | x |
| H/W Igunga | | | | | x |
| H/W Ikungi | 2 | | | | X |
| H/M Ilala | | x | | | x |
| H/M Ilemela | 2 | X | | X | X |
| H/W Iramba | 3 | x | | X | x |
